# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, BAHARI CONSTITUENCY HELD AT KILIFI PRIMARY SCHOOL

## ON

**THURSDAY, 2ND MAY 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, BAHARI CONSTITUENCY, HELD AT KILIFI PRIMARY SCHOOL, ON THURSDAY, 2ND MAY, 2002**

**Present:**

Com. Mrs. Phoebe Asiyo
Com. Ibrahim Lethome Asmani

**Secretariat in Attendance:**

Joash Aminga - Programme Officer
Rachael S. Kitonyo - Asst. Programme Officer
Patricia Mwangi - Verbatim Reporting
Eunice Kasisi - Sign Language Interpreter

**Meeting was called to order at 9.00 a.m. with Com. Ibrahim Lethome in the chair.**

**Com. Lethome:** Watu huwa mwanzo wakiwa wachache, lakini saa zingine watu huwa wengi sana. Sasa tutaanza moja kwa moja "Isha Allah". Na kawaida yetu tunapoanza mikutano yetu, hutaka tuwe na baraka za Mungu "Supana wa'aalam" tukianza. Kwa hivyo tutamuomba Sheikh mmoja wa kiislamu halafu kama ndugu wakristo wapo, mmoja pia atatuombea. Kwa hivyo tunataka "dua" kutoka kwa Sheikh wa Kiislamu kisha maombi kutoka kwa mkristo yeyote tuweze kuanza shughuli zetu za leo. Haya tupate Sheikh mmoja basi.

**Sheikh:** Salamu Aleikum waraha matulahi tahana wabarakatu. (in Islam). Ewe Mwenyezi Mungu, Mungu wa pekee yake,

twajiweka katika muongozo wako kwa kusikizana na usalama na kufikia mkomo katika jambo hili kwa haki na radhi yako wewe Mwenyezi Mungu "Wahatha Salamu Aleikum waraha matulahi".

**Com. Lethome:** Asante. Tuweze kupata kasisi yote kutoka kwa wakristo.

**Prayers:** Baba wa Mbinguni, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo uishiye na kutawala milele, twaomba Mungu wa Israeli. Baba tunakushukuru jinsi ambavyo umetuongoza kutoka majumbani kwetu salama salimi tumefika hapa. Baba kabariki kusanyiko hili ambalo liko hapa, ili kwamba ukatupe maarifa, ukatupe ujasiri, ukatupe hekima za kibinguni, ewe Mwenyezi Mungu, ili kwamba yote tukayo yanena, yote tukakayo yatoa Baba yawe ni baraka kutoka kwako. Zaidi tukiwa tunashughulikia Kenya yetu, tunashughulikia mambo mbali mbali, Baba nenda ukawe kiongozi, ukawe mwenyekiti wa mkao huu. Baba ukatubariki, nasi tukiondoka tukiwa hali ya usalama na baraka kutoka kwako Mungu wetu, tutakushukuru sifa na utukufu ni vyako. Baba tunaomba ni katika jina la Mwanayo Yesu Kristo Bwana na Mwokozi wetu. Amen.

**Com. Lethome:** Nashukuru sana kwa hayo, sasa tutaanza. Ningependa tu kwanza kuwajulisha wale tulionao hapa wa Commission na wengine kutoka idara yetu Nairobi. Nafikiri mwenyeji wenu mnamujua, ambaye ni District Co-ordinator, Bwana Daniel Mwaringa mnamujua huyu. Huyu ndiye mwakilishi wetu katika wilaya ya Kilifi. Tulikuwa naye tangu Mariakani, Kaloleni na hapa leo na bado tutazidi kuwa naye, mpaka tutakaporudi Nairobi. Kisha tunaye Bwana Aminga ambaye ni Programume Officer wetu, yeye anashughulikia mambo ya idara. Shughuli zote tunazofanya yeye ndiye amesimamia. Upande huu tunaye Patricia Mwangi, kazi yake ni ku-record na kunasa sauti na kila jambo linalozungumzwa lazima linaswe na hiki chombo, na pia ana-record kwa shorthand. Kisha pale tuna Eunice, yeye kazi yake ni kutafsiri kwa wale ambao hawasikii, viziwi. Anatumia ile inaitwa sign language, kwa sababu hao ni wakenya pia, na lazima maoni yao yachukuliwe pia. Kwa hivyo ni kazi yake, lakini nyinyi ndio mtakayotujulisha, akija mtu yeyote ambaye pengine ana udhaifu kama huo, tuweze kujulishwa ili aweze kufanya kazi yake. Nasikia kuna skuli hapa ya watu kama hao pengine wataweza kufika hapa, wakifika tujulishwe, na tutafanya kazi hiyo. Halafu tunaye Racheal, kazi yake ni ku-record, hatutaki neno hata moja litupite. Hii Katiba tunayounda hivi sasa, ni ya watu, maoni ya watu lazima yachukuliwe. Commissioners tulionao mmoja kwa bahati mbaya ameugua, amerudi Mombasa, Commissioner Isaac Lenaola ilibidi arudi akatafute matibabu, anaona kisuunzi. Yule bibi nafikiria mnamjua yeye, alikuwa ni mbunge wa zamani kutoka Karachuonyo, ni mheshimiwa, Commissioner Phoebe Asiyo, na mimi ni ndugu yenu Ibrahim Lethome na nitakuwa kinara wa leo, kuendesha shughuli hii. Na katika hizi shughuli kuna baadhi, hata mchezo wa mpira una masharti yake, kila jambo lina masharti yake, ama sivyo Sheikh? Hakuna jambo ambalo linaweza kwenda bila masharti yake. Kwa hivyo tusikizaneni tangu mwanzo, ili kazi iendelee vizuri.

Sharti ya kwanza. Hata nyumbani kwako wakati mwingine wewe una maoni tofauti na mama watoto, lakini ndio mwisho wa kuwa katika familia. Mnaishi pamoja, mnaweka sheria tu basi, kila mmoja akizifuata zile sheria mnaendelea kama familia. Sasa akija mtu hapa atoe maoni pengine ambayo wewe hukuridhika nayo, mwachie hayo ni maoni yake. Usimusomee wala nini, mpe nafasi yake atoe maoni yake, hayo ndiyo anayaona yeye. Kwa hivyo tumpeni haki, hakuna kusomeana.

Pili, hiki sio kikao cha kisiasa. Utakuja kuzungumza habari ya siasa kumkashifu fulani au fulani ama kumtoa fulani. Hatukuja hapa kwa sababu ya kumtoa fulani, tumekuja hapa kuangalia mstakbani wa nchi, tunataka tuhukumiwe vipi. Ni fursa ya kitarifu ambayo tumepewa. Tumeingoja miaka thelathini na tisa, imekuja na unaulizwa wewe Mkenya unataka kuhukumiwa vipi. Fursa sema hiyo, na vikao vya siasa vitakuja wakati wake. Kwa hivyo sio kikao cha kisiasa hiki; ni kutoa maoni. Kisha toa maoni, kuna watu wengine kidogo husitasita, naona mimi si mwana sheria bwana, hii mambo ya sheria nitawezaje kuzungumza ile lugha ya kisheria? La, tungetake lugha ya kisheria tungealika mawakili pekee yao, tumealika kila Mkenya. Zungumza kwa lugha yako mwenyewe, unavyofahamu, unavyotaka. Kama tatizo lako ni chifu anachukua kuku wako, unataka Katiba iandike hivyo, tuambie tu hivyo. Zuieni chifu kuchukua kuku wangu bila ruhusa yangu. Sisi tutajua namna ya kuiandika na lugha ya kisheria. Kwa hivyo usisite kuzungumza, zungumza maoni yako unavyotaka. Kisha tunajua kuna watu wengine wana memorandum, maandishi, wametayarisha. Muda nitakaokupa ukiwa una maandishi ni dakika tano, eleza yale ya muhimu, zile mikaso muhimu muhimu, katika hiyo memorandum yako kisha utatukabidhi. Tutakupa dakika tano, ikiwa Commissioners wana maswali, watawauliza. Lau hauna hiyo memorandum unataka kuzungumza tu, tutakupa dakika kumi. Usimame hapa, ueleze unavyotaka. Sasa pia hapa ningependa kuwapa faida kidogo, hizo dakika kumi ni chache sana, usione kama ni nyingi, ni chache mno. Ukianza kutupa hadithi nyingi, hutafaidika na hizi dakika kumi, utagongewa time imekwisha, kwa hivyo usianze story nyingi na kutoa mifano. La, matatizo tunayajua sote, sote ni wakenya twajua matatizo yetu. Sasa pendekeza, matatizo unayajua, pendekeza; matatizo yangu ni minazi inakatwa sana, pendekezo unataka sheria ifanye nini minazi iwache kukatwa? Sijui kuna wizi mwingi sana, pendekeza kufanywe nini. Kwa hivyo, toa mapendekezo, hadithi nyingi, visa vingi, baadaye tutazungumza hayo. Kwa hivyo nafikiri tutaanza hivyo, na nitaanza kuwaita watu moja moja, mkija hapa anza kuzungumza, na ikiwa pengine una memorandum na hutaki kuzungumza kabisa, tukabidhi utasajiliwa pale kwenye daftari yetu, kisha sasa utapumzika usikize wengine, la si hivyo una uhuru wa kuondoka. Kwa hivyo hiyo ndio taratibu ambayo tutakayofuata. Nafikiri tumeelewana sote. Haya, bila kupoteza wakati tutaanza, na naanza na huyu bwana ambaye anaitwa James Katana.

**James Katana:** Mimi nitaanzia kwa Jamhuri yenyewe ya Kenya. Mimi naitwa James Katana Muranga kutoka sehemu ya Roka.

**Com. Lethome:** Haya endelea James.

**James Katana:** Taifa likiwa liko na makabila arobaini na matatu, litaendelea kuitwa Kenya. Kusiwe na ubaguzi kati ya raia wa Kenya na upendeleo kati ya kabila fulani lililo kwenye mamlaka ya wakenya wengine ukome. Haki za kila raia zilindwe na mali zao. Kuwe na utandawazi katika kila jambo. Usawa wa kiuchumi kwa raia wote. Hati za kusafiri zipatikane kwa urahisi, kwa kila raia. Kitambulisho la kitaifa na njia za kukipata ziimarishwe kuuzuia wasio raia kuweza kukipata.

Naenda kwa bunge: bunge, kuwe na mabunge ya mikoa au majimbo. Bunge liwe na Tume huru lenye uwezo usioweza kuingiliwa. Tume hiyo iwe na uweza wa kuharisha na kuvunja bunge, sio Rais. Bunge lisiwe na uwezo wa kubadilisha Katiba

bila idhini ya kura ya maoni kutoka kwa umma. Kupiga kura kutokuwa na imani kwa serikali kuungwa mkono na theluthi mbili za tatu ya bunge ya majimbo. Bunge liwe na uwezo wa kumchagua kiranja wa bunge na naibu wake. Bunge litachagua waziri mkuu. Wabunge maalum wateuliwe na vyama vyao vya kisiasa. Mbunge awe raia wa Kenya mwenye umri usiopungua miaka thelathani na mitano. Mbunge awe na ufasaha na lugha yake kwanza na lugha ya Kiswahili na Kiingereza na sifa nzuri za uongozi. Mbunge achaguliwe kwa kila kipindi cha miaka mitano. Raia wawe na uwezo wa kumkataa mbunge wao kwa kura ya kutokuwa na imani, katika eneo lake la uwakilishi. Bunge liwe na uwezo wa kumshtaki Rais.

Naenda kwa mahakama. Kuundwe Judiciary Service Commission. Mahakama za Jamhuri ya Kenya ziwe huru kutekeleza kazi bila muingilio wa Rais ama ofisi yeyote kuu. Ofisi ya mkuu wa sheria iwe huru kutekeleza bila muingilio wowote. Kuundwe baraza la mashtaka lililo na uwezo kamili. Kuundwe mahakama ya kikatiba. Wananchi wawe na uwakilishi wa kisheria wa bure mahakamani. Hakimu mkuu atateuliwa na bunge likishirikiana na Judiciary Service Commission. Hakimu mkuu atahudumu kulingana na sheria za Judiciary Service Commission. Polisi wasiwe na uwezo wa kunyanyasa au kupekua raia, bila kibali maalum kutoka mahakamani. Kuwe na mafunzo ya kisheria mashuleni. Raia wasiteswe kwenye korokoro za polisi hadi watakapohukumiwa. Kesi zote zinazohitaji kibali cha mkuu wa sheria, zirudishwe katika ngazi za wilaya ya kupitia mwakilishi jimboni. Kuwe na mahakama maalum ya kufufua kesi zilizofutwa na mkuu wa sheria kinyume cha matakwa ya mlalamishi, mkuu wa sheria akiwa mamlakani au akiwa ameondoka.

Naenda kwa haki za kumilki ardhi. Haki zote za kumilki ardi ziwe mikononi mwa majimbo. Kila jimbo liwe na haki ya kutoa au kutoa ardhi kutoka mwaka sitini na tatu, tarehe kumi na moja mwezi wa kumi na mbili. Settlement Trust Fund ivunjiliwe mbali na iwapo serikali ina nia ya kutoa ardhi ya mtu binafsi kwa sababu ya madini au mafuta, basi mtu huyo alipwe ridhaa kiasi cha asili mia ishirini na tano ya mapato ya mafuta au madini yale, hadi yaishe na wale watakaomtegemea vivyo hivyo. Ma-squatter wawe na haki ya kumiliki ardhi baada ya mwaka mmoja, akiwa anaishi katika ardhi hiyo, ardhi ya serikali. Mabadilishano yote ya ardhi yafanywe kwenye majimbo. Mkenya yeyote awe na uhuru wa kumilki ardhi kulingana na masharti ya majimbo anamoishi. Waume na wake wawe na haki sawa katika umilkaji wa ardhi, kwa kuandikishwa wote katika hati za title deed. Hati zote za kumilki ardhi ziwe absolute. Raia watengeneza au waache wasia kabla ya kufariki. Masikizano yote yaliyokuwemo baina ya serikali na mkoloni kuhusu ardhi zote Kenya yafutuliwe mbali kwa sababu Mkenya halisi hakuhusishwa kwenye mapatano hayo. Kwa mfano, Coastal Strip na Mazrui Land. Na mtu aruhusiwe kumilki kiasi cha hekari mia tatu pekee yake.

Serikali za wilaya: ma-mayor na wenye viti wa mabaraza wachaguliwe moja kwa moja na wananchi.

**Com. Lethome:** Naona dakika zako zinakatika sana. Sasa una dakika moja.

**James Katana:** Ma-mayor na wenye-viti wachaguliwe kwa kipindi cha miaka miwili. Na Local Authority Act – chapter 265 section 86 (a) iondolewe kumpa diwani uwezo zaidi. Elimu ya chini ya ma-diwani iwe primary level. Mwananchi apewe uwezo

wa kumfuta diwani kwa kura ya kutokuwa na imani naye. Waziri asiwe na uwezo wa kuvunja baraza, uwezo upewe ma-governor wa majimbo. Nimekomea hapo.

**Com. Lethome:** Asante sana bwana Katana. Twameshukuru, maoni yako inaonekana umeyapanga yakapangika. Asante. Swali moja tu. Umesema kuwa mtu awache wasia kabla hajafariki, sasa wataka iwe ni lazima ashurutishwe na sheria, lazima kila moja aandike wasia?

**James Katana:** Ndio.

**Com. Lethome:** Okay.

**James Katana:** Kwa sababu kuleta utatanishi baadaye watu wakagombania mali ya mtu ambaye ashaafariki zamani, kwa sababu yeye mwenyewe hakupanga.

**Com. Lethome:** Haya, asante sana. Kwa hivyo ukabidhi memorandum, hiyo ni yetu.

**Com. Asiyo:** Sasa hiyo ni yetu.

**James Katana:** Utapewa, iko na huyu mzee, huyu ndiye anapresent.
***Interjections:***

**Com. Asiyo:** Wewe, hiyo hamwezi kuchukua. Hiyo ni mali yetu.

**Com. Lethome:** Sasa hiyo ni mali yetu. Tunataka kila neno ulililoliandika hapa, ni letu. Jiandikishe hapo. Sajili jina lako, hizi ni kumbu kumbu ambazo zitabaki hata baada ya miaka mia mbili ama zaidi. Asante. Tunaendelea tunamuita Bwana Dickson M. Kalama.

**Com. Lethome:** Una memorandum? Anza kwa jina, sema jina lako.

**Dickson M. Kalama:** Mimi naitwa Dickson M. Kalama kutoka Roka location. Katika memorandum hii ambayo mtangulizi amesoma, mimi ninaisoma ofisi ya Rais, uwezo na nguvu za Rais wa Jamhuri.

**Com. Lethome:** Hiyo hiyo moja?

**Dickson M. Kalama:** Hiyo moja, lakini kila mtu amechukua kipande chake.

**Com. Lethome:** Sasa uko na dakika tano, uangalie nukta muhimu muhimu. Asante.

**Dickson M. Kalama:** Ofisi ya Rais: Rais asiwe juu ya sheria. Akithibitishwa ya kuwa raisi amefanya makosa ya jinai, ashtakiwe yeye pia awe na uhuru wa kumshtaki mtu akikosolewa. Rais asiwe na mamlaka juu ya ardhi ya mita mia mbili kutoka ufuo wa Bahari ya Hindi. Asiwe na uwezo wa kuondoa kesi yoyote mahakamani. Nguvu za kusamehe, yaani kwa wafungwa, zipelekwe kwa Mercy Commission itakayoteuliwe na bunge la kitaifa, litakalowakilishwa kutoka mikoa yote ya majimbo. Rais asiwe na uwezo wa kumchagua makamu wake, bunge lichukue wadhifa huo. Rais asiwe na uwezo wa kuteua watu wanaofuata makatibu wa kudumu, mabalozi, mawaziri, wakuu wa mashirika ya umma, governor wa Benki Kuu ya Kenya, kuunda au kuvunja Tume za kushikilia mambo ya kitaifa, kuteua mkuu wa sheria, hakimu mkuu, kiongozi wa mashtaka na Kadhi mkuu. Asiwe na uwezo wa kuteua Tume ya kuajiri watumishi wa umma, asiwe na uwezo wa kumteua mhasibu mkuu, na mkaguzi mkuu. Uwezo wote wa kuteua uwe na bunge la kitaifa likishirikiana na wabunge wa majimbo. Pia asiwe na uwezo wa kumchagua commissioner wa polisi na magereza.

Sasa naenda katika haki za kimsingi: raia awe na haki ya kuishi. Uhuru wa mawazo, maoni, kutembea, kushirikiana na watu wengine, kujumuika na kutobaguliwa, haki ya kupata chakula, elimu, nguo, malazi, makaazi, mazingra safi, ulinzi, na haki ya usalama wake na mali yake, haki ya mawasiliano, uhuru wa kuabudu akiwa pekee yake au na wengine. Haki za watoto zimarishwe, haki za kina mama kulindwa. Katiba itafsiriwe kwa Kiswahili na ifunzwe madarasani. Waliostaafu kupata nyongeza za marupurupu iwapo kutakuwa na nyongeza kwa mishahara ya wafanyi kazi wa umma. Walipwe pamoja, pesa zote mara moja bila kuchelewa. Kuundwe Tume ya kuchunguza matumizi ya pesa za mashirika yasiyo ya serikali.

Sasa bwana mwenyekiti mimi naenda kwa Finance. Bunge liwe na mamlaka ya kuidhinisha matumizi na uangalizi wa pesa, kamati za bunge kama vile Pick na Pack zitiwe nguvu zaidi. Kila jimbo litapeleka kwa serikali kuu mapato yake ya kiasi asili mia ishirini, na kubaki na asili mia themanini. Bunge la Jamhuri litamuajiri mhasibu mkuu na auditor-general kwa kushirikiana na baraza la kuajiri wafanyi kazi wa umma. Watumishi wote wa umma kutangaza utajiri wao hadharani, baada ya kila miezi kumi na miwili. Pesa za Kenya zisiwe na sura ya kiongozi wa nchi, ziwe na ile court of arms na rahamani ya Kenya. Mabunge ya mikoa yasimamie bei za bidhaa zote na chakula. Wakuu wa wilaya majimbo wasiwe na uwezo juu ya pesa, uwezo upewe mhasibu wa pesa wa wilaya au jimbo. Kutaundwa ofisi ya malalamishi, ili kusikiliza malalamishi ya raia. Rais asiwe na uwezo wa pesa za consolidated fund, uwezo huo upewe bunge la kitaifa na controller mkuu, pamoja na waziri mkuu. Mali zote asili zitamilikiwa na jimbo moja kwa moja na mapato yake sehemu ya asili mia ishirini kupelekwa serikali kuu, na asili mia themanini kubaki jimboni. Sasa hapa bwana mwenyekiti nitaenda kwa jinsi ya muundo wa majimbo.

**Com. Lethome:** Una dakika moja tu.

**Dickson M. Kalama:** Hapa katika uchaguzi muundo wa majimbo kutakuwa na governor, ambaye atachukua mahali pa PC

na kutakuwa na governor mdogo katika district kuchukua mahali pa DC, na kutakuwa na governor mdogo wa taarafa kuchukua mahali pa DO, na kutakuwa na council of elders katika location kuchukua mahali pa chifu, na village elders council kuchukua mahali pa assistant chief. Ma-chifu wote bwana chairman tumewafuta. Provincial Administation yote tumeshafuta. Nimeshukuru bwana chairman na mwenzangu atakuja aendelee na ingine.

**Com. Lethome:** Swali moja tu. Hawa ma-governors sasa hawa watateuliwa au watachaguliwa, na kama watateuliwa, watateuliwa na nani au watachaguliwa na nani?

**Dickson M. Kalama:** Governor atachaguliwa na Regional Assembly na kikao cha district assembly kitamchaguwa yule tumemuita assistant governor wa wilaya. Na kikao cha division kitamchagua yule tumemuita divisional governor akiongoza ili tuliyoita divisional council of elders. Na kwendelea mpaka sub-chief.

**Com. Asiyo:** Vile ningependa kujua mzee ni kwamba nani atakayeongoza council of elders kwa location na village elders?

**Dickson M. Kalama:** Ni chairman ambaye atachukua mahali pa chief.

**Com. Asiyo:** Na huyu chairman atafika aje pale?

**Dickson M. Kalama:** Atachaguliwa na raia. Ile council of elders itachagua watu ambao kutokana na watu wale watachagua.

**Com. Asiyo:** Na hawa ma-assistant governors watachaguliwa ama watakuwa appointed?

**Dickson M. Kalama:** Ni kuchaguliwa, watachaguliwa na district assembly. Katika hawa ma-governors munaosema kutoka mlolongo wa regional mpaka village. Vile vikao vile ambavyo sasa sisi katika council of elders katika village, wakikaa wale elders watachagua governor.

**Com. Asiyo:** Shida yangu ni nani atamchagua. Nani atakayechagua hawa elders?

**Dickson M. Kalama:** Ni wale elders ambao watakuwa wamechaguliwa kwa kura.

**Com. Asiyo:** Si wananchi wangewachagua?

**Dickson M. Kalama:** Ndio watachaguliwa na wananchi, lakini kile kikao kile cha kama watakuwa ni kumi kutoka moja ambaye atachaguliwa otherwise it can be vice versa.

**Com. Asiyo:** Shida yangu ilikuwa ni yule ambaye atakayechagua wale ma-elders.

**Dickson M. Kalama:** Watachaguliwa na wananchi.

**Com. Asiyo:** Haya.

**Com. Lethome:** Haya basi utatukabidhi, hiyo ni mali yetu sasa bwana Kalama. Kama ulikuwa haujatengeneza copy basi ndiyo hiyo imekwenda. Hiyo mali yetu. Haya tunaendelea vizuri sana tunamuita Ustadh Habshi Saidi.

**Ustadh Habshi Saidi:** Mimi sina la kuzungumza zaidi lakini nitaleta hii memorandum yangu.

**Com. Lethome:** Bila kuzungumzia?

**Ustadh Habshi Saidi:** Eeeh….

**Com. Asiyo:** Sema kidogo tujue ni kitu gani umeongea.

**Com. Lethome:** Ruhusu aslam.

**Ustadh Habshi Saidi:** Hapo mwanzo. Mimi naitwa Habshi Saidi. Utawala ambao kwamba tunautaka uwe ni utawala wa majimbo. Na lingine ambalo kwamba ni muhimu kuhusu mambo ya Kadhi. Kadhi tunaona, Kadhi ana cheo ambacho kwamba aweza akazungumza kesi, baada ya kesi kama ile kuizungumzia mfano ametoa uamuzi, lakini utakuta baada ya siku fulani utakuta Kadhi kama yule yuandelea na kesi hupokonywa karatasi zake za kesi akaambiwa kuwa Kadhi kesi hii imepelekwa High Court.

**Com. Lethome:** Ungependekeza jambo gani?

**Ustadh Habshi Saidi:** Mimi ningependekeza ya kuwa, Kadhi iwe apate nafasi ya kuwa na cheo ambacho kwamba kiko juu, iwe kesi yake yeye aweza akaimaliza yeye mwenyewe, ama kuwe kuna wa Kadhi wadogo ambao kwamba watahukumu kesi kama zile, yule Kadhi mkuu iwe ndiye mwenye kumaliza High Court.

**Com. Lethome:** Yaani unasema kuwe na Kadhi's court of appeal.

**Ustadh Habshi Saidi:** Eeh ndio. Kwa hivyo hilo ndilo la muhimu ambalo ningezungumzia. Hayo mengine yako hapa.

**Com. Lethome:** Maswali haya. Sasa hivi sasa tunajua ma-Kadhi tunajua wanateuliwa, wanapochaguliwa. Sasa ungependa waendelee hivyo hivyo, ama pengine una pendekezo fulani kuhusu kuchaguliwa ma-kadhi, wachaguliwe na nani au waajiriwe na nani?

**Ustadh Habshi Saidi:** Ma-kadhi kuajiriwa kwao, waajiriwe na wanachuoni ambao kwamba wameaminika kielimu, wawachague awe Kadhi kama yule ni mjuzi kwa elimu yake ya kuweza aweza kutoa hukumu za kisawa sawa katika sheria ya kiislamu.

**Com. Lethome:** Na ungependa kiwango cha elimu cha ma-kadhi kiwe kipi?

**Ustadh Habshi Saidi:** Kiwango cha elimu ni kuwa Kadhi asomee sheria ya kiislamu.

**Com. Lethome:** Pekee yake ama na sheria hizi zingine?

**Ustadh Habshi Saidi:** Na sheria zingine pia.

**Com. Lethome:** Haya, tuje kwa Chief Kadhi.

**Ustadh Habshi Saidi:** Naam.

**Com. Lethome:** Chief Kadhi ungependa achaguliwe na nani?

**Ustadh Habshi Saidi:** Chief Kadhi ningependelea pia achaguliwe na watu ambao kwamba ni wajuzi wa masheria za kidini.

**Com. Lethome:** Na umri wake?

**Ustadh Habshi Saidi:** Na umri usipungue miaka arobaini. Yaani, iwe ni mtu ambaye kwamba ni mtu mzima.

**Com. Lethome:** Na miaka ya juu zaidi, ama wataka hata akiwa na miaka mia moja aendelee?

**Ustadh Habshi Saidi:** Aah, asifikie umri wa miaka ambayo kwamba itakuwa ni ule utu uzima wa sana hata zile fahamu zake huwa ziwe zinafanya kazi.

**Com. Lethome:** Pendekeza miaka.

**Ustadh Habshi Saidi:** Miaka kama sabini iwe ndio mwisho.

**Com. Lethome:** Na sasa tunajua ma-kadhi walioko, hata Chief Kadhi anafanya kazi za sheria kortini kama majaji wengine na pia anachukuliwa kuwa ni kiongozi au mzungumzaji kwa niaba ya waislamu, kwenye ada ya kiislamu pia. Kwa hivyo ni kiongozi wa dini na pia ni Chief Kadhi. Ungependa aendelee hivyo ama ungetaka vipi, kuwe na nidhamu gani?

**Ustadh Habshi Saidi:** Mimi ningependa Chief Kadhi aendelee hivyo, lakini yaani isiwe Chief Kadhi awe ataamrishwa na serikali afanye jambo fulani. Iwe Chief Kadhi atoe maoni na sheria kutokamana na sheria ya kiislamu.

**Com. Lethome:** Awe huru?

**Ustadh Habshi Saidi:** Awe huru.

**Com. Lethome:** Tunashukuru sana, ukabidhi mali yetu tafadhali. Haya asante. Sasa tunamtaka Ustaf Mohamed. Ustaf Mohamed, karibu.

**Mohamed Salim:** Mimi naitwa Mohamed Salim.

**Com. Lethome:** Haya endelea Ustaf. Jambo la kwanza ambalo ningelizungumzia.

**Com. Asiyo:** Unaweza kusema kwa sauti.

**Com. Lethome:** Yule bibi analalamika mnazungumza kwa haraka sana. Halafu tumieni Kiswahili cha kibara bwana, msitumie cha huku.

***Interjections:*** *Hata kidogo?*

**Interjection:** Kama mumeleta wrong person badilisheni mlete m-Pwani hapa.

**Com. Lethome:** Haya asante.

**Interjection:** Mlituambia tutakuwa na dhuluma ya kila aina.

**Com. Lethome:** Haya asante. Endelea.

**Mohamed Salim:** Swala ambalo ningelizungumzia narudi pale pale pa mahakama ya Kadhi. Mahakama ya kadhi ningependelea igawanywe mara mbili. Kuwe na mahakama ya Kadhi ndogo, na mahakama kuu ambayo itakuwa ni Kadhi's High Court. Na Kadhi huyu awe atahukumu kwa sheria ya kidini. Na ile ofisi yake iwe itakuwa na Kadhi kama jinsi ya vile Jaji Mkuu atakavyokuwa na kile cheo. Yaani cheo chake kiwe ni kama kile cha Jaji Mkuu wa Kenya, au popote pale.

Na jambo lingine ni kuhusu uhuru wa dini. Kuna tofauti ya uhuru wa kuabudu na uhuru na wa dini. Uhuru wa dini, ni watu kuwa huru kufanya ibada zao pasina kusumbuliwa na yeyote, na kutangaza dini yao wanavyopenda, huo ndio uhuru wa dini. Na kusiwe na ubaguzi, kwa mfano mzuri katika makazi, katika ma-passport, katika vitambulisho, kusiwe na ubaguzi.

Na la mwisho, katika hali ya kutilia mkazo lile swala la ….. alivyozungumza ni yule ambaye kwamba atachaguliwa kuwa Chief Kadhi, iwapo atachaguliwa na serikali, basi iwe atachaguliwa mtu ambaye kwamba amekuwa ana ujuzi. Yaani mtu ambaye kwamba ana maarifa ya kuendeleza zile kesi za kiislamu vizuri.

Na la mwisho kabisa ambalo kwamba singeweza kulifafanua, mwenzangu atakuja kulifafanua ni kuhusu uminikajia wa ardhi.

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini?

**Mohamed Salim:** Mwenzangu atakuja eleza zaidi.

**Com. Lethome:** Ngoja, ngoja.

**Com. Asiyo:** Umeongea kwamba kuna ubaguzi wakati wa kuchukua pasipoti na hata identity cards, kwa watu gani hawa, kwa wakina mama, kwa vijana?

**Mohamed Salim:** Umeuliza swala nzuri. Majina yako tofauti, kuna Mohamed, kuna Saidi, kuna John, kuna Karisa, iwapo wewe kwa bahati mbaya waitwa Mohamed, basi huwa ni taabu kupata passport au kupata kitambulisho kwa hii Kenya yetu, kwa mda huu tulionao.

**Com. Lethome:** Swali langu ni kuhusu uhuru wa dini. Wasema Katiba mpya ihakikishie kila mtu uhuru wa dini yake. Sasa mimi nimeamua dini yangu ni kumuabudu shetani, tutumie kipengele hicho kuhifadhi haki yangu hiyo? Dini yangu ni kumuabudu shetani, ushasikia devil worshipper? Unataka nitumie kipengele hicho cha Katiba niseme mimi imenihifadhi imenipa uhuru wa dini? Dini yangu ni kuabudu shetani.

**Mohamed Salim:** Ile yategemea na imani ya mtu, kwa sababu haki iko wazi.

**Com. Lethome:** Hebu tumpe uhuru wake pia.

**Mohamed Salim:** La, ile haki iko wazi, na dini ya haki yajulikana kwamba ni dini gani.

**Com. Lethome:** Aah, ngoja ngoja. Sasa twazungumzia uhuru wa kuabudu au uhuru wa dini, ni dini ya kumuabudu nani?

**Mohamed Salim:** Kumuabudu Mungu.

**Com. Lethome:** Na hivyo ndivyo tunavyotaka. Asante. Haya tukabidhi kama una memorandum tukabidhi, kama huna utajiandikisha. Mr. Saidi.

**Saidi Omar Komora:** Mimi naitwa Saidi Omar Komora.

**Com. Lethome:** Nataka jina lako linaswe, tukienda Nairobi tusikie jina lako pia hapo.

**Saidi Omar Komora:** Na mimi nasema hivi, naitwa Saidi Omar Komora.

**Com. Asiyo:** Saidi Omar.

**Saidi Omar Komora:** Mimi sina mazungumzo. Langu ni moja tu, mengi yako katika memorandum ambayo tumeichapisha. Sasa hapa ni neno ambalo kwamba haliko pale. Mapendekezo yangu ni kwamba, kwa kila maeneo ya waislamu ambao kwamba wanaopata elfu hamsini, iwe la Kadhi na naibu wake, ili, iwe sahali zaidi kule kuwahudumia. Nafikiri hilo ndilo langu.

**Com. Asiyo:** Je, ungependa serikali ya aina gani?

**Saidi Omar Komora:** Katika pendekezo langu kwa serikali, kwanza iwe ni serikali ya democracy iwemo kwamba tunaitaka zaidi. Pili, majimbo pia tunayataka. Kwa hivyo hayo ndio yangu.

**Com. Lethome:** Katika ngazi gani hayo majimbo yenyewe wataka katika daraja gani?

**Saidi Omar Kamora:** Majimbo, kama vipi?

**Com. Lethome:** Katika wilaya; wilaya iwe jimbo au pengine mkoa, au pengine taarafa au location.

**Saidi Omar Komora:** Okay, sasa majimbo ambayo tunayataka ya mkoa. Kwanzia mkoa mpaka kuteremka chini yote.

**Com. Lethome:** Na huyu kiongozi wa jimbo tumuite aje?

**Saidi Omar Kamora:** Governor.

**Com. Lethome:** Haya kajiandikishe pale. Haya, tumpate Joseph M. Kingi, Josephat M. Kingi?

***Interjections:*** *Kwa hivyo baadaye.*

**Com. Lethome:** Tukiendelea, tumpata hapa Daniel S. Mwangome. Daniel Mwangome yuko? Karibu. Kwa vile una memorandum dakika tano.

**Daniel Mwangome:** Dakika tano. Kwa ruhusa yako mwenyekiti nitasoma haraka na nimeyaandika kimombo.

**Com. Lethome:** Asante, endelea.

**Daniel Mwangome:** Jina langu ni Daniel S. Mwangome. This presentation is made in a very short form based on few major points of our Constitution of Kenya. It shall be observed and respected by all future Governments and generation.

The Constitution: this noble document has reached the stage that it must be reviewed and re-written after serving for almost four decades – 40 years.

**Com. Lethome:** Mr. Daniel wacha nikusaidie sasa.

**Daniel Mwangome:** Nataka kutafsiriwa muelewe ninasema nini.

**Com. Lethome:** Haya sawa.

**Daniel Mwangome:** Iliaibiwa hayo.
***Interjections:***

**Com. Lethome:** Utapata, kila moja atapata. Lakini hii ni yetu sisi. Bwana Daniel utatusaidia hapa, huo unajua ni utangulizi unaosoma sasa. Hebu ingia katika mapendekezo.
**Com. Asiyo:** Mapendekezo.

**Daniel Mwangome:** Type of government: due to mis-trust amongst the communities and fair distribution of the national cake, the majority of Kenyans and in particular the small and unprivileged communities that have been marginalized since Kenya became independent, feel the best Constitution to serve their interests should be the same as that of India, Nigeria, Germany and America. These countries and others have Regional Governments and appear to be the best solution for Kenyans now. The establishment of Regional Government, majimbo, will enable each region to plan its development projects, priorities without Central Government in Nairobi, that is health, education, agriculture, communication, infrastructure, socio-economic and political activities.

Revenue: each region will collect its revenue and decide how to spend it. All regions to employ its civil servants and parastatal employees and run all Ministries activities. Regions shall remit 25% of its revenue to the Central Government, the Central Government shall only be responsible for matters of national importance, that is national budget – finance, defence, security and national foreign policies.

Regional Government – majimbo: the Regional Government shall have an elected assembly representing all districts. The assembly will formulate government policies that will create enabling environment to govern its citizens and lift their living standards or so to create conditions that will allow its easy flow of investors within its jurisdiction. Each region shall be governed by Governor and shall be elected by regional assembly and be a neutral person with no alignment of any political party. The governance shall have powers to employ and sack the senior government employees on recomumendation of the regional assembly.

Employment: all employees in all regions will come from the indigenous people and only 25 % be reserved from all regions or expatriates, but must receive approval of the regional authorities. The regional government will ensure that properties from communities of other regions shall be protected, provided they were obtained in the right manner.

Regional or Central Government: senior employees shall be required to declare their wealth before taking up their posts. Such employees should not stay long in their positions as means of avoiding fraud, corruption and misuse of power or office. There shall be no favouritism when making such transfers or as means of punishment.

Governance: the parliament be established to have a House of Representatives, its members will come from each region and be contested by political parties. Regional Government will have lower house or regional assembly. It's members will come from districts and depending on the number of voters. Members of regional assembly shall only come from the indigenous people of that particular region. No refugees, foreigners or communities from other regions will be allowed to contest as seat without the consent of the assembly. The regional government shall execute all matters related to land and no interference from the central government. Land obtained through favouritism, corruption or misuse of power shall be repossessed from such people and given to landless people, squatters. Hence, all regional files shall be transferred to concerned regions where proper security

shall be done before action is taken.

Government machinery, President: the new Constitution should not allow an executive president in Kenya. We need only a ceremonial president that will perform ceremonial duties. The holder of this post will be elected or nominated by the parliament or House of Representatives to serve for a five-year term. He/She will constantly be in touch with the Prime Minister to ensure smooth running of the government, but must be a Kenyan citizen of both mother and father with good background. No vacancy of vice-president.

Premiership: the Central Government shall be headed by a Prime Minister. The holder of this post will come from the parties that has majority elected members. He/She will submit list of names to the House of Representatives for approval before taking up their posts.

Cabinet: the cabinet shall be composed of the Prime Ministers, Ministers and Attorney General - government legal advisor as as ex-officio without voting powers' rights. They will have collective responsibility in the running of the government and can be dismissed at the discretion of the Prime Minister after consultation with the government or President.

Public offices: the Prime Minister shall have powers to appoint or dismiss any person in public office, except for offices created and governed by the Constitution. However, there are public offices to which once appointed the Constitution provides security of tenure; the Attorney-General, Controller and Auditor-General, Electoral Commission and Judiciary.

Prerogative of mercy: the matter be left to the President to take appropriate action after receiving a report from the Presidential commmittee and his advisors on the judgement of the death penalty by the court.

Impeachment: once the President, Prime Minister, Deputy Minister and top senior government officials are found to be involved in crime matters, they should be impeached to allow them face legal action. One can be reinstated if not found guilty by the law.
Commission: each region to have powers to establish their own Commissions, such as Human Rights Commission, Anti-Corruption Commission, Land Commission. The above Commissions to be put in the Constitution. Thank you.

**Com. Lethome:** Thank you very much Mr. Mwangome. John Kombe. Ikiwa una memorandum hapa naona memorandum.

**John Kombe:** Kwa jina John Kombe Kiti. Marekebisho ya Katiba ya Kenya, maoni ya wananchi wakaaji wa Ngerenya location. Kwanza wananchi wa Ngerenya wanapenda serikali ya majimbo. Pili, uwezo na mamlaka ya rais yapunguzwe. Tatu, wabunge na ma-councillor kuwe na uwezekano wa kusimamishwa na kuchagua mwingine kabla ya miaka mitano kama hashirikiani na wananchi waliomchagua. Nne, mkuu wa mkoa kama PC awe anatoka mkoa huo huo atakaouhudumia. Tano,

ma-DC na ma-DO pia wawe wanatoka kwa wilaya zile watakazozihudumia. Sita, ma-chifu na ma-naibu wao pia wawe wanatoka zile sehemu watakazozihudumia. Pia wanachaguliwe na wananchi wenyewe badala ya kuchaguliwa na DC wa wilaya. Saba, wanawake watakaofiliwa na mabwana zao, kusiwe na lazima ya kurithiwa na ndugu za mabwana zao, bali wawe chini ya hawo ndugu za mabwana zao, ili wasije wakafuja mali zilizoachwa. Nane, mila na desturi za ndoa zifuatwe na ziheshimiwe. Kisha mtoto wa kike asipate urithi wa babake moja kwa moja, bali abaki mikononi mwa mamake. Kumi, hali ya u-squatter imalizwe kwani kila mwananchi anatakiwa apate kibali cha kumiliki ardhi. Kumi na moja, tembo linalotoka kwa minazi lidumishwe na kufanyiwa utafiti na lihalalishwe. Kumi na mbili, minazi, mikanju, miembe, michungwa na rasilmali zake zitambuliwe kwa hali ya juu. Kumi na tatu, elimu ya shule za msingi itolewe bure. Kumi na nne, elimu ya kidato cha tano na sita iregeshwe na lile somo la siasa na mazingira pia yaregeshwe. Kumi na tano, malipo ya matibabu kwa hospitali zipunguzwe au yapunguzwe. Kumi na sita, mfadhili akitaka kuingia kwa sehemu zetu, akutane na wananchi wenyewe ndipo baada ya mazungumzo washirikiane kupanga miradi. Kumi na saba, ufadhili wa miradi ufaidishe au unufaishe wananchi moja kwa moja bila ya nusu ya malipo. Kumi na nane, si ruhusa mtu awai yoyote kuingia shamba la mwenyewe bila ya idhini. Kumi na tisa, serikali tunayoitaka iwe na Rais na waziri mkuu. Ishirini, kila mkoa uwe na majeshi yake ya kulinda usalama. Ishirini na moja, mikoa iwe ina mtu aitwaye Governor. Majeshi yote ya nchi yawe mikononi mwa waziri mkuu badala ya kuwa mikononi mwa Rais. Ishirini na tatu, kila kikundi kilichojiandikisha kiwe na uwezo wa kuchanga pesa bila ya permit. Ishirini na nne, ma-pastor wawe na uwezo wa kufungisha ndoa. Ishirini na tano, wenye vitu wa jua kali wawe wana uwezo wa kusimamia viwanja vyao kikamilifu, bora tu kuwe kuna kamati madhubuti kwenye shedi zao bila ya society kuingilia shedi. Ishirini na sita, mvulana atakayeharibu msichana wa mwenyewe kimasomo na tabia za kuishi, huyu mvulana atoshwe faini ya shilingi elfu kumi, na afungwe jela mwezi mmoja na kiboko kimoja. Ishirini na saba, mtu yeyote atakayefanya mapenzi na mke wa mwenyewe akijulikana, atozwe faini ya shilingi elfu kumi, kisha afungwe miezi miwili na achapwe viboko viwili na huyo mke pia achapwe kiboko kimoja. Ishirini na nane, mtoto asiye- kamilisha umri wa miaka kumi na minane, asiruhusiwe kuingia vilabu vya tembo, au kwenye vyumba vya cinema, au vya aina yoyote ya starehe. Ishirini na tisa, hali ya ufisadi ikomeshwe kwa kila atakayehusika apatiwe adhabu ya kutosha na mahakama. Thelathini, wasichana wanaobahatika kupata mimba hali wakiwa shuleni, baada ya kuzaa, waruhusiwe kuendelea na masomo. Thelathini na moja, waizi wa hali yeyote ya wizi wasikubaliwe kutoka nje ya rumande kwa bond, bali kesi yake mpaka imalizike. Thelathini na mbili, wazee wa kijiji watambuliwe kwa kupatiwa malipo fulani, ama malipo kidogo. Thelathini na tatu, mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya makosa aliyoyafanya na mahakama iamue kumnyonga, basi mtu huyu anyongwe kwa mkoa wake, mbele ya watu wake na wa upande wa walalamishi, ili kusiwe siri ya kinyongo chake. Hiyo nimemaliza.

**Com. Lethome:** Haya asante sana.

**Com. Asiyo:** Hapo mzee umeongea juu ya wasichana kurithi mali za baba zao.

**John Kombe:** Ndio.

**Com. Asiyo:** Unaweza kufafanua zaidi? Hapa wanategemea mali ya mzee, basi atapata mali wapi ya kugawia mtoto wake msichana?

**John Kombe:** Kwa kawaida wasichana huwa wanaolewa na akiolewa huwa ametoka kwa babake na huwa anaenda kuenda kujenga maisha mapya yeye na bwana yake kule, na kama ni shamba atapatiwa shamba na bwana yake. Kwa hivyo haina maana ya mtoto wa kike kurithi na hali yeye ataolewa. Sasa ni kama kuchukua hii mali ya babake kwenda kumfaidisha bwana yake. Kwa hivyo hiyo si vizuri.

**Com. Lethome:** Asante bwana Kombe kwa maoni yako. Tukabidhi memorandum. Francis Charo Ngala.

**Francis Charo Ngala:** Ninaitwa Rev. Francis Charo Ngala, nina maoni. Mapendekezo yangu nataka serikali ya majimbo yaanzie kwenye mkoa. Mambo ya jua kali: hii jua kali wenye viti wa sheds wawe wanatambulika zaidi na kumiliki vile viwanja za sheds. Pasipo wale watu wa association, kwa sababu kuna watu wale wa association huwa nao wanataka waingilie katika sheds. NGOs wale wafadhili wakitoka huko waje moja kwa moja kwa wananchi, kwa sababu wananchi ndio ambao wanajua matatizo ya miradi yao waliofungua.

Ma-pastors: ma-pastors wawe na uwezo wa kupewa vyeti vya kufunga ndoa, kwa sababu ma-kasisi huwa ndio wenye uwezo, lakini sasa hao huwa hata ukiwaita wana shida sana kufika kuenda kufungisha ndoa. Hayo ndio yangu ambayo ni-nayo.

**Com. Lethome:** Haya, asante sana Bwana Francis. Ukajiandikishe pale kwenye kitabu yetu. …. (inaudible). Tutamsikiza Mohamed Amin.

**Mohamed Amin Mohamed:** Jina langu ni Mohamed Amin Mohamed. Kumbu kumbu yetu ya maoni na mapendekezo ya baadhi ya waislamu wa hapa Kilifi.

Namba moja, Katiba ya nchi iwe juu ya Katiba ya chama chochote kitakachotawala, kitawale. Chama chochote kikitawala kifuate Katiba ya nchi sio Katiba ya chama.

Rais wa nchi akiwa mkristo, au wa dini yoyote, au asiye na dini, makamu awe muislamu, au Rais akiwa muislamu basi makamu awe si muislamu.

Tatu, uislamu na waislamu wathaminiwe, waheshimiwe, sawa kwa kupewa mamlaka sawa na kazi za juu, kama makatibu wa wizara mbali mbali, ma-balozi, waziri, sio kuweka muislamu mmoja na wengine wote sio waislamu, huko ni kudanganyana. Ardhi za waislamu zisipewe wasiokuwa waislamu. Waislamu wasiingiliwe au kulazimishwa kubadili Katiba ya Allah ambayo ni Quran na hadithi. Muongozo na muongoza wa "Mutume Mohamed Salam Allha Wasaalam". Kuwe na serikali ya majimbo ili

majimbo yaliyo na waislamu wengi kwa mfano kama Coast na North-Eastern, waweze kutumia sheria ya Allah, yaani hukumu ya Quran takatifu. Waislamu wawe huru kuwa na taratibu zao za elimu, za dini, na elimu hiyo ipewe kipimo sawa na elimu nyinginezo, ili walio na elimu ya uislamu waajiriwe kazi zinazohusiana na uislamu, kama ukavi, ualimu, wakfu wa commission na kadhalika. Mkenya yeyote raia au hata rais, wote wawe chini ya sheria, wakikosa wahukumiwe. Kifungu chochote cha Katiba kihitajiapo marekebisho au kuongezwa chochote lazima kikubaliwe na raia, sio rais wala bunge wala Tume. Dini na mila zote ziheshimiwe na kubaki kuendelea vile zilivyo. Elimu yoyote ya dini ya kiislamu itambuliwe na ipewe uzito sawa na elimu za shule au university. Mkenya yeyote akifika umri wa kupigania au kugombea wadhifa wowote aruhusiwe. Ikiwa ni wadhifa rais, makamu, mbunge, mayor, madiwani. Tena bila masharti ya ki-elimu au kifedha wala chama. Hawezi kugombea hata kama hakupata chama, wala kufanyiwa mtihani wowote. Rais au makamu au wa-bunge au ma-mayor na ma-diwani wachaguliwe moja kwa moja na raia, sio bunge, wala council wala rais. Yeyote atakaye- haribu au kutumia vibaya ofisi yake, tangu diwani hadi rais, asimamishwe, ashtakiwe, achaguliwe mwingine, sio kungonjea kipindi kumalizika, wala asichaguliwe tena maisha.

Human Rights yaani haki za kibinadamu, zisiwahusishe waislamu, kwa sababu waislamu wamepewa au wamepangiwa waume na wake haki zao zote na Allah kuhusu mufumo wote wa maisha yao. Mabaraza yaendeshe shughuli zao kupitia majimbo, yaani mapato ya kila baraza yawe ni ya jimbo hilo, wala isiingiliwe na serikali kuu. Utawala wa nyimbo uwekwe mikononi mwa wenyewe. Kwa mfano, jimbo la kaskazini mashariki, wakuu wa idara zote za serikali kutoka PC mpaka askari, wawe wote ni wa huo mkoa. Na mikoa mingine ifuate kama hiyo. Idara zote za serikali zihudumie wananchi bila malipo yoyote, wala vitisho na kutohudumiwa kwa kubaguliwa. Mambo ya hongo yaondoke. Mali ya asili yawe huru kwa wenyeji wa sehemu wanayoishi, waweze kuzalisha uchumi, kwa mfano, bahari, maziwa, mito, samaki, ardhi, misitu, mikoko, madini na mengineo. Kusiwe na kuingiliwa na serikali kuu. Binadamu awe na utukufu wake kuliko mnyama au mgeni.

Kitambulisho kisihitaji baada ya kabila, ukoo wala mlango. Badala yake kuandikwa majina kamili ya muobanji, mkoa, wilaya, tarafa, mji na kijiji au mtaa. Wala jina la kiislamu lisiwe kikwazo cha kutokupatiwa kitambulisho, passport, birth certificate, death certificate, burial permit, na kadhalika. Town centres kuwe na eneo litengwe kwa harakati za waislamu, iwe msikiti, makaburi, madrasa na kadhalika. Ufisadi ukomeshwe. Ardhi zote zilizopeanwa za watu kwa kimakosa zibadilishwe na kupewe wenyewe halisi. Hata iwapo ardhi hiyo imeshaa tumiwa, na kusiwe na ridhaa. Bado kidogo bwana nimalize. Hukumu zote waislamu kwa waislamu ziendeshwe na ofisi ya Kadhi na uteuzi wa ma-Kadhi ukifanyika walio na elimu ya dini kwa upande wa madrasa waajiriwe. Na katika kamati ya kuteua ma-Kadhi, Kadhi Mkuu ahudhurie na mawakilishi wa baraza kuu na ma-imamu wawepo. Uteuzi wa wabunge na madiwani maalum uendeleee. Nafasi hizi zipewe kabila zilizo na idadi ndogo ya watu, igawanyike sawa nusu waislamu na nusu wasiokuwa waislamu. Sehemu zilizo na idadi chache ya watu na zilizo nyuma ki-maendeleo zipewa viti vya uwakilishaji bungeni, sio tu kuangalia wingi wa watu. Wafanyi biashara ndogo ndogo wawe huru kufanya biashara zao, bila malipo ya leseni. Badala yake wapewe mikopo na mafunzo ili waweze kuendelea, ili baadaye wawe kulipishwa leseni. Haya ndio mapendekezo yetu bwana, kiasi hicho tulichofika. Yuko mwenzangu ambaye vile vile naye atakuwa kidogo na ufafanuzi au kuongezea katika haya.

**Com. Lethome:** Umesema kuhusu haki za binadamu umesema waislamu wawe exempted - wasihusishwe katika haki za kibinadamu. Hebu fafanua.

**Mohamed Amin Mohamed:** Ilivyo kwa mfano bwana, sisi hivi sasa ilivyo kwamba Quran yetu takatifu imempa muongozo muislamu kamili. Na kwa ukweli ni mwanadamu yeyote, lakini right now kwa imani ya kwamba ziko tofauti, sasa twasema sisi ambao ni waislamu hatuna tatizo lolote sisi, ya kwamba tutahitaji tufikiriwe human rights, ushasikia. Isipokuwa human rights imo ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu tayari. Yaani haki zimegawanywa kulingamana na mtu alivyo na itakanavyo awe. Kama ambavyo Quran ni mfumo alioupanga Mwenyezi Mungu kwa maongozi ya mwanadamu kuanzia kuzaliwa mpaka kufa kwake.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo una maana hapo kuwa haki za binadamu zinapo tekelezwa zizingatie pia maadili ya kidini au mafundisho ya kidini.

**Mohamed Amin Mohamed:** Sawa.

**Com. Lethome:** Kwa mfano unapozungumzia juu ya mwanamke apewe haki za urithi, zizingatiwe pia mwongozo wa dini?

**Mohamed Amin Mohamed:** Muongozo wa dini ndio, sawa.

**Com. Lethome:** Asante.
**Mohamed Amin Mohamed:** Nashukuru bwana.

**Com. Asiyo:** Nina swali moja kwako mzee. Hapo mbele umesema pengine sikusikia vizuri, umesema kwamba ulinzi wa watu wa mkoa, kuliko na wenzangu wengi kama hapa chini Pwani au North-Eastern, vitunzwe na sheria ya Sharia.

**Mohamed Amin Mohamed:** Eeh ya kiislamu.

**Com. Asiyo:** Ya kiislamu, na hiyo ni kusema kwamba kama kuna serikali kuu ya Kenya hiyo serikali haitakuwa na uhusiano wote kabisa na hii serikali ingine ya sharia ya Coast na ya North-Eastern.

**Mohamed Amin Mohamed:** Sasa hiyo twazungumzia ikiwa serikali kama mapendekezo yatafaulu kuwa ni ya kimajimbo, sasa jimbo litakalo-kuwa kwa mfano lina waisilamu wengi.

**Com. Asiyo:** Na sasa wale wakristo na wengine watakuwe namna gani?

**Mohamed Amin Mohamed:** Kwa kawaida watakuwa wahukime kwa haki zao vile vile. Hakuna upinzani hapo.

**Com. Asiyo:** Lakini umeona shida Nigeria imepata kwa kujaribu kufanya mambo kama hayo.

**Mohamed Amin Mohamed:** Situmaini kuna shida yoyote isipokuwa ni matatizo madogo yatatokea.

**Com. Asiyo:** Lakini kumetokea matatizo mengi sana Nigeria.

**Mohamed Amin Mohamed:** Yako matatizo, sasa ile ni kati ya sisi wenyewe kutokuwa na mipango sawa sawa au upande mwingine ni kulingana na ile hali au pressure, uzito wa yale mazingara. Lakini matatizo yaliyoko Nigeria, ikiwa kweli wafuata maongozi ya Quran, yatakuwa hakuna matatizo yataondoka. That is an assurance.

**Com. Lethome:** Asante Mohamed kwa maoni yako.

**Mohamed Amin Mohamed:** Asante.

**Com. Lethome:** Masoud Shaban Mohamed.

**Masoud Shaban Mohamed:** Asante mwenyekiti pamoja na wenzako. Kwa jina naitwa Masoud Shaban Mohamed. Natoka tarafa ya Kilifi, kijiji cha Tezo. Naomba haki na usawa kati ya kila mwananchi itekelezwe. Usawa katika mahakama: kwa walio waislamu wawe na mahakama maalum inayo hukumu sawa na dini yao. Hakimu wa waislamu achaguliwe na wajuzi wa dini ya kiislamu, wanazuoni. Hakimu wa kiislamu apewe uwezo kamili kama mahakimu wengine. Muislamu apewe uhuru wa kufuata maagizo ya dini yake, bila ya kuingiliwa. Muongozo wa dini uheshimiwe sawa na umuhimu wake popote alipo muhusika. Kiongozi anapodhubutu kupatikana na makosa, ahuzuliwe, aondolowe katika madaraka na ahukumiwe sawa na makosa yake. Kiongozi ajulikane vyema usawa wake tangu kuinukia kwake, kabla ya kupewa madaraka. Kiongozi awe na elimu na ujuzi wa kutosha na hekima ya uongozi. Mpaka hapo asanteni. Nashukuru.

**Com. Lethome:** Haya asante. Moses Kahindi Mzerella, karibu.

**Moses Kahindi Mzerella:** Asanteni, mimi sikupanga memorandum nitazungumza vile ninavyotaka.

**Com. Lethome:** Asante.

**Moses Kahindi Mzerella:** Kwa jina mimi ni Moses Kahindi Mzerella, nimezaliwa hapa hapa Kilifi.

**Com. Lethome:** Kidogo mzee tafadhali.

**Moses Kahindi Mzerella:** Kwa jina naitwa Moses Kahindi Mzerella, mzaliwa wa hapa hapa Kilifi. Nataja juu ya serikali tu pekee yake. Mambo mengine ya dini au nini hapana. Serikali niitakayo mimi ni ya majimbo na majimbo yenyewe yawe ya kujitawala. Kuwe na governor wa jimbo. Governor wa jimbo achaguliwe na raia na wale wabunge wake, regional assembly. Bunge ziwe mbili. Rais aweko, na atachaguliwa vile vile kulingana na wale wabunge wa regional assembly. Na kuwe na waziri mkuu, atakayechagua mawaziri. Rais awe hana ruhsa ya kuchagua mawaziri, au majaji au watu wengine wowote. Na katika zile sehemu zile za wale watakaochaguliwa, wale watu wa senate watachaguliwa vile vile kutoka katika district. Ni hivyo tu ndugu yangu.

**Com. Lethome:** Bwana Mzerella, waziri mkuu wasema yeye ndiye ana uwezo wa kuchagua baraza la mawaziri au mawaziri, na yeye achaguliwe vipi na achaguliwe na nani?

**Moses Kahindi Mzerella:** Waziri mkuu atachaguliwa kutokana na raia.

**Com. Lethome:** Umesema kuwe na cheo cha Rais na je cheo cha makamu wa rais?

**Moses Kahindi Mzerella:** Hakuna lazima ya cheo cha makamu wa rais, kama kuna waziri mkuu.

**Com. Lethome:** Haya asante Bwana Mzerella, nenda ukajiandikishe pale. Naona tunaendelea vizuri, maoni tunayapata mazuri kabisa. Tumpate Bwana Albert J. Rua.

**Albert Jeremiah Rua:** Mimi ni Albert Jeremiah Rua kutoka Roka location nawakilisha Kenya Herbalists & Traditional Dancers.

Kwa vile nchi yetu hii imekuwa na maafa mengi au maendeleo yetu yamezorota kwa shauri ya neno “uchawi”, ni mapendekezo yetu, sisi kama waganga wa kienyeji, kwamba Katiba itambue mila, desturi na tamaduni za kila raia. Hii iwe ni pamoja na waganga wa kienyeji. Waganga wenye uwezo wa kutambua wachawi watambuliwe na Katiba. Kazi za kuwatambua wachawi ziwe na usaidizi kisheria na wachawi washtakiwe na kuadhibiwa. Ni hayo.

**Com. Lethome:** Tungependa kwanza utupe mwangaza mambo ya uchawi. Wachawi, waganga hawa, fafanua.

**Albert Jeremiah Rua:** Sawa.

**Com. Asiyo:** Tunataka kujua kama wachawi na waganga ni sawa?

**Albert Jeremiah Rua:** Wachawi na waganga si sawa. Maanake mchawi huenda kivyake pekee yake usiku ama mchana, lakini mganga huwa yeye anauguza au kwa kumtambua yule mchawi.

**Com. Asiyo:** Astahili awatambue wachawi na waganga.

**Albert Jeremiah Rua:** Hasa, hasa. Wachawi na waganga watambulike hapo utapata ule muongozo wa kwamba kubainisha je mchawi ni yupi na mganga ni yupi.

**Com. Lethome:** Sasa katika kule kutambuliwa kwao, mchawi akishatambuliwa ndiye huyu, afanywe nini? Na mganga akishatambuliwa ndiye huyu, afanywe nini?

**Albert Jeremiah Rua:** Ndio hapo tumependekeza kwamba ashtakiwe na kuadhibiwa.

**Com. Lethome:** Mganga ashtakiwe.

**Albert Jeremiah Rua:** Mchawi ashtakiwe. Mchawi.

**Com. Lethome:** Na mganga naye?

**Albert Jeremiah Rua:** Mganga kazi yake ni ile ya kutengeneza ile sawa. Uuguzi.

**Com. Lethome:** Kuna tofauti yoyote baina ya mganga na hawa ambao wanajiita herbalists, wanaotibu kwa kutumia miti shamba?

**Albert Jeremiah Rua:** Hakuna tofauti hiyo sana, maanake ile miti kila mganga anatumia ile miti. Ni kwa shauri tu pengine yule mwingine amepata ujuzi zaidi wa hii sasa.

**Com. Lethome:** Na washirikina?

**Albert Jeremiah Rua:** Washirikina pia wale ni mali ya mtu.

**Com. Lethome:** Watoto wa waganga ni washirikina au sio washirikina?

**Albert Jeremiah Rua:** La, kuna ushirikina. Hapo upo, lakini hata hivyo ule ushirikina unapozwa na ile ile dawa ile ya kule msituni.

**Com. Lethome:** Asante, twasoma somo ambalo ni ngumu.

**Com. Asiyo:** Asante.

**Com. Lethome:** Mbona umejisogeza na tumetatanika. Daktari jiandikishe huko. Andrew Shuba.

**Andrew Tuva:** Mimi naitwa Andrew Tuva na ni mwenyeji wa hapa Kilifi. Ijapokuwa vidokezo vyangu nilikuwa nimeandika kwa lugha ya kiingereza nitaweza pia kuongea kwa lugha ya Kiswahili.

**Com. Lethome:** Haya vizuri zaidi.

**Andrew Tuva:** La muhimu sana ni kwamba ninapendekeza sheria ya majimbo au mfumo wa majimbo wa kisiasa. Mfumo huu wa majimbo wa kisiasa uwe katika kiwango cha mikoa. Mkubwa wa jimbo hili awe anaitwa Governor na Governor huyu atakuwa amechaguliwa na waakilishi kutoka katika sehemu za wilaya, tarafa na hata location. Kwa hivyo ninavyosema ni kwamba watu kutoka chini wachague watu watakaoweza kuwaakilisha katika kiwango kile cha mkoa. Kisha katika kiwango kile cha mkoa ambapo tutakuwa na bunge ambalo litakuwa likiongoza masilahi ya mkoa, watachagua waakilishi wao kuwaakilisha katika serikali kuu. Katika serikali kuu waakilishwi katika kutoka kwa mikoa watachagua waziri mkuu na-mi ninapendekeza kuwe na Rais ambaye hana mamlaka ya kuendesha serikali, yaani ceremonial president. Katika kiwango kile cha kuendesha serikali kuu, waziri mkuu atakuwa na uwezo katika wizara fulani fulani. Kwa mfano, wizara ya kuweza kujikinga au defence, wizara ya mambo ya nje, na wizara zingine ambazo haziingiliani kwa njia yeyote au kugorogana na maslahi ya mkoa. Mikoa ni lazima iendeshe shughuli zake bila kuingiliwa na serikali kuu. Na iwapo pengine katika kwendesha mambo yao, kuna jambo fulani ambalo lina kwarusana na jambo la kitaifa, basi hapo itabidi mwakilishi wa mkoa aweze kuasiliana na waziri mkuu na pia kuweza katika kushirikiana huku wataweza kuamua ni vipi wanaweza kusuluhisha jambo hili.

Ningependa pia mahakama yaweze kuwa katika majimbo mpaka kiwango cha high court. Katika serikali kuu kuweze kuwa na ile korti tunayosema ni korti ya appeal. Iwapo sasa mambo yatakuwa yamekwama kabisa mpaka kiwango kile cha high court, court of appeal ambayo itakuwa inaendeshwa na Central Government ndio inaweza kusuluhisha kesi hiyo.

Katika kupendekeza serikali hii ya majimbo nitataka pia kusema ya kwamba stakabadhi za muhimu kama vile birth certificate, kama vile passport, kama vile kitambulisho viwe vinaweza tu kutolewa kutokana na mapendekezo ya watu wa kutoka chini, yaani wazee wa mitaa kwenda mpaka juu. Ikifika juu yule wa juu tu atakuwa anaangalia huyu amependekezwa kutoka huko chini, kwa hivyo bila shaka anastahili kupata stakabadhi hii na apate mara moja.

Hivyo hivyo, nitataka pia kusema ya kwamba umilikaji wa ardhi uwe unatekelezwa kwa njia hiyo hiyo, kwa sababu ni wazee

wa kijiji ndio wanaweza kujua fulani ameishi hapa kwa mda gani, na anastahili kupata nini. Kwa hivyo sisi sote tunakubaliana na yeye arithi ardhi hii. Hatutaki mtu wa kutoka nje ya mkoa ambaye hata hajui historia ya ardhi hiyo awe anaweza kupitia kwa njia ambazo hazitambulikani na aweze kurithi ardhi. Kwa kupendekeza sheria ambayo itakuwa ina-regulate hivi ama itakuwa inaongoza mambo haya, ningependa pia turudi nyuma ki-historia tuangalie ni nani ambaye amepata ardhi kwa njia ambayo si ya halali. Hizo sheria hizo ziteguliwe kwani kuna uwezekano kwamba kuna watu fulani fulani ambao wamepata ardhi kwa njia ambayo si halali. Nasi hatuwezi kukubali tuendelee kupata shida kwa sababu ya kitu ambacho kilitendeka au kilitendwa na watu ambao walikuwa hawastahili uongozini.

Ningependa pia iwapo katika serikali hii mpya, Attorney-General atakuwa bado ana nguvu au mamlaka, awe hana haki ya kusimamisha kesi wakati wowote. Kesi itakuwa tu inaweza kusimamishwa na hakimu mwenyewe, lakini sio awe yeye anaweza kuingilia ile kitu inaitwa 'nolle proseque'. Ningependa pia kuwe na kipengele fulani cha kuweza kumkinga mtu yeyote ambaye amefanya kosa, kwa mfano kuua awe anaweza kuwekwa korokoroni kwa mda fulani. Tunavyo-ona sasa ni kwamba watu fulani wana-wekwa korokoroni hata miaka kumi bila kuhukumiwa. Nafikira inakubalika ya kwamba haki ikicheleweshwa huwa ni haki ambayo mtu amekoswa. Kwa hivyo kuwe na kiwango fulani, iwapo wale prosecutors watakuwa hawawezi kupata ushahidi wa kutosha mtu huyo awachiliwe, lakini asiwekwe korokoroni kwa mda muingi. Ningependekeza pengine akizidi sana mwezi moja, waufanye uchuguzi wao.

Ningependa pia kupendekeza kwamba mayors wawe wanachaguliwa moja kwa moja na raia, ili waweze kupata nguvu zaidi za kuweza kuendesha shughuli zao. Ningependa pia kupendekeza ya kwamba, kuwe na kipengele fulani ambacho kina ruhusu watu kuwania viti vya bunge bila kupatiwa tikiti ya chama fulani. Ikiwa mimi nataka kwenda bunge sina haja na kuwa kupata tikiti ya Kanu, au ya Ford People, ama ya Shirikisho. Niwe ninaweza kupatiwa tikiti ya moja kwa moja na raia. Independent candidates, kuwe na kipengele kama hicho.
Nitasema pia, rasilmali za muhimu katika mkoa ziwe zinaendeshwa na serikali ya majimbo. Na pengine asili mia fulani tu iwe inachangiwa kuendesha shughuli za serikali kuu. Hii itakuwa inaweza kuamua ni mambo gani katika hilo jimbo ambayo yanaweza kutambuliwa. Kwa mfano tunaona vipengele fulani ambavyo vinaumiza maslahi ya jimbo hili. Tembo la mnazi kwa mfano linaitwa brew au tembo ambayo inatengenzwa na sisi tunajua wazi halitengenezwi, na pengine hii inaweza kuwa ni sababu ambayo imefanya chombo hili kuchukuliwa kama ni tembo ambalo halifai, lakini ni tembo ambalo tumepatiwa na Mungu mwenyewe, halitui chochote, halitui sukari. Lakini sheria ya Kenya inasema ni brew, inafananishwa na chang'aa, busaa ambavyo vinatengenezwa kwa njia ambayo si halali.

**Com. Lethome:** Pendekeza kuhusu mnazi bwana.

**Andrew Tuva:** Kwa hivyo ningetaka mnazi, mkorosho au cash crops zozote ziweze kutambuliwa. Na katika kutambuliwa huko kuwe na vipengele fulani ambavyo vinaweza kuweka bei fulani ambayo itakuwa inatambuliwa kitaifa. Hii yote ikiwa ni kwa madhumuni ya kuinua hali ya kimaisha ya wenyeji wa mkoa huu. Ilivyo sasa ni kwamba mimea kama hii haitambuliwi na

ndiposa tukawa na mtambo wa korosho ambao umekufa, tukawa na biksa factory ambayo imekufa, tukawa na mtambo wa sukari ambao umekufa. Ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu serikali haijatambua mimea hii. Kwa hivyo, yangu ni hayo kwa sasa na asanteni sana.

**Com. Lethome:** Ngoja kidogo. Mimi nina malalamishi kidogo. Naona kina mama hapo wamejiandikisha, kina mama wote wamesema hawataki.

**Com. Asiyo:** Lakini itakuwa makosa kubwa sana tukitoka hapa bila kusikia sauti ya kina mama, maana hawa pia ni binadamu. Lakini ni wachache sana. Tangu asubuhi hawajafika na wanasema hawataki kuongea. Sasa mambo haya ya Katiba yataundwa na wanaume pekee yao jamani.

**Com. Lethome:** Hebu ngoja, Lilian Wesa yuko hapa? Martha Salama, hajafika hapa? Kwa sababu wote wanasema hawataki kuzungumza.

**Com. Asiyo:** Sasa wanakuja nini, wasiozungumza.

**Com. Lethome:** Esther Muohe yuko hapa? Esther Mganze, yuko hapa? Mary N. Tsuma, yuko hapa? Hebu njoo hapa mama Tsuma.

**Com. Asiyo:** Kuja kama huwezi kuuliza maswali.

**Com. Lethome:** Haya sema majina.

**Mary Nyevu Tsuma:** Kwa jina ni Mary Nyevu Tsuma, natoka kata ya Tezo, kata ndogo ya Kibarani. Maoni yangu tulikuwa tumempatia mwenzetu aje aongee, lakini kwa sababu hajaingia, nitaongea vile ambavyo tulikuwa tumezungumza.

**Com. Lethome:** Sawa.

**Mary Nyevu Tsuma:** Mimi nitaongea juu ya wakina mama. Akina mama kuna kuonewa wingi ambako kumeendelea kwa mda mrefu. Ninalo-zungumza ni kwamba akina baba huwa mara nyingi wakiwa wameoana na kina mama, wanakaa kwa mda wakiwa wanapendana vizuri, lakini inafika wakati ambapo mara nyingine huwa kuna kukosana. Kunapotokea jambo hilo la kukosana wanapoachana, ni kama kuonewa mama yule analazimika mpaka kulipa mahari. Pengine wamekaa kwa mda wa miaka kumi ama miaka hata ishirini wamezaa, lakini utakuta ya kwamba baba yule atasisitiza ya kwamba mimi nataka mahari yangu. Anasahau ya kwamba amefanya mambo mengi mazuri mazuri na yule mama, ambayo ni zaidi ya ile mahari. Ningependekeza kwamba akina mama wakiwa wameachana na kina baba, kusiwe na kulipana mahari.

Lengine ni kama kina mama hivyo hivyo, kama wameachana tena ama kwa njia ya kifo. Kina mama huwa wananyimwa ile haki ya kurithi zile mali za yule bwana. Ningependekeza ya kwamba kina mama kwanza wasirithiwe kama baba amekufa, Wakae huru na wawe na urithi sawa ya ile mali ambayo yule mzee ameiacha.

Lingine ambalo ningependekeza ni ya kwamba akina mama hivyo hivyo, wawe na urithi kwa wazazi wao, kwa sababu wao wananyimwa haki kama wale si watoto kwa yule mzazi. Wavulana ndio huwa wanapatiwa ule urithi, lakini akina mama huwa wananyimwa. Wangepatiwa haki sawa sawa na wale akina baba pale kwao nyumbani, hata kama kule kwa bwana pia atarithi, lakini pale kwao pia awe na haki ya kurithi kwa mzazi wake. Na ningependekeza ya kwamba pia kina mama wapate haki ya kusomeshwa sawa na wavulana, kwa sababu huwa wanasomeshwa halafu inafika mahali wanakwama katikati, wavulana ndio wanapatiwa elimu mpaka mwisho. Halafu unasikia ya kwamba yule mzazi, tegemeo lake linakuwa kule kwa yule msichana badala ya kumtegemea yule mvulana. Kwa hivyo haki ingekuwa sawa kote kote wakapate elimu sawa, ili kwamba itafika wakati ambapo yule msichana pia ataweza kutegemewa vizuri katika ile familia yao. Kwa hayo machache nasema ni asentani.

**Com. Asiyo:** Unajua ni kwa dini ya kiislamu hakuna shida ya urithi, kwa vile wasichana wanaweza kurithi pande zote. Na siku hizi kwa wale watu ambao hamwezi kurithi kwa wasichana, kuna wasichana wengi ambao hawaolewi na tunaambiwa pia hawawezi kupata urithi. Pia hapo ungesema namna gani kwa wale makabila ambao hawapeani urithi kwa wasichana, na tumesikia wengi wao hawaolewi?

**Mary Nyevu Tsuma:** Hiyo ndiyo kuwaonea hawa wasichana, kwa sababu akiwa amekaa pale kwa mzazi wake, kwa bahati mbaya hakupata kuolewa na kukaa katika nyumba yake kisawa sawa, pale nyumbani anategemewa na wale wazazi na anategemewa na ile familia ambayo ameileta yeye mwenyewe. Sawa angepatiwa urithi pale nyumbani kwao, ili kwamba akaweza kujitegemea kwanza yeye mwenyewe na familia yake, tena wakati wa wale wazee wanahitaji usaidizi kutoka kwake, akaweza pia na kuwasaidia kwa sababu atakuwa anategemewa. Lakini hakufanyiki hivyo. Msichana anatupwa mbali, anategemea wale vijana wamebaki pale nyumbani, halafu inafika wakati wale vijana hawamtambui, wanamsukuma mbali, anaenda anakaa tu kama chokora, ambayo hiyo si sawa. Ingekuwa sawa na yeye pia akapatiwa haki, akaweza kujitegemea kama wale wavulana ambao wanajitegemea. Maana itafika wakati wale wavulana watamsukuma kama yule mzazi amekufa kwa bahati mbaya. Atasukumwa atakuwa hata hatambulikani pale nyumbani, na hana tegemeo lolote. Yule mzazi awagawie sawa sawa wakati bado yuko hai, ama awaandikie Will ya kwamba kila mtu portion yake ndio hii, ili kwamba akaweza kujitegemea kivyake.

**Com. Asiyo:** Na je msichana akizaa na hajaolewa huyu. Mtoto ungependelea awe ni wa yule jamaa wa kutoka huko kwa kijana au awe ni mtoto hana kwao.

**Mary Nyevu Tsuma:** Hapa kwetu Pwani, msichana kama amezalia pale nyumbani kabla hajaolewa, pengine anaweza kuzaa akiwa bado ni mdogo na atakaa pengine atazaa huyu mtoto mmoja halafu ajute, anakaa, anafikia umri wa kutaka kuolewa,

anapata mchumba, anaolewa.  Yule mtoto ambaye alimzaa huwa anabaki, wanasema ni ufagio wa pale nyumbani.  Lakini atakuja kutupwa, hatapewa ule urithi mtoto, atakuja kusukumwa, maanake mamake atasemwa alizaa tu hivi hivi. Hatatambulika yule mtoto.  Kwa hivyo, sawa kama yule mama amependa kuolewa na anaona kule ambako ameolewa kuko sawa sawa, inatakikana yule mtoto amtunze yeye mwenyewe.  Atakapofika, umri wa kujitegemea, atajitegemea kivyake yule mtoto.  Ama awe ana uwezo kama vile atakuwa amepatiwa huu urithi, yule mtoto atakuja kurithi pale mzazi wake amepatiwa. Itakuwa ni urithi kwa yule mtoto.  Lakini kama ametupwa, basi yule mtoto atakuwa ni "chokora" maana hatakuwa akijitambua lolote.  Sawa angekuwa anakaa na mzazi wake, atunzwe lakini sasa mama ameamua kuoelewa baadaye.  Na tena kama amezaa kabla hajamaliza masomo, sawa ingekuwa ni arudi tena asome, apatiwe nafasi tena aendelee na masomo yake, ajute ya kwamba alikuwa amekosea na aendelee na kusoma.  Atakapomaliza, anapata urithi pale pale kwa mzazi wake.  Kisha yule mtoto ambaye amemzalia pale atarithi pale mahali mzazi wake amepewa.  Na yeye kama atataka kuolewa baadaye, aende aolewe.

**Com. Lethome:**  Nina swali.  Na hawa wanaume wana mtindo wa kuwapachika hawa wanawake au wasichana mimba kisha yeye anapotea, iko anabaki ya yule mwanamke au yule mtu wa kike.  Ungependa wachukuliwa hatua gani kisheria?

**Mary Nyevu Tsuma:**  Kama mvulana alikuwa amepachika mimba msichana na amejulikana wazi ya kwamba ni mvulana fulani, ama hata kama huyu ni msichana mwenyewe aseme vile walikuwa wamesikizana na yule mvulana.  Na hatua zichukuliwe za kisawa sawa ya kwamba atunze huyu mtoto, kwa sababu ni damu yake, ni wake.  Amtunze mpaka atakapofika umri wa kujitegemea mwenyewe.  Ikiwa atashindwa kufanya hivyo, basi hatua za kisheria zichukuliwe.

**Com. Lethome:**  Kama zipi?

**Mary Nyevu Tsuma:**  Kama ni kuwekwa mahakamani ahukumiwe sawa sawa.

**Com. Lethome:**  Afungwe, miaka mingapi?

**Mary Nyevu Tsuma:**  Mpaka yule mtoto atapokomaa.

***Laughter:***

**Com. Lethome:**  Tumesikia maoni mengi hapa kuwa mila za utamaduni za watu ziheshimiwe.  Sasa kuna mila moja inaitwa ufa, sijui kama mnaita ufa.

**Mary Nyevu Tsuma:**  Ndiyo nimesema ya kwamba msichana ama mama kama ameolewa na bwana amekufa, asiolewe pale nyumbani kwa yule bwana, maana alikuwa ni shemeji ya alikuwa akimheshimu.  Itakuwaje basi wakati yule ndugu yake

amekufa aanze kuchakura chakura, ana chakura vitu gani? Aache huru yule mama. Akae akitegemea ule urithi ambao baba amemuachia.

**Com. Lethome:** Unajua kuna maswala mawili; kuna kule kutaka kuolewa na ndugu ya bwana kwa hiari yake, na kuna kule kulazimishwa. Sasa wewe unapinga kule kulazimishwa au unapinga pia na hiari, asiwe na hiari ya kutaka kuolewa na shemeji yake?

**Mary Nyevu Tsuma:** Sidhani kama kuna hiari yoyote. Kama huyo alikuwa ni shemeji yako mlikuwa mkiheshimiana kutoka mwanzo, hakuna uhiari wowote. Ama pengine alikuwa ni mpenzi wako kutokea kitambo. Lakini kama ni shemeji yako, yule wa haki, hakuna haja ya kuchakurana kuchakurana. Baki hivyo hivyo. Kama utataka kuolewa na mtu mwingine, kando na yule shemeji yako.

**Com. Lethome:** Asante kwa maoni yako.

**Mary Nyevu Tsuma:** Asante.

**Com. Lethome:** Haya, Lilian Wesa ashafika, Lilian Wesa? Mama jina lako ni nani? Umeshajiandikisha hapa. Esther nani? Esther Kacho. Haya. Umeandikisha kuwa hutazungumza, lakini tumekuambia zungumza. Kuna sababu ya kuwaita kina mama hivi, kwa sababu siku zote inakuwa kina mama sauti zao zina kichombo, tunataka watoe sauti zao leo.

**Esther Kacho:** Mimi naitwa Esther Kacho kutoka Mnarani lakini mtanisamehe sijui koo. Mimi kwa niaba ya kina mama ningezungumzia kuhusu girlchild education. Mara nyingi sana wasichana wanaachwa nyuma katika masomo yao. Watu wanabagua wavulana pekee ndio wanapelekwa shule, wasichana wanaachwa nyuma. Hayo huwa yanaharibu maendeleo na baadaye tunakuta kina mama hawako katika ngazi za juu za kimasomo ama katika kazi, kwa sababu ya kubagua watoto wa kisichana. Ningependekeza watoto wapatiwe haki sawa, kama mvulana anavyosoma mpaka afike university, first priority ipatiwe msichana asome kwanza, hata kama ni wote wamepita msichana asome yeye kimbele yule mvulana afuatie. Kwa sababu tunachelea hii mambo ya wasichana kukomaa na akiachwa nyumbani bila kupelekwa shule, ndio mara wasichana watungwa mimba bila sisi kutaka. Na baadaye inakuwa mambo ya familiy zinaongezeka bila kutarajia na pia kuna magonjwa ya zinaa, na wakiwa ni wadogo, huwa hawaelewi kunaendelea nini.

Jambo lingine ambalo nitazungumzia, tunataka serikali ya majimbo. Tuna vijana wetu wengi ambao wamesoma na tunajua tunaweza kujitegemea sisi wenyewe. Tunataka wakuu wa mikoa wawe wanatoka huku huku. Tuna mahoteli mengi, rasilmali nyingi sana ambazo vijana wetu hawana kazi, na tunataka wapate nafasi ili wapate kazi katika serikali yetu hii. Kwa hivyo, tungependekeza serikali igeuzwe ili at least hao vijana ambao wanaranda randa wamesoma wamefika university na kazi hakuna, tuna mahoteli mengi sana tupate ile kuwaingiza ndani.

Jambo lingine ni kuhusu kina mama huwa tunalemewa sana wakati tumeolewa na mabwana zetu wamekufa. Tunaona licha ya kuolewa na ndugu, ile mali ya urathi mara nyingi sana tunanyimwa haki zetu. Bwana amekufa, amekuwa na mali, ile mali unapokonywa, unafukuzwa pale ulipokuwa unaishi. Wanakuja wale mashemeji wanakuwa sasa mali ni yao, kwa sababu wewe ni wao, mahari walitoa, sasa wanakuchua hata wewe wanakutupa nje, kwa sababu wanasema ulikuja pale kwa sababu ya mahari. Kwa hivyo tungetaka hiyo iondolewe kabisa. Mama kama bwana wake amekufa, inahakikishwa na serikali kuwa ana-maintain ule urithi wake bwana wake aliouwacha, sio kutolewa nje. Pia hakikisho kwamba watoto wake wanasoma kwa vizuri mpaka wanamaliza shule.

Jambo lingine ni kina baba saa ingine wanatugandamiza sana kwa hii mambo ya malu. Malu saa nyingine sana wanajaribu kuwaambia kama kina mama kutoa aibu, kina mama wanasema wewe tumekushika na mwanaume ni lazima utoe malu. Na yeye tukiwashika na wanawake atoe malu.

**Com. Lethome:** Malu ni nini?

**Esther Kacho:** Malu ni ile fee inatolewa kama mtu ameshikwa na bibi ya mwenzake, yaani wakifanya mapenzi, kuna kiwango fulani kimewekwa tunaita malu.

**Com. Lethome:** Anayelipa ni nani?

**Esther Kacho:** Anayelipa ni yule bwana, analipa bwana mwenzake. Sasa sisi kina mama tunasikia uchungu. Saa nyingine hata huko ndani ndani nasikia cases nyingine hutokezea, baba anatuma bibi yake kwa sababu school fees hana, anaenda anaambia bibi yake nenda kwa yule baba akakutongoze ili pale tutapata mali ya kulipa school fees, ambayo baadaye inatokezea ni aibu kwa kina mama kufanya namna hiyo. Sasa sisi solution tunataka pia bwana wangu nikimshika na mwanamke, huyo mwanamke alipe hiyo malu, ili tumalize hii kitu isiendelee.

**Com. Lethome:** Lakini swali ni hili, huyu mwanamke kweli analazimishwa na mzee lazima uende ukatafute malu?

**Esther Kacho:** Sometimes it happens, hiyo huwa inatokezea wakati mwingine.

**Com. Lethome:** Sasa wewe unapendekeza ipigwa marafuku ama malu ikubaliwe pande zote, mke na mume wawe sawa?

**Esther Kacho:** Either ipigwa marufuku ama kama itakubaliwa kwa kimila yetu, maanake they call it a "mila" iwe ni ya both. Mwanamke akishikwa na bwana, mwanamke analipa yule bibi mwenzake. Yule bwana akishikwa na yule bwana mwenzake, bwana analipa yule bibi mwingine.

**Com. Lethome:** Unapendekeza iendelee au ipigwe marufuku mama?

**Esther Kacho:** Inaweza kuendelea kwa sababu tunataka kuvunja hii mambo ya zinaa pia, maanake ikiendelea ndio watu wakilipa malu itakuwa ile aibu iko. Mtu hatarudia kufanya kile kitendo. Lakini ikikatwa, watu wataendelea na itakuwa sasa ni free.

**Com. Asiyo:** Lakini mama, miaka sabini sio kama mika ishirini iliyopita. Kuna magonjwa mbaya sana ambayo yanatokana na mambo kama haya. Je, ukisema malu iendelee si watu watakufa wote?

**Esther Kacho:** Ndiyo itakatika. Ndiyo itakuwa watu hawafanyi, lakini ukisema it's free wafanye, they will be doing it openly. Kwa sababu hata ukinishika na bwana hunipeleki mahali. Lakini akijua kuna fee itatolewa kwa bwana na bibi wote wataogopa.

**Com. Lethome:** Hayo ni maoni yako, tumesikiza maoni yako. Ulisema watoto wa kike wapewe haki zao za kielimu. Wajua wazazi wengi si kupenda kwao kutowapeleka watoto shuleni, wawe ni wa kike ama kiume, kwa sababu ya school fees. Imewalemea watu wengi. Sijui utapendekeza chini ya Katiba mpya hilo tatizo litatuliwe vipi?

**Esther Kacho:** Ningetaka serikali iwe na kiwango fulani ambacho kinaweza kusaidia sana watoto wa kike, kwa sababu si sana utaende ofisi nyingi ukute watoto wa kike ndio ni wengi. Kwa hivyo tungetaka serikali iangalie sana mambo ya girl-child education.

**Com. Lethome:** Yaani wapewe free education.

**Esther Kacho:** Yes.

**Com. Lethome:** Girls pekee, ama watoto wa kiume pia.

**Esther Kacho:** They can be both, lakini first priority should be given to the girls.

**Com. Asiyo:** Kuna nchi zingine ambapo wanafanya kwa mambo ya elimu, wanaelimisha watoto wasichana na wanaume pamoja kwa hivyo si education ya primary, lakini ikifika secondary ambapo saa zingine wazazi hawawezi kupata mali ya kwenda kuelimisha wote wawili, wasichana hupatiwa elimu ya bure ya secondary, halafu nao kina baba wanahimizwa kutafuta mali ya kuwasomesha. Je, ungependelea vipi?

**Esther Kacho:** Mimi ningeiunga mkono hiyo ya kuwa wasichana wapatiwe hiyo pesa/ fees waende shule, au wavulana baba yao pengine anaweza kufanya bidii na akapata pesa.

**Com. Lethome:** Kuna swala la domestic violence. Matatizo yanayotokea kinyumbani baina ya mke na mume, unakuta mama asubuhi anaamka jicho limevimba kwa ngumi. Unaweza kushtaki mambo ya nyumbani. Je, ungependekeza kitu gani? Au wakati mwingine kama baba hupigwa, wengine hutolewa meno?

**Esther Kacho:** Hilo kweli limekuwa tatizo gumu sana katika familia zetu, lakini tungetaka ni sawa, hatuwezi kusema ni ya nyumbani maanake wakishapigana wakiumizana haya inakuwa ni mambo ya madaktari waingilie, mambo ya polisi waingilie, lakini hata polisi wakiingilia si ati wafunge yule bwana ama wafunge yule bibi. Ni wahakikishe kuna fine fulani ambayo itawekwa. Wewe ukipiga bibi yako ukimuumiza kuna fine fulani utalipa na bibi naye akipiga bwanake akimuumiza kuna fine fulani atalipa.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo wakifungwa ni fine?

**Esther Kacho:** Hakuna kufungwa, maanake wakifungwa bwana atateseka, ama bwana akifungwa bibi atateseka, ama bibi akifungwa bwana atateseka, na watoto watateseka. Hata pengine yale yalikuwa ni mambo yametokezea ghafla na wakaanza kupigana mahali pale. Kwa hivyo iwe ingechukuliwa tu, ukifanya kosa kama hilo unapatiwa fine. Lakini mambo ya kwenda kwa chifu kila wakati, ukifika chifu ana-favour one side, pengine anamuogopa yule bwana ama amepatiwa hongo kidogo ana-favour kule kwingine. Hata mambo yatakuwa hayatengenezeki, itarudi vile vile, wakifika nyumbani itakuwa kuwa mimi ndio bwanako, si unaona sasa hakuna lolote limefanyika? Kwa hivyo kama kungekuwa na fine fulani imewekwa hiyo ingekuwa, at least ingetusaidia katika domestic violence. Halafu na wakati mwingine, kuna kina baba huingilia watoto wao, kama kuwanajisi watoto wao wakiwa wadogo. Jambo kama hilo linatusikitisha sana. Kama mimi nimeolewa halafu nime-divorce kwingine nimekuja tena nimeolewa kwingine, yule baba ambaye ninakaa naye hatamuheshimu yule mtoto. Ni rahisi sana hapa kwetu baba kumnajisi yule mtoto. Sasa inakuwa yaani pale nyumbani hakuna raha, huwezi ku mu-report yule bwana na hata ukamshtaki yule bwana hakuna action yoyote saa nyingine inachukuliwa.

**Com. Lethome:** Haya pendekeza, achukuliwe hatua gani mzee kama huyu?

**Esther Kacho:** Afungwe ama kwa mda kidogo, lakini apigwe fine.

**Com. Lethome:** Wewe bado unamuhurumia tu, bado unamuhurumia tu.

**Esther Kacho:** Na yule mtoto aondolewe at least awe anaishi kwingine na kisha amsomeshe mpaka amalize shule.

**Com. Lethome:** Asante, jiandikishe pale. Tuendelee na list yetu. Wellington Rasi, Wellington Rasi, karibu bwana.

**Wellington Rasi:** Jina langu ni Wellington Rasi. Kabla sijazungumza ningelipenda kusema hivi. Hii nchi mwanzo, ilikuwa na serikali ya majimbo ambayo ilipatikana huko Lancaster House mwaka wa sitini na mbili. Sasa kwa sababu nafasi hiyo haikupewa ikafanya kazi, mimi hapa nimeandika napendekeza ya kuwa Katiba hiyo ya majimbo ya Lancaster House 1962, mda huu ambao tunatayarisha Katiba ingine, ijaribiwe. Ni hayo tu, asanteni. Kwa sababu mengi hapa imeandikwa.

**Com. Lethome:** Haya, yatukabidhi huko. Haya, Saidi Rasi.

**Saidi Rasi:** Asante bwana mwenye kiti, mimi pia sina mengi ya kuzungumza kwa sababu mengi yamekwisha andikwa huko. Lakini nitapendekeza mambo fulani fulani. Kama alivyotangulia kusema yule mwenzangu, kulikuwa na serikali za majimbo, hii ni Federal Government. Kulikuwa na serikali za majimbo zikiongozwa na viongozi watatu; Rais akiwa anaongoza sehemu yake na vile vile waziri mkuu awe anaongoza sehemu yake. Na sehemu ya tatu inakuwa ni Regional Government. Kutokana na mafungu haya matatu ya uongozi, tutapata Rais anasimamia hali za nchi maendeleo ya nchi, pamoja na jeshi la taifa awe anasimamia Rais na huduma zote za kitaifa. Hii itakuwa ni kazi yake Rais, na kazi ya pili itakuwa ni wa waziri mkuu. Waziri mkuu atasimamia serikali ya katikati, uchumi wa nje, na uchumi wa ndani, chini ya serikali kuu.

Halafu, fungu la tatu ni serikali za majimbo, Regional Government, ambapo huko kutakuwa na Governor ama waziri mkuu awe ni wa majimbo. Hawa watakuwa na assembly yake ambayo itakuwa na viongozi kutoka katika mkoa huo. Sasa hawa watakuwa wanasimamia serikali ya kijimbo kutoka chini mpaka kufikia ngazi ya huo mkoa. Watakuwa wanaweza kusimamia kila kitu kwa urahisi, kwa sababu nchi yetu ya Kenya haina uwezo kuwa mtu mmoja kutawala nchi nzima. Serikali hizi za ki-majimbo zitaondoa uchafu wote ambao sasa tumeushuhudia kwa miaka arobaini. Serikali za majimbo zipewe uwezo kutoka kuajiri jeshi la polisi. Jeshi la kulinda usalama ni la polisi, liwe linasimamiwa na Regional Government. Regional Government iwe na uwezo wa kumuajiri polisi na kumfuta kazi saa yoyote, ili kusudi kuhakikisha kila kitu kitakuwa kinaenda sawa. Mimi sina mengi nafikiri hayo yametosha, kwa sababu wengi wamependekeza hayo hayo mamoja. Kwa hivyo ninasema asante kwa hayo.

**Com. Lethome:** Katika huo mfumo wa serikali ya majimbo, je kutakuwa na vyeo kama vile PC, DC na viongozi wengine tulio nao?

**Saidi Rasi:** Regional Assembly hazina uhusiano na PC, kwa sababu huyu waziri mkuu ama governor, ndiye anayesimamia hilo jimbo, kwa hivyo yeye atakuwa ana uwezo katika hiyo region yake, atakuwa na assembly yake.

**Com. Lethome:** Hatutakuwa na ma-DC, DO na ma-chief?

**Saidi Rasi:** DC, chifu hawa wanakuwepo kwa sababu ndiyo nguzo ya hiyo government.

**Com. Lethome:** Wachaguliwe na nani?

**Saidi Rasi:** Sasa hawa watakuwa wanachaguliwa kupitia kwa assembly.

**Com. Asiyo:** Sio wananchi wenyewe wanachagua ma-chief?

**Saidi Rasi:** Regional Government itakuwa imechaguliwa na wananchi wenyewe kisha na kupendekezwa na serikali kuu, kisha hiyo regional assembly ndizo watakuwa wanasimamia wanawapa uwezo wananchi kuchagua ma-chifu. Chifu ni mtu muhimu sana katika nchi, kwa sababu yeye ndiye anayeisimamia chanzo cha mtoto hata akiwa tumboni.

**Com. Asiyo:** Unataka naye chief achaguliwe na wananchi wenyewe?
**Saidi Rasi:** Lazima achaguliwe na wananchi wenyewe.

**Com. Asiyo:** Na councillor?

**Com. Lethome:** Ma-diwani?

**Saidi Rasi:** Councillor si ndio hawo tunasema ni regional government ndio inaweza kutoa uongozi wa kuwachagua hawa ma-diwani katika town council.

**Com. Lethome:** Na ma-diwani kiwango chao cha elimu kiwe kipi?

**Saidi Rasi:** Kulingana na maendeleo ya kisasa, diwani ni lazima awe na elimu ya form four, kwa sababu diwani anaweza kumpokea diwani kutoka nchi ya nje ambapo angeweza kuja kuzungumza naye, kuwa rafiki na yeye, ni lazima wawe kiwango cha elimu ya juu, ili awe na kujua lugha za kazi, ili aweze kuwasiliana na wenzake vizuri.

**Com. Lethome:** Asante bwana Saidi, jiandikishe pale. Tupate sasa Abubakar Kuchi.

**Abubakar Kuchi:** Asante sana. Nilikuwa pamoja na ile group ingine ambayo imesomwa vitu vingi, kwa hivyo ni kuongezea vile ambavyo vilikuwa havijatajwa. Kwanza nashukuru kwa kutupa nafasi hii ya kurekebisha Katiba, tumepata mafundisho mbali mbali namna ya kujiandaa mojawapo tukiambiwa tusiwe na hofu ya chochote tuseme fikira zetu, wala hatutashtakiwa kwamba tumesema kitu. Kwa hivyo hivyo iwe ni hivyo. Tuko hapa kutoa maoni yetu.

**Com. Lethome:** Tunakuhakikishia…

**Abubakar Kuchi:** Naona hapa ndani hivi kuna ma-ofisa, makachero pengine.

**Com. Lethome:** Ngojeni niwahakikishie jambo moja. Sisi Tume hii imebuniwa na sheria iliyopitishwa na bunge, na sheria hiyo imesema lazima serikali na watu wote wahakikishe kuwa kuna mazingara yatakayomwezesha Mkenya kusema anavyotaka. Kwa hivyo hapa tuko chini ya himaya ya sheria inayosema maadam hatuvunji sheria yoyote, tuna uhuru wa kusema lolote tutakalo. Na mimi nawaambia hivi, katika vikao vyetu vyote, tunakuta ma-polisi wenye uniform hapo, na wengine tusiowajua wapo pia ndani yake, lakini hawatuzuii kusema tunalotaka. Tunakuhakikishia, na ikiwa utapatikana na matatizo yoyote kwa sababu ya yale uliyoyasema hapa, tukamilishe na sheria tutachukua hatua. Kwa hivyo makachero waweko waendelee na kazi yao, wachakue wanaotaka kuchukua. Hakuna wasi wasi bwana. Haya.

**Abubakar Kuchi:** Asante sana. Basi maoni nyongeza ni kwamba:

No.1. Kuhusiana na pesa au sarafu ya nchi. Picha za maraisi ziondoke kwenye pesa. Kuwe na picha za mali ya asili, wanyama, samaki, ndege, milima, na kadhalika. Ili isitatize Rais mwingine akija naye achapishe zake, mwingine akija achapishe zake, hii itakuwa kupoteza pesa. Maana kuchapisha pesa ni kutumia pesa.

La pili, ma-Rais na makamu wake au wao, au wafanya kazi wa serikali waliokosea, waliofuja mali na kwenda kinyume na ilivyo takikana, hawa washtakiwe ijapo hawako ma-ofisi kamwe. Isiwe leo wale ambao watashtakiwa ni kwanzia leo, hata tuliye naye sasa kitini ikiwa kulipatikana na hatia au makosa, kupatikane kipengele cha kumshtaki na wengine wanaohusika wote washtakiwe.

Cha tatu, mali ya asili kama mikoko na kaure na vitu vingine, mara kwa mara hutangazwa kufungwa na kufunguliwa baada ya kwenda kupigia magoti watu fulani. Hivi vitu vya Mungu wamepewa binadamu, ili waweze kuvitumia na kuweka hali zao ziwe nzuri, kwa hivyo zisifungwe vitu hivi bali zifanyiwe bidii zipatiwe masoko ya nje. Kama vile kunavyofanywa kukipatikana soko la kahawa na chai, mkoko nao na kaure ziwe zitatafutiwa masoko ya nje.

Watoto au wanafunzi wa kiislamu wasilazimishwe wala kuruhusiwa wala kushawishiwa kusoma somo la ukristo mashuleni. Badala yake wizara ya elimu ilazimike kutafuta waalimu na kuwaajiri wakasomeshe elimu ya kiislamu.

Maendeleo ya nchi: kibarabara. Kama barabara za lami, simu, sitima, maji, na kadhalika, zisambazwe sawa sawa nchini, sio sehemu fulani zikawa leo wanaondoa lami wanaweka lami ambapo kwingine hata murram hakuna.

Elimu na afya: serikali ihudumie kikamilifu 100% watoto wote wa taifa kuwapatia elimu ya bure, ndio jukumu la serikali iweze

kufanya mpango maalum kila mtoto asome bure. Watoto wengi ambao ni mahodari humalizikia katikati kwa sababu hawana uwezo wazazi wao wa kuwamalizia ili wapatikane watoto wale kuhudumia taifa. Na huduma za afya nazo kadhalika ziwe ni bure kwa kila mtu, kusiwe na cost-sharing, kwa sababu cost-sharing watu wengine hawawezi kabisa. Hayo niliongezea katika ile karatasi iliyosomwa na mwenzangu, kama dakika zangu zimebakia mwenye kiti.

**Com. Lethome:** Bado mbili.

**Abubakar Kuchi:** Asante sana. Namba saba katika karatasi ile ilisema waislamu wawe huru kuwa na taratibu zao za elimu za dini, na elimu hiyo ipewe kipimo sawa na elimu zingine, ili walio na elimu ya uislamu waajiriwe kazi zinazohusiana na uislam, kama u-kadhi, ama ualimu, ama wakfu wa commission, na kadhalika. Hivi ni kusema watu walio na elimu kabambe ya dini hutupwa nje kwa sababu hawana certificate za form four ama form six. Napendekeza hapa elimu za waalimu wetu wanaosoma madrasa zipimwe, zitafutiwe kipimo sawa, kikiwa kama ni cha diploma basi awe awarded diploma, ili kama hakuna kazi yoyote ambayo inahitaji diploma na ile ya madrasa nayo ichukuliwe ni elimu.

Halafu namba kumi na mbili nilisema Mkenya yeyote akifika umri wa kupigania au kugombea wadhifa wowote aruhusiwe. Wadhifa wa u-Rais, makamu, bunge, mayor na ma-diwani tena bila sharti ya ki-elimu au ki-fedha wala chama. Aweze kugombea hata kama hakupata chama wala kufanyiwa mtihani wowote, kwa sababu wale watakaomchagua, wengi hawa kusoma. Sasa hatuelewi kwa nini anaenda kuwakilisha wale ikiwa wananchi wenyewe wataridhika na kiasi cha uerevu wake asiende kule. Iwe maadam hana form four basi hafai. Kwa hivyo atahiniwe kidogo kiasi ya kuonekana si mtu ambaye hawezi kusema. Kama ilivyo sasa mtihani ule unafanyiwa na Electoral Commission. Namalizia bwana.

Katika namba ishirini na moja, town centres kuwe na eneo litengewe harakati za waislamu ijapo ikiwa sehemu hiyo hakuna waislamu wengi. Isiwe kwamba wakati waislamu wamepatikana sehemu hiyo, huwe hawakutengewa makaburi, wala hawana eneo la misikiti wala madrasa. Ikipangwa town fulani ijulikane hapa kutakuwa na makaburi ya waisilamu, hapa ni ya ambao sio waislamu, na pengine hapa ni misikiti, hapa ni makanisa, na kadhalika. Kusiwe kwamba kwa sababu hakuna mtu kwa sasa, ama ni wawili, watatu, basi iondoke kitu hicho. Wanadamu wanaendelea kua. Asante sana.

**Com. Asiyo:** Nilichotaka kujua mzee, umesema kwamba elimu iwe ni ya bure, lakini hujatuambia ifike kiwango gani, ni kidato au ni class cha nane unataka elimu ya bure iwekwe na serikali.

**Abubakar Kuchi:** Asante sana. Elimu ni ile ambayo itamnufaisha msomi. Kusema akifika primary eight tu hiyo ndiyo iwe ya bure, hamjampa mtoto elimu sababu standard eight hapati hata kufagia. Kwa hivyo ni elimu ya bure moja kwa moja mpaka university. Maana ile ni 8-4-4 eight katika primary, ukimaliza tu uende secondary ufikie four nyingine, halafu ufikie four maanake ndiyo system, 8-4-4-. Sasa unamfanisha eight tu, kwa sababu hana pesa haendi four, na akimaliza four, university haendi four.

**Com. Lethome:** Asante bwana, na hiyo ni mali yetu sasa.

**Abubakar Kuchi:** Hii ni yenu.

**Com. Lethome:** Sasa pia tungependa hapa kumkaribisha mwenyeji wetu hapa ambaye ni councillor Ahmed A. Barak, yeye ni Town Councillor hapa Kilifi. Kwanza atukaribishe, ndiye mwenyeji wetu, kisha achukue fursa hiyo pia kutoa maoni yake kwa sababu nasikia anarudi kwenye mkutano. Kwa hivyo, bwana councillor Ahmed, karibu.

**Councillor Ahmed A. Barak:** Watu wa Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya wakiongezwa na mama Pheobe Asiyo, mimi ni mwenyekiti wa Kilifi Town Council, Councillor Ahmed Barak, mnakaribishwa hapa Kilifi. Na mama Asiyo nakukaribisha maanake mimi nilikuwa Karuochonyo kule kwenu mtu wa Pwani wa kwanza kuwa "japunji" katika kule upande wa Nyanza. Kwa hivyo karibuni.

Nimesikia mawaidha ama hoja za watu mbali mbali tunapewa dakika tano, lakini mimi kama mwenyeji ninasimamia watu wengi na watu wengi hawakuja hapa nataka niongezewe muda kidogo, sio mwingi. Mama Asiyo kutembea ni kuona mengi. Na watu hupata elimu kwa kutembea mahali tofauti tofauti. Hapa kwetu Kilifi mjini kuna watu zaidi ya elfu ishirini na tano, lakini watu waliokuja kutoa hoja zao hawafiki mia mbili. Katika mikutano mbali mbali ya kimaendeleo ambayo yatadhuru watu wetu ama yataendeleza, hii ndiyo hali yetu unayoiona. Na Katiba hii ikitengenezwa, itachukua miaka sabini au themanini kurekebishwa, hata mia mbili na watu wa Pwani hapa na Kilifi mtakuja nyinyi mlie mseme, kwamba, ooh tumedhulumiwa tumefanya hivi. Nafasi mnapewa na hamji kwenye mikutano ama kitu ambacho ni muhimu kabisa katika maisha yetu. Sisi tutakufa sote, wale wajukuu wetu na vitukuu watapata taabu kwa sababu ya sisi, kama vile tunapopata taabu kwa Katiba ile iliyotolewa mwaka sitini na mbili.

Nikianza kwa utangulizi: Katiba tuliyo nayo tunaambiwa ni Katiba mbovu, lakini Katiba tuliyo nayo si Katiba mbovu. Wale ambao watekelezaji wa Katiba ile ndio wambovu. Na tumeshindwa kutekeleza hii Katiba mbovu tuliyo nayo. Mfano tumeuona juzi hapa, kwamba katika sheria ya Local Government Act, hakuna kifungu chochote ambacho kinaweza kumtoa mwenye kiti ama mayor wa baraza la mji, ni aidha amekufa, ajiuzulu mwenyewe ama afungwe zaidi ya miezi sita. Katiba hii si ya Hamid, si ya mama Asiyo. Sisi ambao twataka Katiba mpya na wale ambao wameweka majukumu ya kulinda hii Katiba mbovu, wao ndio wanavunja hizi sheria. Wanatoa mayor, wanasema kwamba amesema hivi na hivi na bado hajahukumiwa.

**Com. Lethome:** Pendekeza sasa.

**Councillor Ahmed A. Barak:** Sasa natoa ni utangulizi. Je, hii Katiba mpya itaheshimiwa, ikiwa hii mbovu haiheshimiwi? Tusikizane chama wala mtu wala nini, awe ni mjinga ni mwerevu, sheria ni za watu wote Kenya. Kitu cha kwanza, watu wa Kilifi District na Pwani, namna ya utawala wa majimbo ama sio majimbo hautatusaidia, kitu kitakachotusaidia ni kumiliki na

kuzi-control rasilmali zetu, uchumi. Mambo ambayo hayakuzungumzwa hapa. Napendekeza kwamba uchumi wa Pwani na Kilifi District ni utalii. Katika Katiba mpya asili mia sabini na tano ya wale wanaoandikwa kazi katika sehemu mbali mbali za kiwanda cha utalii, wawe watu wa hapo. Napendekeza pia, mtu yeyote awe ni mgeni anaweka rasilmali katika mkoa wa Pwani, asili mia arobaini na tisa ya rasilmali ile imilikiwe na watu wa hapa. Ndio tutaweza kulipa fee na tutaweza kwenda hospitali na tutaweza kulipa pesa na mambo mengine.

Jambo la tatu, rasilmali ya Pwani kubwa ambayo inatia pesa zaidi ni Port ya Mombasa. Port ile ya Mombasa bandari, hivi sasa inataka kuwa privatized, yaani iwe kwa mikono ya watu binafsi. Na inafanywa hivyo kwa sababu Katiba mpya ikija mambo yale yawe yashafanywa. Privatization haitakikani, isifanyike, na umilikaji wa rasilmali ya bandari ile inatengeneza zaidi ya bilioni moja kila mwezi, iwe itanufaisha watu wa hapa. Sio pesa itoke hapa ikajenge barabara Rift Valley ama Central Province. Ule ni urithi wetu watu wa Pwani.

Kuingia upande wa ardhi: Kuna watu wanaitwa absentee landlords, wale watu walipewa mashamba na ardhi wakati wa Sultan na kuna wengine walipata wakati walikuwa wao ni watu wa siasa wakapewa kwa sababu walikuwa karibu na Rais ama walikuwa na nguvu. Wale watu ambao mashamba yale hawakuyakaa zaidi ya miaka kumi na tano, mashamba yale yachukuliwe yagawanyiwe wale watu waliokaa pale. Mfano, ni Mnarani huku upande wa Fumbini, Konjora, Roka na kwingineko.

Kitu cha pili, sheria iliyoko katika Katiba ya sasa, kwamba Mkenya yeyote anaweza kuwamiliki ardhi mahali. Katika land adjudication, ile kukata mashamba kama upande wa Dida, Nyari, Sokoke, adjudication act inasema kwamba shamba ikifanyiwa adjudication ni watu wa pale asili mia mia moja watapata mashamba pale. Lakini kuna ujanja katika Ardhi House, kwamba hui-change wakafanya ni settlement scheme na katika settlement scheme act ni kwamba settlement scheme mtu yeyote kutoka Kenya anaweza kuingia. Ndio hapo walunguzi huwa wanaingia. Mfano ni Mboyani Settlement Scheme hapa Shauri Moyo, mzungu ambaye ni kaburu tumepigana na mbunge Jembe Mwakalu, tukapatiwa sehemu acre elfu mbili na mia nne. Katika zile sehemu, Kapecha, Gureni, Vipingo, Shauri Moyo na Kazinuni, zina watu wamekaa zaidi ya miaka mia na mzungu hakuwasumbua lakini title deed anayo yeye. Tukamtilia fujo, akatoa hizo ardhi na private surveyor akatoa. Akatoa sehemu nyingine acre mia mbili na hamsini Boyani, kwamba watu wakiwa congested kule wanalokaa waletwe huku. Wizara ya ardhi na makao, ilipopatiwa zile block plan titles za kule wakaenda wakachukua hiyo Boyani wakaifanya settlement scheme na ma-squatter wote hapo, kwa sababu hakuna mtu watoka Ardhi House. Kutoka waziri aliyekuwa director, nani, nani, nani wote, hata mjumbe pia aliingia huko, ambaye alikuwa akipigania hapo, badala na waziri akaja akatoa stakabadhi akasema tunapunguza tatizo la ma-squatters. Lakini zile acre sabini za baharini walizochukua hawo hawakuzisema. Na kule ambako mzungu tulikuwa tunapigania Kapecha, Bureni, Kasinunu na Vipingo, yeah, those are the areas, watu wamekaa, serikali imekaa hakuna hata mtu mmoja hawafanyiwa sub-division kwa sababu wanajua hawapati kitu, kuna watu tayari. Kwa hivyo hii maneno ya kwamba settlement scheme mtu yeyote anaweza kumiliki ardhi, leo tukifanya statistics tuki tazama, watu wangapi wa Pwani wamepata ardhi Rift Valley, Nyanza, Western Province, hawafiki hata asili mia moja. Pengine ni uwe mkubwa

Japheth Kiti, Katana Ngala, Baya ndio utakwenda pewa. Lakini huku ndio wakenya wanaweza kuja chukua, lakini kule sisi si wakenya hatuwezi chukua. Hii irekebishwe na siasa ya kwamba mtu ambaye amekuja hapa Pwani akafanya kazi na akapata mali na akanunua mali, ya kwamba ile ni siasa ya upotofu ya uvivu ya kusema kwamba aondoke aende kwao, hakuiba, alifanya kazi. Na mtatazama ndugu zangu kama mmetembea, ile miji ambayo haina uchanganyifu wa watu, hawakuchanganyika, miji hiyo imezorota na haikuendelea. Mfano ni Kabarnet, Nyeri. Kwa nini Nyeri ni Provincial Headquarters, Thika inaendelea zaidi. Ina diwana hata mjaluo hapo, ina diwani mkamba, kabila mbali mbali. Mkiwa hamtashirikiana na wenzenu mkakaa, hamwezi kuendelea. Hiyo ijulikane. Upande mwingine wa ardhi, ardhi zilizo tengewa public utilities, ardhi zile ziregeshwe na wale ma-ofisa wa ardhi ambao walipitisha kuchukua hizo public utilities wachukuliwe hatua, hata kama ni serikali nyingine.

Upande wa afya: mimi nina maoni tofauti. Mwenzangu hapa aliongea kuhusu kwamba kitu hospitali ziwe bure, cost sharing ziwe bure, hakuna bure siku hizi. Bure ni ya maiti, siku ile ikibebwa akienda akitiwa kaburini. Ni kwamba kodi zitakazopatikana hapa, hii nchi ina utajiri mwingi sana, lakini ufisadi na poor planning ndiyo inafanya mpaka tunakopa nje. Ikiwa kila mwananchi analipa kodi, na pesa haziibwi, hakuna ufisadi, kwa nini miaka sitini na sabini tulikuwa tukienda hospitali tunapata dawa kama zile za Aga Khan hospital, sasa hatuzipati? Vijana ambao tumeambiwa wameingia waambiwa hao ndio wataendesha nchi vizuri, hawana ile patriotism, uzalendo wa nchi yao. Tukitazama wale viongozi walikuwa mwaka sitini na tatu waliochukua mawaziri wengi asili mia themanini ni maskini kwa sabubu walipenda nchi yao. Wengine wako kina Otiende, kina Mathews Ogutu, Robert Matano hawakuiba, walikuwa kuwa wanataka kutumikia watu. Hawa mnaambiwa young turks wa sasa, wezi watupu, wanakuja wanatafuta mali, hawatafuti kuja kuwasaidia nyinyi. Kwa hivyo kodi inayopatikana hapa Pwani, rasilmali ziliopo hapa Pwani zinaweza kuendesha vituo vya afya, na tukawa na best vituo vya afya katika mkoa wa Pwani. Sio hapa kupatikane rasilmali zipelekwe Nairobi zikatengeneze mahali pengine; hapa ziwe hapa. Central Government iweko lakini modalities za economy za region zi-benefit ama zisaidie lile jimbo liliomo. Lakini tukisema kwamba sisi tunataka majimbo, kusema ni rahisi. Nigeria walijaribu Central Government ikawashinda kwa sababu kuna extra money, wale wabunge watakaopatikana na nini na kila kitu ni pesa. Kitu muhimu ni rasilmali za upande wetu zinufaishe watu wetu.

Economy: upande wa good governance ama mambo ya kujitawala. Sheria, tukija kwa upanda wa mabaraza, mwenzangu ambaye alisema kwamba mtu aweze kusimamia kitu chochote hata akiwa hana elimu. Basi si tuseme pia mashule yafungwe yote, ikiwa watu wetu hawana elimu tuwafanye wawe na elimu. Maanake kule ofisini circular zote zinazokuja zimeandikwa kiingereza, sheria zote zinazokuja zimeandikwa kiingereza. Zimeandikwa hata uzitafsiri wewe Kiswahili, na watu wa nje wakija wakitaka kujua miradi fulani wanazungumza kiingereza. Kwa hivyo tusipotoshwe tuseme kwamba lazima watu wanaokwenda pale lazima wawe ni watu ambao wanaweza kusoma kizungu, na wanaweza kusoma sheria za local government act, na waweze kuzitafsiri, waongoze wale ambao hawakusoma, na tufanye bidii watoto wetu wasome, ili tuwe kama watu wa Western Kenya na watu wa Central, tusiachwe nyuma.

**Com. Lethome:** Utapendekeza kiwango cha elimu cha councillor na madiwani.

**Councillor Ahmed A. Barak:** Madiwani na wabunge. Madiwani kiwango cha elimu kiwe form four na kisha form four ile, siku hizi ile form four tuliyosoma na 8-4-4 tunayosoma sasa, kuna tofauti. Mimi mwenyewe nilikuwa mwaalimu. Leo unaweza kuchukua manamba uka-m-register kwa mtihani form four, aende akaandike jina lake na index namba yake, atapata E na atapata certificate. Je, umetatua tatizo la ukosefu wa elimu? Kwa hivyo iwe pegged minimum requirement. Lakini mkisema form four, mtakuwa wale ambao hawakusoma badala ya mwambie wasipite na mlangoni watapita na dirishani. Na tatizo litaendelea vile vile.

**Com. Lethome:** Pendekeza hiyo Grade.

**Councillor Ahmed A. Barak:** Napendekeza minimum iwe D+ na equivalent ya third division ya old system. Na wale ambao wanataka ubunge wawe ni first ama second division ama A level. Hiyo itamuezesha yeye kusoma na kujua mambo ya parliamentary standing orders na sheria za bunge na za nchi hii. Kwa hayo nasema kwamba mwisho kabisa ni habari ya electoral laws – sheria. Wakenya ambao wanakaa nje ya nchi ya Kenya waruhusiwe kujiandikisha kura na wapige kura kama vile nchi za ulaya na America. Na vile vile wabunge wasipewe uwezo wa kujiongezea mishahara. Mbunge anapata laki sita kwa mwezi, wengine hatuwaoni miaka miwili, huwa wanamtumikia nani?

**Com. Lethome:** Unataka mishahara yao iwekwe na nani, nani aamue mishahara yao?

**Councillor Ahmed A. Barak:** Mishahara ni kama hivi nyinyi mlivyokuja mtembee muulize hoja za watu, walipwe vipi na benefits zao ziwe vipi?

**Com. Lethome:** Pia umezungumzia juu ya mbunge huyu ambaye tangu mlipomchagua hajaonekana. Afanyiwe nini mbunge kama huyo?

**Councillor Ahmed A. Barak:** Mbunge kama huyo atafutiwe referendum, watu asili mia hamsini watie sign, halafu asili mia hamsini wakitia sign ikipelekwa kwa speaker wa bunge, aachishwe aje aulize mandate mpya kwa watu.

***Interjections:***

**Councillor Ahmed A. Barak:** Kwa hayo machache wenzangu watakuwa na mengi ya kuzungumza nasema asante sana, karibuni Kilifi.

**Com. Lethome:** Asante sana Bwana Ahmed.

**Com. Asiyo:** Councillor, hebu kuja utuwekee sahihi hapa.

**Com. Lethome:** I wish ungekuwa na memorandum utupatie.

**Councillor Ahmed A. Barak:** Memorandum tutachapa.

**Com. Asiyo:** Lakini ungeandika ingekuwa vizuri. Enda uandike halafu utuletee.

**Com. Lethome:** Daniel Mkombe. Haya endelea Daniel.

***Inrterjections:***

**Com. Lethome:** Halafu baada ya Daniel tuweze kuwa nakina mama, nitawachokoza tena. Mnataka kuwaita kwa majina ama nitawaita. Kwa hivyo mama mwenye buibui jitayarishe baada ya Daniel.

***Laughter:***

**Daniel Mkombe:** Bwana mwenyekiti nataka kuongezea tu yale ambayo mwenzangu amesema. Mimi ni Daniel Mkombe kutoka location ya Roka. Nataka kuongezea tu yale ambayo yamezungumzwa kutoka kwa waakilishi wa Roka. Na nitazungumza kuhusu u-raia. Ni lazima raia awe mzaliwa wa Kenya wa umri wa miaka kumi na minane, baada ya tarehe kumi na moja mwezi wa kumi na mbili, mwaka wa sitini na tatu, na angalau mzazi wake mmoja ni Mkenya au amezaliwa nje ya Kenya na baba yake ni Mkenya.

Kwa kujiandikisha – registration: kwanza mke aliolewa na Mkenya. Pili, raia wa jumuia ya madola – commonwealth, aliishi kwa mda uliyoidhinishwa na awe na umri wa zaidi ya miaka ishirini na moja.

Kwa kununua – naturalization: kisheria si kwa kuzaliwa, awe ana umri wa angalau miaka ishirini na moja, awe ameishi nchini kutoka miezi kumi na miwili iliyopita au kwa uchache miaka minne kati ya miaka saba iliyopita. Awe na tabia njema na anaweza kuongea Kiswahili na awe ana malengo ya kuendelea kuishi Kenya. Pia kwa idhini ya bunge la kitaifa.

Mali ya asili: mali asili kama vile bahari, samaki, misitu na wanyama, mchanga, mafuta na maji, na madini. Hizi zote zitasimamiwa na jimbo moja kwa moja. Mapato yake au kodi kiasi cha asili mia ishirini kitapelekwa katika serikali kuu na kilichobaki asili mia themanini kimilikiwe na jimbo. Ugawaji wa gharama uondolewe katika huduma za umma nchini kote. Huduma za afya za umma zipewe watu binafsi. Kwa mfano, Kenyatta National Hospital, Coast General Hospital na mashirika mengine. Shirika la bandari libaki mikononi mwa serikali ya majimbo.

Uajiri uwe kwa asili mia themanini wenyeji wa jimbo na asili mia ishiri wakenya wengine. Kodi zote zitalipwa kwa jimbo. Kila jimbo liwe na chuo kikuu ambacho kitaandikisha wanafunzi kwa asili mia themanini ya watoto wenyeji wa hapo katika jimbo, na

asili mia ishirini wakenya wengine. Waalimu wahamishwe kutoka jimbo moja hadi lingine kulingana uajibikaji wao kikazi.

Kuna cottages za watalii. Hizi cottages zifungwe. Zinanyima serikali kuu na jimbo pesa za kigeni. Matumizi yote ya kitalii yalipwe hapa nchini badala ya mtalii kulipa ng'ambo. Watoto wa shule wasitozwe malipo katika taasisi kama vile museum au taasisi zote za kuelimisha.

Kodi za ziada za mapato kwa mfano VAT ziondolewe. Mtu akiacha kazi kabla ya miaka hamsini alipwe malipo yote ya NSSF.

Widow and child pension zilipwe mara moja mtu anapostaafu. Kuundwe board za kusimamia malipo ya fidia kuhusu watu waliopatwa na ajali na malipo yote yaliyotolewa na mahakama. Mawakili wote walipe professional fees zao kupitia board hiyo. Mawaziri wa kitaifa wawe katika daraja ya ushauri katika jimbo. Na pia kikosi cha askari tawala kivunjwe. Viwanda vyote vijengwe mashambani ambapo kuna maligafi.

Kushiriki katika utawala: mashirika yasiyo ya kiserikali yapewe jukumu fulani katika hali ya utawala. Kwa mfano, kuelimisha wakenya kuhusu mambo fulani yanayohusu kila siku, magonjwa na kadhalika. Wasiojiweza walindwe kisawa kikatiba kwa kupewa nafasi sawa ya kuelimishwa na kazi.

Jinsi ya uchaguzi: uchaguzi wote utakuwa wa moja kwa moja kwa wananchi na wa siri. Waziri mkuu atachaguliwa na bunge la kitaifa likishirikisha wabunge na majimbo. Kura ya mafungu asili mia ishirini na tano itahitajika kwa majimbo matano kwa Rais kutangazwa mshindi. Ikiwa mshindi hakupatikana, basi wagombea wa kwanza na wa pili watarudi kwa uchaguzi – runner-up. Wabunge na ma-diwani watachaguliwa moja kwa moja. Uchaguzi wote utaendeshwa na Tume ya Uchaguzi iliyo huru. Ni sharti walioshinda waeleze Tume ya Uchaguzi matumizi yao yote katika uchaguzi wao. Ni hayo tu.

**Com. Asiyo:** Ulipoanza kuongea bwana Daniel haukusema aina ya serikali ungependa iwe hapa Kenya. Ulianza na mambo ya citizenship, lakini baadaye ulipokuja hapo mbele ulisema Kenya Ports Authority iwe chini ya serikali ya jimbo. Ni kusema unataka serikali ya majimbo, maana hujasema hivyo.

**Councillor Ahmed A. Barak:** Muundo wa serikali ambayo tunataka ni ya majimbo.

**Com. Lethome:** Nina swali pia kuhusu u-raia. Umesema mwanamke aliyeolewa na Mkenya apewe uraia. Swali langu ni, kwa mfano Mkenya akioa mwanamke kutoka nje, yule mwanamke apewe uraia. Na je, mwanamke Mkenya akiolewa na mume asiye Mkenya je, yule mume apewe uraia au hapana?

**Councillor Ahmed A. Barak:** Ana haki ya kupewa uraia.

**Com. Lethome:** Haya tunamwalika mama. Mbona mpaka wasukumwe ndio wanakuja hapa, na wakija hapa wanatoa maoni mazuri sana.

**Com. Asiyo:** Wanasema maoni mazuri sana sijui kwa nini hawataki kukuja.

**Mwanajuma Ali:** Jina ni Mwanajuma Ali. Mimi yale muhimu muhimu yote yamezungumzwa hapa, lakini mimi nitaongezea kidogo.

**Com. Lethome:** Hata hayo ukitaka kuyarudia, yarudie. Kwa hivyo kitu kimoja ambacho hamjafahamu hapa kila jambo likikaririwa sana ndilo linapata watu wengi. Kwa hivyo usione kuwa usizungumze kwa sababu limezungumzwa. Tutakwenda kuhesabu. Watu wangapi walisema wataka majimbo, wangapi walisema kina mama wafanyiwe hivi. Kwa kuwa ukilikariri ndipo linapata nguvu zaidi.

**Mwanajuma Ali:** Maoni yangu mimi kwa mfumo huu wa Katiba mpya. Jambo la kwanza napendekeza hii Katiba mpya iwe itafundishwa iwe kama somo. Iwe hata wale ambao watukuwa wakiongozwa na huu mfumo wa Katiba mpya wawe wanaelewe Katiba yao ya Kenya yasema nini. Kwa sababu kama sasa kuna kina mama wengi hawaelewi Katiba ni nini wala serikali yake ni nini. Iwe itafundishwa vitabu viwekwe kwa library watu wanunue wakisoma, ifundishwe haswa mashule iwe kama somo.

La pili, kuna hii mambo ya ijara hii, waarabu yani kututoza kodi hapa. Sisi kama waafrika tuseme hapa ni kwetu, sasa kama, nitatoa mfano kidogo. Kwa mfano kama sisi wenyewe pahali tunaishi kwaonekana sio kwetu. Ukienda uangalie title deed yasema Aliwagundi Hadj Muslim Farm ndio mwenye shamba hiyo. Ukienda kwa lands Mombasa waambiwe uende ufanye search, ukifanya search yatoka hiyo shamba ni ya muarabu. Kwa hivyo mimi tayari najihesabu sina makao Kenya hii, kwa sababu pale mimi iko tayari sio kwetu. Hata ningependa hii mambo kama haya, yale mashamba yote yalichezewa mchezo na warabu, yawe tutaregeshewa wenyewe na title deed tupewe wenyewe. Manake sasa mimi ni squatter hata ile kuja kutoa maoni, nitatoa maoni gani kama mimi mwenyewe ni squatter sina makao. Sasa na kama hatuna makao na hapa ndio kwetu tulizaliwa hapa, mwarabu ndiye atutoza ushuru hapa sisi wa pale mahali. Kama hivi sasa hiyo shamba ambayo nahesabu ndio mimi nimezaliwa hapo na sina kwingine kwa kwenda. Itabidi tumtafute yule mwarabu, tumlipe kwa bei atakayo, ndio hiyo shamba iwe yetu. Kwa hivyo sasa hatuna makao hapo. Ningesisitiza sana turegeshewe wenyewe na pia title deeds zitolewe kule tuje tupewe wenyewe.

**Com. Asiyo:** Na mbona ulingojea usukumwe ndio uongee mambo hayo.

**Mwanajuma Ali:** Utumwa, wafikiri serikali ya utumwa iliisha, lakini tukijiangalia bado tuko kwenye utumwa. Utumwa haujatuondokea kabisa.

**Com. Lethome:** Hii ndio fursa ya kujiondolea, pendekeza. Kuondolewe kwa utumwa kwa njia gani? Anayeumwa ndiye husema anaumwa na mahali fulani.

**Mwanajuma Ali:** Pili twataka kama hii Kenya Ports Authority ile mali yote ambayo yaingia pale ibaki hapa hapa Pwani, sio iende huko. Kwa mfano, kama mafuta hivi. Sisi hapa mafuta yako hapo Mombasa, twanunua lita shilingi thelathini na Nairobi huko wanunua lita shilingi ishirini na sisi mafuta yako hapa. Itakuwa aje na mafuta yapitia hapa wakaunganishiwa hiyo Kenya Pipeline imepeleka mafuta huko na ni bei nafuu, na sisi hapa twanunua ghali.

**Com. Lethome:** Pendekezo, ungetaka aje?

**Com. Asiyo:** Sema tu. Wataka aje?

**Mwanajuma Ali:** Ningependekeza tupunguziwe bei tununue mafuta bei nafuu kushinda wale ambao wako mbali, wanunue wao ghali. Na jinsi watakapo nunua ile mali ibaki hapa hapa.

**Com. Lethome:** Na hiyo Ports Authority?

**Mwanajuma Ali:** Ports, kila kitu ofisi zake ziwekwe hapa. Sio vitu vije hapa vipelekwe Nairobi, mizigo ikapimwe huko waende wakapime halafu irudishwe hapa, twaja kuuziwa ghali TV shilingi elfu sita! Halafu watu wa huko wananunua kwa bei nafuu. Hiyo hatuwezi kukubaliana nayo. Vipite hapa viende vikapimwe huko Nairobi, mizigo yote ipimwe huko halafu ndio iregeshwe hapa, maanake ni ile kupeleka kule kupima kurudisha hapa ndio twanunua ghali.

**Com. Lethome:** Na wafanyikazi wa Port?

**Mwanajuma Ali:** Na wafanyaji kazi wa Port ningependelea pia mkubwa awe wa hapa na wanyaji kazi pia wawe ni vijana wetu wa hapa. Tatu, ningependelea maoni yangu mimi, ningependela hawa ma-commissioners kama ma-DC awe ni mtu wa hapa hapa. Kwa sababu DO kwa mfano, au DC, yeye akiletwe hapa kama ni mkikuyu hatajui …….. shamba imepakana vipi, imepakana vipi. Watu wanauana huku kwa sababu hajui mipaka. Lakini kama ni wa hapa atajua Mzee Mwaraji hapa amepakana na kabila nyingine na huyu amepaka na hii. Lakini unakuta watu watiana mapanga na kupigana nyuta, kwa sababu yule haielewi. Atabebwa na huyo mgiriama kwenye landrover apelekwe huko huyo mkubwa na akifika atapendekeza yule ambaye atamchinjia mbuzi na pesa ampe, halafu akiondoka huko watu wauana. Lakini kama ni wa hapa hawezi akakubali hiyo kitu ifanyike. Hatakubali kabisa watu wake wauane, ile wanafanya vile kwa sababu yule aliyewekwa mwenye wadhifa huo ni mtu wa bara. Kwa hivyo hatupendelei, mimi kama mwana Pwani, singependelea. Nataka ma-commissioners wawe ni wa hapa hapa. Nafikiri ni hayo.

**Com. Lethome:** Habari ya Pwani ya Pwani, je unazungumzia habari ya jimbo ama. Ungependelea serikali ya umoja wa kitaifa kama ile tuliyo nayo?

**Mwanajuma Ali:** Hiyo basi ndiyo ni majimbo tayari. Majimbo. Hakuna kitu kitatuokoa sisi watu wa Pwani, isipokuwa ni majimbo kwa sababu uchumi wote uko hapa na pesa hazisaidishi watu wa Pwani. Kwa hivyo mimi tayari ni majimbo hayo.

**Com. Lethome:** Sasa na mimi nikiwa mu-Maasai na ninamiliki ardhi hapa Pwani, baada ya hayo majimbo mimi na ardhi tutakuwa aje?

**Mwanajuma Ali:** Tutafanya na nyinyi kazi pamoja na utalipa vile tutakavyo. Sio kuwa twawafukuza, tutafanya kazi pamoja. Tutafanya biashara. Hatuna chuki na wao lakini tutafanya nao kazi. "Cha kaisari apewe kaisari cha Mungu apewe Mungu"

**Com. Lethome:** Na kuyapata yale ya Pwani tusema yaliyo hapa. Hiyo asili mia yote itakapopelekwa katika serikali ya kitaifa?

**Com. Asiyo:** Kwa vile mambo ya jeshi kuu, au ulinzi wa nchi, na kadhalika

**Mwanajuma Ali:** Kila jimbo kutokana na mali yake watatoa kile kiwango ambacho kitakuwa chalipwa hawa watu.

**Com. Lethome:** Sasa wewe pendekeza asili mia fulani?

**Com. Asiyo:** Kiwango gani ambacho unataka?

**Mwanajuma Ali:** Hiyo kama asili mia ishirini.
***Laughter:***
**Com. Lethome:** Ishirini kwa mia.

**Mwanajuma Ali:** Kama mimi basi hapa, si robo, robo ukiwapa pia ni nyingi.

**Com. Asiyo:** Kwa 80% ibaki hapa na 20% iende kule national government.

**Mwanajuma Ali:** Pendekezo ni nyingi zibaki hapa.

**Com. Lethome:** Themanini zinabaki na ishirini yaenda. Kina mama na utawala na uongozi?

**Mwanajuma Ali:** Kina mama na uongozi pia hatujakataa. Kina mama waongoze kulingana na elimu atakayokuwa nayo. Akituongoza tutamkubali, atuongoze vizuri. Tukimuona haongozi vizuri twabadilisha.

**Com. Asiyo:** Na hutajali kama kukiwa na mama ndiye anaongoza?

**Mwanajuma Ali:** Bora ni wa hapa, awe mama awe baba bora awe ni mtu Pwani, ndio ataelewa matatizo ya wananchi vizuri. Tumechoka watu wanauana sana, wajua.

**Com. Lethome:** Kuna lolote kuhusu polisi?

**Mwanajuma Ali:** Ma-polisi pia huwa wana maonevu sana.

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini?

**Mwanajuma Ali:** Kuhusu maonevu ya polisi, yaani kupendekeza ki namna gani?

**Com. Asiyo:** Tuseme amekushika na pombe ya mnazi kama wewe uko tu ulipewa na Mungu vile watu wamepewa umeenda kuandikisha.

**Mwanajuma Ali:** Kwa mfumo wa Katiba mpya ama kwa sasa.

**Com. Lethome:** Kwa mfano wewe Mwanajuma ukikutana na polisi pale amekudhulumu, amekuambia utoe kitu kidogo la sivyo akuweke ndani, utamlalamikia nani kwa sasa?

**Mwanajuma Ali:** Sina wa kumlalamikia.

**Com. Lethome:** Wapendekeza nini?

**Com. Asiyo:** Kwa nchi zingine sasa za kiafrika hata za . inaudible, wanakuwa na maofisi kama zile wanaitwa ombudsman, kama Tanzania tuseme, ambapokama mtu akidhulumiwa anaweza kwenda akapeleka file yake, kwa maana kupeleka kwa yule mkubwa ni mkubwa wa yule jamaa, pengine hawezi kusikiza vizuri. Kwa hivyo unaweza kwenda, lakini hapa kwetu hatuna.

**Mwanajuma Ali:** Tungependekeza basi kuwe na ofisi ya kuwa ukishikwa kama hivyo wapitia pale kwanza, wayaeleza malalamishi yako ili wale waweze kututetea. Haya na lingine la mwisho kabisa ni hawa ma-sub-chief na ma-chief, wasiitwe

kwenda kufanya interview. Tuwapigie mlolongo nyuma.

**Com. Asiyo:** Yaani wachaguliwe na wananchi.

**Mwanajuma Ali:** Tujachugue sisi wenyewe wananchi maanake ndipo tutajua pengine chief atachaguliwa haelewani na familia nyingine. Mtu hawezi kwenda akamhudumia vile inavyotakikana. Lakini awe wa hapa hapa. Wasimamiwe mlolongo kama zamani vile ilivyokuwa.

**Com. Asiyo:** Mama ulikuwa na fikira safi na unakaa nazo tu.

**Com. Lethome:** Kina mama wa Pwani inaonekana hawataki kuongea. Haya Councillor Haji, karibu.

**Councillor Mwinyi Haji:** Mimi naitwa Councillor Mwinyi Haji kutoka Roka, mimi ni majimbo tayari. Kwa lile ambalo ninazungumzia hivi sasa shida moja ambayo inatupata sisi bwana ni wale ambao tunaishi karibu na msitu. Tuna shida ya ndovu. Wanyama wanatuingilia, wanatulia mimea yetu, halafu hakuna sheria ambayo inalinda wananchi kama wale. Ni kwamba sasa sheria ambayo iko ni mwananchi akifa, analipwa shilingi elfu thelathani. Mtu ambaye atapata kilema kwa pengine mamba amemtafuna ni shilingi elfu moja, ambayo hiyo ni kitu cha chini. Mimea hailipwi kabisa. Muundo wa kiserikali hivi sasa inavyosema ni kwamba wanataka kuondosha umasikini. Sasa ikiwa mumea kama mnazi unachukua umri wa miaka saba na ndovo aje auangushe, ni kama huyu mkulima umefanya maskini. Kitu tunasema mwananchi akifa zile pesa za chini atakazolipwa si chini ya milioni moja. Na kama atadhurika na kiungo chake kitadhurika, pengine aumwe na mamba mguu uende, hicho kiungo kiwe kitafanyiwa takmini na atalipwa kulingana na kiungo chake. Kwa sasa tunapata mbunge akiumia pua, kuna insurance itamlipa. Akiumia ukucha, insurance itamlipa, lakini mtu ambaye ameumwa na mamba mguu umekatika analipwa elfu moja tena athibitishe. Mimea ambayo imeharibiwa ifanyiwe takmini ipigwe, pesa zake zijulikane, mkulima alipwe, umasikini umuondokee. Hivi ndio inafanya ofisi hizo za serikali kwa vile wanajua hawatakikani kulipa vitu kama hivyo. Ndovu kama hao wanawaachilia na mambo mengine.

Jambo la pili, sisi wananchi tunaona maovu ambayo yanafanyika na vyombo vya serikali. Ufisadi umekuwa mwingi, na ufisadi ndio unaua nchi. Sasa kama ni ufisadi kuwe na kitengo hicho cha ombudsman. Kiwe mwananchi wa kawaida anaweza kupeleka lalamiko lake lolote kwa hicho kitengo, tena kiwe independent kiasi cha kwamba iwe waweza pia kushtaki, kuchukua hatua ya yule mtu ambaye atakwenda kusema kule. Kama ni askari wa traffic ameangushiwa shilingi mia, hiyo road block mwananchi wa kawaida aende akaseme, na ifikie hapo wale watu waende wakachukue uchunguzi, na akipata ni sawa, wamshike huyo mtu ambaye anafanya ufisadi.

Jambo lingine, mashirika ya kiserikali yote yote yasibinafsishwe. Utapata mashirika ya kiserikali yanabinafsishwa na mwisho unapata wale wanaobinafsisha ni watu wawili, watatu. Unapata kampuni mbili, tatu, ndizo zimechukua KPA na ni za watu wakubwa. Ndio wamechukua posta, ndio imechukua mambo yote. Kama ni shirika za kiserikali linataka kubinafsishwa, hiyo

serikali irudi kwa wananchi, waje wawaambie wananchi kwa nini wanataka kubinafsisha hilo serikali, ili wapewa idhini ya kubinafsisha hilo shirika.

Mimi husitikita sana msichana wangu ametungwa mimba na mvulana shule, halafu yule msichana aende nyumbani akae, yule mvulana bado abaki shule anasoma. Mimi ningesema kama msichana atakuwako yuko nyumbani amekaa na anaangalia mimba yake, na yule mvulana naye kiasi kile kile akae huko kama sheria mpaka kama msichana atarudi shule na yeye aruhisiwe kurudi shule. Lakini sio umharibie msichana, msichana wangu namlipia fee amefika form four, atungwe mimba, mvulana aachwe aendelee kusoma, msichana wangu amebaki nyumbani, nasikitika. Na yule mvulana naye abaki kule nyumbani, kwa sababu wamekubaliana amemtunga mimba na imedhiirika ni kweli, yeye abaki kule nyumbani yule msichana wangu yuko huko na yeye naye adhabu ile iliyompata miezi tisa naye abaki kule. Ile sehemu ambayo anakosa yule msichina wangu, na yule mvulana naye akose. Msichana wangu nikimrudisha naye arudishwe, kama sikumridisha naye asirudi.

**Com. Lethome:** Na gharama za kumsimamia yule mtoto?

**Councillor Mwinyi Haji:** Amsimamie. Gharama ziwe, mtoto akizaliwa kama tutakubaliana amuoe, amekataa amsimamie huyo mtoto. Haiwezekani apelekwe katika sheria na afungwe miaka mingi sana.

Mimea yetu hasa Pwani imekataliwa kwamba si mimea ya kifedha. Ndio nafakiri imeachwa haishugulikiwi. Hizi sasa sisi tuna kila mumea ambao ni wa kifedha uko na board. Tuna Sugar Board, kuna Sisal Board, kuna Coffee Board, kuna Pyrethrum Board, lakini hakuna Mnazi Board, hakuna Mkanju Board, hakuna Maembe Board, hakuna Mkilifi Board na yote hii inatengeneza sabuni na kila kitu. Kitu tunaomba kuwe na Board ambayo itakuwa inasimamia mnazi, iwe na Board ya kusimamia korosho, kuwe na Board ya kusimamia mkilifi, maembe, ili wawe wanaweza kufanya research. Kama korosho haitoki ni kitu gani watafanya ili korosho itoke. Ni kitu gani kitafanyika mnazi utoke, lakini sio kwamba ile mimea kule ndio hiyo imebaki kule.

Nasema kina mama wa Kilifi wamekuwa wapole kutoka kuzungumza. Viti vya uongozi katika ngazi zote wapangiwe asili mia thelathini akina mama wapewe. Awe anaweza, aweze akubalike aingie, kwa sababu hivyo vyeo ni nafasi asili mia thelathini. Uongozi wowote maslahi ya kina mama yawe yanazungumzwa na wale asili mia thelathini, katika ngazi zozote za hayo majimbo. Kama tunaanza na village, location, kokote mpaka ngazi ya jimbo kuu. Hata mpaka serikali kuu, kuwe na asili mia thelathini ya kina mama wamepewa. Hizo ni seats zao wawe watazitumia vile wanavyoweza.

Umilikaji wa ardhi: tatizo ambalo liko ni umilikaji wa ardhi. Utapata kuna mwananchi ana hekari elfu ishirini, hekari elfu hamsni. Yeye yuko nazo yeye pekee yake. Hata kwingine mpaka wake hakujui. Tuwe na kiwango cha mwananchi wa Kenya awe atakuwa anaweza kumiliki ardhi, mpaka kiwango cha chini tuseme hekari mia tatu, ukizidisha mia tatu na moja, hiyo moja irudi kwa jimbo.

***Interjections:*** *Mia tatu?*

**Com. Lethome:** Jamani maoni yake. Chungeni masharti tuliyoweka asubuhi bwana, za sheria natoa "red card" saa hizi hapa.

**Councillor Mwinyi Haji:** Na ardhi zote ambazo tunasema ambazo zimezidi kwa sasa. Wale ambao wako na zaidi ya hekari mia tatu, yale majimbo ambayo ardhi hizo ziko, hayo majimbo yachukue hizo ardhi wagawanyie wananchi ambao hawana ardhi. Umiliki wa ardhi katika kutoa title deed, maoni yangu ni kwamba title deed ya Kenya iwe absolute, isiwe na masharti mengine yeyote: lease, nini, ina kitengo gani, ina nini, isimfunge mwananchi ambaye atapata ardhi. Utapata title deed hivi sasa mwananchi amepewa, lakini imekuwa charged mpaka kwa hao watu wa mashamba Settlement Trust Fund wame-charge. Mwananchi ana hicho chombo lakini bank haiwezi kuchukua hicho chombo, kwa sababu imekuwa charged na iko na hiyo lease mpaka amalize hizo pesa. Akipewa title deed apewe absolute na haina matatizo yoyote. Aweze kuifanyia vile anavyosikia.

Mwisho nasema kiwango cha kusoma. Wako wenzetu wamekuja wakasema, wakazungumza. Tumekuwa na shida na kiwango cha kusoma hasa kwa ma-diwani. Wewe ni diwani uko katika panel ya interview ya kumuandika mfagiaji ambaye unataka D+, wewe ni diwani huna hata O+.

**Com. Lethome:** Pendekeza kiwango cha elimu.

**Com. Asiyo:** Eleza sasa.

**Com. Lethome:** Kiwango gani cha elimu?

**Councillor Mwinyi Haji:** Kiwango cha elimu 'O' level iwekwe pale, at least yule unayemtihani ni mfagiaji unataka D+, wewe ni diwani huna hata, uko standard eight hapo. Sasa yule ni mfagiaji, atakuja wewe anakusalia mi "mheshimiwa habari", lakini amekupita kwa kiwango cha elimu, na ulikuwako hapo, hata akianza kusema kile kizungu wewe unakuwa basi wewe ukisha pita.

**Com. Lethome:** Endelea, ninakupa dakika moja umalize tafadhali.

**Councillor Mwinyi Haji:** Mimi nafikiri nimemaliza, wenzangu watakuja watwange saa zaidi. Asante.

**Com. Lethome:** Asante. Naona viongozi wenu pia wanatoa maoni na tunashukuru sana. Haya tunaendelea, Reynold Mwangunya. Halafu baada ya Reynold, huyu mama hapa aliyejifunga kanga atazungumza, atakuja baada ya Reynold. Lakini mama wengine mkae tayari, nitawaaita mmoja mmoja.

**Com. Asiyo:** Hata vijana pia, youth, vijana pia nao hawaongei.

**Com. Lethome:** Haya sawa.

**Com. Asiyo:** Wazee.

**Com. Lethome:** Haya Reynold endelea.

**Reynold Mwangunya:** Bwana mwenyekiti mimi jina langu naitwa Reynold Mwangunya, ninajiwakilisha mimi mwenyewe, pia nawakilisha maoni ya District Povertry Eradication Committee. Kuna mwenzangu aliyetangulia kusema hapa kuhusu elimu. Tumeambiwa kwamba kwa sababu ya ukosefu wa elimu, watu wengi hawakuweza kuja kuhudhuria mkutano wa maana kama huu. Mimi ningependekeza jambo la kwanza kabisa. Kuondoa ukosefu wa elimu Kilifi, elimu ifanywe bure na lazima mpaka darasa la kumi na mbili, ili tuondoe shida hii ya watu kutoelewa.

Bwana mwenyekiti ningependa nipendekeze kuhusu wajumbe. Mara nyingi tumechagua wajumbe ambao hawakutekeleza wajibu walioupewa na wananchi. Wajumbe kama wale wana hakikisho la kukaa kwa miaka mitano, raha mstarehe. Mimi ningependekeza kwamba wajumbe ambao hawatafanya kazi zao kutegemea na wananchi wanavyotaka, waweze kuitishwa nyumbani kwa asili mia ya ishirini na tano ya wale waliompigia kura. Waregeshwe ili waje watafute mandate nyingine.

Ningetaka nipendekeze kitu fulani kuhusu kazi na uajiri. Kuna mtindo ambao kwamba umeendelea kwa miaka mingi labda tangu Kenya ianze, kwamba mtu mmoja anaweza kusimama kule bunge au katika wizara na aseme mgomo fulani si halali. Na watu wale wenyewe wanatafuta haki zao, lakini waziri akasema hiyo si halali, mgomo huo si halali. Mimi ningependekeza kwamba, wakati shirika au chama chochote, au wafanyaji kazi wanapogoma, bunge liitwe hata kama liko kama liziko, liitwe na lijadili mgomo ule. Kukiwa kuna uhaki wowote bunge lipitishe kwamba hatua ya kuwasaidia wafanyaji kazi wale ichukuliwe na serikali. Kwa hivyo waziri asiwe na uwezo wa kikatiba wa kutangaza mgomo, kwamba si halali.

Ufisadi ni kitu ambacho kimekula maisha ya wakenya wengi. Tumeona katika nyakati fulani kwamba mtu fulani anaweza kutajwa kwa ufisadi, katika gazeti pengine, na hatachukuliwa hatua yoyote. Mimi ningependekeza kwamba kiongozi yeyote wa serikali, anapoandikwa katika gazeti kwamba yeye ni mfisadi, mara moja serikali ichukue hatua ya kumuachisha kazi, uchunguzi ufanywe, na kila kitu alichokipata kwa hali ya ufisadi kiregeshwe kwa serikali, hata akiwa ni nani.

Maendeleo ya nchi yetu yamepewa kikundi kile kinaitwa DDC. Kama wasemaji wengine walivyosema DDC chairmen ni ma-DC ambao mara nyingi huwa sio watu wa sehemu zile. Kwa sababu hawaelewi maisha na madhumuni ya wananchi wa sehemu zile, huwa hawajali. Mimi ningependekeza, bwana mwenyekiti kwamba, Katiba mpya ianzishe mpango mpya wa DDC, ambapo mwananchi kuingia katika kamati ya DDC ni achaguliwe, ili tupate viongozi ambao watajali maslahi yetu.

Uchaguzi wa bunge na kadhalika: kuna kamati ambayo imechaguliwa ili kuendeleza mambo ya uchaguzi hapa Kenya, lakini kamati ile haina uwezo. Utakuta kwamba mgombeaji fulani anaweza kuchukua sheria mikononi mwake hata akamuua mpinzani wake, na kamati ile haiwezi kumshtaki yule mtu aliyefanya ubaya ule. Mtu yule mara nyingi huachwa huru. Mimi ningependekeza kwamba kamati ya uchaguzi ipewe uwezo, na kadhalika iweze hata kushtaki inapoona mgombeaji wa kiti chochote amevunja sheria. Mara nyingi mwananchi hana mahali pa kupeleka malalamiko yake, akienda kwa chief, chief anaweza kumviringa, akienda kwa polisi, polisi wanaweza kumviringa. Mimi ningependekeza, bwana mwenyekiti kwamba, kuwe na ofisi kamili, na iwe katika kila wilaya na hata ikiwezekana katika kila division, hata location, mahali ambapo mwananchi anaweza akaenda na akapeana malalamiko yake, na hatua ichukuliwe. Mengi nimeyaandika katika Memorandum yangu, na ninata waachia. Hayo machache asanteni.

**Com. Lethome:** Haya mama karibu, nafasi ni yako sasa. Jina lako?

**Com. Asiyo:** Haya mama tueleze jina lako.

**Kadhis Catherine:** My burning issue is kuna wakati mwingine wazazi wanatukosea. Utakuta atakuoza, na wakati ule atakuoza atachukua mahari na pengine hatachukua nyingi atachuka kama elfu saba. Lakini akichukua zile elfu saba, kuna wakati pengine mtakuja mkae na yule bwana pale nyumbani. Lakini wakati ule utakuwa na yule bwana atakinena, atasema "after all mimi sina haja na wewe. Kwanza wewe hata si chaguo langu, sikuwa natazamia kuwa niolewe na wewe, kwa hivyo hiyo ni kazi yako. Utarudi ukae. Mwambie baba yako alete mahari, hataleta basi kaa namna hii". Sasa wewe utakuwa in "suspense", uhuru hapo hutakuwa ukipata, raha hapo hutakuwa ukipata, hata utafukuzwa hapo nyumbani. Na wakati ukifukuzwa pale nyumbani, utaambiwa nenda ukae nyumbani utulie kwa babako, vile amekuzaa amekuzaa. Pengine kutakuwa na sababu hapo, itatokea wakati ambao utakuwa yuko kazini, lakini sasa wakati ukifika kazini kwake ukakute mwanamke mwingine yuko juu yake, sasa hapo wanafanya mapenzi yao. Sasa vile alikuwa akikuelezea kuwa wewe mwenyewe hasa alikuwa hana haja, sasa ukimuuliza anasema after all huu ni mke wangu, nilikuambia mimi sina haja nawe. Sasa pale kama nilivyotangulia hapa na yule mwingine alipopitia hapo, Esther Kacho, akasema kuwa kuna haki ya malu katika kimila. Ukimshika namna hiyo, utakuwa unasikia kitu chakuuma katika maishani mwako, kwa sababu utakuwa unasema huyo ni mume wangu. Sasa yeye pia atakuwa anasikia kitu kingine katika maisha.

**Com. Lethome:** Sasa ungependekeza kitu gani?

**Kadhis Catherine:** Sasa mimi ningependekeza pale ndani, kama nikuulizwa chochote makosa pale ni yeye alipe.

**Com. Lethome:** Alipe malu?

**Kadhis Catherine:** Eeh alipe ile malu. Kwa kuwa nitakuwa nasikia kitu kinanikera.

**Com. Asiyo:** Lakini mama kuna swali mimi pia nataka kukuuliza. Kama mzazi wako ndiye alifanya mpango uolewe na mtu, na wewe hukupeana consent yako, yaani ukiwa huyu mzee hukukubaliana naye kwamba uolewe naye, ilikuwa mpango wa baba pengine mpango wa wazazi, na umeenda umekaa na huyu mzee, ndivyo unasema? Halafu anakuacha anachukua mwingine, ndiyo hii unasema? Ungesema kwamba ingekuwa vizuri saa ile unaozwa kuwe na registration ya kusema kwamba sasa huyo amekuoa na kuwe na certificate, hata kama sio ya kanisa.

**Kadhis Catherine:** Hakuna certificate, inakuwa tu hivi hivi.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo ingekuwa vizuri kuwe na certificate ya kuolewa hata kama ile ya kinyumbani, ili ijulikane kwa kweli huyu mzee amekuoa, amelipa hiyo shilingi saba uliyosema?

**Kadhis Catherine:** Certificate ya nyumbani ya kimila ndio wako nayo, lakini hiyo ya nini hakuna.

**Com. Lethome:** Na katika hiyo ndoa ya kimila, hii ni ya yule mwanamke mtakutana ama analazimishwa ama huwa ni kwa hiari yake. Huwa anashauriwa yeye anakubali ama inakuwa aje?

**Kadhis Catherine:** Kulazimishwa hawalazimishwi. Wakati mwingine wakifika nyumbani wakalima pengine kunde hivi.

**Com. Lethome:** Aka?

**Kadhis Catherine:** Akalima kunde pale nyumbani. Sasa mtu kama huyo ndio sijui kama ilikuwa ikichukuliwa namna gani.

**Com. Asiyo:** Nikisema yeye ameolewa lakini hana na uwezo wa kusema kama anampenda huyu mzee au hampendi. Huyu bwana amepeana mahari. Sasa nataka kukuuliza hivi, ungependelea njia kama hizi za ndoa ziwekwe registration ndio ijulikane kweli huyu alikuwa ameoa au ameolewa?

**Kadhis Catherine:** Sawa ni registration vile mumekubaliana kwa sababu kuna wakati, hata kwa wakati huu, yule mwenyewe sasa ambaye tulikuwa namna hiyo, yuko. Kuna wakati mwingine ambao ilikuwa tarehe ishirini na tano disemba. Sasa hapo kulikuwa na mvulana mwingine pia yuasema huyo siwezi shikana na yeye. Yeye ni mume wako, ukipenda atakuoa asipokuoa basi yaishe, mimi nitakuwa na mambo yangu.

**Com. Asiyo:** Na umesema vizuri.

**Com. Lethome:** Haya asante mama tutaangalia.

**Kadhis Catherine:** Kwa hivyo the second point ni hivi. Kuna wakati mwingine katika makanisa yaani huwa kuna uhuru,

lakini katika wale ambao mtakuwa wawili, kama kwingine waenda kanisani na mwenzako bado haendi kanisani, itatokea wakati ambao atakuambia huna wakati. Kwa hivyo chukua panga twende tukate miti, tuchukue miti mistuni kwa kuwa hapa unajenga nyumba. Sasa vile najenga hii nyumba hapo twende mitini kama saa tatu. Sasa huo kwa kumtii utamheshimu utaenda na yeye. Sasa ukienda na yeye kule msituni kule ndani sana, ataenda akakugeukia atasema "ah mimi leo nitakumaliza. Vile nitakumaliza hiyo ni kazi yako. Utanijulisha yule ambaye kule kanisani unaenda kuzungumza na nani?" Wewe hasa unaambiwa yule pastor hasa ni mumeo, kwa mfano sasa. Sasa hapo atachukua panga vile ameliinoa vizuri na kila kitu na kuchama chama, piga magoti uombe msamaha leo nakuua. Sasa unaona?

**Com. Asiyo:** Tumesikia.

**Kadhis Catherine:** Sasa hapo kama hakuna uhuru pia..

**Com. Asiyo:** Kwa kuabudu Mungu?

**Kadhis Catherine:** Eeh kwa kuabudu Mungu.

**Com. Asiyo:** Tume shukuru sana, mama.

**Com. Lethome:** Peana jina lako pale, tuna shukuru kwa maoni yako mazuri. Kasiwa, Kasiwa? Na baada ya hapo tunampata mama mwingine.

**Com. Asiyo:** Tupatie jina.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Kwa majina naitwa Emmanuel Kasiwa Ngala. Mimi ni mwenyekiti wa chama cha Shirikisho (SPK) Kilifi District, wilaya ya Kilifi.

**Com. Lethome:** Una memorandum?

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Nimeletea Commission memorandum ambayo ina maelezo yote yanayohusu hiyo Katiba ya sasa, ambayo tumeiweka kwa urefu sana. Kwa hivyo singependa sana kurudisha lakini pengine ni gusie gusie kidogo katika ile first round.

**Com. Lethome:** Haya gusia.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Ule msingi, serikali yetu ni ya majimbo by the way.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Pengine nitarudia. Kwa majina naitwa Emmanuel Kasiwa Ngala, mimi ni mwenyekiti wa chama cha Shirikisho cha Kenya (SPK). Nimesema kwamba tumefanya mapendekezo yetu hapa Kilifi, na yapo katika memorandum, kwa hivyo nitaitoa hii memorandum baadaye, lakini tu labda kugusia gusia kidogo, ikiwa nitaruhusiwa.

**Com. Lethome:** Utaruhusiwa.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Kenya ni muungano wa watu wa jamii mbali mbali zenye tofauti ya kihistoria na kiutamaduni. Kabla ya kuja kwa utawala wa mkoloni, watu wa-Kenya waliishi kwa vikundi vya ukabila, ingawaaje kila jamii ilifurahia siasa, utamaduni, dini, na kujitegemea ki-uchumi na mambo mengine. Hata hivyo walijumuika na kushirikiana pamoja katika mambo mengi, hasa kwa nyanja za biashara, uchumi, kuoana na kujilinda na adui zao na pia wakati wa maafa. Alipokuja, huo ni mda ule ambao tulikuwa hatujakuwa katika utawala wowote. Baada ya kuja mkoloni, mkoloni alitambua jambo hili.

**Com. Lethome:** Bwana Emmanuel, ngoja kidogo. Mimi naona muda huu uutumie kupendekeza.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Ndio hivyo najenga ule msingi, ni kidogo sana.

**Com. Lethome:** Tuyagange yajayo.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Nafikiri ikiwa tutaharakisha wakati ile purpose to be defeated, itakuwa hakuja haja.

**Com. Lethome:** Wajua ni nini, tumekubaliana asubuhi lakini nafikiria haukuwako bwana Emmanuel, tukasema huu mda tunaokupa ukianza kuzungumzia habari ya historia yetu, haitatusaidia.

**Com. Asiyo:** Utakosa kupendekeza.

**Com. Lethome:** Watu hawa wataweza kuzungumza, tunataka mapendekezo, pendekeza, pendekeza.

**Com. Asiyo:** Juu ya Katiba mpya.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Okay. Asante. Sasa nafikiri kama nilivyosema nilikuwa nimegusia katika vipengele vyote vya sheria, pengine nitapitia tu yale ambayo tumependekeza.

Katika executive of government tumesema kwamba the present Constitution awards too much power to the President. Tukapendekeza kwamba, we propose that the new Constitution should limit the powers and duties of the President, as

follows:-

He will be the Head of State and the symbol of Kenya's sovereignty in the relations with other nations.

He shall be the Commander-in-Chief of the Armed Forces and may declare war against any aggressor Nation with the advice of the Senate.

The Federal President will represent the country in its international relations and will conclude treaties with other nations on its behalf.

He shall also accredit and receive envoys.

The Federal President will have powers to nominate members of the Cabinet, Federal Judges, Federal Civil Servants and the commissioned and non-commissioned officers of the Armed Forces. However, the President's nomination shall be subject to confirmation by the Senate, although he may have power to nominate, he is denied powers to dismiss. Atakuwa hawezi ku-dismiss. This power is vested on Parliament. The advantage of this arrangement is that it may discourage the current practice of appointing kinsmen, friends or relatives to national positions. It will also protect officers appointed on merit, from the fear of being dismissed from office, if they do not follow the details of the incumbent President.

The Federal President personifies the country's political unity in a special way. He is the link between all elements in society, regardless of party distinctions. Although his tasks are mainly on a representational nature, he can exercise considerable personal authority through his neutral mediating functions. By comumenting on the fundamental aspects of current issues he can rise above general party's political controversy and set standards for public political and moral guidance.

The Federal President will have powers to sign bills into legislation. He may vetto legistration if he reasonably believes such a vetto is in the interest of the federal country. However such a bill shall become law if it is vetted by two-thirds majority of both Houses. In the event of two-thirds majority of both Houses, then the House has not bee attained then the bill will fail, will be defeated.

The Federal President shall be elected together with the Vice President as his running mate for a term of four years, but he shall not be eligible to serve for more than 2 terms.

**Com. Asiyo:** If you have already put that on paper, peana zile headlines.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** I wanted to say the President, then the rest. This was important. Okay.

***Interjections:***

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Upande wa ardhi, we propose that ultimate ownership should be in the hands of the individuals and in some cases, communities.

**Com. Asiyo:** Individuals …

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** In the hands of individuals and in some cases communities. Niendelee au niwache?

**Com. Lethome:** Mimi naona ukikabidhi hiyo memorandum.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Ndiyo hiyo lakini nilikuwa nasema kwa faida ya wenzangu. Kwa hivyo kama hivyo ndivyo munavyotaka.

***Interjections:*** Wasoma kizungu.

**Emmanuel Kasiwa Ngala:** Ooh, samahani. Kama hii nilikuwa ninasoma Kiswahili.

**Com. Lethome:** Sema jina lako halafu uendelee. Basi tusikizaneni hapa tumsikize huyu mama tumpeni nafasi. Anza kwa jina lako mama tuendelee. Una memorandum? Una memorandum ama utazungumza?

**Councillor Amina Kisasa:** Nitazungumza kidogo in short, halafu niko na memorandum nitawapa.

**Com. Lethome:** Haya.

**Councillor Amina Kisasa:** Kwa majina naitwa Councillor Amina Kisasa kutoka Junju location.

(a) Mwanzo nitaanzia upande wa uraia. Tunakuta kuwa upande wa sheria ya uraia wananchi wa Kenya hasa upande wa kina mama tunapata taabu sana. Utapata mwanaume akipata kama ni mwanamke wa kizungu beach, akitaka kumuoa inakuwa kwake si tatizo. Lakini mama wewe utakuwa hapa pengine umepata mwanaume ametoka ni Uganda, ni Tanzania ama hata mzungu,utatiliwa vikwazo kweli kwenye sheria. Tungeomba serikali yetu ichukulie haki ya uraia kwa mwanamke na mwanaume kuwa sawa.

(b) Upande wa vitambulisho: watoto wetu wanapata taabu sana na vitambulisho. Mimi nafikiri vitambulisho ni vya

kufanya mwananchi awe mwananchi. Utapata mtoto hana pengine baba, mama akienda kule ataambiwa aende akalete birth certificate ya nyanya. Nyanya zetu walikuwa hawana birth certificate. Mtoto yule atahangaishwa leo nenda, rudi mpaka mwisho ataishiwa na nauli ataamua anakaa. Serikali ingefanya kama wakati wa likizo, watoto wote wale wanamaliza vidato vya nne, wawe wanaenda kwa ma-chifu, wazee wawekwe pale wanajua huyu ni mtoto wetu, watoto wote wapewe vitambulisho kwa jumla. Wanajua kama pengine baada ya miezi mitatu kutakuwa kunatolewa vitambulisho, ili watoto wawe hawapati taabu ya vitambulisho sana.

(c) Jambo jingine kuunganisha na hapo. Utapata wasichana wakiwa "chotara" pengine amezaa na muarabu. Msichana akienda pale atahangaishwe kweli kweli. Tuko na cases nyingi za wasichana ambao wanaonekana ni half-cast, lakini hawazungumzi hata kigiriama. Amezaliwa, nyanyake ana handa pengine ametoka Richaka Umbu. Msichana yule pengine utapata leo hawana vitambulisho kabisa na ni wananchi wa Kenya iko thibitisho, chifu yuajua, utapata kuna vetting. Vetting officer ni mjaluo ametoka bara, anamuhangaisha yule mtoto, karatasi ikija inaandikwa red, iende, irudi. Tungependa upande wa vitambulisho iwe hata kama ni skuli mtoto akifika form four, viwe vinapelekwa skuli watoto wote wanapata vitambulisho. Na wale ambao hawakujaliwa kusoma pia isiwe ni tatizo kwao.

(d) Muundo wa serikali mimi ningesema tungependelea serikali ya majimbo.

(e) Vyama vya kisiasa: vyama vya kisiasa ninapata vinakuwa vingi mpaka vinatuletea matatizo. Tunaishi-lia kuchagua mtu ambaye hatukumtegemea wala kumtarajia. Kwa kuwa kila chama kinasimamisha mtu wake, kinasimamisha mtu wake, pengine kuna mtu ambaye angetufaa kwenye chama fulani, lakini kwa vile vyama vimekuwa viingi sasa, imekuwa ni vurugu na tatizo na mwisho twabakia twachagua watu ambao hatukutegemea.

**Com. Lethome:** Kuhusu vyama?

**Councillor Amina Kisasa:** Kuhusu vyama nimependekeza katika memorandum yangu, tungekuwa na kama vyama vinne tu vya kisiasa.

**Com. Asiyo:** Na independent candidates?

**Com. Lethome:** Na wasiotaka kujiunga na chama chochote?

**Councillor Amina Kisasa:** Wasiotaka kujiunga katika vyama vile vinne, sidhani kama, kama zamani kulikuwa na KANU na KADU. Si ilikuwa vyama viwili, lakini unaangalia wapi inakufaa. Vilikuwa viwili.

**Com. Lethome:** Habari ya independent candidates – wakubaliwe, wasikubaliwe? Ukitaka kusimama na huna chama?

**Councillor Amina Kisasa:** Hiyo itatuletea matatizo sana. Kibinafsi mimi, naona hiyo itatuletea shida. Kila mtu angesimama kivyake, ndiyo yale ninalokataa tangu mwanzo kwao vikiwa vyama ni vingi ama watu ni wengi inakuwa ni matatizo.

(f) Mahakama: nimesema katika mahakama mwananchi asiwe na uwezo siku zote anakuwa anaonewa. Kuna mambo mengi yanayotendeka katika mahakama, ambayo mwananchi wa chini anaumia sana. Kuwe na sheria ambayo upelelezi zaidi ufanywe katika mahakama yetu ya Kenya. Unaweza kuwa mwenyewe umeenda kortini kusikiza kesi, ukaona hiyo kesi kabisa mtu anadhulumiwa, lakini mahakama ikatoa vingine na huwa hakuna budi. Pengine kukata rufani ni pesa tena, yule mwananchi wa chini huwa hana pesa ya kukata rufani, unatoka pale unabaki unaomba Mwenyezi Mungu wako tu akusamehe, basi mambo yanaishia hapo.

(g) Halafu nimesema upande wa dini ya kiislamu, tungeomba wamama waislamu wakafiwa na wanaume wapewe ruhusa ya "eda" ya mieze minne na siku kumi iwe ni leave ambayo itaeleweka Kenya nzima. Baada ya mwanamke awe anajifunga maninja atoke akienda kazini, iwe ni leave kama vile maternity leave. Mwanamke akifelewa na mume iwe itaeleweka awe anapewa miezi minne na siku kumi akae eda mpaka amalize eda.

(h) Upande wa ndoa, tunapata sana sana kina mama tunatatizika baada ya kina baba wakitukataa. Utakuwa umechuma na mwanaume mumenunua mashamba, mko na mali, mko na watoto, mwanaume siku ameamua hakutaki atakwambia toka, nenda. Vile vyote mlivyochuma vinabaki wewe huna lolote, huna cha kupata kutokana na pale. Tungeomba, mwanaume asiwe ana achana na mwanamke, serikali yetu iwe kuwe sheria. Mali wanaochuma kuanzia pamoja igawanywe sawa kwa sawa, kila mtu achukue nusu yake akaangalie zake mbele.

(i) Haki za ardi: tumepata kuwa katika haswa location yangu ninayokaa ardhi kubwa inaenda kupewe mtu mmoja na wananchi wengi utapata wanatatizika, ndio jambo hili la squatters bado laendelea. Kuna waliokuwa mbele yetu katika serikali wakiwa na vyeo vya juu, wamechukua maeneo makubwa makubwa, sana ya mashamba ya Pwani. Wananchi wa Pwani tunateseka. Utapata karatasi ya haki ya ardhi inatoka Nairobi. Mtu anakuja na karatasi kutoka Nairobi anakuja mahali mtu amekaa pengine miaka ishirini, hajajua njia tu za kutafuta usawa wa ile shamba. Unakuja kuambiwa utoke hapo, mtu amekuja na karatasi. Na sheria inachukuliwa kuwa mwenye karatasi ndiye mwenye haki. Kabla ya mwenye karatasi hajapewa haki, serikali iwe itachunguza kwanza yule mwananchi aliye pale amekaa kwa muda gani. Kwa hivyo ningependekeza, mwananchi akiwa amekaa kwenye ardhi zaidi ya miaka kumi, ardhi ile iwe itakuwa ni yake bila mapigamizi yoyote. Kwa kuwa ile miaka kumi mtu atakuwa yuko hapo, mpaka aje akuondoe wewe ambaye umeishi miaka ishirini au thelathini, akija akidai sehemu ile ni yake. Na utapata watu wetu wanadhulumiwa inabidi mtu yule, mama mtu mzima pengine amefelewa hana njia, yabidi aondoke amwache yule aliyekuja na karatasi kutoka ofisi, hata mara ingine hajui, anapitia kwa chifu. Chifu ndio aende akamtaftie hiyo mahali, basi ni hapa na pana watu tayari. Wananchi tunapata taabu sana.

(j) Sheria za ma-chifu za magogoni: ikiwa hii kesi za magogoni ni ziendelee, tungependelea ama tungeomba kuwe na wanawake sawa na wanaume kwenye hivi vikao vya magogoni vya ma-chifu. Unapata mwanamke anaenda pale, wanaume watu wazima wamejaa ishirini, thelathini, mama yule hata hajui ajieleze aje, pengine ana kesi yake matatizo ya nyumbani na mume, yabidi aeleze wazi kwenye hadhara, mpaka mwisho mengine yanamshinda kusema. Unapata mume yule anapewa haki, mwanamke anakosa haki yake kwa kutoweza kujieleza ile usawa.

(k) Mapato na mishahara ya wabunge: tunaona wabunge wetu wanapewa pesa nyingi sana sana. Ikiwezekana, wakatiwe mishahara yao nusu wanavyopata sasa, ili mwananchi mwingine awe atafaidi. Mwananchi ambaye hana kazi, tuseme vijana wetu ambao hawana kazi, kuwe na kiwango fulani cha mshahara, ambao mwisho wa mwezi huenda kuchukua ili kupunguza uhalifu wa nchi hii.

**Com. Lethome:** Haya mama sikilizeni nitakupa nafasi ikiwa utazungumza. Haya endelea.

(l) Upande wa serikali za mitaa: tungependa ma-chairman wa mabaraza wawe watachaguliwa na wananchi wenyewe. Tunapata jambo hili linaumiza sana sana. Inakuwa ni matatizo madiwani kule wakipewa kitu kidogo wanabaki wanachagua yule wanaomtaka wao wenyewe, huku hawafikirii matatizo ya mwananchi chini. Kwa hivyo ma-chairman wawe wakichaguliwa kutokana na wananchi wenyewe, sio madiwani. Halafu madiwani wawe na kiwango cha elimu cha kidato cha nne, inakuwa ni tatizo sana kwenye mabaraza. Singependa kuchukua muda mwingi, unajua wengi wanangoja, nitapeana.

**Com. Lethome:** Ngoja kuna maswali mawili, matatu.

**Councillor Amina Kisasa:** Asante.

**Com. Asiyo:** Kwanza ningependa kujua juu ya hizi magogo yaani zile mahali wazee wanakaa wakikata hizi mashauri. Je, mapendekezo yako ni kwamba hata kina mama wale wazee wawe wamekaa pale?

**Councillor Amina Kisasa:** Kusema kweli jambo hili mwanzo latutatiza, hatujui kama liko kwenye sheria ya Kenya wajua sheria yenyewe hatuijui sisi, kwa hivyo twatizika. Na ikiwa iko kwenye sheria, haiko case za magogoni. Mwanzo mwanachi anaambiwa alipe pesa nyingi sana. Unaweza kuwa na kesi yako unamaliza miezi miwili una kiwango ambacho si hulipa ambacho ni ulipe ambacho kinaitwa “jamvi”. Unaenda ukirudi utapata wazee, mtu ile kesi iko lakini yaenda ikitafuta ile pesa ya “jamvi” kwanza.

**Com. Lethome:** Mimi ni wakili na haiko kwenye sheria.

**Com. Asiyo:** Haiko.

**Councillor Amina Kisasa:** Basi ikiwa haiko kwenye sheria.

**Com. Lethome:** Zile ambazo ziko zinakubaliwa kuna zile zinaitwa Tribunals – Land Tribunals hizo zinatambulika na sheria, lakini hizo za magogoni hatutambui.

**Councillor Amina Kisasa:** Kwa hivyo tufanye aje kama wananchi?

**Com. Asiyo:** Sasa wewe ndio utuambie.

**Councillor Amina Kisasa:** Haya ikiwa ziendelee maoni yangu, nimesema hapo mwanzo mbeleni, ikiwa ni ziendelee mwanzo, tungependa usawa. Ikiwa ni wanaume kumi wanakaa pale, wanawake kumi iwe sawa kwa sawa. Ikiwa ni wanaume watano wanawake pia wawe watano, ili waangalie usawa wa kesi zote za kina baba na kina mama kisawa.

**Com. Asiyo:** Lakini pale mbele kulikuwa na watu ambao walionelea ni vizuri kuwa na ombudsman, ambaye mtu akiwa na shida anaweza kuenda. Na watu wengi wamesema hivyo. Je, kama kuna ofisi kama hiyo ya ombudsman, kuna haja tena kuwa na hiyo ya magogo?

**Councillor Amina Kisasa:** Itakuwa si lazima.

**Com. Lethome:** ….. (inaudible) sababu hatujui sisi ni wageni hapa. Katika hizi kesi tunazofanya huko magogoni ni kesi ya aina zote kwa mfano ya wizi, matatizo ya kinyumbani, mambo ya mashamba, au ni kesi ya aina gani inayofanya mtu magogoni?

**Councillor Amina Kisasa:** Ukiwa huna uwezo wa kuenda mahakama ukienda kwa chifu wako unapewa wazee wakusaidie kutatua.

**Com. Lethome:** Uamuzi kwa mfano wakitoa ulipe gharama fulani, ukikosa kulipa watakufanya nini?

**Councillor Amina Kisasa:** Haishughulikiwi ile kesi.

**Com. Lethome:** Haishughulikiwi ile kesi. Ndiyo nakwambia haina uzito wowote wa kisheria ile. Haina uzito wa kisheria. Haya. Ulisema kuwa watu wengine wanamiliki vipande vikubwa sana vya ardhi, sasa wewe ungependekeza kiwango cha juu zaidi mtu humiliki ardhi mtu mmoja ni ngapi? Hekari ngapi?

**Councillor Amina Kisasa:** Sasa katika sheria za Kenya hivi sasa unaona kama hino 99 years of lease, utapata kama Vipingo Estate kuna wazee pale kuna miji fulani ambayo sisi inatutatiza mpaka hatujui twende wapi. Kuna wazee wameishi kwenye boma forty years, mpaka dakika hino wanaitwa squatters, hawana vibali tumejaribu kupigania, kuna sehemu fulani mwenye shamba ametoa. Tumepigania wamepata sehemu fulani, lakini kuna sehemu fulani mpaka dakika hii wananachi wetu wanaweza wakaondolewa saa yote kukaundwa. Nafikiri ukifika Vipingo pale unaona "land for sale", kwa nini land kama ile mwananchi asiuziwe kwa bei nafuu. Nimeandika kwenye memorandum yangu hapa inauzwa 1.5m. 1.5m mwananchi wa kawaidi atakwenda ipata wapi? Ikiwa ni kuuza serikali ifanye mbinu ya kuchukua ardhi ile, imurudishie mwananchi yule ambaye yuko pale afaidike, badala ya kumuachia mzungu auze akiuza.

**Com. Lethome:** Bado hujajibu swali langu. Umetupa maneno mazuri. Mtu mmoja, kwa mfano mimi, nikiwa na uwezo wa kununua ardhi, ni kiwango gani cha juu ambacho nitakubaliwa kumiliki? Ama nikitaka kumiliki hekari pengine milioni moja, nina haki hiyo?

**Councillor Amina Kisasa:** Mimi naona kwa Pwani yetu kiwango cha juu kabisa cha ardhi mtu angepewa ni hekari thelathini, iwe ni za mtu mmoja. Yaani, kila mtu awe atalima na kunufaika na yeye.

**Com. Lethome:** Kuna watu ambao wana ardhi, lakini ile ardhi haitumii inakaa tu bure bila kutumiwa. Pengine hata hayuko hapa Kenya, yuko kwao huko lakini ana ardhi hapa. Ungependekeza nini?

**Councillor Amina Kisasa:** Ningependa ardhi zile serikali irudishe kwa wananchi. Serikali ichukue ili iweze kurudishia wananchi, wananchi wafaidike.

**Com. Lethome:** Mishahara ya wabunge umesema kuwa mishahara yao ni ya juu sana?

**Councillor Amina Kisasa:** Juu sana.

**Com. Lethome:** Walijiamulia wenyewe

**Councillor Amina Kisasa:** Ndio.

**Com. Lethome:** Je, ungependelea katika Katiba mpya waendelee hivyo hivyo kujiamulia mishahara yao, ama kuwe na mpango gani?

**Councillor Amina Kisasa:** Lazima kuwe na mpango, si unaona waalimu wanavyopata taabu saa hizi wanataka mshahara. Mwaalimu ametoka wapi, au mbunge ametoka wapi? Mbunge ametoka kwa mwaalimu. Mtu yeyote yule hata sisi hapa sote tumetoka kwa mwaalimu, lakini sasa mwaalimu anatatizika sana. Angekuwa mwaalimu ana mshahara wa kutosha,

kusingekuwa na hizi vilasi vya kusomesha watoto wetu mpaka usiku, mchana, jumamosi, jumapili, wangekuwa ile kazi wanaopewa jumamosi na jumapili, wanapeana kwa wanafunzi ili wanafunzi waweze kwenda kwa madarasa kama ya dini siku za jumapili. Lakini tumepata wanafunzi wetu mpaka waenda madrasa.

**Com. Lethome:** Mshahara wa MPs ukatwe na nani?

**Councillor Amina Kisasa:** Na wananchi.

**Com. Lethome:** Na MPs ambao wanakwenda mbunge halafu wanalala? Wakifika huko wanalala hawafanyi kazi, wafanywe nini? Unapendekeza kitu gani?

**Councillor Amina Kisasa:** Ningependekeza kuwe na muda ambao wanapewa wakionekana haonekani analala kabisa, wananchi wakae wa amue iwe percentage fulani iwekwe ya wale voters waliompigia kura. Wakipitisha atolewe, atolewe.

**Com. Lethome:** Asante sana councillor. Kina mama wa Kilifi wanaringa. Pale mwanzo tulikuwa na wamama wana mambo wengi. David Mramba.

**Com. Asiyo:** Lazima uende pale uweke sign.

**David Mramba:** Mimi naitwa David Mramba natoka Junju location, Kilifi. Haya ni maoni ambayo siyatoi mimi pekee yangu, lakini ni baadhi ya wenzangu tumekaa sote kule kwetu na tukatoa maoni kama yafuatayo.

(1) Katika Katiba, kuwe na uhuru wa kumiliki ardhi zetu bila kudhulumiwa au kunyanyaswa.

(2) Pili, uhaki wa kutumia mazao ya mimea yetu bila kusumbuliwa na serikali hasa polisi, hasa mumea wa kule kwetu ni mnazi. Kuna watu wetu wamesumbuliwa sana na polisi mpaka kuingia ndani ya nyumba usiku, kuvunja hata na mchana, kiasi cha kuiba pia.

(3) Mali za asili zisaidie wenyeji wa mahali pale, ambapo zinatoka mali hizo. Asili mia sabini na tano za mapato zisaidie wenyeji wa mahali pale. Pia hiyo sheria mpya ama Katiba mpya iwe ya sheria ya nchi iwe na uwezo juu ya mwananchi yeyote, awe raisi, waziri, mbunge au raia.

(4) Wananchi wawe na uwezo wa pamoja kuamua jambo badala ya kuwachiwa Rais aamuulie watu wote wa nchi nzima.

(5) Mahakama ipewe uhuru wa kufanya kazi bila kuingiliwa na wakuu wa serikali, kama vile mtukufu Rais kuingilia. Pia

tukasema kwamba mgeni yeyote asiruhusiwe kumiliki ardhi huku mwenyeji amebaki kuitwa squatter sugu. Pia tukasema ya kwamba wenyeji wapewe beach plots, kwa sababu ziko beach plots nyingi kama wasemaji wenzetu waliotangulia zinapewa tu matajiri, sisi kina yahe tunaachiwa tu namna hiyo. Pia tukasema ya kwamba ofisi kuu za serikali ziwe mikoani. Pia tukasema wafanyi kazi wa serikali wahudumu sehemu walizozaliwa. Kusiwe na ukabila katika kazi ama miradi yoyote. Tukasema pia kuna matajiri haswa wazungu, wahindi na waarabu walipe wafanyaji kazi wao mishahara kulingana na maisha yalivyo sasa. Kuwe na usawa katika kuajiriwa kwa wananchi. Watawala kama ma-chifu, ma-DO wachaguliwe na wananchi. Tukasema pia kuwe na uhuru wa kutumia hoteli za kitalii bila ubaguzi wa rangi au utajiri, kwa sababu kufikia sasa kama huna gari, ama u-mwananchi tu wa raia wa kawaida, kuna hoteli nyingine hapa karibu, kwa mfano Whitesands Beach huwezi kuingia pale kama huna gari. Huu ni ubaguzi.

(6) Kwa upande wa viongozi tukasema maoni yafuatayo:-

haswa Rais awe mtu amesoma kuanzia ‘O’ level mpaka kufika chuo kikuu
awe ameoa
awe mwananchi wa Kenya
awe mwenye umri kwanzia miaka arobaini mpaka sabini
mwenye kujiweza kiuchumi
awe ana akili timamu
mwenye tabia njema na muaminifu.
mwenye hana ukabila
mwenye kuhudumia raia bila kuwabagua
mwisho tukasema atawale kwa vipindi viwili tu. Na hayo asanteni.

**Com. Lethome:** Asante Bwana David Mramba. Kuna mambo mengi pale chungu nzima nakupa nafasi hii uzungumze. Karibu mama. Anza kwa jina lako mama. Endelea mama.

**Regina Bonoventure Kalume:** Mimi ni mtu kutoka district ya Kilifi kama mgiriama hata hivi basi nataka niongeee maneno kwa ajili ya wagiriama wenzangu ambao pengine hawako au hawakuchangia. Mimi ninashukuru sana kusikia Katiba. Nafasi ya Katiba hii tulikuwa tukiingoja kwa muda mrefu, sisi haswa watu wa Coast, haswa watu wa Pwani. Sisi ndio tumelemewa na utumwa, hata kama kuna utawala, sisi bado hatukuuonja, bado hatujakula matunda ya uhuru, sisi. Kwa sababu, ikiwa ni beach plot naanza na hiyo kwanza iko hapa, iko nchi ya Coast iko Pwani. Nairobi hakuna beach, India hakuna beach hii ya kwetu hapa. Baraarabu wana beach zao mimi sijafika huko, lakini sio hii iliyo hapa. Sisi hakuna hata mgiriama mmoja m-coast, nisema m-coast hata mmoja aliyeonja matunda ya shamba ya hapa kwetu. Kwa hivyo tunalalamika kutoka utawala uingie mgiriama hasa mijikenda, hajakula, hajaramba kitu katika mdomo wake, kuramba. Nafasi ya mchanga wake huwa Pwani ambapo sisi tungekuwa tuna …. ya hata ndege. Sisi tuko maskini na watoto wetu, hilo liwe la kwanza kuondoka. Ikiwa

serikali ya mkoloni na huyo mazrui na huyo sultan ndiyo walilopanga hilo neno, leo liondoke, lipangwe upya. Tutafurahi sana, tena tunajua Mungu anatupenda pengine ameleta hii Katiba igeuzwe kusudi mgiriama, miji kenda naye aweze kuingia kwenye gari. Kwanzia hiyo bahari ni yetu, mpaka huko Katendewa, hii ni nchi yetu sisi ni Africa. Mimi nafikiri hakuna mgiriama angeenda kujiunga India ajiandikishe uananchi wa India, apewe utawala au uwezo kama power ya wenzetu wageni walio hapa. Sisi hatuna power kama wale wenzetu. Sisi wenye mji hatuna power hiyo. Na sisi ni maskini, hata dakika hii. Mimi hivi nisemavyo na wenzangu wa rika yangu hata hawa watoto wetu hakuna hata mmoja aliweza kuonja matunda ya Uhuru ya mchanga wetu. Kama wenzangu wametangulia kusema kuna u-squatter basi ni kweli, kama hamjasikia nyinyi makaabara mjue u-squatter wote uko hapa.

Sasa hilo liwe la kwanza liondoke na ikiwa inawezekana hao wote ambao sio wazaliwa wa hapo. Mimi sijajiunga sana kusema majimbo nimeyapasisha, lakini naongea kwa wilaya hii. Hawa wote ambao hawakuzaliwa hapa wawe power yao iko chini, sisi wazalia tuwe power yetu iko juu. Na kama alivyoongea hata Councillor Hamidi hiyo ni sawa, kwamba kazi zote zitakazokuwa katika nchi yetu hii, hasa Kilindini, ndio tamaa yetu kubwa. Waandikwe watoto wetu kwanza halafu wageni nyuma, hata kama amejiandikisha ni mwanakenya, tena yeye si mzaliwa hapa amefanya kuja kuomba na kupenda akakubaliwa anaishi, lakini mwenyeji ni yule mmijikenda, coast , Pwani ambaye amezaliwa hapa. Hiyo ni mali yetu. Hayo nafikiri yanaweza kutosha, ikiwa nime-cover habari ya kumiliki ardhi na mashamba.

Sasa ingine ni kwamba, tunaingilia upande wa serikali. Unakuta kama watu walivyosema, viongozi wetu wa serikali, kusema kweli, wengi hawafanyi haki. Si kwamba nitasema kwa leo hivi, hata toka ianze serikali, ma-chifu, kitu gani watu wanateseka sana si urongo. Unakuta mtu hana ukweli wake hapa, lakini hataupata. Haswa kama alivyosema mwenzangu kwamba hata akiwa hana elimu anaonewa kabisa, tunaonewa. Hakuna haki inayopita pale, hiyo ichunguzwe sana hiyo.

**Com. Lethome:** Pendekeza, unataka gani ichunguzwe sasa? Nataka upendekeze.

**Regina Bonoventure Kalume:** Napendekeza igeuzwe, wa ile ya kwamba kuwe na ile ofisi iliyotajwa mbeleni iwe maoni yote yanaweza kupelekwa pale kusudi usawa upatikane.

**Com. Asiyo:** Na huyu DC ambaye anadhulumu watu achaguliwe na watu au na nani?

**Regina Bonoventure Kalume:** Na ifanywe hiyo ya kura.

**Com. Lethome:** Mumpigie kura.

**Regina Bonoventure Kalume:** Eeh, naifanywe hiyo ya kura.

**Com. Lethome:** Na awe ni mtu wa kutoka wapi huyo chifu?

**Regina Bonoventure Kalume:** Kutangulia wenzangu walivyo-ongea ni kama wamejigawanya wakasema hii ni shirikisho majimbo. Maana ya shirikisho majimbo, ni kuonyesha kwamba mwenyeji wa coast hapa anapenda mgeni. Atakaribisha hata aliyetoka wapi, lakini awe ameshirikiana naye akiishi vizuri hapa pamoja na sisi.

**Com. Lethome:** Na DO, unakubali ma-DO wa kutoka nje ama ma-DO pia wawe mijikenda au wa coast?

**Regina Bonoventure Kalume:** Sasa hivi nilivyotaja shirikisho, nafikiri kutakuwa kuna mchanganyiko. Shirikisho haikutenga Mkenya awe hakanyagi Pwani.

**Com. Lethome:** Si kuganyaga sasa, nikuja kuwa kiongozi pale, kutawala pale. DO atolewe mahali popote aletwe hapa, au awe ni mtu wa hapa hapa?

**Regina Bonoventure Kalume:** Katika ile ofisi itachagua maoni. Mimi ningesema kwamba tusibaguane kwamba mtu anayetoka Kenya awe hawezi kuja kutawala hapa. Inawezekana tu, bora ile Coast yetu iwe na mamlaka. Mimi ningependa hapa katika Coast maanake hivi sasa nyinyi viongozi nyinyi mumekuja kuuliza maneno juu ya watu wa Coast. Sasa mimi ningependekeza Coast yetu hii iwe na mamlaka. Mamlaka yale ndiyo yataongoza viongozi wetu wote watakaoishi hapa.

**Com. Lethome:** Haya, asante mama. Twashukuru sana kwa maoni yako, ukajiandikishe pale. Tuna Mzungu Augustus. Augustus is here? Jaribuni kuharakisha watu ni wengi, wengi ajabu.

**Com. Asiyo:** Vile mnataka kuongea, pendekeza.

**Com. Lethome:** Pendekeza, pendekeza.

**Com. Asiyo:** Jina kwanza.

**Augustus Mzungu:** Jina najiita Augustus Mzungu mkaazi wa Junju location na kule ninakaa tatizo ni ardhi. Tumekuwa ma-squatter kwa miaka hata karibu themanini, mpaka leo hii bado tunaitwa ma-squatter sugu, kwa sababu mwaarabu saa hii yuko Arabuni kule, lakini bado anamiliki shamba pale. Kuna wazungu bado wanamiliki shamba pale.

**Com. Lethome:** Unapendekeza kitu gani?

**Augustus Mzungu:** Mimi napendekeza zile shamba zigawiwe wananchi wenyewe, hata kama watalipa kodi kidogo, lakini

ziwe zao sasa. Wawe wako huru kujitawala.

**Com. Asiyo:** Hawa wahindi na wazungu tuwaachie kiasi gani cha haya mashamba tukiyapeana kwa watu?

**Augustus Mzungu:** Labda kama ni nyingi sana hekari kumi na mbili pekee yake.

**Com. Asiyo:** Waachiwe?

**Augustus Mzungu:** Na pia, umilikaji wa mashamba ningependekeza ya kwamba wale wangekuwa na hekari nyingi kabisa, wakuwe na mia mbili pekee yake, yule wa nyingi kabisa. Kwa sababu hata saa hii kuna watu wanamiliki ma-hekari elfu tano, hata elfu kumi, na ni mtu mmoja pekee yake, mwingine pale hana shamba. Halafu pia kupunguzua umaskini ningependekeza kwamba serikali ijayo waangalie upande wa vijana. Yule mwenye hana kazi kuwe na percentage fulani kama 25% iwe inapelekwa kwa Central Government ili kwamba zile zigawiwe wale vijana ama wale wenye hawana kazi, mwisho wa mwezi wanaenda kupata pesa kidogo za matumizi, ndio hapo tutapunguza wizi na ujambazi.

Pia upande wa Rais, napendekeza ya kwamba awe amesoma na kama ni elimu ya chini awe amefika kidato cha nne, na bado akuwe na grade, kuanzia B+ kuendelea. Kwa sababu mtu kama huyo mwenye amepata B+, huyo anaonekana ni mzuri lakini pengine ni matatizo ya kifedha ndio imemfanya asiende mbele. Na pia awe ameoa, kwa sababu mtu mwenye bibi nafikiri ni mtu mwenye family, na akiwa na family kuna uwezo wa kuona kwamba anaweza kukaa na family yake na kuiongoza vizuri.

Upande wa elimu, ningependekeza irudi ile ya zamani sijui ilikuwa 7-2-2-2?

**Com. Lethome:** 7-4-2-3.

**Augustus Mzungu:** Haya. Kwa sababu hii ya 8-4-4 inaonekana haina mazao mazuri. Sana inagandamiza wanafunzi. Utapata hata mwanafunzi siku hizi, hawezi kupanda huu mti, zamani sisi tulikuwa tunapanda hii vizuri, tunaenda kutunda zile mbegu ama tunawinda ndege pale juu, lakini saa hii hawana hiyo time, ya kucheza pia hawana. Kwa hivyo imezorotesha sana nchi. Kwa hayo machache nafikiri nikomee hapo, iko mengi lakini wengine pia wanachangia.

**Com. Asiyo:** Machache tu.

**Com. Lethome:** Ile part uliyotaka kutoa kwa bibi yule anataka kwenda, kabla hajaenda aje atoe maoni yake. Ni wewe.

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Mabibi na mabwana hamjambo? Mimi kwa jina naitwa Maglass – Mama Maglass.

**Com. Lethome:** Na majina mengine?

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Jina lingine naitwa Zena Tuva. Ukitafuta langu hutalipata. Mimi naunga mkono Amina Kisasi. Shida tuliyo nayo wananchi wa Kilifi ni kuhusu ardhi na haki zetu. Kwa kusema kweli hawa mijikenda hatuna haki, hasa kina mama. Mama mimi nimeolewa nimeachwa pale, mwenye ardhi ile aje anisumbua mimi mama, baba hayuko. Nimeishi Mnarani, nimezaliwa Mnarani, nimekua Mnarani na mpaka sasa na miaka arobaini na mitano bado mimi ni squatter. Mwenye ardhi yangu yuko India. Tuna shida. Tuko ready kwa nia, haswa, haki za kina mama, hatuna haswa mijikenda. Mtoto yule atazaliwa mmoja tu kwa baba. Pendekezo langu, tafadhalini serikali ichukue hayo maoni. Mtoto moja wa kike, baba amekufa, mama yule atachukuliwa ufa, kwa sababu baba ataka kurithi ile mali. Mama yule atakataa lakini kwa vile ana mtoto wa kike atachukuliwa ufa, kwa sababu baba wa ufa arithi ile mali. Shida hiyo iko kwa mijikenda. Twaomba serikali yetu ya Kenya ikiwezekana liondoke, kila mmoja apewe haki yake kisawa sawa.

Tatu, elimu yetu ya kimijikenda hasa sisi mijikenda, elimu ya kike, watoto wa kike ni kidogo, watoto wa kiume ni kubwa. Twaomba serikali ya Kenya tuwe sawa na wale watoto wa kiume.

Nne, kuolewa kwetu sisi mijikenda si kwa sheria. Unahalwa – kuna kuolewa na kuhalwa. Ukishahalwa hakuna certificate yoyote, hakuna marriage certificate pahali popote. Kwa hivyo mali ile nitayokuwa nimeolewa, si yangu, ni ya mulumangu muhoho. Tunaomba serikali ya Kenya ifuate hayo mambo.

**Com. Lethome:** Na hiyo muhoho tunataka tusikie kwa Kiswahili cha kueleweka.

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Mume wangu mdogo.

**Com. Lethome:** Na kuhalwa?

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Kunahalwa ni kuhalwa kule kuwa nimekuja, nimekuoa, twende. Kuolewa na ile twende. Twende nimekupenda, hakuna chochote kielelezo, karatasi yoyote. Akija yule ameniambia come and stay, akifa, basi got nowhere to go. Kwa hivyo twaomba serikali yetu ya Kenya sisi watoto wa kike wa mijikenda tuna shida, mpaka hivi ninavyosema. Sina haki kwa mume wangu, sina haki kwa babangu. Nikisha kuachwa na mume wangu kwa babangu sina pa kwenda. Niliuzwa. Kuna msemo mijikenda husema “ameuzwa”. Tunaomba serikali yetu ya Kenya iondoe.

**Com. Lethome:** Kuna maswali hapa. Hizo ni mila za mijikenda, ama si hivyo? Tunasema kwamba sheria iheshimu mila na tamaduni za watu. Sasa unasema halwa iondolewe, ndoa ya halwa, na hiyo mume muhoho iondolewe. Sasa tutaweza aje kusawazisha? Tunasema tuheshimu mila, huku tunasema ondoeni mila zingine.

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Kuheshimu mila ni sawa, na kuondoa vingine ni sawa, kwa sababu leo hivi tuko katika kugeuza Katiba. Katiba hii tunayogeuza ni kuwa kila moja awe sawa na yule mwingine. Sasa ikiwa itakuwa ile mila itakuwako kule kugandamizwa ni lazima kuwe huko vile vile.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo kuna mila zilizopitwa na wakati?

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Eeh, zishapitwa na wakati.

**Com. Lethome:** Kuhusu habari ya elimu, watoto wa kike wapewe elimu. Nafikiri utakubaliana na mimi mama wengine hawakupenda watoto wao wabaki nyumbani, lakini ni umaskini, hawawezi kugaramai skuli, sijui ungependekeza nini?

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Sawa, hawezi kunigaramia mimi pekee yangu skuli, lakini Hassani anaweza akaenda skuli. Yule mumu akipata elimu kodogo na mimi nami nipate elimu kidogo. Sikuwa yule anaenda kutoka one mpaka four, mimi nabaki kabisa nyumbani. Mpaka niolewe mimi ndio pesa zile ninazoolewa apewe Hassani aendelee form four. Haiwezekani. Serikali ya Kenya iangalie.

**Com. Asiyo:** Iangalie kwa njia gani? Watu wamependekeza kwamba elimu iwe ni ya bure mpaka sekondari.

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Sijakataa, sasa elimu ikiwa ni ya bure mpaka sekondari na mimi pia nitasoma. Lakini ikiwa elimu itaenda kama hii vile Coast ilivyo, nazungumza katika Coast Province, Coast Province hatuna hata ile bursary. Bursary yenyewe hakuna. Bursary niliona juzi kwa Karisa Maitha, lakini katika hii Kilifi District hakuna bursary inayopewa mtoto kutoka form one mpaka four. Mtasoma aje?

**Com. Asiyo:** Pendekezo?

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Sasa pendekezo langu, likiwa ni kusoma bursary zile zinaziotoka kule, zigawanyiwe katika district zote, zipewe sawa.

**Com. Lethome:** Haya mama tosha, twashukuru. Kajiandikishe pale. Haya Ndala Mwagajoni.

**Com. Asiyo:** Eleza jina lako na uanze kuongea.

**Ndala Mwagajoni:** Mimi naitwa Ndala Mwagajoni natoka Timboni, Sharianyambe, Junju location. Mimi mwanzo niengendekeza na ningependa kutaka iwe kama inawezekana.

**Com. Lethome:** Ndala sauti bwana watu wakusikie.

**Com. Asiyo:** Sauti.

**Ndala Mwagajoni:** Mimi ningependekeza ikiwezekana elimu kwanza iwe bure na lazima. Wananchi walipe kodi ya kufidia elimu na matibabu, kwa sababu ndio kitu kikubwa kinasumbua wananchi.

Halafu, isiwe na tofauti elimu ile na mtu ambaye hana elimu lakini ana ujuzi. Tena kuwe na uhuru wa vibali vya kwamba mtu yule ambaye hana elimu lakini ana ujuzi aweze kufanya kazi hata kama ni nchi za kigeni kulingana na ujuzi wake.

Haya, jambo la tatu: seli ya polisi. Polisi wawe na huruma sana na wananchi badala ya kuwashika na kuwatesa, ili wakifika mahakamani kule wakifika wapatikane na makosa, wawe ni vilema na hawajiwezi bila kulipa fidia yoyote.

Nne: mahakama iwe na uwezo wa kumpa dhamana mshtakiwa siku hiyo hiyo akikataa mashtaka yake kulingana na mashtaka aliyosomewa. Mfano, mtu ameshikwa anakojoa barabarani apelekwe seli, apelekwe kesho kortini. Akikataa, anawekwa seli baada ya siku kumi na nne rumande ndipo kesi ije isikizwe tena ambapo huwa si kesi ya kuwa imuweke siku zote. Mimi asanteni sana, nafikiri nimemaliza.

**Com. Lethome:** Asante Ndala. Rashid Abdalla. Ndala jiandikishe. Rashid hayuko? Haya Rev. Amos Lewa.

**Com. Lethome:** Kuhusu habari ya elimu watoto wa kike wapewe elimu. Nafikiri utakubaliana na mimi mama wengine hawakupenda watoto wao wabaki nyumbani, lakini ni umaskini, hawawezi kugaramia skuli, sijui ungependekeza nini?

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Sawa, hawezi kunigarimia mimi pekee yangu skuli, lakini Hassani anaweza akaenda skuli. Yule mume akipata elimu kidogo na mimi nami nipate elimu kidogo. Sikuwa yule anaenda kutoka one mpaka four mimi nabaki kabisa nyumbani. Mpaka niolewe mimi ndio pesa zile ninazo-olewa apewe Hassani aendelee form four. Haiwezekani. Serikali ya Kenya iangalie.

**Com. Asiyo:** Iangalie kwa njia gani? Watu wamependekeza kwamba elimu iwe ni ya bure mpaka sekondari.

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Sijakataa, sasa elimu ikiwa ni ya bure mpaka sekondari na mimi pia nitasoma. Lakini ikiwa elimu itaenda kama hii vile Coast ilivyo, nazungumza katika Coast Province, Coast Province hatuna hata ile bursary. Bursary yenyewe hakuna. Bursary niliona juzi kwa Karisa Maitha, lakini katika hii Kilifi District hakuna bursary inayopewa mtoto kutoka form one mpaka form four. Mtasoma aje?

**Com. Asiyo:** Pendekezo?

**Mama Maglass – Zena Tuva:** Sasa pendekezo langu, likiwa ni kusoma bursary zile zinazotoka kule, zigawanyiwe katika district zote, zipewe sawa.

**Com. Lethome:** Haya mama tosha, twashukuru. Kajiandikishe pale. Haya Ndala Mwagajoni.

**Com. Asiyo:** Eleza jina lako na uanze kuongea.

**Ndala Mwagajoni:** Mimi naitwa Ndala Mwagajoni natoka Timboni, Sharianyambe, Junju location. Mimi mwanzo ningependekeza na ningependa kutaka iwe kama inawezekana.

**Com. Lethome:** Ndala sauti bwana watu wakusikie.

**Com. Asiyo:** Sauti.

**Ndala Mwagajoni:** Mimi ningependekeza ikiwezekana elimu kwanza iwe bure na lazima. Wananchi walipe kodi ya kufidia elimu na matibabu, kwa sababu ndio kitu kikubwa kinasumbua wananchi.

Halafu, isiwe na tofauti elimu ile na mtu ambaye hana elimu lakini ana ujuzi. Tena kuwe na uhuru wa vibali vya kwamba mtu yule ambaye hana elimu lakini ana ujuzi aweze kufanya kazi hata kama ni nchi za kigeni kulingana na ujuzi wake.

Haya, jambo la tatu: seli za polisi. Polisi wawe na huruma sana na wananchi badala ya kuwashika na kuwatesa, ili wakifika mahakamani kule wakifika wapatikane na makosa, wawe ni vilema na hawajiwezi bila kulipa fidia yoyote.

Nne: mahakama iwe na uwezo wa kumpa dhamana mshtakiwa siku hiyo hiyo akikataa mashtaka yake kulingana na mashtaka aliyosomewa. Mfano, mtu ameshikwa anakojoa barabarani apelekwe seli, apelekwe kesho kortini. Akikataa, anawekwa seli baada ya siku kumi na nne rumande ndipo kesi ije isikizwe tena ambapo huwa si kesi ya kuwa imuweke siku zote. Mimi asanteni sana, nafikiri nimemaliza.

**Com. Lethome:** Asante Ndala. Rashid Abdalla. Ndala jiandikishe. Rashid hayuko? Haya Rev. Amos Lewa.

**Rev. Amos Lewa:** Kwa jina naitwa Rev. Amos Lewa ni mwenyekiti wa NCCK hapa Kilifi na nina walikilisha makanisa ya jumuia ya NCCK. Vile tumeandika memorandum lakini kuna mambo machache ambayo nitayataja ambayo wachungaji na wakristo wamependekeza kwa mageuzi au katika Katiba hii.

Jambo la kwanza ni kuhusu msemo wa umoja wa Katiba yetu tunauona katika Katiba yetu ya sasa msemo ule wa kusema sisi wakenya haupo, na tunapendekeza kwamba kuwe na msemo ambao utajumuisha sisi wakenya, twakubaliana kuunda Katiba hii ambayo itatuunganisha kama jamii ya wakenya.

Jambo lingine ambalo tumependekeza ni juu ya aina au muundo wa serikali, na tumesema ya kwamba Kenya iwe ni taifa la kuendesha kidemokrasia ambalo litatawalwa katika muundo wa kimajimbo. Na tukasema katika muundo huo kuwe na Rais ambaye atakuwa ana mamlaka, Executive President. Na huyu Executive President atakuwa anachaguliwa na wananchi na uchaguzi wake utakuwa kwamba vyama vyote vinaweza vikaingiza ma-candidates wao kwa round ya kwanza. Halafu ipigwe kura ambayo itatuchagulia watu wawili pekee yake, ambao tutapiga kura na hawa wawili tupate the best candidate. Hilo ni pendekezo letu. Baada ya yeye President kama mtawala wa u-Rais wa jumuia wa taifa la majimbo, katika mikoa tuwe na Regional Head ambaye atakuwa ni Governor, naye pia atachaguliwa na wananchi. Pia chini yake kuwe na local authority ambayo itaongozwa na mwenyekiti, achaguliwe pia na wananchi, na iende hadi village council, au chini kabisa katika wodi ambayo pia itasimamiwa na mwenyekiti. Katika utawala huo tumepunguza pia mamlaka ya Rais na tukasema kwanza Rais hatakuwa na mamlaka mengi, kama vile ambavyo yuko nayo sasa, na tukasema yeye atakuwa ndiye mwenyekiti wa serikali ya majimbo au kiongozi wa serikali ya majimbo, atakuwa pia commander wa majeshi, na pia yeye ataendesha ceremonies au sherehe zote za kitaifa na atakuwa akiweka sahihi sheria zote zilizopitishwa na bunge. Na tukasema pia huyo huyo Rais katika qualifications zake awe na umri wa miaka thelathini na mitano kwenda juu, lakini asizidi miaka sabini. Rais yeyote ambaye yuko zaidi ya miaka sabini hastahili kusimamia kiti hicho. Awe pia yuko above reproach, awe anaheshimika, awe pia amesoma na elimu ya degree, awe ameoa, awe na afya na akili njema, na huyo Rais atawale kwa miaka mitano, kwa vipindi viwili pekee yake.

Tukasema pia mapendekezo yetu kuhusu bunge na tukasema katika serikali ya majimbo kuwe na aina mbili za mbunge, kuwe na National Assembly na Regional Assembly. Na katika hiyo National Assembly tumesema hii itakuwa ni bunge ambalo litakuwa likiwapigia kura na kuwachagua mawaziri wote ambao wanataka kuwa mawaziri lazima wawe vetted na hiyo assembly. Assistant Ministers pia, wale makatibu wakuu, ma-ambassadors ama balozi, wale wakubwa wa ma-parastatals, Chief Justice na ma-judges wote, Chief of General Staff, Commissioner wa polisi, Controller & Auditor-General, Public Service Commission, na Head of Civil Service, hawa wote lazima wawe vetted na parliament. Na tukasema pia ya kwamba powers za parliament tumeipa uwezo mkubwa sana katika lile bunge la kitaifa. Watakuwa na uwezo kuendesha mambo yao wenyewe kulingana na standing orders za bunge.

Na tukapendekeza hawa wabunge katika uwezo na mamlaka yao, hasa katika mishahara tukapendekeza kuwe na what we call commission ya wabunge, ambayo itasimamia mishahara yao yote na marupurupu yao. Tukapendekeza mambo mengine ya kwamba, wabunge umri wa wabunge uanze kutoka miaka kumi na minane, kama Mkenya anaruhusiwa kupiga kura miaka kumi na minane, aruhusiwe kuingia hata bunge. Katiba hiyo ielezee. Lakini pia tukapendekeza, pendekezo lingine sijui kama litapinga hilo lakini tukasema umri wa kutoa kitambulisho na kuchukua kadi ya kura urudishwe chini hadi miaka kumi na sita,

kwa sababu miaka siku hizi imepungua ya maisha na vijana wengi wanakomaa haraka. Kwa hivyo miaka ya kuchukua kitambulisho ianze miaka kumi na sita. Tukasema ile kura ya kuwa na imani kama Rais amekosea, ipunguzwe iwe hamsini na tano kama amefanya makosa ya vote of no confidence. Hayo ni baadhi ya mambo tumeyapendekeza.

Tukaja tena katika jambo lingine la kuhusu defence and national security. Tukasema katika majeshi yetu ya Kenya, kwanza kuundwe committee of permanent commission ya armed forces, itakayoshughulika kurecruit hawa na kuwatrain na kuwapangia mishahara yao. Na tukasema katika wanajeshi wachukuliwe on quota basis, katika kila region. Tukasema pia, kuhusu mambo ya vyama vya kisiasa, political parties, tukasema vyama vya kisiasa visiwe na mipaka. Viwe vingi iwezekanavyo, lakini katika hivi vyama vingi ndivyo vitakavyoweza kuingiza wale candidates ambayo mwishowe kutakuwa na opinion poll. Tukasema pia vile vyama viwili vitakavyosimamisha candindate au Rais wa kupigania kiti cha Kenya kama Rais, vile vyama viwili viwe funded na serikali kuu, the Federal Government wafund hawo presidential candidates wawili, ili wapige siasa sawa sawa na kusionekane kuna upendeleo wowote.

Pia tukaongea kuhusu local government na tukasema ya kwamba katika local government, mayors na wenye viti wote wa mabaraza wachaguliwe na wananchi wenyewe, lakini ma-mayors na wenye viti wapewe kutawala kwa miaka mitano. Kwa sababu ikiwa miwili hawawezi kufanya maendeleo yoyote, ni muda mfupi sana. Tukapendelea miaka hiyo mitano akichaguliwa kama mayor aendelee mpaka atakapomaliza.

Tukaja katika mambo ya land na property rights, tukasema ya kwamba mwananchi yeyote wa Kenya ana haki ya kuwa na ardhi mahali popote Kenya. Na anaweza kununua, lakini wenyeji wana haki ya kumiliki hiyo seheme. Every Kenyan has a right to buy land anywhere, but the locals to have the right to own that land. Nafikiri hiyo ni statement ambayo iko abit technical, lakini imeeleweka. Na tukasema wananchi wa Kenya waruhusiwe kupata ardhi na kila Mkenya hekari kumi na mbili. Lakini atakayekuwa na zaidi ya hekari kumi na mbili alipe land rates kwa kila hekari moja at 5% per month. Kwa hivyo haijalishi hata kama utakuwa na milioni kumi za ardhi, lakini kila hekari moja utailipia 5% kama land rates per month, every month. Hiyo itawazuia wengi kushika ardhi kubwa tu.

Tukaja katika management and use of natural resources. Sorry.

**Com. Asiyo:** Just one more minute and then you let us have your memorandum.

**Rev. Amos Lewa:** Yes. Nataja tu point moja. Tukasema katika management and use of natural resources ni kwamba katika serikali hii ya majimbo wapewe nafasi ya kuweza kuendesha rasilmali zao, lakini waweze ku-remit 40% of the profit in terms of finances to the Central Government, to the Federal Government. Na tukasema wale ambao watasimamia public offices, kwanza wao wawe wameoa, tena wawe wametangaza utajiri wao, na wawe wana tabia njema katika jamii.

Tukaja katika basic rights, ambayo ninamaliza hiyo. Kwenye basic rights kwanza tumetaja education, elimu, na tukasema Federal Government ihakikishe kila jimbo litakuwa na university yake. Tukasema pia kuwe na education policy katika Katiba mpya iweze kuelezea education policy ambayo itaelezea muundo wa aina ya elimu ambayo tumependekeza ni ile ile ya 7-4-2-3. Na ielezee elimu itaendeshwa aje katika Kenya, sio kila mtu atakayeamka anakuja na yake. Tukapendekeza pia ya kwamba public holidays ziwe limited. Kuwe na New Year holiday, Labour Day, Madaraka & Jamhuri, sio kila mtu atakayekuja tawala anakuja na holiday yake.

**Com. Asiyo:** Christmas?

**Rev. Amos Lewa:** Na Christmas and religious holidays imeingiza kwa hiyo kipengele. Zingine zote zifutwe. Tukasema walemavu washughulikiwe, walemavu wa Kenya washughulikiwe. Walemavu wapewe elimu ya bure, walemavu wapewe afya ya bure, walemavu wasio na kazi washughulikiwe, hata maintenance yao. Wapewe a certain percentage ya kifedha kila mwezi kuendesha mambo yao. Tukapendekeza pia ya kwamba wazee, wazee washughulikiwe kwa kupewa maintenance fee ya maisha yao. Kuanzia miaka sitini kuendelea, hawo ni wazee ambao hawana kazi. Wapewe maintenance fee hata kama hakusoma, kila mwisho wa mwezi apewe elfu moja, pale kwa utawala ambao unamuendesha. Tukapendekeza pia ya kwamba ile ofisi ya ombudsman ya malalamishi iweko, na tukasema pia kuwe na commission ya kushughulikia mambo ya makanisa. Siku hizi tunakuta mambo ya makanisa imekuwa ni sekta kubwa. Na ikiwa ni sekta kubwa ya makanisa tukasema iwe na ofisi yake na kuwe na commissioner au commission ambayo itashughulikia kazi za makanisa, kesi za makanisa, registration ya makanisa na vyama vinavyohusika na mambo ya makanisa. Commission iwepo hiyo. Na tukasema pia serikali iweze kutoa wakili kwa kila Mkenya anayeshtakiwa kortini na hawezi kupata wakili kwa fedha. Serikali iweze kumpatia wakili wa bure, automatic lawyer na amsimamie kesi yake. Tukasema pia kuhusu kura, election laws, tukasema kwamba kura zihesabiwe pale pale zinapopigwa. Na tukasema kura zichukuliwe wakati wowote. Na tukasema walemavu wapewe haki na hata kusaidiwa kupiga kura, kama hawezi kutembea. Na umri wa kupiga kura urudishwe chini hadi miaka kumi na sita.

Katika kuchagua wabunge maalum kwenye National Assembly ya Federal Government na hata Regional Assembly, kuwe na uteuzi ufuatao: kuwe na uteuzi wa watu wa dini, wawakilishwe bunge, walemavu, wakina mama, makabila madogo, wafanyi kazi na wengine wote. Hayo ni baadhi ya mapendekezo tuliyoweza kuyatoa, yako mengi ambayo yako hapa ndani sitayataja, mtayaona, asanteni sana.

**Com. Asiyo:** Tumeshukuru sana Bwana Lewa unaweza kupeana ukiweka sahihi pale kwa register yetu na hiyo sasa karatasi ni yetu, sio yako tena. Baada ya miaka hamsini mtoto wako anaweza kwenda akaiona kwa archives, vile ulivyoongea. Kwa sasa tuna nafasi kwa huu anaitwa Samuel, sijui kama Samuel ameongea? Francis Mwangala Nyamawi. Haya Bwana Francis endelea.

**Francis Mwangala Nyamawi:** Asante sana mwenyekiti. Mimi sitakuwa na mengi ya kuzungumza maanake hata nina maandishi hapa na tayari nimeona kwamba mengi yamezungumzwa na wenzangu, lakini pamoja tu na hivyo nitagusia yale

ambayo yamebakishwa bakishwa katika hii. Jina langu ni Francis Mwangala Nyamawi.

**Com. Asiyo:** Francis Mwangala.

**Francis Mwangala Nyamawi:** Niendelee?

**Com. Asiyo:** Haya endelea, ndio.

**Francis Mwangala Nyamawi:** Kwa kuanzia tu kwanza kabla sijatoa mapendekezo mengi, oni la kwanza ni kwamba ningeonelea hii Katiba ibadilishwe iwe tayari irekebishwe hivi sasa kabla ya uchaguzi haujafanywa. Yaani kusiwe na uchaguzi kabla hii Katiba haijakamilika maanake ikiwa tutafanya uchaguzi na Katiba hii, na iwe ndio tayari watu watachaguliwa wataanza kutawala na Katiba hii, mambo yataweza kuharibika. Hilo ni jambo la kwanza.

Pili, iwapo hii Katiba itarekebishwa ambavyo sasa tunang'ang'ania, basi mamlaka ya Rais yapunguzwe. Na ninapozungumza mamlaka hapa namaanisha madaraka,uwezo na hata uhuru wake. Utakuta kwamba wakati huu, Rais yeyote yule anaingia kiti cha Rais hapa Kenya, anapewa uhuru na madaraka mengi sana, yeye anakuwa karibu ni kila kitu na vile kwamba Rais anachaguliwa na nchi, Rais amezaliwa hapa Kenya ni mwananchi mwingine yule, wakati anapoingia kwa uchaguzi anaomba kura kwa wananchi, halafu baadaye akishaingia kwenye mamlaka anaambiwa kwamba yeye yuko juu ya sheria hata kwamba akifanya makosa hawezi kupelekwa kortini, hii kitu iondolewa. Iondolewe vile kwamba yeye si mkamilifu wala si Mungu, ni mwanadamu na ana haki za ubinadamu na anaweza kuingia katika hatia yoyote, na ikiwa sheria ina ruhusu hata yeye mwenyewe inamtawala na wakati anapoapishwa yeye mwenyewe anasema atailinda hiyo Katiba. Katika kuapishwa kwake anasema atalinda Katiba ya Kenya, na Katiba ya Kenya inatawala kila mmoja, ambaye ni mwananchi wa Kenya. He is a statesman, sioni kwa nini awe above the law. Kwa hivyo wakati amekosea awe anaweza kuhojiwa na anapatikana na makosa apelekwe mahakamani na kama inawezekana achukuliwe sheria za kisheria, kulingana na Katiba.

**Com. Asiyo:** Mapendekezo.

**Francis Mwangala Nyamawi:** Kwa hivyo hiyo kwamba yuko above the law iondolewe. Ingine tunaona kwamba katika Katiba ya sasa vile vile inatoa mamlaka makubwa sana kuhusu mshahara na marupurupu ya Rais. Hii pia ni ya kuangaliwa vizuri sana na mapendekezo yangu hapa ni kwamba yeye Rais, akiwa amefanya kazi kwa muda ule ambao wananchi wamempatia na imezungumzwa kwamba iwe ni ya miaka mitano mitano kwa mara mbili, basi wakati anapotoka ofisini yeye achukuliwe kama mfanyi kazi mwingine yule wa serikali, na afanyiwe haki zake zile za mfanyi kazi yeyote ambaye amekuwa kazini na ameondoka, na sio apewe marupurupu maalum vile kwamba anapewa security, anapewa pension ya hali ya juu, anapewa na ulinzi, vile kwamba anakuwa tofauti na mtu yeyote yule amekuwa kazini na ametoka. Aonekane kama amefanya kazi kwa miaka aliyopewa na wa raia, wakati wake umemalizika, na arudi kwa wananchi, na awe kama mwananchi mwingine

kama wale wengine. Hiyo ni kuhusu mambo ya Rais.

Utawala wa mikoa: hapa nimezingatia hasa ma-chifu na manaibu wao mimi. Hawa watu wawili hawa ni msingi wa maendeleo vijijini na mitaani hawa. Na ikiwa kwa kweli maendeleo hii ionekane kule, basi viongozi hawa ni wawe watu ambao wana sifa ambazo ni za kimaendeleo. Sio watu ambao wataitwa kwa panel ya interview huko kwa DC wakafanye interviews, halafu wanapewa tu maanake eti wamesoma, hapana. Hivi sio sifa ambazo tunazingatia hizi. Sifa ambazo tunazingatia hii mimi katika maoni yangu ni kwamba, watu hawa wachaguliwe na raia wenyewe kwanza na katika hali ile ya kuchaguliwa na raia wawe na sifa zifuatazo:

Wenye sifa za kuigika kwanza, kuigika ni kwamba wawe role models. Wawe wana mfano ya maendeleo kule wanakotoka. Uongozi wao uwe unajulikana sana na wananchi wenyewe na wananchi hawa wajue unyonge wao na uwezo wao hawa ma-chifu ni kitu gani, na uamuzi wao uwe utalengana na maongozo ambayo yataleta maendeleo katika vitongoji vyao, yaani mitaa na vijiji.

Hivyo basi kiwango cha chini kabisa cha huyo chief na assistant chief iwe form four na hata zaidi. Ili anapoambiwa afanye project proposal au a sample proposal ya wananchi wenyewe, ajue watu wanazungumza lugha gani. Nimesema kwamba awe na mifano yote ya maendeleo na awe kielelezo katika sehemu ile. Kwa hivyo ni apigwe torch na wananchi wenyewe na aonekane kwamba yeye anastahili kuwa mtu wa maendeleo na anastahili kuwa kiongozi.

Awe na uhusiano mzuri na wananchi, sio mwenye kuleta uadui

Nidhamu yake iwe katika hali ya juu sana na ambayo inarekebisha kijamii kule.

Na asiwe na dalili za uongozi wa asili ya kikabila. Kwa hivyo si yeyote tu yule ambaye anaweza kuingia pale, mpaka aaminikiwe sawa sawa na anapotimiza sifa hizi aingie kwa mlolongo wa kura wa u-chifu au naibu wake.

La tatu ni utekelezaji wa miradi ya kijamii, community projects. Muundo wa DDC na sub-DDC na kadhalika. Badala ya watawala wa mikoa, yaani DC, DO, Chief, Assistant Chief kuwa wenye viti kwa hivi vikao hivi vya DDC na sub-DDC, hii iondolewe sasa, maanake tumeona haifanyi kazi. Badala yake, hawa wenye viti wa vikao hivi, yaani DDC, sub-DDC, sub-location DDC na vyovyote vile, viti hivi vichukuliwe na wananchi walioteuliwa kutoka vijijini ambao wanajua matatizo ya wale wenyewe kule na wanajua maslahi yao. Kwa hivyo si mtu ambaye ametoka corner ile ya kule ya nchi aje awe mwenyekiti hapa na hajui tatizo la mtu wa mahali panaitwa Kibokoni tatizo gani. Aache mtu wa Kibokoni na wa Junju waketi kwenye DDC wazungumze matatizo ya watu wao. Serikali kama itatoa au wafadhili watatoa rasilmali au hazina yoyote ya miradi, hawa watu wajue hizi pesa zinaelekea wapi, na zitashughulikiwa na kina nani, na ni kamati gani ambayo itashughulikia hawa. Sio mambo yazungumzwe kwenye maofisi huku, halafu unaambiwa wamepatia shilingi elfu arobaini na pesa zile hazijulikani zitakuwa

zinafanya miradi gani. Kwa hivyo pendekezo langu ni kwamba wenye viti wa sub-DDCs wawe wateule kutoka kijijini.

Sheria, usalama na utengamano: sasa upande wa polisi na mahakama. Hapa nimependekeza kwamba hii ni sehemu moja ambayo ni nyeti sana, sensitive na inalinda usalama na hata afya za watu. Mara kwa mara tunakuta kwamba polisi au askari yeyote awae yule, anaposhika mwananchi eti kwa jina la kuwa ni Mkisiwa, ana hali tayari ya kumdhulumu kwa ajili ya kwamba yeye tayari ni mahabusu, na mtu huyu hajafika kortini huyu. Nafikiri mtu yule ambaye ana hatia ni yule ambaye ameingia kortini, amehukumiwa, amekwenda kortini amehukumiwa na amepatikana na hatia ndio anaadhibiwa. Lakini hii habari ya kwamba mtu ameshikwa na tayari anadhulumiwa, anateswa kabla hajafika mahakamani, hili ni jambo ambalo linatendeka lakini si sawa sawa. Kwa hivyo badala ya kwamba mtu ashashikwa, na ameshikwa kama Mkisiwa, na tayari aanze kuadhibiwa na kuteswa na kudhulumiwa, hii iondoke mpaka aingie mahakamani, akishapatikana na hatia apewe adhabu inayostahili na mahakama.

***Interjections:***

**Francis Mwangala Nyamawi:** Mashamba na haki za kumiliki hayo mashamba. Haya yamezungumzwa kwa muda mrefu sana, sina haja ya kurudia rudia, lakini kitu kimoja ambacho nataka kusisitiza hapa ni kwamba kumekuwa na tabia siku za nyuma katika upande wa kugawa ardhi. Kuna hii ardhi hapa yavua bahari hapa. Wakati ardhi hii inapogawanyiwa watu hii, inasemekana kwamba kuna 200 metres beach plots. Inasemekana kwamba siku zote ni government land. Na sioni kwa nini ile government land ile haiwezi kumilikiwa na mwananchi wa kawaida, na unakuta hata hiyo government land inasemekana hivyo inakuwa hapo, na baadaye unakuta kwamba watu wengine wanaojiweza wanakuja wanamiliki hiyo ardhi kwa jina la beach plots. Kwa hivyo, mimi mapendekezo yangu ni kwamba yule mtu akiwa amepewe shamba ambalo limepakana na ufuo wa bahari, vile vile apewe uwezo wa kumiliki hata (……. inaudible) maji kabisa huko baharini.

***Interjections:*** *Ni mali yetu, eeh.*

**Francis Mwangala Nyamawi:** Kwa hivyo hii 200 metres (….. inaudible) ndio government land iondolewe na watu wapewe ardhi hiyo, waimiliki mpaka wapakane na hiyo bahari.

***Interjections:*** *Eeh hiyo ni zawadi yetu tumepewa na Mungu.*

**Francis Mwangala Nyamawi:** Ukulima na uchumi. Hii pia imezungumzwa na wenzangu na hii tu ilikuwa inazungumza habari ya ile mimea ambayo inaonekana kuwa imekuwa sidelined, yaani imetengwa kama mikanju, mikorosho, miembe na minazi. Pendekezo tu ni kwamba yaani hii mimea hii hapa Pwani ikiitwa minazi, mikorosho na miembe na mingineo inafuatana, iwekwe katika hali ya mashauri fulani, katika board, izungumzwe ipitishwe na iwezeshwe vile kwamba nayo inaweza kuzingatiwa katika utafiti na ikapewa hali mashahuri zake, na masoko yake na bei zake zikawekwa viwango ya kwamba, mwananchi yule ambaye anashughulikia kukuza mimea hii atafaidika kama yule mwingine ambaye anakuza kahawa, anakuza majani ya chai, anakuza

pyrethrum yaani pareto, na kadhalika. Kuwe na usawa katika uchumi.

Na pengine ni hii hali ya kuajiri watumishi au wafanyi kazi wa serikali. Hapa pia tunaona kwamba kidogo kuna uonevu ambao tungeona kwamba urekebishwe hapa. Jambo la kwanza, hii mamlaka ya Rais ku-appoint hawa.

**Com. Asiyo:** Hiyo unaweza ukatupatia.

**Francis Mwangala Nyamawi:** Hali ya kuajiri wafanyi kazi wa serikali. Mamlaka hii ya kwamba hawa ma-Commissioners, Directors, ma-Chairman wa Ports Authority wanafanya kuwa appointed na Rais. Hii nafikiri ingeachiwa hii halmashauri ya waajiri wa serikali, inaitwa Public Service Commission. Hii ikawaita hawa watu ambao wana sifa zinazostahili kwa ki-elimu, kwa uongozi, kwa ujuzi wakaja wakawahoji na kama watu wamepita sawa sawa ile mitihani, wakapewa kazi na hii Commission na sio watu kusema kwamba fulani amechaguliwa mwenyekiti wa halmashauri fulani, fulani amechaguliwa director wa mahali fulani, na nani? Ametumia kisheria gani huyu mtu?

**Com. Asiyo:** …… (inaudible).

**Francis Mwangala Nyamawi:** Eeh, kwa hivyo haya mambo yarekebishwe haya. Na pengine la mwisho kabisa.

**Com. Asiyo:** Bado ya mwisho?

**Francis Mwangala Nyamawi:** Hili la mwisho la kufungia ni kwamba, pia wakati wafanyi kazi wa serikali wamestaafu, na wametoka kazini kwa uaminifu, na wamefanya kazi katika serikali zao kwa uaminifu, na wametoka hapo bila hatia, hawa wanakuwa ni wananchi ambao wameonyesha uzalendo katika nchi yao.

**Com. Asiyo:** Basi pendekezo.

**Francis Mwangala Nyamawi:** Pendekezo ni kwamba wakati serikali inaangalia kuongeza marupurupu ya wale wafanyi kazi waliobaki kule ndani, hawa waliowatoa nje nao wakiwa ni wazee wao, wawe nao wanaongezwa mishahara vile vile. Ninayo mengi lakina kwa vile nahimizika..

**Com. Asiyo:** Lakini umeandika kwa (…. inaudible). Kila kitu tutaingia ndani yake.

**Francis Mwangala Nyamawi:** Lakini kama ungenipatia kama dakika mbili, tatu…..

***Clapping, laughter:***

**Francis Mwangala Nyamawi:** Basi nashukuru, nashukuru hata hivyo. Mungu awabariki.

**Com. Asiyo:** Onesmus, kama Onesmus hayuko? Bwana Joseph Mwamuye. Joseph Mwamuye atafuatwa na Francis Mwangola, kuna Mwangola hapa? Wewe ni bwana Onesmus? Joseph Mwamuye.

**Joseph Mwamuye:** Kwa jina naitwa Joseph Mwamuye, mimi ni katibu wa chama cha wakulima, chama cha wafanyi kazi cha kikorosho.

Kwanza kutakuwa na nchi inaitwa Republic of Kenya ambayo inapakana na Indian Ocean na nchi ya Somalia huko upande wa mashariki, na itapakana na Uganda na Sudan huko upande wa magharibi, that is West. Nchi ya Ethiopia huku kaskazini, na nchi ya Tanzania huko chini, au South inclusive of the air, the water and the soils, huenda pengine nikachanganya kizungu na Kiswahili, kwa hivyo mtanuia radhi.

Pili, Constitutional supremacy: the parliament will have the Government administrative supremacy. Bunge litakuwa na sheria ya kuweza kutawala nchi hii. Constitution amendments will be by people through referendum supervised by an independent Electoral Commission monitored by the civil societies and accredited observers, after two years as need arises through parliament approval. Kutakuwa na referendum ikiwa kama ni kugeuza Katiba ya nchi hii.

**Com. Asiyo:** Sema na lugha moja, unasema kwa Kiswahili, sema kwa Kiswahili.

**Joseph Mwamuye:** Okay, nitakuwa tu haraka haraka. Kama litakuwa liko na mageuko kwenye hiyo referendum, wananchi wenyewe wataweza kutoa maoni ya kugeuza hiyo Katiba.

Citizenship: kutakuwa na mwananchi au mwananchi wa nchi hii kwa kuzaliwa, either amezaliwa na mama mmoja, kitu kama hicho. Pili, kutakuwa na registration au umetoka nchi ingine umekuja hapa Kenya unajiandikisha kwa kuji-register, na hiyo utaruhusiwa katika kuji-register hapo mahali baada ya kuwa umekaa hapo kwa miezi sita. Ukiwa katika hiyo area ya district au area ya district hiyo baada ya miezi sita, unaweza kujiandikisha na ukawa mwananchi au mwananchi wa sehemu hiyo.

Defence and National Security: the President to be the Commander-in-Chief. Parliament will have the powers to declare wars and use ordinary powers to avert national crisis. Hapo, bunge litakuwa na uwezo wa kuweza kuita hata vita na kukabiliana na majanga yote ambayo yanaweza kutokea. The President shall have power to evoke these emerging powers through …. (inaudible) haka hivyo ikiwa bunge itatoa sheria hiyo ya kuita vita, lakini kupitia na President. Ni lazima iende parliament na iende ikakubaliwe.

Political parties: there shall be as many political parties as possible. Ni sawa kwamba kuwe na vyama viingi kuwezekanavyo, ili kwamba kila mmoja apate fursa ya kuweza kujumuika kuitafutia kura viwavyo. They will be independent, hivi vyama vyote vitakuwa independent. Havitategemea serikali au havitategemea pesa kutoka kwa serikali. Kila chama kitajisimamia chenyewe ili kwamba kiweze kuonekana u-maarufu wake katika kusimamia au katika kutafuta kura. Vyama hivi vinaweza pia kuunda Katiba au kuunda serikali yao ambayo itakuwa haitambuliki, parallel government, ambayo itakuwa haina portfolio wala itakuwa haitambuliki serikalini. Hii itakuwa ni serikali ambayo imeundwa ili kwamba kuifanya ile serikali ambayo iko kwenye mamlaka iweze kuhimizika na kuweza kutoa, the required goods. The political parties' incumbancy will be the government's supremacy in all public affairs. Kama nilivyoamulia kusema kwamba political party ile ambayo itakuwa kwenye mamlaka itakuwa na uzito wa kuanzisha serikali.

Structures and systems of Government: hapa tumekuja katika yale majimbo ambayo mnayasema. Kutakuwa na Federal Government ambapo kutakuwa na devolution of powers, ambapo nguvu au mamlaka yataanza kutoka chini. Mamlaka haya yaanze kutokea huko chini grassroots, huko nyumbani at village level. Yaruke yaje at locational level, na yaje at divisional level, yaje at district level, yaende mpaka national level. Na muundo huu wa Federal system ambao ninautaja mimi hapa, ni kwamba pale pale katika locational level kuwe kutakuwa na diwani ambaye atachaguliwa kama kawaida. Achaguliwe na wananchi na madiwani wale wawe wanaweza kukutanika katika division level. Hapo watakuwa na kikao ambacho kuna divisional officers ambao watakuwapo kumiliki au kusimamia locations, sub-locations huku chini wakiwa katika division. Katika division kutakuwa na council, divisional county council, ambapo ma-diwani wote watakuwa na vikao. Na wataongea kuhusu locations zao, ambapo kila diwani atakuwa na uwezo wa kuongea kuhusu location yake, anataka nini, mabarabara yako vipi, elimu iko vipi, sheria inadumishwa ki hali vipi, itakuwa inasimuliwa kufikia katika divisional level. Na hapo kila diwani atakuwa na uhuru wa kusema atakavyo, kutokana na kamati hiyo ya divisional level watachagua hapo mwenyekiti wao, wamuite mwenyekiti – let them call him a chairman.

**Com. Asiyo:** Umeandika hiyo yote kwa hiyo karatasi?

**Joseph Mwamuye:** Haiko hapa mama. Nipe nafasi. Hiyo itafanya council hiyo kuweza kukaa chini ya mwenyekiti huyo. Na mapendekezo yao kutokea hapo ma-diwani hao wataweza kuchagua mjumbe wao, mjumbe huyu naye pia achaguliwe na wananchi hali kadhalika. Hii inaeleweka kwamba kutakuwa na uchaguzi wa ma-diwani, halafu tutakuwa na uchaguzi wa wajumbe. Baada ya hapo, mjumbe yule ambaye atakuwa amechaguliwa ambaye atakuwa ni chairman at that divisional level, atawakilisha wajumbe wote at district level. Kwa hivyo inamaanisha kwamba katika Kilifi district tuko na division saba, kutakuwa na MPs saba ambao wataketi katika Kilifi County Council, ambapo hapo wata deliberate shughuli zao zote ambazo zimetoka kule, akiwa ametumwa kama mjumbe kutoka huko division. Atadeliberate shughuli zote zile, iwe ni ki-elimu, iwe ni ki-barabara, aina yoyote ile, ataileta huko katika hiyo division level. Baada ya hapo, mjumbe huyo huyo atawakilisha au katika hiyo district watachagua pia katika hapo county council, iwe watachagua mayor watamuita governor. Awe atakuwa ndiye mwenyekiti.

**Com. Asiyo:** Lakini, sio kwa mfano sema kabisa.

**Joseph Mwamuye:** Huyu awe governor wa hapo katika district level. Huyo governor huyo atachaguliwa na baadha ya wale members of parliament ambao watakuwa wamekutana au wawe wame-converge katika hapo District County Council. Na katika hapo watatengeneza budgets zao, zitakuwa zimeanza kutoka huko chini zimeletwa katika district level. Budgets zao hizo, estimates, annual … (inaudible) zitapitishwa na zitazumgumzwa. Na basi yule governor atawakilisha hayo mapendekezo yake huko katika Central Government, ambapo pia hawa wabunge saba nao wataenda katika Central Government hali kadhalika. Hali hiyo itakuwa tumepata mjumbe ambaye ameanza kutoka mashinani, amekuja katika division level, amekuja katika district level, sasa ameenda kwa parliament. Kupitia na parliament, pale juu sasa, hapo kutachaguliwa wajumbe, nakuja kwa upandea wa executive sasa.

**Com. Asiyo:** …… (inaudible).

**Joseph Mwamuye:** Okay, tunakuja kwa upande wa executive. Upande wa executive sasa ikifika kule katika Central Government, serikali au the President atakuwa na powers za kuweza kuchagua Ministers, Assistant Ministers. Na achague hata pia heads of departments ambao watakuja right at down level in the district. Katika wale chairmen wa county council or the mayor wa county council or the governor, na wale wote ambao watakuwa hapo chini, hawa watu ndio watakuwa the heads of the executive. Kutakuwa na department of heads ambao watafuata huyo msururu wote huo, mpaka sub-locational level au locational level. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumepata kiongozi ambaye, tukimshika hapo juu atakuwa anatema mpaka hapa chini, maanake ni kiongozi ambaye tumeshamchagua kutoka grassroots amepanda na ameenda mpaka huko juu.

Judiciary: there shall be Attorney-General, Chief Justice, Magistrate and all other judicial officers. The court shall serve all the Kenya nationals in all spheres of life. There will be Chief Judges for Kenyans, to cater for all Kenyans interests irrespective of race, colour, religion and so forth. The rule of law shall be above all Kenyan citizens irrespective of race, colour, religion, position in government or party. The judiciary should decentralise down to village level where justice will be softly administered.

**Com. Asiyo:** Kuna wengine ambao wanataka kuongea.

**Joseph Mwamuye:** Okay. Katika kwa upande wa judiciary. La mwisho.
***Interjections:*** *Natosha hiyo.*

**Com. Lethome:** Peana pale.

**Joseph Mwamuye:** La mwisho, Electoral system: kutakuwa na Commissioners ishirini na wanne. Kutakuwa na voter education ambayo itachukulia kufundisha wananchi jinsi ya kupiga kura. Kutakuwa na voter registration iendelee kama kawaida, isiwe ni jambo la kufanywa leo halafu linamalizikia.

La mwisho, land property rights: absentee landlords, hapa nitakolea hapa. There will be no land leases. Government land leases to private land should be cancelled and the land allocated to the public, hii imesemwa tayari. Land disputes and allocations itakuwa vested to the village councils. Langu la mwisho madam.

**Com. Asiyo:** Umesema mara nyingi, haifai.

***Interceptions:***

**Joseph Mwamuye:** La mwisho kabisa. There shall be a Public Service Commission appointed by the Parliament. Auditor General & Controller office will be decentralized. Okay.

***Interjections:***

**Com. Asiyo:** Asante sana. Wakati huu ningependa kumuuliza bwana Donald Gambo aje aongee kwa kifupi. Donald Gambo.

***Interjections:***

**Com. Asiyo:** Haya endelea mzee, jina lako halafu sema mapendekezo yako juu ya Katiba mpya ya Kenya.

**Donald Gambo:** Jina langu naitwa Donald Gambo Maktuu, mzaliwa wa hapa Kilifi ni mlemavu. Hata mimi nitasema yangu kwamba, hata watu huitwa walemavu hawatambuliwi katika serikali ya Kenya. Nasema hivyo kwa sababu ya kwamba haturuhusiwi hata kwenye mabunge, wala haturuhusiwi hata kuwa katika county council ya wale wanaitwa councillors. Tumekuwa watu wa kubaguliwa. Nitachukua mfano mwaka juzi ambayo ilitokea, sijui kama nimekosea, ilitokea kitu kwamba, kunatokea serikali inatoa kidogo ya pesa ili walemavu wapate kujisaidia kimaisha. Lakini kwa bahati mbaya ile pesa ikazimwa na kila tukiuliza tunaambiwa itakuja. Kwa hivyo inaonekana walemavu ni watu ambao wamewekwa nyuma kabisa kimaisha. Hatutambuliwi kivivyote, hata ukifika ofisini unaambiwa wewe uliomba pesa wewe. Mimi nami ni mwanadamu kama wengine, kwa hivyo disability is not a inability. Asanteni.

**Com. Asiyo:** Asante sana bwana Gambo. Asante sana, hujapendekeza vile ungependa walemavu wangefanyiwa kwa Katiba mpya. Ungependa Katiba mpya ifanye aje kwa walemavu? Hata unaweza kuongea hapo.

**Donald Gambo:** Mimi ningependa katika walemavu wawe watatambuliwa kiserikali wawe nao wakifika ofisini watambuliwa kama mwanadamu yeyote ambaye anaishi. Lakini sisi walemavu hatutambuliki kote, kwa hivyo tungependa serikali ya Kenya itambue walemavu sio kuwatambua kwamba tutapatia msaada ama hivi na hivi, lakini kuwe na sauti. Hata akisimama mahali ajulikane ni mlemavu anasema na yeye, tupewe uhuru na sisi wa kuwa majumbe, tupewe uhuru.

**Com. Asiyo:** Hapo umeongea. Kwa hivyo mpatiwe nafasi ya kuingia kwa bunge kwa council, n.k. Asante.

**Donald Gambo:** Asante.

**Com. Asiyo:** Sasa ningependa kumuuliza bwana Mwangola aje hapa aongee. Kama bwana Mwangola hayuko, kuna huyu anaitwa Samuel. Mwingine hapa anaitwa Abbas Karo. Kazungu Karisa, Daudi Bwana Mkuu.

**Com. Asiyo:** Wewe unaitwa aje? Daudi Bwana Mkuu, karibu.

**Daudi Bwana Mkuu:** Nashukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika mahala hapa katika jumuiko la watu wengi. Pia vile vile twaweza kushukuru Tume yetu ambao kwa njia ya uteuzi, au husema kwamba Katiba kuja kuchukua maoni kwa watu wote kwa kuweza kuwasikiliza, yaani wote kwa jumla kuweza kuwatimizia haki zao. Kwa hakika kitu ambacho kwamba nataka kuelezea katika maoni yangu ni kwamba, napendekeza pendekezo langu katika ofisi ya Chief Kadhi yaani wa kiislamu, irudishiwe yaani zaidi na zaidi uwezo wake, isibakie katika korti ndogo tu kipekee, iwe ni kama korti nyingine ambayo kwamba ni kubwa. Yaani wasiilamu wote wakiwa wamefika hapo waweze kuamuliwa kiuislamu pia vile vile na miongoni mwa wengine, katika korti yao kuu waamuliwe kivingine, lakini waislamu waamuliwe na muislamu mwenzao.

Na pia vile vile katika pendekezo langu lingine la pili ni kwamba uchumi wa nchi yetu umeanguka chini sana, na sababu zenyewe ni kwa sababu za corruption. Yaani ikiwa nitapendekeza pendekezo hili kwa serikali ikiwa itaondosha mambo haya ya corruption itakuwa jambo la maana, kwa sababu itaweza kusaidia kizazi chetu cha hivi sasa na kizazi kitakachokuja baadaye. Na pia vile vile miongoni ya wale ambao kwamba wanaendelea na corruption zao, basi serikali iweze kuwachukulia hatua mara moja, ili nchi yetu iweze kuinuka juu na watu wanaoishi katika nchi ya Kenya. Halafu pia vile vile katika yaani usaidizi ambao kwamba twautaka kwa serikali au twaomba kwa serikali, kuna pengine hutokea misaada kutoka nchi za nje huweza kusaidia waislamu na wasio kuwa waislamu, twaomba katika yaani ile sema kwamba malipo yale au kusema kivingine ni charge ile ambayo inahitajika tuweze kuondoshewa na sisi ili watu waweze kujimudu hali ya uchumi. Na kwa haya machache, sina mengi isipokuwa ni hayo. Nashukuru.

**Com. Asiyo:** Ningependa kuuliza kitu moja, je unasema kwamba Chief Kadhi awe na korti ile ya appeal au ile ile.

**Daudi Bwana Mkuu:** Ile ile lakini iongozewe uwezo kidogo angalao mambo mengine katika kuonewa sisi waislamu na

wasiokuwa wasilamu, pia vile vile iweze kuamua vizuri zaidi. Yaani iongezewe cheo kidogo.

**Com. Asiyo:** Haya Bwana Mkuu tumesikiza hayo. Sasa ni Bwana Mohamed Mueni. Mohamed, karibu. Bwana Mohamed jina lako la mwisho ni?

**Abubakar Mohamed Mueni:** Mueni.

**Com. Asiyo:** Haya endelea.

**Abubakar Mohamed Mueni:** Mimi naitwa Abubakar Mohamed Mueni. Ni furaha kubwa kwanza kuweza kuhudhuria mahala kama hapa kwa kuweza kutoa maoni yetu mbali mbali. Tumefurahi vile vile kwamba tumehudhuria kwa wingi na hapana budi kwamba tutakayoya zungumza hapa "inshala" yatakuwa ni yenye kuchukuliwa na kuonekana kwamba ni yenye manufaa makubwa kabisa. Maoni yangu mimi kwanza nitafuata kama vile wenzangu walivyotangulia kuzungumza. Wenzangu wamezungumza ambayo nilikuwa nikitaka kuyazungumza.

Kuhusu habari ya mashule, habari ya shule imezungumziwa mara nyingi hapa na mimi hapo shule ndipo nimesimamia haswa. Kwamba sisi maskini tuna shida, watoto wetu hawawezi kuenda popote. Vile vile katika elimu hii tu ya msingi hapa, akifika kilasi cha nne, kama mimi mwenyewe nimefika kilasi cha tatu, kwa hivyo mimi naweza nikapata mamlaka katika idara yoyote.

**Com. Asiyo:** Pendekeza mambo ya elimu tufanya namna gani.

**Abubakar Mohamed Mueni:** Mambo ya elimu ningependekeza kwamba iwe ni bure, kama wenzangu walivyotangulia kuzungumza.

**Com. Asiyo:** Kufika kilasi gani?

**Abubakar Mohamed Mueni:** Mimi napendekeza kama vile wenzangu walivyopendelea mpaka ifike form four, kisha kwingine atakwenda mwenyewe yule kijana.

**Com. Asiyo:** Okay, endelea basi.

**Abubakar Mohamed Mueni:** Lingine vile vile ninalopenda kupendekeza, ni kuhusu habari ya msitu huu wetu hapa karibuni hapa. Tuna wanyama wanatusumbua, hata wengine wameuliwa na vimbwagu hapa hapa karibuni. Kuna mnyama aitwa kimbangu, tokea nizaliwe sijamuona, lakini tumeshtukia ghafla tu ameua watu. Msitu uko hata, na sisi tuambiwa hata uta tusishike, tusimpige mnyama. Mnyama yule anatuua lakini sisi hatufai kumuua.

**Com. Asiyo:** Wewe unapendekeza aje?

**Abubakar Mohamed Mueni:** Napendekeza sisi watu ambao tu katika sehemu zile za mustuni, hata kama ni kupatiwa kitu tukaweza kujihamia nacho mara tukiwaona tuwapige, maanake wanatuulia watu wetu.

**Com. Asiyo:** Hutaki serikali ifanye chochote, ni kuwaua tu hao wanyama?

**Abubakar Mohamed Mueni:** Sasa serikali, ioneshe serikali hii kwamba kwa mambo ya wanyama serikali hii imeshindwa.

**Com. Asiyo:** Tunaongea juu ya Katiba mpya inayotakikana. Kwa hivyo tueleze unataka mapendekezo yako katika serikali mpya na Katiba mpya ifanye nini kulinda maisha ya wale watu wanaoishi karibu na misitu?

**Abubakar Mohamed Mueni:** Ituweze kuweka maanake walizi wa kutosha wanaohusiana na habari ya wanyama. Wasikae maofisini tu huku wanyama wanaua watu.

**Com. Asiyo:** Haya endelea.

**Abubakar Mohamed Mueni:** Lingine ambalo ningependa kupendekeza ni hapa hapa kuhusu habari ya mashule. Hapa kwenye mashule kuna dini tofauti tofauti, kuna wakristo wanasoma na waislamu wanasomea. Na wakristo wanapatiwa nafasi nzuri ya kufanya maombi wakati watoto hawajaingia katika mashule, kama vile wakati wa assembly. Watoto wamesimama pale wanafanya maombi, wale wakristo, waislamu hawapatiwi nafasi.

**Com. Asiyo:** Endelea.

**Abubakar Mohamed Mueni:** Hawapatiwi nafasi, vile ninavyo ongea hata wenzangu wanaweza kuniunga mkono. Wakati ule wako kwenye assembly pale waweze kupata report hao kwanza hawakuelezwa lolote, si lazima kwanza wanaoleta maombi. Waislamu wanatakikana nao walete maombi maanake wao ni watu wa dini, wakristo wakiomba.

**Com. Asiyo:** Unapendekeza aje sasa?

**Abubakar Mohamed Mueni:** Napendekeza wapatiwe nafasi watoto wa kiislamu katika mashule, wawe nao wanafanya kama vile wenzao wanavyofanya. Lingine ambalo ningependa kupendekeza ni kuhusu habari ya ofisi ya Kadhi, kama ilivyozungumzwa hapa. Kwamba Kadhi ndiye anajua sheria za kiislamu na ndiye anafaa kuweza, tunapogombana tunapoteta tunapofanya nini, yeye aweze kuwa ndiye jaji wetu wa kutuhukumu sisi. Lakini leo huwa hapa kidogo kwa jaji huyu ambaye ni

Kadhi wetu kwa dakika mbili halafu unarushwa katika korti kuu kule, ambapo sheria za kiislamu wale walioko kule hawazielewi. Tunahukumiwa katika njia ambayo ni ya dhulma. Kadhi wetu apatiwe nafasi ya kwamba aweza kutuhukumu hata kama …. (inaudible) tuweke kwake, ili hukumu yetu iende kivile vile inapotakikana na dini yetu. Hayo ndiyo mapendekezo yangu niliyokuwa nikitaka kutoa hapa, na kwa hayo nashukuru.

**Com. Asiyo:** Asante Bwana Mohamed Mueni. Fika hapa mbele uweke sahihi kwa register yetu. Sasa tuko na Bwana Alfonse. Alfonse yuko kutoka NCCK? Unaitwa Alfonse nani? Haya, wameandika vibaya lakini hatujali maana umeandika hakuna haja ya kuongea utapeana tu mambo yale ya maana. Asante.

**Alfonse Mwabosa:** Majina yangu ni Alfonse Mwabosa, mimi ni mkaaji wa Kilifi. Nitaongea tu kidogo kama mtu wa upande wa kanisa kidogo – NCCK - na pia vile vile mfanyi kazi kama mwaalimu. Ijapo najua kuna wengine ambao watakuja, viongozi wa waalimu ambao wako hapa, ambao watakuja kuongea zaidi mambo ya waalimu. Mfumo ambao mimi niko nao hapa upande wa serikali, ninaunga mfumo wa majimbo. Napendekeza mfumo wa majimbo ambapo hapo ningependekeza pia hata wale wabunge ambao watachaguliwa, saa hii tunaambiwa kwamba kuna wabunge mia mbili ishirini na mbili. Lakini katika pendekezo langu ningependa hata kila region wabunge hawa wawe wako sawa. Kwa mfano, sisi watu wa Pwani tunaambiwa wabunge wetu hapa tukichanganya pengine namba ya wabunge wengine katika region ingine, sisi ni wachache na region ingine ina wabunge wengi.

Pendekezo langu la pili, ni elimu ya bure, kuanzia standard one mpaka form four. Kwanzia nursery, sorry, mpaka form four. Hii itawezesha kuondoa ile watu kutojua kusoma, kutojua lugha ya Kingereza, kwa sababu tunaona kwamba hii elimu ya primary level haitoshi kuwa mtu anaweza kujieleza vizuri. Kwa hivyo ningependekeza elimu ya bure, na nikisema elimu ya bure hapa, ningependekeza pia serikali iwe itatoa pesa na hata vifaa vya shule bure, ili management ya shule na masomo pia yaendelee kwa sababu kutakuwa elimu ni ya bure, lakini serikali itatoa vifaa na hata pia pesa za kuendesha shule.

Tatu, wafanyi kazi wa serikali pamoja na waalimu: hapa mimi napendekeza kuwe na scheme of service, ambayo utakuta kwamba mfanyaji kazi anaanza kufanya kazi miaka yake thelathini. Amefanyia kazi serikali miaka thelathini, mfanyaji kazi wa serikali. Mwaalimu awafanyia kazi zaidi ya miaka thelathini, lakini anabaki yeye ni P1. Anabaki yaye ni P2, anabaki yeye ni P4. Kwa hivyo ningependekeza kuwe na mpango maalum wa scheme of service hali kwamba mwaalimu akiwa amefanya kazi kwa mda wa miaka mitano kuwe na grade nyingine ambayo atapanda bila kuweka mambo ya interview ama nini, kwa sababu yeye ana ujuzi wa kufanya kazi kwa miaka hiyo mitano.

Mambo ya viwanda: ningependekeza hapa kwamba mahali ambapo kutakuwa na rasilmali fulani, kwa mfano sisi wa Pwani tunao mkoa wetu wa bahari, tunao mkorosho, tunao mnazi, ni muhimu sana viwanda vile ambavyo vitakuwa vya korosho, mnazi, hata hotel industry iwe kile chuo kitajengwa mahali pale, yale mapato yatakuwa yako hapo hapo, kwa mfano tunaona beach plots ziko huku, utalii uko huku, lakini tunasema kwamba Utalii College iko Nairobi. Hivyo basi ningependekeza mahali

rasilmali ile inatoka, pia colleges ziwe zitajengwa pale pale na hata pia companies ziwe zitajengwa pale pale, ili ziwe za kunufaisha watu wa mahali pale.

Vile vile medical care: kuwe na matibabu ya bure kuanzia watu ambao hawana kazi na hata wale ambao wana kazi, kwa sababu tukisema wale ambao wana kazi, wengine wana kazi lakini mapato yao ni ya chini. Kwa hivyo ninapendekeza kuwe na matibabu ya bure, kwa kila mtu ijapokuwa private hospitals ziweko, kwa wale ambao watakuwa wana uwezo wa kuenda kwa private.

Power za Rais: ningependa powers za Rais, ningependekeza kuwe ziwe za kiasi, kwa sababu wakati huu tunaona kwamba Rais ndiye ambaye ana mamlaka makubwa ya kupita kiasi.

Councillors na wabunge wawe watachuguliwa kulingana na uwezo wa chama chake. Kusiwe na limited parties kuwe na vyama vingi, lakini pendekezo langu ni kwamba katika vyama hivyo vingi kuwe na opinion poll, ambavyo vyama viwili viwe vitapeleka Rais na vile vile kuwe hivyo vyama viwili ndivyo vitafadhiwa na serikali ya Federal.

**Com. Asiyo:** Vile vingine havitakuwa na maana?
**Alfonse Mwabosa:** Vile vingine vitakuwa vimeshindwa na opinion poll, kwa hivyo hakutakuwa na maana katika …(inaudible).

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo hawawezi kusimamisha watu kwa bunge au kwa … (inaudible).

**Alfonse Mwabosa:** Wanaweza kusimamisha lakini kujitegemea. Nimesema hivi viwili vitategemea na serikali ya Federal.

**Com. Asiyo:** Okay.

**Alfonse Mwabosa:** Hayo ndiyo mapendekezo yangu kwa kifupi.

**Com. Asiyo:** Asante Bwana Alfonse. Kuna mtu anajiita Bwana Kabulaka. Bwana Kabulaka yuko hapa? Kama hayuko kuna mwingine anajiita Lawrence Kasani Ngohu. Ni wewe mzee, haya pita mbele. Wewe unaongea kwa niaba ya watu wa Kisima Ndogo?

**Lawrence Kasani Ngohu:** Kwa majina, kwanza natoa shukrani kwa mama mwenyekiti kwa nafasi hii ambayo nilipewa. Kwa majina naitwa Lawrence Kasani Ngohu, mimi ni mzee wa kijiji cha sehemu inaitwa Kisima Ndogo hapa Kilifi. Ninawasilisha memoranda ya wanakijiji haswa Kisima Ndogo na tena haswa wa asili ya ki-mijikenda ndio walionituma. Niko na memoranda lakini labda pengine nitapewa nafasi ya kuongea mawali, matatu. Najaribu kuenda mbio mbio maana ule

wakati nimepewa ni mdogo.

Kwanza, kanuni za fera ya dola: wakenya wenyewe ndio watapewa uwezo wa kuchagua wabunge wawakilishe bungeni. Na pia, twapendekeza kwamba katika Katiba kuwe na kifungu kinachowapa wakenya kupiga kura ya kutokuwa na imani na mbunge wao, kutokuwa na imani na diwani, au kutokuwa na imani ya Rais, vote of no confidence.

Nikienda mbio mbio, bunge, ukuu wa Katiba: bunge lisiwe na uwezo wa kubadilisha sehemu yoyote ile ya Katiba. Napendekeza kwamba uwezo huo wa kubadilisha Katiba uwe ni wa Tume kama hii ambayo inaendelea hivi sasa.

Uraia: katika uraia, raia wa Kenya ambaye atapata automatic citizenship, ni yule ambaye ana asili la kabila ya Kenya. Hata akiwa ni mwaafrika lakini ni wa kutoka mahali pengine pasipokuwa Kenya, Uganda na wapi asiwe na automatic citizenship, bali ni mwananchi ambaye asili yake kikabila ni wa hapa hapa Kenya. Huyo atapata automatic citizenship. Ni maoni ya wale walionituma. Watu ambao asili yao si ya wakenya wanaweza kupata citizenship na wapewe uraia, lakini kwa kujiandikisha na wakiwa wana masharti fulani fulani. Na katika hawa kuna wenzetu wale ambao ijapokuwa wao si waafrika, labda wana asili ya kiarabu, labda wana asili ya kihindi, lakini kuna wale ambao wameishi Kenya kwa muda ambao hata ukimwambia arudi kwao, hajui ni wapi, labda pengine ni babu na mababu ndio walikuja. Yeye ukimsukuma hapa, pahali pa kwenda hajui, mtu kama huyo akichunguliwa sawa sawa akionekana ni wa vizazi vya kama kabla ya hata utawala wa kiingereza uje, apewe automatic citizenship.

Waume na wake wale ambao wameoa kutoka nchi zingine. Mwanamke ambaye ameolewa hapa Kenya na Mkenya, apewe citizenship. Mtoto pia, lakini ile iwe ni ndoa ya halali, wawe ndoa yao ni ndoa ya halali, si kuwekana. Mwanamke huyo apewe citizenship. Mtoto pia vile vile, ambaye amezaliwa, kama amezaliwa na mwanamke na bwana yake ni mzungu au m-asia, hata akiwa si citizen, akiwa mama yake ni citizen, mtoto ule awe ana-qualify kupata citizenship. Vile vile ikiwa mwanaume ameoa mtu ambaye si Mkenya na azae naye mtoto, na wawe walioana kihalali, mtoto yule awe anaweza kupewa citizenship. Mke na mume ambao wana Kenya citizenship, na ameipata kwa sababu ameoana yeye ni Mkenya, ameonwa na mwanamke ambaye ni Mkenya, halafu wakosane wa-divorce, basi huyo citizenship yake iwe cancelled. Kwa sababu pengine alikuwa anataka amuoe kwa madhumuni ya kupata citizenship, halafu labda amuache. Nitakwenda mbio mbio naona tunaharakishwa ki-time pale.

Ulinzi na usalama wa mataifa: Rais aendelee kuwa mkuu wa majeshi. Mambo ya discipline ya askari na majeshi, hiyo kuwe kuna code of conduct, ambayo itaweza kufanya kwamba pengine akifanya makosa anaweza akaadhibiwa. Rais awe na uwezo kamili wa kutangaza vita. Rais awe na mamlaka ya kutumia uwezo huo wa pekee, na aweze hata kutangaza vita na pia hata mengineo kama hayo.

Vyama vya kisiasa: napendekeza kuwa kuwe na vyama viwili pekee yake, badala ya kuwe na vyama vingi, kwa sababu vyama vingi vinaleta mgawanyiko wa kikabila. Na baada ya hiyo tulipendekeza kwamba kuwe na wabunge wa kujisimamia, independent candidates. Iwapo mtu yule atakuwa anapendwa na wananchi, lakini amekataliwa na chama hiki na kile kingine, lakini wananchi wameona kama anaweza kuwasilisha matakwa ya wananchi, awe anaweza kupewa ruhusa ya kusimama kama

independent candidate awakilishe wananchi wake.

Muundo na aina ya serikali: muundo wa serikali niliotumwa nije niseme unatakikana ni ule wa majimbo. Muundo huu wa serikali ya majimbo, tunaona ndiyo utakuwa ni mzuri sio kwa wa Pwani pekee yake, lakini kwa kila mahali. Kwa sababu sasa kuna mahali ambapo labda tutaelekea mambo ya ardhi, watu kuchukua mashamba ya watu wengine halafu watu wanauana, halafu kunakuwa na Commission za kuchunguza watu waliuana namna gani. Na ukiangalia bila kuficha ni mambo ya mashamba. Mambo ya ardhi ni sensitive, kwa hivyo majimbo.

Bunge: bunge lipige darubini utoezi wa maafisa kama mkuu wa polisi, mkuu wa magereza, mkuu wa majeshi, mkuu pia wa ardhi.

Umri: umri wa wapiga kura uwe ni miaka kumi na nane. Umri wa chini wagombea-viti vya bunge, uwe miaka ishirini na tano. Umri wa chini wa wagombea-viti vya udiwani uwe miaka ishirini na tano. Umri wa wagombea-viti vya u-rais uwe kati ya miaka arobaini na miaka themanini.

**Com. Lethome:** Maoni yake, maoni yake.

**Lawrence Kasani Ngohu:** Mitihani ya lugha: ile mitihani iliyoko ya lugha naonelea inatosha.

Wabunge na ma-diwani na hata Rais: kuwe na kanuni za kitabia ambazo zaelekea kuonyesha mfano mwema, kwa vile watakuwa ni viongozi machoni pa raia wote. Kama vile kutokuwa mlevi wa kupindukia, alewe lakini asipindukie. Kutokuwa msherati wa kihadharani, kama itakuwa ni lazima labda afichane. Kutotumia madawa ya kulevya. Wawe wanafanya wajibu wao kulingana na kazi waliopewa na wananchi. Na wananchi wawe na uhuru wa kuwafuta hawa wote kutoka diwani, mbunge, Rais wao ikiwa watakuwa wanaona hafanyi kazi yake kwa kupitia ile kura ya kutokowa na imani naye, vote of no confidence, wakati wowote ule hata kabla miaka hiyo mitano kwisha.

Mishahara na marupurupu ya wabunge hiyo napendekeza kwamba isiwe ni kazi yao, kwa sababu wao wanatuwakilisha, sisi ndio tunawalipa. Kwa hivyo fugulishwe Tume, Tume hiyo iwe ndiyo itachunguza marupurupu yao na mishahara yao. Imependekezwa kwamba Tume hiyo iwe na asili mia ishirini ya wabunge, iwe na asili mia ishirini ya waongozi wa kidini mbali mbali, iwe na asili mia ishirini ya wafanya kazi wa serikali, wawakilishwe pia nao, iwe na asili mia ishirini ya wafanyi biashara na asili mia ishirini ya viongozi tu kutoka vyama vya wafanya kazi kama vile COTU na kadhalika, vyama vya waalimu na nini. Wasiwe wawo ndio wanajipa pesa na watu wengine wananyimwa pesa, hiyo haiwezekani.

**Com. Lethome:** Dakika zako zimekatika.

**Lawrence Kasani Ngohu:** Zimekatika?

**Com. Lethome:** Utatukabidhi hiyo memorandum yako.

**Lawrence Kasani Ngohu:** Ndio sawa sawa. Mambo ya ardhi ndiyo sensitive hata ningeanza na hayo ingekuwa afadhali kidogo, lakini kwa vile.

**Com. Lethome:** Tutayasoma yote.

**Lawrence Kasani Ngohu:** Ilikuwa ni tapike mambo hapa, lakini basi kuna lingine sikuliongeza, yale mabeach naona watu wanapewa mpaka ufuoni kule.

***Interjections:*** *Peleka memorandum.*

**Lawrence Kasani Ngohu:** Hilo sikuingiza hapa, nimekumbuka nikiwa hapa. Ukifika pale ufuoni unakuta huko mbeleni unakokwenda, watoto wetu atakuwa anasoma juu ya ile bahari lakini haioni. Kwa sababu ukienda ukifika pale, kila mahali umekanyanga ni trespass. Tunataka mita hamsini kutoka kule mpaka huku, iwe hiyo itakuwa ni public beach, watu wanaweza wakatembea bila kukamatwa na askari, bila kufanywa nini. Ili kwamba watu wote waone bahari yao. Si waisome kwa historia tu pekee yake.

**Com. Lethome:** Asante, asante. Tunamtaka huyu bwana anaitwa Timothy K. Mbura. Halafu afwatwe na watu wa KNUT. Sasa wataingi moja moja baada ya huyu bwana.

**Timothy K. Mbula:** Kwa jina naitwa Timothy Kiti Mbula na nimetoka Majaoni, Tezo location. Pendekezo langu la kwanza ni habari ya ufisadi. Ningetaka kuzungumzia na nipendekeze pesa za umma. Ningependekeza ya kwamba wale wafanyi kazi wa serikali wote ambao wamefuja mali ya umma, wala kutoroka na mali ya umma, kabla ya serikali ijao, wala kabla ya Rais mwingine kuchukua, wawekwe kizuizini pesa zile ziletwe hata kama wametoa nje ama wamezifuja, halafu ndio baadaye serikali ile mpya ichukue, ama yule Rais mwingine achukue. Kwa sababu bila ya kufanya hivyo itakuwa ni shida kubwa kwa yule Rais ambaye atakuwa amerithi mambo mabaya. Hata usipohonga labda tutanunua mia tatu ama zaidi, kwa sababu pesa itakuwa hakuna. Leo hii nikisema ukweli wenyewe tumekuja hapa na nikiuliza wale labda pengine wamekunywa chai hapa, wanaweza kuwa wasifike hata nusu. Wengi hawakunywa chai kwa sababu pesa hazipatikani, pesa zimefujwa. Kuna vitu kama poverty eradication, hizi ni programmes ambazo zime-fail kabisa, kwa sababu pesa hakuna. Nitaweza aje mimi kumlisha mtoto wangu kama mimi mwenyewe nina njaa? Programmes hizi zime-fail kwa sababu ya hizi pesa ambazo zimefujwa, ndiposa napendekeza ya kwamba washikwe wale ambao wamefuja pesa hizi, mpaka zirudishwe.

**Com. Lethome:** Haya pendekeza jambo lingine.

**Timothy K. Mbula:** Haya la pili, habari ya Kenya Police. Polisi wetu wametuonyesha aibu sana, kwa hivyo napendekeza ya kwamba wapate mafunzo mapya haraka, hata ikiwezekana kabla ya serikali ingine. Polisi wanatuonyesha aibu kwa sababu hawafanyi ile kazi ambayo wanatakikana wafanye. Wanazunguka wawili wawili kusumbua kina mama na watu usiku, bila sababu yoyote. Akiona mama ana drum ama mama ana toma cha tembo, wanamsumbua wanampeleka pahali ambako siko. Akikosa hivyo basi wanachukua kama ni ile pombe ama vitu vingine wanaenda navyo. Lingine kwa upande wa polisi vile vile ningependekeza ya kwamba wakiona mtu wakati wa usiku, awe amelewa, awe ni mgonjwa wamsaidie. Badala ya kumpiga mateke, pengine ni mgonjwa yule mzee ama mtu ni mgonjwa wanampiga teke wanasema wewe umelewa, na si ule pengine ni ugonjwa. Kwa hivyo polisi badala ya kutesa wananchi inatakiwa wasaidie wananchi.

Pendekezo la tatu, kuna jambo hili la mwambao wa Pwani, ardhi. Habari ya 10 miles coastal strip nataka ikomeshwe kabisa. Haya mambo yamekuwako kwa wenzetu katika hizo sehemu za bara, ambazo zilikuwa zikiitwa white highlands. White highlands hizi zimechukuliwa na serikali sasa, ambapo ile ilikuwa ni ardhi mwaafrika alikuwa haruhusiwi kukanyaga, lakini sasa wamezichukua na wananchi sasa ndio wanafurahikia matunda ya Uhuru. Hapa Pwani hakuna, imekuwa ni mwambao wa Pwani, 10 miles coastal strip, ardhi ya Sultan Bin Ali. Kwa hivyo, hili jambo ningetaka likomeshwe.

Pendekezo lingine ni habari ya majimbo. Naunga mkono kabisa mfumo wa serikali ya majimbo. Najua ni wengi ambao, mimi nimefanya uchunguzi wangu binafsi, wanataka hayo majimbo lakini ukisikiza wanasema ya kwamba eti pengine kutakuja fujo, pengine tukifukuza watu wa bara pengine itakuwa taabu. Sivyo basi. Hiyo taabu haitakuweko. Hata wale watu wa bara pia tutafanya kazi nao. Wakati hatuna daktari pahali fulani tutajaza mjaluo kutoka Kisumu tumwaambie wewe chukua hii kazi na tutamlipa sawa sawa. Kwa hivyo tunataka tuchukue yaani ule uchumi wetu wa Pwani uwe katika mikononi yetu.

**Com. Lethome:** Na mjaluo akinunua ardhi hapa Pwani?

**Timothy K. Mbula:** Kununua ardhi kwa masikizano, itakuwa sasa hiyo ni sawa kwa sababu mumesikizana. Lakini ule uwezo wa mashamba uwe na wananchi wenyewe. Pendekezo la nne, hapa Pwani ni kama ambao hatujapata uhuru, kwa sababu ya matunda yetu wenyewe. Ningetaka kuzungumzia haswa habari ya hii tembo ya mnazi. Watu wengine ukitaja tembo la mnazi wanasema, mimi ni muislamu sitaki kusikia habari ya mnazi. Lakini uchumi wetu mnazi ni shina la uchumi wa hapa Pwani. Wengine wetu, wengi wetu tumesoma na mnazi, wengi wetu tumewaelimisha watoto wetu na mnazi. Lakini leo hii hatuna uhuru kwa sababu utakuta pahali wazee wanapumzika wakati wa jioni wanaangalia huku na huku, hawana uhuru hata kidogo, kwa sababu ukifanya hivyo tu unaona jamaa wawili wanakuja hata hawana uniform, hawana search warrant. Wanakuja kuwasumbua, haya wekeni chini. Kweli huu ni uhuru ambao tunautaka? Nashangaa. Kwa hivyo polisi wakomeshwa kushika akina mama ambao wana mnazi, watu ambao wanafanya biashara hii ya mnazi na mnazi uhalalishwe.

Langu la mwisho, hawa polisi hawa nawaingilia tena zaidi kabisa, nitawaingilia kabisa kwa sababu sasa wamefanya maovu, ya

kwenda mpaka nyumbani kwa akina mama kule, badala ya kuwachukua wawapeleke mahakamani wakachukua ma-drum ya pombe, wakakimbia nayo wakamuacha mama akilia. Jambo ambalo limefanyika juzi, hata ukipita pahali popote naweza kwenda sema hilo kabisa sehemu ya hapo Majaoni kwetu na Chumani hapo. Kwa hivyo, polisi tafadhali wa-train upya kama nilivyosema mwanzo na wawache kusumbua wananchi. Kwa hayo machache natoa shukrani zangu.

**Com. Lethome:** Haya asante sana. Sasa watu wa KNUT waanze kumiminika hapa. Joseph Ndingi Kahindi. Waalimu hawa.

**Joseph Ndingi Kahindi:** Asante Commissioners ambao wako hapa na wenzangu. Nitawakilisha wale wenzangu kutoka KNUT, na mwanzo kabisa ningetaka kusema ya kwamba twashukuru hii process inaendelea na maombi yetu ni kwamba process hii ya kutengeneza Katiba isiunganishwe na uchaguzi wa mwaka huu. Hii ichukuliwe kama process ya kipekee yake na ipewe muda wa kutosha, kwa sababu tunatengeneza Katiba ambayo itatusaidia sasa au itatuongoza sasa na miaka mingine mingi sana ijayo. Kwa hivyo kusiwe na ule uharaka wa kupeana labda dakika mbili mbili, kama vile ambavyo inaendelea hapa.

Jambo lingine, tunasema kwamba ni jambo moja kuwa na Katiba nzuri, na tunaamini ya kwamba hii process ikiendelea vizuri tutakuwa na Katiba nzuri katika Jamhuri yetu ya Kenya. Lakini kuwa na Katiba nzuri ni jambo moja, kufuata Katiba ni jambo lingine. Kwa hivyo tungetaka ndani ya Katiba hii, kuwe na reflections ambazo zitaweza kutumiwa dhidi ya watu au viongozi ambao hawafuati Katiba. Na tungetaka kutoa mfano ule wetu wa sasa wa waalimu, tumefuata Katiba vizuri tumefuata mazungumzao mpaka tumefikiana tumeweka agreement, lakini mmoja wa wale ambao wameweka agreement hataki kufuata. Na inaonekana sasa ni kama hakuna jambo linaweza kufanywa dhidi ya mtu yule ambaye hataki kufuata ile Katiba ile agreement vile ilivyo. Hii ni mbaya, hata tukitengeneza Katiba iwe nzuri lakini tuwe hatuna cheti, tutakuwa tuko pale pale tulipo mpaka sasa.

Kuhusiana na mambo ya serikali ya government, sisi tunasema tunapendeka mfumo wa Unitary Government, lakini powers ziwe kwa local authorities. Powers zaidi zitoke kwa Headquarters lakini ziwe katika local authorities. Wale chairmen wa hizo societies, ama wale mayors wawe na nguvu zaidi za kuendesha mambo ya eneo lao ambalo wanatoka.

Kuhusiana na Presidency tunakubaliana na wenzetu waliosema ya kwamba umri wa chini kabisa wa mtu ku-qualify kuwa Rais iwe miaka thelathini na mitano, na wa juu zaidi uwe miaka sabini.

Term of office: ziwe mbili za miaka mitano mitano twakubaliana. Functions zake President awe pia ni Head of State na awe pia Head of the Government, na aendelee kuwa Chief wa Armed Forces. Lakini sasa kuna powers fulani ambazo tungetaka ziondolewe kutoka kwa wadhifa huu wa u-Rais. Kwanza Rais asiwe juu ya sheria, above the law. Kumweka mtu juu ya sheria ni kujihatarisha, kwa sababu hata anapofanya makosa, hamwezi kumshtaki. Rais si lazima awe chancellor wa public universities zote, kila public university iwe na chancellor wake tofauti. Rais asiwe ndiye atayekuwa aki-appoint senior civil servants, kama

permanent secretaries na wale wengine. Hawa wawe appointed na Commission au board ambayo itakuwa imeundwa kwa kazi hiyo pekee yake.

Kura za u-Rais zifanywe separately kutoka kwa kura zile za parliamentary na civic ones. Watu wapige kura kwanza wa wabunge wamalize na za ma-councillor, halafu baadaye sasa ndio tuje tupige kura za u-Rais.

Uwezo wa ku-dissolve parliament usiwe na Rais, lakini uwe na kamati maalum ya bunge. Tena tungependekeza kwamba huyu Rais asiwe mbunge wa mahali popote. Kazi ya ubunge ni kubwa, sasa yeye mtu ni Rais kisha halafu mbunge wa constituency mara moja mahali fulani, inakuwa sasa ni shida kwa ile constituency. Ni kama ambao haina representative katika parliament, na huku mnasema mtu akikosa vikao fulani kwenye bunge, akose kiti chake.

Wale ambao wangetaka kuchaguliwa kuwa Rais ingekuwa vizuri wa-declare wealth yao, utajiri wao wameupata vipi. Tuhakikishe kwamba umepatikana kwa njia sawa ndio tuwaruhusu waendelee. Wakati wa kura za u-Rais tungetaka kila candidate awe na running mate, awe na mwenzake ambaye wanakimbizana pamoja, na yeye akipata basi yule mwenzake awe Vice President wake automatically. Tumeshasema ya kwamba Rais akifanya makosa kuwe na njia za kumpeleka kortini kama ni ahukumiwe, kama mwananchi mwingine yeyote. Pia kuwe na uwezo wa ku-move vote of no confidence wakati ambapo tunaona hatuendeshi vizuri.

Kuhusiana na wizara tunasema kwa sababu ya uchanga wetu, kuwa na wizara zaidi ya kumi na tano si sawa. Tungependekeza tuwe na wizara kumi na tano na tumeziandika. Tumesema pia katika kila wizara yule waziri awe appointed na ile committee ambayo tumetaja, na huyu waziri si lazima awe mbunge. Sisi tunataka waziri ambaye atakuwa ana ujuzi na ile kazi ambayo anapewa kuiendesha. Kwa mfano kama ni waziri wa afya, tungetaka mtu ambaye ana ujuzi na kazi hiyo ya afya, awe daktari, au mtu wa aina hiyo. Lakini si kuchukua labda mbunge tu ambaye amechaguliwa kwa sababu he is popular, halafu uende ukampatie wizara nzima ambayo labda yeye hana ujuzi wowote wa kuiendesha. Twasema Ministers must not necessarily be Members of Parliament. Nafikiri hapo tusha kubaliana. Then of course kukaa kwao na kuendesha zile wizara kutategemea kazi yao, iwapo kazi yao ni nzuri, wataruhusiwa kuendelea, iwapo kazi yao si nzuri basi waweze kusimamishwa mara moja ili tuweze kukata janga ambalo wanaweza kuingiza nchi hii. Janga moja ni kama misappropriation of funds. Tunaona kwamba wizara nyingi zinapoteza fedha nyingi kwa sababu ya kuzitumia ovyo ovyo kiholela. Sasa mawaziri wawe held responsible wakati kama huo ukitokea.

Provincial Administration tumesema tayari iwe replaced na local authorities ziwe reinforced. Mayors and council chairman should also be elected directly by the people, hiyo tunakubaliana.

Kwa mambo ya elimu, tunakubaliana na wenzetu waliosema ya kwamba elimu iwe ya bure, na tunaongeza iwe ya bure na pia ya lazima kwa darasa la kwanza mpaka la nane. Maoni ya waalimu sasa ni kwamba tukisema pia elimu ya form one mpaka

four iwe bure, pengine itakuwa ni mzigo sana, hayo ni maoni yetu. Lakini kwa hii basic education kutoka nursery mpaka standard eight , iwe free and compulsory. Sasa tunaposema free and compulsory, tunaweza kuwalazimisha watoto wengi wakaja shule, lakini utakuta kwamba katika nchi hii, kuna wanafunzi wengi wanaenda mashule na wanakosa waalimu kwa sababu hakuna waalimu wa kutosha katika Jamhuri. Kwa hivyo iwe pia ni constitutional right ya kwamba mtoto apate mwaalimu, ili akikosama mwaalimu kwa sababu serikali haijaandika waalimu wa kutosha, basi Minister wa elimu aweze kuwa held. Hata kama ni kumshtaki, tumshtaki kwa sababu anakosesha elimu kwa watoto ambao wanaistahili. Na hatutaki madarasa ya watoto arobaini, arobaini na watano. Tungependekeza madarasa ya watoto between 25 – 30 kwa sababu wako manageable. Kama private schools ambavyo zina uhuru wa kuchagua kama wanataka elimu ya 8-4-4 au ile ya 7-4-2-3, tungetaka pia public schools zipewe huo uhuru. Siku hizi tuna uhuru wa kuchagua, kwa hivyo hatungetaka sheria zigandamize public schools ambazo zenyewe zingetaka ile old system of education. Kama watu wanataka ile ya zamani, waruhusiwe kuendelea na ya zamani, kama wanataka ile mpya, waendelee na ile mpya. Matatizo mengi ambayo yako kwa elimu yanaletwa na kule kutotilia maanani ma-report ya elimu ambayo yametengenezwa. Tungetaka Katiba yetu iweke nguvu kwa Commissions ambazo zitakuwa zimeundwa ili wakiwa na report ambayo wameipresent, basi report hiyo iweze kutekelezwa. Twashukuru serikali inapeana mikopo kwa haswa wanafunzi wa elimu ya juu, universities, tungetaka mikopo hiyo iwe extended kwa hizi colleges, kama Primary Teacher Colleges, Youth Polytechnics, lakini pia kuwe na muongozo maalum wa ku-recover zile pesa ambazo watu wamepewa kwa kusomea. Tungetaka pia kuongeza ya kwamba Members of Parliament should not be have unlimited powers and control of the proceedings. Kuwe na committees kwa mambo ya mishahara, nafikiri hii ishazungumziwa na hatutairudia.

Language tests nakubaliana, ziwe replaced na ile ‘O’ level education ambayo nafikiri kiwango cha chini kiwe D+.

Of course, Members of Parliament awe na sound moral and ethical qualifications. Wakati tunaona mbunge wetu hafanyi kazi vile tunataka, tuwe na uwezo wa kumuita kwa constituency yetu na either tuwe na votes ya kumruhusu aendelee, au tuweze kumsimamisha kazi na tuchague mwingine. Tusifinywe na mbunge ambaye hafanyi kazi kwa miaka mitano.

Finally, najua kuna mambo mengi na wenzangu nao pia wangetaka kuzungumzia tungetaka kuzungumia habari ya uajiri au employment. Mara nyingi tunaona kwamba kazi zatangazwa kwenye magazeti, halafu qualifications watu wanasema moja ni lazima awe na experience ya miaka mitano. Sasa hii tunaona si vizuri, its not fair. Maanake mtu ambaye amemaliza polytechnic leo, ama amemaliza college hivi leo, university hivi leo hawezi kuwa na ile experience. Kwa hivyo zile qualifications ziwe ndio kitu ambacho kinahitajika wakati tunaajiri watu. Na kuwe na automatic insurance cover kwa wafanyi kazi ambao ni wa serikali au wa mashirika au hata wa viwanda vya watu binafsi. Mara nyingi tunakuta serikali inapoteza pesa nyingi kwa ku-train watu, kama hapa kuna institute ya agriculture, wanafunzi wanafundishwa halafu baada ya mafunzi hayo hakuna kazi. Ama kama Teacher Training hakuna kazi. Hii tunaona ni kupoteza pesa za serikali, kwa hivyo serikali ifunze au iweze ku-train watu ambao inawahitaji. Tukifika kiwango cha kuona we don’t need any more, nafuu tutumie hizo institutions kwa kufanya mambo mengine kuliko kuendelea na ku-train agriculturalists na hali hatuwahitaji katika sekta zetu.

Civil servants mara nyingine wangependa kusimamia kura, either mtu awe councillor au awe mbunge. Requirement ni kwamba uache ile kazi yako, u-resign, ndio uende ukapiganie kiti, tunasema hiyo si sawa. Mtu ambaye anataka kupigania kiti aombe tu ruhusa, leave of absence, kama ni miezi mitatu au mnne, aende akapiganie kiti. Akipata aache hii kazi aliyokuwa nayo, akikosa arudi aendelee na kazi yake. Kisha kila mfanyi kazi twasema awe na automatic allowance ya kuwa na trade union. Kuwa wafanyi kazi wengi sana hasa katika hapa Pwani tunawaona, hivi viwanda vya wahindi wahindi wako hapa kama ile ya fruit pale, hawa wafanyi kazi hawa wengi ni vibarua tu kila siku. Mtu amefanya kazi zaidi ya miaka kumi lakini ni kibarua, ni mtu ambaye anaweza kufutwa hata kesho asubuhi. Hii tungetaka Katiba ilinde watu kama hawa. Mtu akifanya kazi akimaliza miezi sita, aandikwe as permanent and pensionable, na awe na trade union.

**Com. Lethome:** Sasa malizia, malizia.

**Joseph Ndingi Kahindi:** Kuna idleness nyingi sana katika civil service, idleness. Watu wanaandikwa kazi lakini wanabaki tu idle kwa muda mrefu. Kwa mfano, tuchukue wafanyi kazi wa armed forces, wanaenda wanafanya training yao ya miezi tisa kisha halafu wanaenda kwa kambi. Sasa wanabaki kwa kambi hiyo kupiga rangi viatu na kufua na kupiga pasi, lakini hakuna kazi wanafanya. Na huku mashule hayana waalimu, hakuna mafundi wa barabara. Tungetaka wale watu wa armed forces kwa mfano waende training yao ya miezi tisa, wakimaliza wapitishwe labda kwa Teacher Training Colleges afanye miaka miwili au mitatu, atoke kama mwaalimu au atoke kama nani. Sasa badala ya kumpeleka kwa kambi akakae, apelekwe hospitali akafanye kazi na wenzake, au apelekwe shule afanye kazi na wenzake. Siku kukiwa na vita, ataitwa aende akachukue bunduki apigane na wenzake. Nina mengi ya kuongea, lakini nafikiri tumeandika yote lakini we have not finalized our report, but we will give it to you.

**Com. Lethome:** Lakini tumeandika yote hapa. Sasa baada ya sisi kurudi Nairobi, mtu anaweza kuwakilisha maoni yake kule, kupitia kwa mwakilishi wetu au moja kwa moja. Asante sana bwana mwaalimu.

**Joseph Ndingi Kahindi:** Ushanimalizia? Ninasema tu citizenship. Citizenship, mambo ya vitambulisho sisi waalimu twasema kwa vile tumesema wanafunzi wanaenda mpaka darasa la nane, na tumesema hii elimu hii mtu akitoka darasa la nana anaweza kuandikwa kazi, yuko self-reliant, sio tumekubaliana? Basi akitoka tu standard eight awe na kitambulisho mara moja, sio aende akangoje mpaka afike miaka kumi na nane. Yeye amemaliza standard eight yuko fourteen. Angoje miaka minne ndio aweze kupata kitambulisho. Hata hii miaka minne hapa katikati atakuwa anafanya nini? Kwa hivyo, mtoto akifika darasa na nane term ya mwisho kufanywe arrangement apewe kitambulisho, ili akitoka atoke nacho. Asanteni.

**Com. Lethome:** Asante sana mwaalimu.

**Seradama Chitavi:** Nawasalimia mchana. Kwa majina naitwa Seradama Chitavi, mkaaji wa Kilifi, msimamizi wa mambo ya

kina mama, kina baba na vijana. Kwa vile wakati ni ule umesikia, pia kwa vile hali zinaendelea na pia niko na karatasi yangu, nitagusa tu kidogo sana. Nataka nigusie kwanza kuhusu kina mama, kwamba kina mama ni kiungo cha pekee katika wilaya katika kila pahali nikijumlisha kitaifa. Mama kulalamika na amelalamika na hata tumesikia mengi kupitia hapa hapa ya kina mama. Moja tu ambalo nitaanza nalo ni kuhusu ule utawala ambao uko sasa na vile ambavyo waalimu wamezungumzia saa hii na vile ambavyo utaratibu hufanyika. Tunaulizwa tutoe maoni vizuri sana, lakini utekelezaji wa maoni yetu baadaye, huwa duni sana. Kwa hivyo huwa ni kama ambao tunajichukua tunachoka kutafuta maoni, lakini baadaye unatarajia lilo lilo ulizungumza litekelezwe ama litimizwe halina mtekelezaji. Kina mama wamependelea kuwe na mwili ambao wameuita Gender Commission. Gender iwe inapewa uzito na Katiba mpya ili waweze kuendeleza mpaka wafikie maoni hayo yaweze kuingia bunge, yaweze kuwa karibu na parliament na iwe hicho ndicho chombo cha kuweza kupitishia mambo. Litakalokuwa haliendi tuwe twajua tunapitia msafara upi, ili gender iweze kutekelezwa vile tungeonelea.

Mengi yamezungumzwa kuhusu gender, lakini nataka niguse na urithi. Na urithi ni kwamba kina baba na mila zetu tunazoziheshimu sana tunazipenda maana ni zetu tangu duni. Lakini utakuta sisi mila zetu ni kwamba mama, mwanamke, hana pahali anapata urithi. Kimila ni watoto wa kiume wapate urithi wa baba, na nafikiri mnaelewa kabisa tukirudi upande wa kuolewa maana nimeheshimika nimeolewa, kwa bwana pia sina urithi kwa sababu wale waume, ambao ni ndugu ya bwana yangu ndio watasimamia urithi. Kwa hivyo kwa baba hakuna, na kule kwa bwana hakuna. Narithi wapi? Tumependekeza urithi uwekwe kisawa, kama vile wenzetu walivyozungumzia hapo awali.

Nagusia magogo: Magogo yamesha tanguliwa kusemwa, lakini magogo haya kwa nini yako sehemu sehemu. Ni kusema huo mwili huo kama tulivyosikia tayari kwamba ni kama ambao ni chombo ambacho sijui watu walikeka ili waweze ku-safeguard mambo yao. Kwa hivyo kama kunazo sehemu ambazo ziko na hiyo, leo nafikiri tumeigusiwa kwamba ni mwili ambao hata hiyo Katiba inayoenda huwa mwili huo. Kwa hivyo tunauliza tu kama kuna mwili huo hata humu wilayani, sisi kina mama tunaona huo mwili tutaanza kufuatiliza ili either twende nao sambamba, ama turuhusiwe tusema usiweko. Asante.

Tukiongezea kuhusu elimu, imeguswa sana elimu. Lakini elimu ya msichana kama kawaida *(in ki mijikenda dialect)* yaani kusema Kazo ataolewa. Kazungu Karisa asome. Hata kijijini twaona elimu yaenda vizuri sana, hata ukiangalia vilasi KNUT zile wanasema, wasichana hawana taabu. Lakini tukiingia huko chini mashinani, wasichana wa kike ama watoto wa kike bado wangali na taabu. Elimu ya msichana, Katiba mpya iweke kifungu cha kusema baba atake ama asitake, huyu msichana aweze kuingia kilasini bila matatizo.

Tumekumbuka wale walemavu: Walemavu tumesema tumeona sana wanasaidiwa, hata kama haya yameongewa, sisi tumeendelea kusema wapewe yale mahitaji ya kawaida. Apewe nyumba, apewe nguo, apatiwe mahitaji yale ambayo serikali itasimamia kabisa. Wakishawafanyia hivyo, kwa nini hatujawaona walemavu wakisimama katika mlolongo wakipigia mtu wao wanayemtaka. Kina mama wanasema kuwe na mbunge wa kuchaguliwa kutoka mashinani mlemavu, tuende nao kama ni wawili watatu wanataka unini, basi twende nao hivi mpaka kila province. Tuweze kupata mbunge mlemavu. Si mmoja tu

ambaye ametoka Kinangop ama mmoja aliyetoka wapi, hapana. Kila province uweze kuwakilishwa na mbunge mlemavu. Na tutafurahia Katiba ikiweza kutupatia kifungu hicho. Yale mengi ambayo yako hapa, nataka niwaambie yako katika karatasi hii na yatakuwa hayana tofauti na yale wenzetu waliyosema. Asanteni sana kwa kinisikiliza, yaliyobaki tutaendelea kuyaweka.

**Com. Lethome:** Asante sana mama. Tupate sasa .. Mwangala. Mwangala, hayuko? Tupate Washington Mbaga.

**Washington Mwambura Mbaga:** Mimi kwa jina mumesikia Washington Mwambura Mbaga na ninatoka Mtwapa, Kikambala. Maoni yangu haya ambayo nitayaeleza ni maoni yangu na nasikitika kuwa watu wa Kikambala hawako hapa, division ya Kikambala mko? Vizuri ikiwa mko. Lakini ni wachache sana, ilikuwa kuwe kutakuwa na kituo sehemu ile, lakini vituo vimewekwa viwili tu, hapa Kilifi na sehemu za St. Teresa, Chonyi. Kwa hivyo sehemu ile ya division ya Kikambala haikupatikana kituo. Kwa hivyo sisi tunasikitika sana lakini ingekuwa mumekuta watu wengi sana kwa Kikambala, maana walifundishwa na walikuwa wanataka kutoa maoni yao.

Kwanza nitaanza na mambo ya ardhi. Mambo ya ardhi kama mnavyoona ni mambo ambayo yametutatiza sana haswa sisi watu wa Pwani. Maana hata sasa tunaitwa ma-squatter. Hata mimi ni squatter. Ardhi imegawanywa lakini kile kigawanywa kunaletwa watu wa bara na wanapewa zile sehemu kwa sababu ni settlement scheme. Na ikiwa imegawanywa kwa scheme kila Mkenya anastahili ama kwa sababu ni Mkenya anaweza kwenda kukaa mahali popote. Na kwa hivyo yeye akipata pale ni sawa sawa na yule mtu wa pale akikosa pia ni sawa sawa.

**Com. Lethome:** Pendekezo?

**Washington Mwambura Mbaga:** Pendekezo langu ni kuwa zile sehemu ambazo zimechukuliwa zimepewa watu wengine, serikali hii ijayo ambayo ni ya majimbo, iwe sehemu hizo zichukuliwe na ikiwa yule mtu aliuza, ikiwa mtu aliuza, maana wamepewa mashamba hayo na wameuza, ifuatiwe ni nani aliyeuza, na imenunuliwa na nani, ili serikali imlipe pesa na wagawiwe wananchi. Ile ardhi iwe imerudi kwa community, iwe ni mali ya community, wala si mali ya mtu binafsi. Na ikiwa yule mtu ataishi pale, apewe lease. Ikimalizika lease irudi kwa serikali. Na hivyo ndivyo tunavyotaka ndivyo maoni yetu.

Tuje kwa security: security tungetaka polisi wawe watakuwa wa majimbo, lakini armed forces wawe ni wa serikali kuu. Tunataka polisi wawe wa majimbo kwa sababu akiwa ni Katana ama Karisa na akimfanyia uovu, tunamjua hapo anapotoka. Kwa hivyo tunaenda tunamwambia wewe jana ulikula hongo mahali fulani mtoto wangu ulimtoza kiasi fulani. Kwa hivyo ataona aibu. Lakini ikiwa ni mtu wa bara yeye hajui Katana, hajui Charo; yeye hatampendelea mtu yeyote. Kwa hivyo ndio tunaona askari wawe chini ya majimbo, na wale askari wa vita wawe katika Central Government, yaani serikali kuu.

**Com. Lethome:** Umesema kuwa polisi akitoka bara hapendelewi, kwa hivyo ungependa wale wanaopendelea?

**Washington Mwambura Mbaga:** Ningependa wale ambao ni watu wetu huwa wanaona aibu kuchukua hongo.

**Com. Lethome:** Wanafuata sheria au wanaona aibu?

**Washington Mwambura Mbaga:** Wanafuata sheria na pia wanaona aibu, maana tunamjua kweli mtoto wa nani yule na akikufanyia vibaya babake, mamake atakuja atamwambia kuwa ulimfanya mtoto wangu hivi. Kwa hivyo ataona aibu kuchukua hongo ama kumfanyia vibaya.

**Com. Lethome:** Haya endelea.

**Washington Mwambura Mbaga:** Nilikuwa nataka kusema machache juu ya mnazi na mkanju.

**Com. Lethome:** Pendekeza, pendekeza.

**Washington Mwambura Mbaga:** Pendekezo langu, mnazi na mkanju ushafanyiwa research ya kutosha, na research zote zikaenda zikawekwa katika archives. Zimewekwa katika store ili mtu wa Pwani asifaidike. Kwa hivyo tumeonewa sana. Tukipata majimbo tutataka tupate yale makaratasi yote ambayo yamefanyiwa uchunguzi, na tuendeshe wenyewe. Kuna factory ishirini na mbili ambazo zinaweza kutengenezwa kwa mnazi, lakini serikali hii haijatufanyia chochote. Kwa hivyo ninataka ijitimize tuwe nyuma na nyuma zaidi ili tuweze kujitawala. Maana ikitawala mtu ambaye ameelimika atapata shida, lakini mtu ambaye hakuelimika ni rahisi kumtawala na kumfanya awe mjua, awe maskini na amletee unga na mahindi, wakati wa kura anampigia kura yeye.

Mambo ya elimu: katika Pwani hatuna chuo hata kimoja.

**Com. Lethome:** Pendekeza.

**Washington Mwambura Mbaga:** Na vyuo vyote viko bara.

**Com. Lethome:** Pendekeza.

**Washington Mwambura Mbaga:** Pendekezo ni kuwa tumeanzisha chuo hivi sasa. Tuna chuo tumekianzisha na ninamueleza hivi leo tumeanzisha chuo ambacho ni private na kanisa ya Methodist Church, huko Kaloleni. Na tumewafanyia interview watoto na tumeona wazi wazi kuwa watoto wetu wanalazimishwa kuchukua.

**Com. Lethome:** Mzee pendekeza. Umependekeza kuwe na chuo cha Pwani. Sasa interview … (inaudible).

**Washington Mwambura Mbaga:** Chuo cha Pwani tena si kimoja. Chuo cha Pwani kisiwe kimoja. Hapa Kilifi kuwe na chuo, tugeuze hiyo KIA kiwe chuo, Shanzu hiyo college iwe ni chuo, na sehemu za Kwale kuwe na chuo. Kwa hivyo sehemu za Tana River kuwe na chuo. Katika kila district kuwe na chuo chake.

**Com. Lethome:** Basi endelea. Umebakisha dakika moja tu.

**Washington Mwambura Mbaga:** Nilikuwa nataka kusema juu ya urathi.

**Com. Lethome:** Sema, hiyo dakika moja inatosha.

**Washington Mwambura Mbaga:** Juu ya urathi, kumesemwa mengi juu watoto wa kike, lakini watoto wa kiume wamesahauliwa. Kwa sababu katika mila za Mijikenda anayechukua urathi huwa ni mtoto wa kiume. Maana yule mtoto wa kike huolewa, na kwenda akarithi mali ya mumeo. Kwa hivyo wale ambao wamesema, wamesemea mtoto wa kike kwa sababu hawaolewi.

**Com. Lethome:** Pendekeza hayo kuhusu huyu mtoto wa kiume.

**Washington Mwambura Mbaga:** Mtoto wa kiume ana haki kupata urithi mara mbili kuliko yule wa kike, kwa sababu mtoto wa kiume ataketi pale, mtoto wa kike ataolewa na kule atakwenda arithi mali ya bwanake na tena yeye ni trustee kwa wale watoto wake wote. Kwa hivyo mali ya mumewe hiyo ni mali yake, kwa hivyo akiwa atapata urithi kule na huku kwa babake aje apate urithi itakuwa sasa amempita yule mtoto wa kiume, yeye ana mali mara mbili. Kwa hivyo mtoto wa kike ikiwa ni kugawanywa urithi, mtoto wa kike apate sehemu moja na mtoto wa kiume apate mara mbili.

**Com. Lethome:** Haya asante sana. Haya Mwakaya Raymond, Mwakaya Raymond.

**Com. Asiyo:** Asante. Thank you very much.

**Mwakaya Raymond:** Bwana mwenyekiti wa Tume hii ya marekebisho ya Katiba kwa mkao huu wa leo nasema asante sana na wote mliohudhuria *sumi lani*. Kwa majina mimi naitwa Mwakaya Raymond Chengo nawakilisha matarafa matatu ya Bahari Constituency, yaani Chonyi, Kikambala na Bahari Division. Mimi ndimi katibu wa vijana katika matarafa hayo matatu. Nina mambo matano ambayo nataka kuongea ikiwa jambo la kwanza ni kuhusu Katiba, jambo la pili nitaongea juu ya elimu, halafu la tatu nitaongea kuhusu tourism yaani utalii, la nne nitaongea kuhusu vijana, la tano nitaongea kuhusu mambo ya jumla, halafu na ardhi.

Kwanza nikianzia kuhusu Katiba: Katiba ya Kenya haipatikani rahisi, sio kama kitabu ama Bibilia unaweza kuipata kwa duka. Kwa hivyo ningependekeza Katiba hiyo ipatikane kila mahali. Tena katika Katiba hiyo imeandikwa katika hali ya lugha ya kiutaalamu sana, ambayo binadamu wa kawaida ama raia wa kawaida hawezi akaitafakari vizuri. Hivyo basi Katiba hiyo iandikwe katika lugha ya Kiswahili, iwe inapatikana katika bookshops na hata makanisani, hoteli, magerezani, mosque na mahali pa kufanyia kazi. Pia vile vile ifundishwe katika shule za msingi na za sekondari, lakini isitihaniwe katika mtihani wa mwisho wa kupeana vyeti. Asante.

Na pia jambo la pili kuhusu elimu: mfumo wa 8-4-4 si mzuri haufai katika nchi hii yetu ya Kenya, hivyo basi ningesema upanguliwe na mfumo ule wa kitambo uendelee. Hii ni kwa sababu mfumo ule wa 8-4-4 uko ghali sana na umewafanya waalimu kuwa wajeuri haswa waalimu wakuu, wamekuwa too arrogant. Hivyo ningependekeza kuwa waalimu wakuu wasiwe waandishi wa B.O.G, PTA, ama school committees. BOG secretaries, PTA secretaries, school committee secretaries wawe wale wazazi wenyewe. Waalimu waachiliwe jukumu la kwendesha shughuli za elimu pekee yake. Pia, vile vile kuwe na elimu ya bure kwa shule za msingi, lakini shule za upili wazazi walipie watoto wao nusu ya malipo ya school fees. Hii inaonekana katika huu ulaghai wa headteachers, mumeona hata serikali imependekeza iondoe malipo, lakini waalimu bado bado vile vile wanataka kuitisha pesa, zile school fees. Pia, vyeti vya shule vipewe watu ama watoto wale ambao wamekalia ama wameenda shule kwa muda ule unaotakikana. Si eti mtu aje akae kwa mtihani apatiwe cheti, hapana. Mtu alianza kama ni kilasi cha kwanza mpaka kilasi cha nane apatiwe cheti. Ameanza form one mpaka form four apatiwe cheti, si mtu anunue mtihani. Hakuna kitu kama hiyo. Na kila wilaya, district, iwe na national school. Kile district iwe na national school na kila province iwe na university. Pwani tuwe na university mbili kwa sababu kuna mchanganyiko wa makabila na watu wamekuwa wengi sana.

Jambo langu la tatu ningetaka kuongea ni juu ya tourism, utalii: utakuta tourism inatia pesa nyingi sana katika mapato ya nchi nzima, lakini zile areas ambazo zinatoa pesa hizo ziko too undeveloped. Pesa zile zinachukuliwa zinaenda huko. Ningependekeza hivi, asili mia arobaini iregeshwe kule kule ule utalii unaotoa hizo pesa. Kama vile huku Pwani kuna hizo mahoteli, 40% iletwe huku itekeleze mambo ya mabarabara na elimu na kadhalika, vile wenyeji watakavyopendekeza. Na pia vile vile college ya utalii ijengwe hapa hapa.

Halafu jambo la nne nataka kuongea juu ya ardhi. Kumekuwa na irregular issuing of land, lakini hata hivyo utakuta population inaongezeka kila siku, lakini ardhi haiongezeki. Hivyo basi imekuwa kuna tribal clashes kwa sababu ya irregularity in issuing of land. Ningependekeza hivi, kila tribe i-settle pale pale, maanake kila tribe inajulikana ilitoka mahali gani. Iende pale pale ikae pale pale, halafu kama mtu atapendekeza kufanya kazi nje ya pale mahali kwao, afanye kazi kulingana na mapendekezo ya wale wenyeji kama wata m-treat kama foreigner ama visitor, kulingana na vile ambavyo watakuwa wamependekeza wao wenyewe wapendekeze hivyo hivyo na yule mtu. Na yule mtu awe atafuatilia vile vile. Halafu watu wasiiuze ardhi ovyo ovyo, mtu awe anaruhusiwa kuuza ardhi acre kumi tu pekee yake kwa mtu binafsi. Na mtu awe hawezi kununua zaidi ya acre kumi. Commercial use, mtu anunue acre hamsini pekee yake, asinunue zaidi ya acre hamsini maanake ardhi sasa hakuna na hatuwezi kuendelea kuuza ardhi hivi hivi. Pia, hivyo hivyo watu ndio wanajaza ardhi, serikali ingekuwa na mfumo wa ku-restrict birth

rate. Familia moja iwe na watoto wawili pekee yake, si zaidi ya watoto wawili. Vijana wamependekeza hivyo, watoto wawili kwa kila familia. Pia, i-discourage polygamy, maanake utakuta baba pengine ameoa, kweli amepata watoto wawili kwa familia hii, lakini ana mabibi tofauti, sasa hapa anapata wawili, pale anapata wawili, pale anapata wawili, yeye mmoja anaweza kuwa na watoto ishirini kwa sababu ameeneza ile polygamy yake. Sasa serikali i-discourage polygamy.

Vijana: vijana wamekuwa side-lined hata hivi nimeona wakina mama walikuwa wakiitwa lakini vijana hawakuitwa, sitaki kuongea zaidi ya hapo. Lakini kulingana na kuwa sidelined vijana wame-suffer especially on the side of education. Kwa sababu wamekuwa sidelined, wame-opt tu kuingia katika uwanja wa child abuse, child labour, kuna pia early marriages, abortion, infant prostitution, ambao vitu hivyo vimekumba vijana sana. Basi ningependekeza hivi, kuwe na Tume ambayo itabuniwa ya kuangalia mapendekezo au mambo ya vijana. Tume hino itaitwa National Youth Commission. Tume hii kazi yake itakuwa inaangalia hasa itamulika mipango ya elimu, mipango ya employment, sports, health na politics. Commission hii itakuwa na one representative from every division. Halafu, out of those representatives wa kila division, wakae wapate one representative ambaye atakuwa mbunge. Kuwe na mbunge wa vijana kutoka kila province, ambao wataenda bunge hilo hilo ambalo liko hapa Kenya.

Nikimalizia mapendekezo yale ya pamoja ambayo nilikuwa nimesema ya mwisho. General views: vijana tunaunga mkono mpango wa majimbo. There should be only two parties in the whole Republic. The President should not be above the law and should declare wealth before sworn in. The Government should limit the number of Commissions in the country. Kuna Commissions nyingi sana utasikia Land Commission, Njonjo Commission, sijui AIDS Commission. Hivi vitu vinamaliza pesa sana. Tume pia ya marekebisho ya Katiba ni nzuri, lakini matumizi yake yako juu sana. Kwa hivyo vijana wanapendekeza Tume hizi zipunguzwe. Shughuli zile ambazo zinafanyiwa na Tume, ziende kwa Ministries. Kazi zile ambazo zingepewa Tume zipatiwe Ministries zifanye. If there are to be provincial administrators, then they should be local people from that very area. To avoid the great number of street children, the Government should legalize abortion. Utakuta mama ama kijana ametungwa mimba, halafu serikali inamlazimisha huyo mama azae huyo mtoto. Hata yeye mwenyewe anajua hatakuwa na uwezo wa kulea mtoto. Kwa nini alazimishwe kuwa azae huyo mtoto?

**Com. Lethome:** One minute.

**Mwakaya Raymond:** Thank you very much. Kwa hivyo vijana wanapendekeza kuwe na abortion ambayo itakuwa ina kuwa carried out na Government hospitals pekee yake.

Councillors, chiefs should be ‘O’ level graduate. Men, women and youth should share nomination of councillorship and members of parliament, equally. Parastatal heads should be appointed by parliament. Members of Parliament should remain as policymakers. High court judges should determine the salaries of MP’s. The Government should form Coalition Government if it fails to get 50% of the votes cast. The President should not be a Member of Parliament. Powers to dissove

the parliament should be vested to the speaker. The country needs a trustee court, nafikiri hiyo kila mtu anaelewa. Kadhi's should not handle other matters, apart from the ones they are currently handling. Mayors should not be councillors and should be elected by wananchi after two and half years. Because the population keeps on increasing, the current geographical constitution system should be changed in accordance with the population increase. Electoral Commission Commissioners should be appointed by parliament. Electorate should have the mandate to recall their MP, if he or she fails to deliver in two years' time. Thank you very much.

**Com. Lethome:** Swali. Umesema kuwa polygamy should be abolished, are you talking of freedom of worship also people should be allowed to devil worship?

**Mwakaya Raymond:** With freedom of worship it should be guaranteed.

**Com. Lethome:** Freedom of worship, should it be guaranteed or not?

**Mwakaya Raymond:** It should be guaranteed.

**Com. Lethome:** Freedom of worship?

**Mwakaya Raymond:** Yes.

**Com. Lethome:** What about those people whom their religions allow them to be polygamists?

**Mwakaya Raymond:** No, that one should not be discouraged.

**Com. Lethome:** Isn't that interference with their religion? Their religion allows them, then you come and say no. Isn't that interference with freedom of worship?

**Mwakaya Raymond:** Now, we've got to change by time, because at first someone could have so many wives, but there was nothing like "Ukimwi".

**Com. Asiyo:** Umesema msichana akipata mimba, huyu mtoto auawe tumboni, huoni kuua binadamu ni kitu kibaya sana?

**Mwakaya Raymond:** Lakini huyo hajakuwa binadamu, hiyo ni damu.

**Com. Asiyo:** Hapana. Mtu akishaumbwa, wewe si wewe umesoma sana wajua, mtoto akishaumbwa amekuwa binadamu ambaye ana fikira zake, ana maumbile zake. Sasa unataka yeye auawe na hatujui kama anaweza kuwa mtu daktari au

mwingine, au jamaa atafaidi nchi hii. Mbona wataka auawe?

**Mwakaya Raymond:** Sawa, asante sana. Nitajibu hivi, hata street kids pia anaweza kuwa daktari, anaweza kuwa President, lakini anashindwa kuwa President kulingana na ile hali aliyo. Kwa hivyo, afadhali damu itoke kuliko street kid awe atateseka.

**Com. Lethome:** Maoni yake.

**Mwakaya Raymond:** Maoni ya vijana.

***Interjections: Inaudible.***

**Com. Lethome:** Tulikubaliana mtu akitoa maoni tumsikize. Ni maoni yake hayo.

**Com. Asiyo:** Umesema kila mtu akioa apate watoto wawili, je kama amepata watoto wasichana wote na angependa kupata watatu angalau0 wa kiume abaki pale nyumbani?

**Mwakaya Raymond:** Asante, tunaposema watoto tunasema tunamaanisha mtoto mwenye uhai, awe mke awe mume, mtoto ni mtoto.

**Com. Lethome:** Na akipitisha wawili achukuliwe hatua gani?

**Mwakaya Raymond:** Anachukuliwa hatua, kwa sababu hii ardhi.

**Com. Lethome:** Sio sababu, hatua gani?

**Com. Asiyo:** Ni hatua gani?

**Mwakaya Raymond:** Ashtakiwe katika hii court of law.

**Com. Lethome:** Na adhabu yake?

**Mwakaya Raymond:** Adhabu yake ni miake kumi.

**Com. Lethome:** Kufungwa?

**Mwakaya Raymond:** Kufungwa kwa kuzaa watoto zaidi ya wawili.

**Com. Asiyo:** Na sasa vile watu wanakufa sana na hii ugonjwa mpya, na pia ukiangalia vizuri hupati wanawake wengi wajawazito hata ukitembea, huoni wanawake wengi wajawazito, na watu wanakufa sana na hii ugonjwa mpya, hapo unasema aje? Ninalinganisha tu itakuja kuwa sawa, itakuwa balanced bila kuua hawo wengine na kukataza watu kuzaa?

**Mwakaya Raymond:** Unajua sasa kila mtu anajikinga, karibu kila mtu ashajua kuwa ukimwi ni hatari na kila mtu anajikinga, kwa hivyo wakati tunavyoendelea kujikinga ndio tunapunguza yale maafa. Kwa hivyo ardhi haiongezeki, lakini namba ya watu inaongezeka.

**Com. Asiyo:** Ni kwa ajili ya ardhi ndio unataka watu wasizae na ndio unataka watoto wauawe?

**Mwakaya Raymond:** Si watoto wauawe. Ni kwa sababu tunataka kila mtu awe anaweza kuishi maisha mazuri.

**Com. Asiyo:** Okay asante.

**Com. Lethome:** Na wale wenye dini kama Katoliki na dini zingine ambao wanaharamisha abortion, watafanya aje?

**Mwakaya Raymond:** Sasa wale watakuwa wanaenda kinyume ya sheria.

**Com. Lethome:** Sasa dini ikigongana na sheria utamuuliza nini?

**Mwakaya Raymond:** Sheria ndiyo inatuongoza, hatuongozwi na dini. Maoni yangu.

**Com. Lethome:** Maoni yako haya. Haya peleka huko.

**Mwakaya Raymond:** Asante sana.

**Com. Lethome:** Swali moja tu nataka kuuliza ngoja. Katika hilo kundi lenu ambalo limeandika hivi, ni vijana wa aina gani mlikutana pamoja? Unaweza kutuambia? Vijana wa aina gani?

**Com. Asiyo:** Waume kwa wasichana.

**Com. Lethome:** Okay, kutoka kwa zingara gani?

**Mwakaya Raymond:** Matarafa matatu.

**Com. Lethome:** Ndani yake kulikuwa na vijana wa kanisa la Katoliki?

**Mwakaya Raymond:** Huwa sisi hatujui huyu anatoka kanisa gani.

**Com. Lethome:** Ni watu wa dini ama si watu wa dini?

**Mwakaya Raymond:** Ni vikundi vya vijana.

**Com. Asiyo:** Hawana jina?

**Com. Lethome:** Wanafuata dini yoyote hawa vijana?

**Mwakaya Raymond:** Mtu anaweza kuwa yuko ana dini tofauti. Wanafuata.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo ndani yake kulikuwa na wakristo, waislamu, na wasiokuwa na dini.

**Mwakaya Raymond:** Wakristo, waislamu, na wasiokuwa na madini.

**Com. Lethome:** Asante.

**Mwakaya Raymond:** Thank you very much.

**Com. Lethome:** Ngoja kuna mzee asubuhi nilimuita ikawa makaratasi yake haijafika alikuwa katika wazee wa kwanza. Josephat Kingi. Tangu asubuhi alikuwa hapa alikuwa mtu wa tatu kujiandikisha.

**Japheth Morris Kingi:** Asante sana bwana mwenyekiti. Mimi kwa majina naitwa Japheth Morris Kingi natoka Tezo location, Bahari division. Nitaongea kidogo kwa sababu mambo mengi yashakuweko tayari mbeleni. Serikali yetu tunayotaka ni ya majimbo. Majimbo haya si ya kila mmoja kuwa kwake nyumbani. Tumesema yafuatayo kwamba ikiwa serikali yetu ni ya majimbo, kule watu wamezaliwa utawala wowote ule, kazi zozote zile kubwa kubwa za uongozi katika tarafa, katika wilaya, katika mkoa, zipewe wale watu asili ya pale. Wale ambao wanatoka sehemu zozote zile zingine za Kenya, wakaribishwe sawa sawa, lakini watu wa kwanza kabisa wawe wale watu ambao ni wakaaji wa pale, wamezaliwa pale na wameishi pale zaidi ya miaka ishirini.

Pia vile vile tukasema, umuhimu wa Katiba: tukaona kwamba Katiba ni sawa ifunzwe shuleni. Kwa hivyo waalimu wahakikishe

kwamba hii Katiba iko katika syllabus. Kwa sababu sisi tunasema tunarekebisha Katiba lakini kisawa ni kwamba sasa hivi ukimuuliza mtu unajua mambo gani ya Katiba, atasema sijui. Kwa hivyo hiyo iende pia mashuleni.

Katika uzungumzi wetu tukafikia mahali tukasema Rais amepewa uwezo mkubwa sana. Kwa mfano, uchaguzi wote ule wa mawaziri, makatibu wa kudumu, jaji mkuu, majaji wengineo, yeye ndiye huwachagua. Tukasema uwezo ule ni mkubwa sana, upunguzwe.

Ikiwa utapunguzwa basi, tukafikia mahali ambapo kazi fulani fulani zipunguzwe. Zinazofuata ni zile ambazo tumesema zipunguzwe. Nimesema kama baraza la mawaziri, mkuu wa sheria, msimamizi mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali, mabalozi, kamishna wa polisi, tume ya uajiri, watumishi wa serikali, na wengine wale wakubwa wakubwa wale, iwe kazi ile itapelekwa bunge. Bunge lipewe uwezo wa kuchagua kama kutakuwa na kamati ya kuchagua watumishi wale wakubwa wakubwa, permanent secretaries, kama kutakuwa na wengine wa kuchagua, fulani anafaa u-balozi wa mahali fulani, kama zile tumempunguzia Rais. Nyingine mtazisoma hapo kwa sababu nitaacha hiyo ripoti yangu hapa.

Mamlaka ya nchi: hii imesemwa kwa kirefu, kwa hivyo sitairudia kama ni miaka mitano na je, akikosa itakuwaje, hiyo imesemwa sana kwa sababu sitaki kurudia. Watu wamechoka.

Haki za kimsingi: kama huduma za afya, kuwe na matibabu ya bure na matibabu hayo yakiwa ya bure sasa hivi, ukienda hospitalini utatoa deposit uhudumiwe. Unapokosa pesa za kulipa zaidi na umepona, unabakishwa pale hospitalini kungoja. Kuwe na watu ama commission fulani ambayo itasimamia mambo kama yale, sio mtu amepoa na hatoki tena hospitali kwa sababu hata kuna mambo mengine kule ambayo anaweza kushika, ugonjwa mwingine, yeye anabakishwa pale pale. Kuwe na namna ya kutoa mtu kama yule ameshindwa na bill ya hospitali.

Maji yako ghali sana, angao yapunguzwe chini zaidi kama shiling moja kwa jerrican ya lita ishirini. Elimu ishasemwa.

Ajira: angalao serikali itakayokuja iweze kupeana mikopo kwa wale ambao hata hawajiwezi kabisa. Tumeongea habari ya poverty eradication, lakini sisi ambao hatujiwezi hatukupewa mikopo na serikali kwamba tunaweza kujiendeleza namna gani.

Chakula: shule, watoto wa shule ili waendelee, ingawa tumesema shule iwe darasa la kwanza mpaka la nane bure. Vile vile kuna upungufu kwa watoto kwenda hata ingawaje itakuwa bure. Hawaendi shule kwa sababu wana njaa. Serikali isimamie pia mambo ya chakula, angalao lunch. Yale mambo mengine sisi wazazi tutaangalia.

Serikali za mitaa: mayor, wenye viti, wachaguliwe na raia, kwani kuna uwezekano kwamba wakienda kule wale wachache waweza kufanya mambo yao tunaiita corruption kimombo na kuona kwamba fulani anafaa na kumbe hata hafai kulingana na vile ameishi huko na haijulikaniwi kama yeye ni mtu mzuri ama namna gani. Kwa hivyo apewe kazi ile ya u-mayor, apewe kazi

ile ya mwenyekiti na wananchi wenyewe. Ninasema nitaguzia pale muhimu muhimu tu.

Rasilimali: tunapendekeza Katiba ihakikishe kwamba serikali inatupatia soko kwa mazao yetu, kama korosho, nazi, maembe na kadhalika. Mimea hii ifanyiwe utafiti na tujue kwa hakika kwamba nasi tuko pamoja na kila mmoja katika Kenya. Kwa sababu imesahaulika kwa muda mrefu.

Tembo: tembo ya mnazi itafutiwe utafiti na iruhusiwe kunywewa na kutafutiwa soko sawa na vinywaji vingine. Yale mengine mtayasoma hapa. Asanteni sana.

**Com. Lethome:** Asante sana Bwana Japheth. Haya, tuna huyu bwana pia alikuja mapema alikuwa anataka kusema, lakini sasa atasema ….. Mohamed.

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Nashukuru kamati yetu ya kuchagua Katiba imefika hapa nami leo nina maoni yangu "mashalao" mtasikia kwa makina imeiva. Sema jina yako: Councillor Sha Mwa Rukia.

**Com. Lethome:** Unawakilisha ward gani?

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Nilikuwa councillor lakini nikaondolewa, lakini jina limebakia pale pale kwa ujumla.

***Laughter:***

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Habari kubwa zaidi iliyoko hapa ni discrimination of IDs. Mambo ya vitambulisho na pasipoti. Hivi sasa mimi "*alakulihali*" hakuna sijui kama mimi ni Mchonyi. Mchonyi safi kabisa kwa baba na mama, lakini nikatagua dini ambayo ni ya kiislamu pengine, babangu ametagua, nikaamini sasa naitwa Mahdi Saidi hiyo. Lakini kabila yangu iko pale pale haibadiliki mimi nadhani. Utukufu wangu, uchini wangu uko vile vile. Lakini nikianza kutafuta kitambulisho hivi sasa au mwanagu akitoa jina la Mohamed Saidi, huwa kuna ubaguzi mkubwa sana sana sana katika mambo ya kitambulisho. Si hapa, si Nairobi, si kokote tutasema. Imebidi mwananchi kama mimi "alakulihali", Ahmed Saidi, nenda kwa ofisi ya kitambulisho, imebidi nifanye vetting mimi au mwanangu afanye vetting. Vetting ni masaala kuwa aangalie mtu huyu, yeye ni Mkenya kweli au si mkweli. Lakini ngumbao, nisikilizeni kwa makini, ngumbao akienda pale kwa habari ya kitambulisho alakulihali bila kubaguliwa, bila jambo lolote. Ambapo mimi na ngumbao tuliosafiriana mjini tu, lakini sisi sote twa moja. Nisikilizeni kwa makini sana, imebidi muislamu yeyote ikiwa ataka kitambulisho hivi sasa, mpaka atoe karatasi chungu nzima, birth certificate, nini, nini. Hapa Kilifi ndio zaidi na nimejeta nao haswa. Twaomba maoni yetu *ala kuli hali* ikiwa ngumbao akwenda pale kutaka ID wakampatia karatasi bila kufanywa vetting, na huyo Ahmed Saidi akiwa ni Mchonyi vile vile kwa sababu eti hii kabila yake ni Mchonyi, awe habaguliwi kama yule mtu ngumbao. Naona maombi hayo yafanywe. Na jambo zaidi bwana wakili kama ulivyosema ya kuwa, baada ya haya maoni tushatoa itakuwa mimi ni kazi ya bure maoni ninatoa sijui Katiba

ambayo nitakuwa nasema, ikiwa ninafanyiwa maovu, kudai haki yangu itakuwa ni urongo. Kama chakula ukipika halafu usikile kile chakula, faida gani itakuwa. Maoni yote tuliotoa hapa baadaye ile Katiba baadaye tupewe iwe booklet, ikiwa mtu amekwenda kinyume cha ile Katiba nijue kifungu gani nitapita kwa kumshtaki yule mtu. Lakini ikiwa sisi hatuna Katiba yoyote itakuwa ni kazi bure.

Jambo jingine ni mambo ya birth certificate kwa ujumla, karatasi ya kuzaliwa: karatasi ya kuzaliwa ilibidi vurugu kubwa ambalo hata mimi mwenyewe ni kama agent wa birth certificate hivi sasa. Imebidi muisilamu yeyote akitaka birth certificate sasa, mimi ni mojapo yatengeneza itabidi apply questionnaire karatasi moja.

**Com. Lethome:** Ngoja, unatengeneza birth certificate?

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Of course, yeah.

**Com. Asiyo:** Kwa nini, si vizuri.

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Si vizuri. Nasaidia.

**Com. Lethome:** Wasaidia.

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Imezidi muislamu yeyote akitaka birth certificate huyu huyu Ahmed Saidi ambaye ni Mchonyi sasa hapa mimi nasimama hapa mremere, itabidi apewe questionnaire, karatasi moja ya kuzunga kwa chifu, kwa sub-chifu, kwa DO na DC. Listen to me. Lakini Anderson akienda, mimi ni Anderson, itabidi wabwahe hapa hii karatasi yote. Itabidi ajaze form saa hii apate birth certificate. Mambo kama haya muyaangalie sana, yasije yakatoa rapsha mbeleni, maanake rapsha litakuja. Rapsha litakuja na tutailalo rapsha. Mambo mengine ambayo, la mwisho kabisa, ni mambo ya kwenda kwa bwana DC ama mawaziri wetu tuliochagua hawa wenye ngazi za juu, lazima ukifika ufanye appointment. Listen to me, ufanye appointment ya kumuona yeye, na kwa bahati mbaya ikiwa wewe hukuenda kama hivi hivi sasa na buni hali, sidhani kama utamuona DC maanake (….. inaudible), au ikiwa huna madaraka itabidi ungojee. Kwa hiyo sipati. Mambo kama haya yatufanya sisi tuwe chini sana, tutweza na nione sina imani na serikali yangu inayotawala ya Kanu kabisa. Imeingia fikira hata sasa mimi anakulihali Kanu sii-support, nitaenda opposition sasa mimi!

***Laughter:***

**Com. Lethome:** Basbas.

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Alakulihali mama, unaona mama Pheobe Asiyo, Member of Parliament for Karachuonyo.

Thank you mama Pheobe Asiyo. Nataka mambo kama haya alakulihali yarekebishwe katika Katiba. Nikitaka kumuona DC wangu, mdogo, mkubwa, mwenye cheo tupate mara moja kumuona, tumalize haja zetu *alaku li hali*. Lakini mambo zaidi uislamu utangamanishwe katika mambo yoyote haya. Be, mzee Ngeza hapo ulipo, ni mjombangu mimi wewe, lakini mimi sio muislamu ……. (in islam). Mimi na wewe twamoja bwana alakulihali. Thank you bwana.

**Com. Lethome:** ……(inaudible).

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Ahmed Saidi hapa, rafiki yangu ule wa …… (inaudible) ukamwambia hivyo……. (inaudible).

**Com. Lethome:** Umesema kusiwe na appointment ofisini. DC anawahudimia watu ishirini kwa siku. Sasa wewe uje tu kutoka huko ukubaliwe kuingia moja kwa moja?

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Very good, ndio haya yanafanya DC sasa anafurahi, maanake sisi tumekaa kwenye bench lakini amekuja mtu pengine yeye ana position fulani. Hayo si mawega, hayo hayo. Very good hayo ndio si mawega.

**Com. Asiyo:** Na wewe ulipokuwa councillor?

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Mimi nilikuwa nikifuata formalities. Siku zote mimi sikuenda kinyume. Mimi nilikuwa nikienda katika ofisi nikiona watu wakiingia. Nikiona bench kuna watoto mara ……. (inaudible) wangekataa ……… (inaudible).

**Com. Lethome:** Wewe mwenyewe ulikuwa ukiwahudumia vipi?

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Aah, mimi nilikuwa nikimwangalia mtu wa chini zaidi kuliko mtu wa juu, kwa sababu mtu wa juu hapigi kura. Mtu wa chini ndiye wangu mimi nilikuwa.

**Com. Asiyo:** Kwa hivyo ulikuwa unaangalia watu wa kura?

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Sana sana sana.

**Com. Asiyo:** Ulikuwa ukitafuta kura?

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Alakulihali ndiyo ilikuwa profession yangu lazima ni heshimu sio wale wadogo wadogo lazima niangalie. Lakini wakubwa pia nawajua kidogo namba, sio.

**Com. Lethome:** Haya, shukrani. Kajiandikishe kule bwana.

**Councillor Sha Mwa Rukia:** Asante bwana.

**Com. Lethome:** Mwaru Ferdinand. Mwaru Ferdinand, hayuko?

**Com. Asiyo:** Yuko, yule.

**Com. Lethome:** Halafu, Nyalle Katali, Nyalle Mwalewa yuko? Haya kaa chonjo wewe, baada yake.

**Ferdinand Mwaru:** Asanteni sana ma-Commissioners na wenzangu nyote, hamjambo? Maoni mengi yametolewa. Jina langu naitwa Ferdinand Mwaru. Maoni mengi yametolewa sana kuhusu ardhi, elimu, afya, IDs, na mambo yote hayo, lakini langu kubwa ambalo nataka kulisawazisha ni habari za vipande. IDs zimeleta ukorofi, zimeleta hongo, zimeleta kazi nyingi sana za ma-chifu na mambo kama hayo yote. Hapa kwa chifu kuna vitu ambavyo vinaitwa birth certificates, ambavyo hivi birth certificates zinatolewa sasa kutokana na chifu na book liko pale pale. Mimi ningeona Katiba hii iseme hivi, maoni yangu: anapozaliwa mtoto, akipata birth certificate yake, isiwe lazima kupewa ID, apewe passport moja kwa moja direct. Kwa sababu ikiwa ni mtoto ambaye amezaliwa hapa Kenya na anajulikana watu wake, haitakuwa nafasi ya msomali wa Somalia, si msomali wa Kenya, haitakuwa nafasi ya msomali wa Somalia kuja kuanza kuhongana mpaka yeye apate kipande, halafu yeye ndio apate tena passport. Kwa nini isiwe moja kwa moja, mtoto amezaliwa ni Mkenya, afanyiwe passport yake moja kwa moja. Kwani ujeramani na hapa tuna tofauti gani?

**Com. Lethome:** Haya endelea hiyo tushapata.

**Ferdinand Mwaru:** Haya, jingine ambalo ningeweza kulizungumza, ni ya huyu alikuwa first superintendent of prisons wa Kenya nzima. Na anajua magereza yetu vile yalivyo. Magereza yetu ni pahali pa uchafu mkubwa: Yamekuwa ni pahali ambapo amefungwa leo, kesho anapata HIV huko huko gerezani.

**Com. Lethome:** Pendekeza?

**Ferdinand Mwaru:** Napendekeza magereza yawe yanaweka watu ambao ni hard criminals na wale ambao wanafungwa leo ambao wana daraja ndogo, ili tuweze kuwatofautisha watu hawa. Kwa sababu kumeingia mambo mengi sana huku: Mtu amefungwa miaka ishirini, hajaonana na bibi wala mtu yeyote, anakaa huko anapelekewa kijana ambaye amefungwa miezi sita. They are bunched together na hapo ndipo kunakuwa na matata.

Pili, katika hayo hayo magereza ni kwamba wale watu wanaopelekwa kule ni watu ambao wanakwenda kufundishwa adabu. Warekebishwe adabu zao. Lakini utaona kwamba kurekebisha adabu kule ni kupigwa, analazwa chini, malazi hapati mazuri,

utamrekebisha mtu huyo namna gani? Ambapo wale kunguni, chawa na mambo hayo yote yanakaa katika hiyo gereza. Akitoka hapo hujamtengeneza huyo mtu, umezidi kumharibu.

Nataka kuzungumza juu ya ardhi ambayo ni hizi settlement schemes. Settlement schemes zetu zimekuwa ni uchumi na ukorofi sana kwa ma-ofisa wa kiserekali. Yaani sisi tumepewa settlement scheme, lakini utakuta pesa inayodaiwa na serikali ni nyingi sana, ambayo watu wa kawaida hawawezi. Ningependekeza ya kwamba, ikiwa kuna mgawanyo wa ardhi ambao ni settlement scheme, kwa nini watu wasipewe mara moja na title deeds zao? At the same time unapopewa shamba unapewa na title deed yako, ili kwamba hii itaweza kusaidia kwa sababu watu wanaweza kwenda kukopa benki mapesa, wakajifundisha kutengeneza mambo yao ya biashara, au mambo ya ukulima. Unakuta hapo inakuwa haiwezekani. Kwa hivyo mapendekezo yangu ni kwamba, kama ardhi ni ya serikali na inawapa watu, kwa nini wawafinye tena? Sisi kwa jumla tumekaa miaka thelathini miaka arobaini tumepata viwanja vya settlement, hatujapata titles mpaka dakika hii. Kuna nini hapo katikati?

**Com. Lethome:** Pendekeza.

**Ferdinand Mwaru:** Pendekezo langu ni kwamba, wakati unapewa title mpaka dakika hii ifutiliwe mbali ile fee, watu wapate titles zao.

**Com. Lethome:** Utaharakisha bwana Mwaru.

**Ferdinand Mwaru:** Mimi namaliza kwa jambo moja tu. Na jambo hili ni kwamba serikali imeweka sheria ya kwamba hakuwezi kuwekwa dispensary ikiwa si kilometa kumi apart. Na watu pale mbele ilikuwa hawana namna. Sasa dispensaries tunataka ziwe nyingi kwa pamoja. Health centres ni maili thelathini mpaka ukakute health centre. Ikiwa ni hospitali ni fifty kilometers. Sasa, inakuwa ina haja gani mtu atoke hapa maili hamsini aende akatafuta hospitali zile ambazo ni za kupelekwa wagonjwa ambao hawajiwezi zaidi? Kwa nini iwe ni maili hamsini? Tunapendekeza au mimi kwa maoni yangu napendekeza ya kwamba, tuwe na hospitali za karibu karibu. Sio hospitali ambazo hata ukitoka hapa ukifika Mombasa utakuwa ushakufa. Hospitali ziwe karibu na equipment za hospitali ziwe sawa sawa zote. Tunapendekeza katika hii Katiba kwamba hospitali zifanywe za kisawa sawa sawa.

Mwisho, napendekeza hata hiyo elimu ambayo inaambiwa tunasema kwamba iwe bure, lakini quality ya elimu. Tuwe na elimu ambayo hiyo inaweza kumsaidia mtoto hata akitoka kilasi cha nane, awe anaweza kuitumia elimu hiyo. Colleges zetu na universities zetu, we churn out thousands and thousands of students. Wakitoka hapo hakuna relevant education waliopata. Mtu amekwenda amepata elimu kubwa, huyu ametoka chuo kikubwa cha University, Nairobi, Egerton, wapi. Lakini haimsaidii elimu ile, haisaidii taifa hiyo elimu. Kwa nini kusiwe na quality education? Kwa nini tusipendekeze kwamba tu-train our people according to what the country needs. Tuwafundishe watoto wetu kwa kulenga ni kitu gani ambacho tunataka nchi hii ifanye kazi na elimu ile. Asanteni. Nashukuru.

**Com. Lethome:** Asante sana. Kabla Nyalle hujakuja. Amos karibu hapa.

**Amos Wamukoya Noah:** Asante sana nashukuru kwa kupata nafasi hii kupanga Katiba, maanake mimi nilizaliwa wakati Katiba inaundwa na mimi nashukuru kwa wakati huu nimepata nafasi na mimi kutoa maoni yangu.

**Com. Lethome:** Anza kwa majina, kamili.

**Amos Wamukoya Noah:** Naitwa Amos Wamukoya Noah. Mimi niko na maoni matatu tu, ambayo yananisumbua roho yangu. La kwanza, mimi ni kijana nafanya kazi katika Beach Hotel, nazunguka huku nikienda. Lakini kitu ambacho kinanishangaza mimi, ninataka Katiba hii ya mwaka huu ipangwe iwe namna hii. Wale wanaume ambao wanafanya ushoga, ambao wanatembe mtaani, kuwe na Katiba wawe wakipatikana wanafungwa kama maisha ya milele, ndani ya jela, ama wanahukumiwa kunyongwa. Kwa sababu wale nafikiri ndio wanaleta ukimwi katika dunia hii. Na ukiangalia unaweza katika Mkoa wa Pwani huu, ukienda mahali kama Lamu utakuta mwanamume mzima anakufuata fuata kama mwanamke. Hiyo tunataka Katiba iwekwe sheria watu kama wale wakipatikana wanafungwa maisha milele ndani ya jela, ama ananyongwa kabisa.

**Com. Lethome:** Huko jela tumesikia kuna hayo mambo pia huko.

**Amos Wamukoya Noah:** Jambo la pili, ndani ya jela, mimi mwenyewe nimekaa jela nimeshikwa karibu mara mbili nimekaa kule na nimeona shida za kule na naweza kukuelezea. Shida ambazo zinafanya wanaume wafanye mambo kama hayo kule, ni mambo kama sigara. Tunataka Katiba ipange jela kuwekwe vitu kama vile. Mtu anapelekewa majani ya chai, sukari, anapika chai kule wanakunywa, anapelekewa sigara, kiberiti, mambo kama yale yataisha kule. Lakini bila kupeleka vitu kama hivyo itabidi mambo kama yale yanaendelea kule na nje pia yanaendelea.

Jambo la tatu la mwisho, tunataka wakati tunachagua wabunge na ma-councillor wapimwe kwanza, maanake tunapata shida. Tunachagua councillor baada ya miezi miwili, ana ukimwi, anakufa, inabidi tuchague mwingine. Tunataka kwanza wapimwe, kwanza kabla hawajaenda, maanake tumepoteza ma-councillor karibu watatu hapa kwetu. Tuna mbunge wetu naye pia yuko hali hiyo hiyo, hatupati chochote huku. Tunataka kwanza wapimwe, tuhakikishe huyu mtu amepimwa, ndiyo anaenda kutetea kiti cha ubunge. Sina mengine, asanteni.

**Com. Lethome:** Mwalewa Nyalle?

**Nyalle Mwalewa:** Kwa majina yangu mimi ni Nyalle Mwalewa. Nina maoni machache hapa ambayo nitaenda kutoa. Jambo la kwanza ni juu ya neno ambalo linatumika au limetumika kwa mda mrefu katika serikali yetu ambayo tunaita liberalization.

Katika hali ya kuangalia kivyangu napata ya kwamba liberalization imeharibu hali ya kuwa sasa tunakuwa maskini. Kuna vyombo vingi tuseme kwa mfano kama sukari na vitu vingine vya agriculture ambavyo tumetegemea kikilimo sisi. Lakini tumepata hii liberalization imechafua hali ya kuwa zinaingia bila mpango. Sasa kwa mfano hapa, tulikuwa tukisaidika na kwa mfano Kilifi Plantation kuchukua maziwa. Hawa sasa Plantation haichukui kwa sababu kuna Dairy Products zinaingia kutoka nchi za nje. Kwa hivyo katika Katiba basi, katika hii term liberalization wacha ikatolewe. Kenya ikawe na mpango wake maalum wa kuangalia jambo hili, kwa sababu ikiendelea kama liberalization, tutabaki kuwa maskini hapa.

Lingine ni juu ya elimu: mimi mwenyewe naongea kama mwalimu, ningeomba hivi: wakati kama kuna mfumo fulani unakuja, au kuna mfumo kama huu 8-4-4 umeletwa na mwalimu akitoa maoni yake. Kwa mfano tuliambiwa masomo ni mengi yanaumiza watoto, ni lazima serikali ikachukue kama mwalimu anatoa maoni, kwa sababu yeye ndiye anaangalia mtoto, lakini kufikia sasa hakuna kitu kama hicho kwamba mwalimu anachukuliwa kuwa maoni yake ni muhimu. Kwa hivyo katika Katiba mpya iangalie kama mwalimu ni very important stakeholder.

Lingine ni juu ya banking ya pesa zetu. Kama tunataka kufufua uchumi, tutaufufua namna gani? Kama tunapora pesa zetu na tunazipeleka nje, kisha tunarudi tena tunaomba World Bank, IMF watuletee pesa? Kama tunachukua pesa tunazipeleka kule? Kwa hivyo hii ya ku-bank pesa nchi za nje should be cut. Kwa sababu kuna watu powerful wanapora pesa wanazipeleka kule, kisha tunasema hatuna pesa tunaomba pesa ya nje. Watu wanataka mishahara hakuna pesa. Kwa hivyo, wapendwa, kupitia maoni hayo matatu, wacha tushukuru, na ikiwa hivyo naona mambo yatakwenda mazuri hapa. Zaidi ya yote, majimbo damu.

**Com. Lethome:** Haya asante. Jiandikishe. Tumsikize Bwana Pancras Mwangala ndilo jina.

**Pancras Mwangala:** Basi kwa jina ni kama hivyo mlivosikia Pancras Mwangala. Mimi ni mkaaji wa hapa Kilifi na nilikuwa na oni moja tu, mimi la kuzungumza kuhusu mabadiliko ya Katiba yetu ambayo iko hapa hivi leo. Kwanza ni habari ya kuleta hii uchaguzi ambao unakuja. Kwa maoni yangu mimi naona huu uchaguzi ingekuwa vizuri sana kama ungefanyika na hii Katiba yetu mpya. Lakini hii Katiba ya zamani ambayo inaendelea hivi sasa, hatuiamini, si mimi pekee yangu, hata nyote nyinyi hatuiamini. Maanake kule nyuma tumeonyeshwa kuwa yule mtu anayetakiwa kule bungeni ndiye anayenda. Either upite ama usipite yule mtu anatakiwa kule anaenda. Kwa hivyo hii Katiba haina maana, ile ambayo inaendelea sasa. Tumekuwa na Katiba tumechagua hapo Ganze tukapeleka mtu wetu ambaye tulimchagua na akaenda kukataliwa huko, kwa hivyo ina maana gani? Kwa hivyo hii Katiba mpya hii tungechaguana, tungefanya uchaguzi na hii Katiba mpya. Hayo ndio maoni yangu, sijui wenzangu wanasema aje?

**Com. Lethome:** Asante, kuna swali.

**Pancras Mwangala:** Mfumo wetu wa utawala ambao ninaotaka ama?

**Com. Lethome:** Haya tumpate huyu Jonathan Mwadime. Haya, karibu bwana.

**Jonathan Mwadime:** Kwa majina naitwa Jonathan Mwadime. Niko na maoni yangu, mapendekezo yangu. Pendekezo la kwanza, serikali yangu mimi ni majimbo.

Pendekezo la pili, rasilmali za katika jimbo hili ziwe zinaweza kutumika hapa hapa bila kutoka jimbo lingine. Kwa mfano, kama mnazi, ningependelea ule mnazi ambao unagemwa hapa, ufanyiwe utafiti wa pombe tofauti tofauti na kiwanda kijengwe na co-operative zijengwe, mnazi ule ukigemwa upelekwe kwa co-operative, co-operative ipeleke kwa kiwanda, ili tuwe tunaweza ku-export pombe zile kama vile tunaona kama South Africa, Madagascar tuonaona malibu inaonekana mnazi ule unaweza kuleta pesa za kigeni katika nchi hii. Kwa hivyo tulipokuwa na kiwanda cha korosho pale, ilikuwa si rahisi kuona mwananchi anachoma korosho na hii mabamba hii. Kwa sababu ni pesa inabidi apeleke kwa kiwanda. Huu mnazi nao watu wanasema wanakunywa kiholela lakini wakati utakuwa unatoa pesa vizuri, unawekwa, unapelekwa kwa kampuni, basi, kusema ule ukweli, watu hawatakuwa wanakunywa vile wanapokunywa saa hii mpaka mtu anapigwa dafrao kule, kwa sababu itakuwa ni pesa zile. Kwa hivyo pesa zile zisimuue, zipelekwe kwa kiwanda.

Kitu chengine, hakuna mtu ambaye atajenga kwa watu, kwa hivyo DDC committee (District Development Committee) iwe itakuwa inafanyiwa kazi na wale watu ambao wanatoka katika hilo jimbo. Imagine, hii ni vote ya DDC imekuja, halafu watu wote wale ni wa kutoka nje. Wao watasema nini? Wacha tuchukue hizi pesa tuweke mfukoni twende, kwani hawa ni kina nani? Hatutajengewa. Lakini ni uongo, tuko tayari, hata kama chairman wa DDC atakuwa ni mgiriama wa hapa afanye nini, apore hiyo mali lakini atakuwa anapora mali wapi? Kwao. Na sisi pia kumrekebisha hi rahisi. Lakini yule wa kutoka kule nje kumrekebisha itakuwa ngumu sana.

Halafu jambo lingine, expatriates: sisi tumesoma hapa, tuna madaktari, tuna ma-accountants, tuna waalimu tuna kila kitu. Kwa nini basi kazi hizi kwa mfano, kule ma-hoteli kule tuna Kenya Utalii hapa tumeenda tumesoma, kwa nini kuje wazungu kutoka nje waje wachukue kazi hizi? Ninapendekeza kwamba kazi hizi ambazo tuko nazo, zisichukuliwe na watu kutoka nje eti wazungu wanakuja hapa wanatufanyia kazi hapa, wakati sisi tumesoma tunaweza kupata kazi kama hizo.

Kitu kingine kuna stakabadhi muhimu ambazo zinatakikana zipatikane. Hakuna haja ya kwamba mtu aende Nairobi, eti Nairobi iwe ndiyo headquarter mpaka kitu title deeds, haiwezi kutengenezwa hapa kwetu mpaka Nairobi, ndio itoke Nairobi ije hapa. Headquarters za Nairobi hatuna haja nazo. Tunataka headquarter iwe mahali popote pale, ile wewe ukienda unataka title deed yako, unaipata mara moja. Tunaweza kusema kuwe headquarter ni district level, district headquarter. Kwa hivyo iko karibu na mimi, hali ya kwamba nikifika pale nikitaka title deed yangu ninaipata mara moja siku hiyo hiyo. Si lazima niambiwe utaingoja hapa mpaka iende Nairobi, halafu inachukua miaka mitano kuipata.

Nyingine, kuna hawa vijana ambao tunasema wanarandaranda, ambao tunaweza kusema wakati mwingine huenda huko beach,

wanaitwa beach boys, wakatafute rasilmali zao kule. Lakini unakuta hawa hawapatiwi wakati mzuri na permit vizuri ili wafanye ile kazi kule. Na yule beach boy, ni beach boy katika mahali kwao. Kwa hivyo yeye ndiye anajua, mzungu akisema nataka unipeleke bush tour, anapelekwa bush tour na nani? Na kijana ambaye anatoka kule. Lakini sasa sisi tunasema ma-beach boys wale wasifanye ile kazi, tunatoa mtu kutoka Kenya Utalii ana tie hajui kwa Chondo ni wapi, halafu anasema nipeleke kwa Chondo. Anamuuliza mzungu: kwa Chondo ni wapi? Huyo mzungu sasa anamuliza kwa Chondo ni wapi? Tunataka beach boys wafanye kazi kule ambao wanatoka hapa mtaani. Tunazuia nini? Ili wasiranderande huku na huku. Ile ni kazi wapate, na wapatiwe kibali kamili cha kutembeza hawa wazungu na wakija hapa wazungu wakileta hapo wanaleta pesa nyingi sana wakija hapa kwetu. Kwa nini sasa mtu atoke Kenya Utalii kule aje hapa na tie yake na hata hajui kwa Chondo ni wapi. Kwa hivyo napendekeza ma-beach boys wapewe vibali vya kufanya kazi huko beach. Yangu ni hayo asante.

**Com. Lethome:** Twampata sasa Mwanderi K.W. Mwanderi hayuko? Zena Tuva. Violet. Hawa waliongea kina mama. Edith wa Mzungu, Benjamin Shida, Japheth Akare, Mohamed Kefa, Councillor Shah ashazungumza Councillor Shah, haya Abdalla Hamisi, Zakia Abdul, Jashon Auko, haya karibu Auko.

**Jashon Auko:** Mwanzo ninasema asante sana. Kwa jina mimi naitwa Jashon Auko, mimi ni mzaliwa wa mluo, kukaa nakaa hapa Kilifi. Na huu ni mwaka wangu wa kumi na sita kwa kukaa hapa. Mimi niko na machache tu. Mwanzo nataka kuongea kwa watu wa gari – sheria ya barabara. Ningependekeza watu waheshimiame kwa barabara ili ikiwa ukishanunua gari lako, usidharau mtu wa baiskeli. Kwamba hiyo barabara ni ya watu wa gari pekee yangu, kama uko na baisikeli yako wanakufyeka nje tu. Ili sheria, barabara ni ya kila mtu. Kama anakuja ajue mimi pia ni kama gari niko mbele na chombo ninapeleka anaweza kunipisha tu akienda zake, asije tu mbio ikiwa anaona hapo mbele hakuna mtu. Sheria iwe barabara ni ya kila mtu.

Ya pili, nitaenda kwa hii mambo ya salary. Ni aibu sana tena ndiyo inaleta mambo ya uchoyo kwa wananchi wa Kenya, kama mwenzako jirani saa ingine boss wake ama mtu fulani ametoka hapo kwao amemuajiri kazi, na yeye ni kama wewe anakula salary kwa serikali anajulikana kwa serikali kwamba yeye ni mwanakenya na wewe huwezi hata kupata salary kidogo. Ningependeza kwamba mtu kama huyu wasiwache watu wa Kenya wengine wale hawafanyi kazi kama si wakenya. Wakumbukwe, yaani serikali wajue wale pia wanaweza kupata kitu kidogo ikifika mwisho wa mwezi ya kulipia nyumba, ama awape watoto chakula, ama akanunue vitabu vile serikali sasa iko na matatizo ya pesa kwa upande wa shule. Mzee hana pesa, mama hana pesa, lakini ikifika mwisho wa mwezi hata miaka ishirini ijao hajulikani ni Mkenya, na mwenzake jirani pale anakula pesa, ananona na watoto wake wanakimbia. Sasa uchoyo unaingia, watu wanapigana juu ya hizo ili wapewe kitu kidogo kama elfu mbili, tatu, kuelekea, hapo mtu kawaida yaani hawafanyi kazi.

Halafu ya tatu, mimi nasema private hospitals, kwa upande wangu ni nzuri lakini zinaleta shida. Kama daktari anaweza kuwa amefundishwa hapa Kenya, amepata hiyo degree yake ya u-daktari hapa Kenya anajua mengi hapa Kenya. Kisha kurudi hapa hataki kufanyia serikali kule kwa hospitali anakimbilia ile hospitali yake ya private na nikipeleka mtu wangu yeye ana charge elfu ishirini ndio amtibu. Mimi ningependekeza kwamba watu kama hawa serikali ifutilie mbali private hospitals ili tupate wale

ma-doctor na ule ujuzi wao watusaidie wananchi zaidi, kama ingefaa.

Ya nne, mimi nasema mambo ya mortuary, upande wa hospitali hiyo hiyo, unakuta private mortuary kama ile ya Pandya hata kama ni Aga Khan, unakuta wale watu kama mtu wako amekufa ukienda pale, ametunzwa vizuri. Na ya serikali ambayo tunafikiri wako na pesa zaidi, unakuta watu wametupwa kuna mainzi ndizo zinatoka kwa watu, yaani hawajali watu wakifa wakipelekwa pale mortuary. Ili wawe waangalifu zaidi kwenye mortuary tukienda pale tuone kama ni serekali yetu wako na wanajali hata wale waliotuacha.

Nyingine, kuna ma-terms zingine tukiingia pale kwa bwana mtu anachaguliwa na President ambaye ni jaji, akifika pale anashika kalamu kivingine sana, kidharau tena. Ni kama mtu amesoma zaidi kukushinda, sasa anachora tu hivi lines zingine hata huwezi kusoma wewe, kujua kwamba hata kama masomo yako haikwenda mbele zaidi waweze kujua kwamba huyu mwenzangu ameshtakiwa kivipi na usome zile maandishi za jaji, hata huwezi ukafahamu ni ipi, yeye anafanya kuchora tu zile lines ndefu, kisha ananza kusema sections zingine pale kali na mwenzako anaona hivi, hata hajui anashtakia kwa nini na zile sections hatukufundishwa na hatujui ni sections gani na unastukiwa section four sijui ngapi ni miaka kumi na miwili. Sasa hizi ni vitu vinatushangaza sana tukiingina kortini wananchi wa Kenya, na tunapendekeza kwamba inawezekana ikiwa Tume hii inaweza kupitisha sisi tufundishwe vizuri, hata ukishikwa unaweza kujua fulani akianza kuzumgumza anaongea ile lugha unaweza kumjibu naye, maanake ukifika pale kuna mtu amewekwa pale anakutafsiria. Kukutafsiria ukijibu hivi ashakuchukulia ujeuri pale, ana kupandika miaka zake anazopenda yeye. Kwa hivyo upande wa jaji mimi nimepinga hivyo na ninapendekeza watu wa Kenya waelimishwe sana kwa hizo lugha wanazozitumia pale na hizo ma-sections zote za kuajibu watu wa Kenya.

Na President wetu tungependekeza, tunapata kazi ngumu wakati wa uchaguzi, sisi wananachi wa Kenya, vile huyu President mmoja yeye anataka u-President hapo hapo na wabunge saa hiyo hiyo. Sasa unakuta corruption inakuja maanake yule mkubwa anataka na watu wake, na yeye yuko na pesa zaidi na anajulikana, saa ingine anaenda huku, anaenda huku sasa corruption inatokea kwa sababu uchaguzi ni ya mchanganyiko sasa. Hatuwezi tukajua ni ipi nzuri ipi mbaya. Kwa hivyo ningependekeza Rais wetu avunje bunge ya President baada ya miezi mitatu, kabla hajavunja ile bunge ya wajumbe. Wajumbe wabaki pale wakilinda serikali na polisi na watu wa sheria. Na President apige campaign yake ya watu wa President. Kwa mfano, Kenya tuko na President Moi wale wanataka kama wakina Matiba wapige ile siasa yao ya u-President kwanza iishe tupate President wetu arudi pale bungeni pale State House ndio avunje bunge ya wajumbe, ili tukiregesha wabunge President will chagua miezi mitatu zilizopita. Ndio tutakuwa na amani zaidi.

Mwisho, nashangaa sasa kuna ma-professors, kuna ma-advocates na kuna wengine kama lawyers, hawa kama uko nao hivi vile tulivyo sasa, polisi hawawezi wakafanya ile heshima yao ya kazi yao, wale wanakuja wanashika watu kama hawa, wale waheshimiwa wanawafahamu kabisa huyu ni mheshimiwa anaachwa, yeye anaambiwa mheshimiwa wewe tunakujua, advocate fulani atatufuata, kwa hivyo wewe wachatwende. Kwa hivyo kosa ni moja tunafanya, tuko mahali moja na polisi anakuja ananichukulia mimi ili waende na mimi tena hawajali mimi ni binadamu, mmoja ameshika huku, moja ameshika mguu

wananirusha kwa gari wanataka kwenda na mimi, na wewe mheshimiwa unabaki pale, kwa sababu umeheshimika sana. Saa ingine watakwambia huyo ni councillor mheshimiwa, saa ingine watakwambia huyo anabaki ni advocate fulani. Na vile vile tukifika nao pale kuna wengine pale hawajui kosa gani imekuleta pale, aanza kupiga kelele kwa station, huyu ni mjinga sijui nini angalia nywele, sijui nini sasa unatukanwa.

**Com. Lethome:** Sasa unapendekeza kitu gani kifanywe?

**Jashon Auko:** Mimi napendekeza tukifika mahali kama hapo polisi wafanye kazi yao vile walivyofundishwa. Kama ni watu wamepatikana kwa makosa wote washikwe na wakipelekwa pale, sio kufungua ile milango na pesa. Maanake ukiingizwa ndani ya seli pale utoke pale eti uandike statement yako ni pesa tena, iwe huru. Ili kama mtu wako amekuja kukuona wasifukuzwe wananchi kuona mtu yao, wala wanaanchi wakifika pale polisini sio mahali pa kifo.

Ya mwisho, tumeona mengi sana kwa upande wa jela. Kama mtu ashagonjeka sana mpaka amekuwa na upele, ateremshwa hivi anapelekwa hospitalini anaambiwa unasikia hapo anatembea pole pole wanaona wanawacheleweshа wale watu wa askari jela. Ndio anapigwa na anamalizwa hapo, kisha wanasema ni ile ugonjwa ndio ilizidi kumuua na anampiga tukiangalia namna hii. Kwa hivyo jambo kama hii mtu kama amepelekwe jela na amepata ugonjwa pale, lazima apewe heshima ya kwamba ni ugonjwa sio kupenda kwake. Lazima apelekwe kwenye hospitali atibiwe vizuri, sio eti kumdhulumu na kumuua hapo hapo, kabla kifo chake hakijafika. Asanteni.

**Com. Lethome:** Haya asante sana Jashon. Tupatie hiyo memorandum na jina lako. Tunamtaka sasa Charles Mwango, Mwango Charles yuko, hayuko? Tumpate sasa Beatrice Lewa. Sijui kina mama walipewa nafasi zao wakatoroka. Kuna Donald, Donald Ngambo nafikiri alizungumza. Aliongea. Justo Nyaga.

**Justo Nyaga:** Kwa jina naitwa Justo Nyaga. Mimi nafikiri nitaongea kuhusu hawa watu tunaita casual labourers wa serikali. Katika sheria ambazo tuko nazo na ni wengi Kenya nzima naona wanadhulumika sana. Itawezekana aje mtu afanye kazi kama miaka kumi halafu asipate kazi? Katika sheria zilizoko za labour, zinasema ukifanya kazi miezi mitatu unafaa uajiriwe kama mtu permanent. Sasa ukiangalia kuna watu wengine ni technical labourers na wana ujuzi. Sasa wanakuja wanabuni form eti unajaza ku-renew contract after those three months ambapo labour inakubali. Sasa ikiwa uta-renew ile contract ufanye hata kama utafanya miaka zaidi ya kumi, kwa nini serikali isiangalie huyu mtu ako technical na aweze kuajiriwa? Malipo ni maduni, ningependekeza walipwe vizuri.

Jambo lingine, hakuna house allowance. Watengenezewe. Hakuna medical cover hakuna. Nafikiri kama tunavyoenda hivyo casual labourers hapewi haki yake kwa sasa, na kama wengine wamenituma hata wamefanya kazi miaka kumi. Una-renew contract na hujulikani, ukiangalia waziri hajui, PS hajui, ukiangalia kama ni wakubwa hawafuatilii. Ukienda unasikia mwishowe unaambiwa eti serikali haiandikani. Sasa kama haiandikani je, kwa nini wasiguduliwe na mnahitaji msaada wa huyo mtu, ya nini

mumuweke? Hiyo form unajaza ningependekeza labour waiingilie kati, na waweze kuandikisha wafanyi kazi wa casual labourers. Wapewe kila kitu kama wale wengine. Haya kuna kwanza.

Kuna hawa wengine tunaosema hawa wakubwa kama wa vyuo vile, ningependelea mtu asiwe na chuo kimoja, kama ni principal, kama ni nani, yaani wakuu wa vyuo hawa. Kama ni wengine mtu asikae pahali kwa miaka tuseme miwili, ndio kusiwe na ufisadi, upendeleo na ukabila, usiweze kudumu hapa. Wakiwa katika idara za serikali wanabadilishwa badilishwa ndio tumalize huu ufisadi.

Haya, mambo mengine ni ya kuonewa na ukabila: katika utendaji wa ukabila ningependa sheria itiliwe mkazo sana. Mtu kama ni ufisadi na kuoneana iaangaliwe. Ukipatikana ukifanya hiyvo uchukuliwe hatua. Kuhusu mambo ya askari. Askari nafikiri sijui kila mtu anarudia. Hiki kikosi kinataka watu sijui achaguliwe Commissioner mwingine ama ziwe scrapped, sijui tutafanya nini. Haswa akiulizwa anatudhulumu sana.

**Com. Lethome:** Wapendekeza wafanyiwe nini?

**Justo Nyaga:** Mapendekezo mimi naoina wapelekewa thorough cleaning na waweze ku-compare katika training waambiwe wa-compare majirani wenu Tanzania.

**Com. Lethome:** Kunao watu wanasema wakiwa polisi wako brutal kwa sababu wanapata mshahara kidogo, wanasikia uchungu na raia, wasema aje?

**Justo Nyaga:** Mimi pia ningependekeza sijui kama mshahara mkubwa utawasiadia. Mimi naona ni training na wachukuliwe nidhamu. Maana hata kama kuna mshahara mkumbwa, utataka nyingi zaidi, mwanadamu haridhiki. Uta adjust na uone ni kidogo, sasa ningependa wachunguzwe sana katika kazi, utendaji wa kazi yao. Na kama unakosa, ujue kweli unaandikiwa kulingana na ile sheria na kikosi haswa wale wakubwa waangalie, wadogo ndio wana shida sana.

**Com. Lethome:** Ungetaka polisi mdogo akikukosea unataka uende ukamshtaki kwa nani ama ukalalamike kwa nani?

**Justo Nyaga:** Mimi vile ningeona tuwape hawa kama ma OCS uwezo.

**Com. Lethome:** Unataka polisi mdogo akikukosea unaenda kulalamika kwa polisi mkubwa?

**Justo Nyaga:** Wale wawe strict na wanaangalia kweli malalamishi, maana tutaenda wapi tena na hawa ndio…(inaudible).

**Com. Asiyo** Si yeye atapelekea mwenzake?

**Justo Nyaga:** Sasa wakubwa waangalie kwa maana lazima yule ndiye atakuwa na hiyo policy. Nikisema sitafanya naye, kwani huwa wanatenda kazi vizuri wale wana…..

**Com. Lethome:** …… (inaudible). Kwa mfano, polisi mdogo ambaye ni constable amekukosea amekudhulumu, sasa unasema uende ukalalamike kwa ule mkubwa, si huyu ni polisi na yule ni polisi? Wote ni polisi?

**Justo Nyaga:** Sasa hapo ningependa kama ndio hivyo yule mtu atakayekuwa anawakilisha karibu sana nafikiri ni councillor. Councillor wanapewa uwezo mwingi sana, maana ndio wako karibu na mimi. Kama ni wewe kuna sehemu zingine hata yeye anapuuzwa. Awe ana uwezo mkubwa sana maana mimi ndiye nimemchagua, yeye ndiye anajua shida yangu. Apewe uwezo zaidi councillor, maana ndiye aliye karibu na mimi sana, awe na uwezo.

**Com. Lethome:** Sasa kuna ofisi ambayo inaitwa ombudsman ambapo hiyo ofisi mwananchi akidhulumiwa na polisi au mfanyi kazi wa serikali, anaenda kulalamika hapo. Sijui unaona aje?

**Justo Nyaga:** Katika hivi tulikuwa tunatumia hiyo njia, Kenya tunatumia hiyo njia kweli, councillor ndiye mwakilishi. Lakini sasa hata hiyo mimi ningependekeza maana kama vile wananchi hatuna imani yaani, na si vizuri hatuna imani. Maana kila mtu hata akituombea tunaenda hivyo hivyo.

**Com. Lethome:** Haya asante bwana Nyaga. Sasa tumpate Samson Ndoro. Karibu Ndoro.

**Samson Hassan Ndoro:** Asante bwana chairman na watu wote walioko hapa. Mimi sina mengi sana ya kusema. Kwa majina mimi ni Samson Hassan Ndoro. Sina mengi ya kusema isipokuwa jambo la kwanza mimi, napenda kupendekeza mfumo wa serikali ile inayokuja iwe ya majimbo. Pili, kuhusu elimu, napendekeza kwamba elimu, ningetaka hata iwe form four ya bure, lakini pengine kwa sababu serikali kulingana na wakati ilipata uhuru na matatizo mengi ya serikali anayo pengine haitawezekana. Lakini ingekuwa iwe ya bure kutoka nursery school mpaka standard eight na kisha hii system ya 8-4-4 kama inawezekana serikali ijayo iigeuze, kwa sababu inaonekana inawapa kazi nyingi sana watoto hata inakuwa ni vigumu sana wao kujua wanafanya nini. Na pia, mwisho kabisa kuhusu elimu ningependekeza kwamba, watoto wanaenda university wakiwa wadogo zaidi, na hata wanaleta mafujo mengi kule, mambo ya migomo migomo. Nafikiria maturity age ile ina-matter pengine kwa masomo pia. Kwa hivyo wangefika wakiwa mature kidogo zaidi kuliko hivi sasa ingekuwa vizuri. Kwa hivyo ningependekeza serikali iangalie hatua za kuchukua ili watoto wafike university wakiwa at least miaka ishirini, mtoto aingie university ingekuwa vizuri.

Kitu kingine ambacho nilikuwa napendekeza kuna watu wengi sana hii Kenya hawana kazi. Na imeendelea hivyo sasa kesho baada ya kesho nyingine wanakuwa wengi zaidi. Lakini mimi naona hapa kuna tatitizo ambalo pengine kama serikali ingefikiria

ingepunguza hawa watu ambao hawana kazi kidogo. Kwa hivyo napendekeza kwamba serikali ile tukayopata tena ama Katiba hii ambayo tunaunda sasa wapendekeze kwamba mtu mmoja kazi moja, kwa sababu hii ya kuwa mtu, mtu mmoja anapewa kazi kule ni Chairman, huku ni Permanent Secretary, huku nini, hii inaleta kwamba sasa inakuwa hiyo national cake anakula pekee yake, wengine wanakosa kabisa na wanakuwa wezi. Kwa hivyo kazi, mtu moja kazi moja ingekuwa vizuri sana.

Na pendekezo langu la tatu ni kuwa ni habari ya umaskini: umaskini tunaona kwamba tofauti baina ya mtu watu hapa Kenya imekuwa kubwa sana baina ya wale matajari na hawa maskini. Na sababu kubwa ni kwamba utakuta katika kama ni kampuni watu wakifanya kazi, utakuta yule mtu anayelipwa chini ni kiwango cha chini zaidi kuliko yule wa kule juu. Kwa hivyo, ningeomba Katiba hii inayokuja ama hata serikali inayokuja ningependekeza kwamba watu wa chini wainuliwe kidogo ili waweze kujimudu katika maisha, kwa sababu naona wengine wanapata hata elfu mia moja na mwingine analipwa elfu sita. Sisi sote tunaenda tunanunua nyama kilo mia moja ishirini, sasa hiyo tofauti sioni kwamba yule apewa pesa nyingi zaidi. Kama ni elimu amesoma, tunakubali amesoma zaidi, lakini kusiwe na ile tofauti kubwa sana ya kimishahara. Tafadhali sana ningeomba hiyo ifikiriwe.

Na kuhusu poverty eradication: serikali imeleta huu mradi ambao tumeona ni mzuri, lakini naona kuna vipengele vidogo ambavyo vinaachwa. Haswa tunakuta katika poverty eradication huyu maskini mwenyewe ambaye ndiye anatetewa ili ainuliwe kutoka maisha ya umaskini mpaka awe kidogo nafuu, anaachwa, hahusishwi katika hii mipango. Sasa utakuta wale wakubwa tayari ambao ndio wana pesa nyingi ndio wanapewa hizi nafasi za kuendesha hii miradi na pesa zinamalizika kabla hazijamfikia yule maskini. Sasa mimi napendekeza kwamba pengine kidogo serikali ingefikiria kununua hata kama ni matingatinga kwa division, ili yule mtu wa kawaida awe anaweza akalimiwa shamba lake, akalimiwa hata kama ni kwa njia ya mkopo. Anaweza akapata mahindi mengi zaidi. Wakati akipata mahindi aanze kulipa serikali, maanake ziko njia za kufuata kupitia ma-chifu, ma sub-chifu watajua nani amelimiwa na amepata chakula cha kutosha. Sasa wakati akipata mavuno awe anaweza kulipa ule mkopo. Sidhani kama kulimiwa kama acre nne mtu na tingatinga ingekuwa ni pesa ambazo zinaweza kumshinda kulipwa. Anaweza akalipa na atakuwa amepata chakula kingi, kwa hivyo itakuwa pesa zake anaweza kuzitumia kulipa serikali baada ya kununua chakula. Hili ni pendekezo lingine ambalo nilikuwa nalo.

Na kuhusu pombe ya mnazi, mimi si mnywaji wa pombe. Kwetu kuna minazi mingi sana, mimi natoka sehemu ya Kaloleni, na sijanywa pombe ya mnazi. Na si kwamba naichukia, lakini mimi naichukulia pombe ya mnazi kwa watu wa mijikenda ama watu wa hapa Pwani, kwamba ingekuwa ni kiungu kimoja cha kufanya sisi tupate maendeleo. Sasa kwa sababu inadharauliwa sana utaona kwamba sisi hatupati hayo maendeleo ambayo mnazi ungefaa utupatie, kwa sababu pengine watu wengi wanaichukulia kivingine maanake kwa mimi sioni tofauti ya ulevi wa pombe ya mnazi na ulevi wa bia. Naona watu wawili wakilewa kama moja amekunywa bia na mwingine amekunywa mnazi. Nafikiria ulevi huo ni sawa tu, lakini sasa utaona watu wengi wanachukulia kama mnazi ni kitu kingine hafifu sana. Kwa hivyo mtu akinywa mnazi ni kama kudharauliwa; yule anakunywa bia ndiye mtu sana. Lakini sasa lazima tujue kuna hii tofauti ya mifuko yetu. Ikiwa mimi mifuko yangu hainiruhusu kuingia bar kununua chupa ya bia, basi mimi naingilia kwa pombe ya mnazi, sababu kidogo iko nafuu. Sasa ile inampatisha yule mtu

ambaye hata hanywi, kama mimi nina minazi, sasa na mimi sinywi. Inafaidisha napeleka na mimi mtoto wangu shule, maanake sina kazi. Lakini sasa ukisema mnazi usigemwe na usinywewe, sasa hapo mimi nitakuwa nimepata hasara, ijapo mimi nina minazi lakini sasa haugemwi mpaka hatuna factory tunauza. Ni hizi za kudanganywa danganywa wanauza nazi moja moja shilingi mbili, sasa hatufaidiki kwa hii minazi yetu. Kwa hivyo naomba napendekeza kwamba serikali hii inayokuja ifanye utafiti wa minazi, ili wale wenye minazi waweze kufaidika na tuweze kuendesha watoto wetu kwa mashule, kwa sababu huku kwetu hatuna kahawa. Hii minazi tunachukulia kama ndio kahawa yetu, kwa hivyo na sisi tuweze kuendesha watoto wetu kwa elimu. Asanteni kwa hayo machache.

**Com. Lethome:** Haya asante Bwana Samson. Maina Mwamuye ameongea. Sasa tunampa nafasi Nelsom Tsuma, karibu Tsuma.

**Nelson Tsuma:** Shukrani Bwana Commissioner na wenzako. Majina ni Nelson Tsuma kama vile ulivyoyataja. Nitapiga haraka haraka kwa sabubu naona ule muda umetuwekea wa dakika tano, mimi ni msemaji kwa sababu nimeajiriwa na kazi ya kufundisha wenzangu, basi naweza kuongea vizuri sana. Lakini nitapiga pale muhimu muhimu ambapo nimeona panastahili. Kwanza, kazi yenu hii ya kwamba iongezwe muda mimi binafsi kama raia ningependelea iongezwe muda kwa sababu kutengeneza hii Katiba yataka muda wa kutosha. Kisha basi, waona hawa watu wamekuja kidogo wana makosa moja ambao lilifanywa kwamba, wameambiwa kufundishwa kule kijijini, kazi yao haijafanyika. Mimi mwenyewe natoka Kinango, Kinango nimekaa huko, sikuona hawa watu waliokuja. Tunafundishwa kwa mashule. Ningelipendekeza kwamba ikiwa tupate Katiba nzuri ni watu wafanye kama vile ile campaign ya census – door to door, watu waelimishwe kule nyumbani ndio wajue. Kuna wakati nilikuwa na hawa watu wa kufundisha. Hawajaelimika vya kutosha. Yeye mwenyewe hajui ni mwaalimu kisha amewekwa pale, atafundisha nini? Watu walikuwa ni wapate watu ambao wameelimika vizuri, wafundishwe kwanza hii Katiba, na ni kwa nini igeuzwe wapate kuelewa. Halafu utaona ni wengi. Angalia hii ni Pwani nzima. Basi, mambo ambayo yanahusu Constitution nzima ya Kilifi, pengine ya Bahari watu hukuja ni handful. Shameful. Na ni mambo ambayo yanawahusu hawo watu. Kesho tunaondwa na Katiba ambayo tulitengeneza wenyewe na saa hii watu wamekuja kumi jamani. Mkiongezewa muda, sisi tunaomba huku, mpewe muda zaidi, na hii kazi ifanywe kwa sababu isiende haraka haraka kwa sababu ya elections. Elections kama ni kubadilisha, wageuze kile kiungo cha mambo ya election, ikipita huko mpewe muda. Ikaliwe vizuri sana, watu waelimishwe vizuri sana zaidi ya vile wamefanyiwa. Nisiendelee sana.

Upande wa utawala: provincial administration: ningalipendekeza hivi kwamba, kwa sababu wale wengine PC, DC, DOs wanakuwa transferred, hawa wengine chifu, sub-chifu kuna watu wanaowatawala wengine kwa sababu ya ubinadamu wamekosea. Tungaliomba kwamba ile Katiba ikiwa itakuwepo, hii ambayo tumetayarisha leo, chifu aweze kupewauhamisho si kwa district lakini katika ile division ya kwao. Ikiwa ni sub-chief naye katika hivyo hivyo, katika ile location kwao pengine wana sub-location kama tatu nne hivi. Hawa wanaweza lea miaka mitano hapa miwili pale kwingine pale. Katika hali ile ile tutaweza kuwarekebisha in case kuna mambo ya makosa wanavyofanya.

Upande wa legislature: upande wa diwani, councillor tungaliomba kwamba au binafsi ningaliomba Katiba inayokuja kwamba

hawa ma-councillor wengine wakiwa huku mashambani wengi hawajasoma. Tunapo musomo ambao ni mfumo ambao tumeingilia sasa, mambo mengi yanahitaji watu ambao wamesoma. Hawa mabwana wasome kufikia at least kidato cha nne. Wale wa kupiganiwa ubunge at least awe ni form four, awe ameenda zaidi amepata kama diploma, advanced diploma na awe anakiba pengine ya degree sio vibaya. Na kisha wakishapewa zile kazi serikali ile ambayo itakuwepo, au ile Katiba iwe inasema kwamba katika zile ikiwa ni constituency headquarters yao, wawe na permanent office. Ikiwa ni councillor naye awe katika ile ward ana permanent office, akitoka yeye councillor mwingine atakuja akalie ofisi ile ile.

Kuhusu mambo ya mashamba: watu wamezungumza kuhusu mashamba ambayo pengine watu hawa ambao wanatoka hapa katika coastal strip wanazungumza mambo ya squatter nini. Pengine mimi sina ujuzi sana wa squatter lakini kule sehemu ambayo tunakaa, inaambiwa ni reserve. Tungalipendelea kwamba kuwe na title deeds kwa Mkenya yeyote ambaye ana ardhi, kuwe ni reserve mambo ya reserve yatoke, ikiwa ni mambo ya mascheme yatoke, lakini uwe mahali mtu anapokaa Mkenya yeyote apewe title deeds.

Halafu kuhusu mambo ya sheria courts: ni kwamba tumeangalia kuhusu mambo ya pengine hata urithi, kwamba kila moja anapokaa hapa anazungumza mambo ya urithi kulingana na kabila yake au na community anayotoka. Ningali ninapendekezwa hivi kwamba, kila community kwa mfano, Giriama itengeneze sheria zao za mila zao. Na kuwe na korti zao. Incase mtu akikosea na aseme ni utamaduni, uwe katika ile korti ile utamaduni ule wake utazumgumzwa pale. Mimi nitaenda kusema ni mduruma, utamaduni wetu wa urithi wasema hivi, unakosana na mwenzangu ambaye ni mkikuyu, urithi mambo ya utamaduni wao ni tofauti. Sasa katika kama wilaya iwe kuna korti hizi ambazo zinashughulika na mambo ya utamaduni wa watu na mtu akisema mambo kesi hii iko katika kiutamaduni iende katika korti ya kitamaduni.

Upande mwingine, nipe radhi bwana nimalize point zangu nne. Watu wamesema kuhusu limits za President, naunga mkono wale wenzetu kwamba zile powers zake nyingi zipate kupunguzwa na zieendelee kulingana na kila wizara fulani kuwe kuna mambo yake yataangaliwa. Halafu nilikuwa na booklet kuhusu mambo ya land hii ya Mazrui. Mambo haya ya Mazrui ni ya kitambo na imeshangaza wengi na hutu tunakaa hapa na imedhulumu wengi, kwa sababu hasa ardhi hii ya Pwani ina shida kwa sababu kuna mambo ya Mazrui, the coastal strip. Nilikuwa napendekeza hivi kwamba ile sheria ile iwe nullified kutoke sheria mpya na mambo ya coastal strip, Mazrui, sijui family in maasai land yaweze kukataliwa, tuwe na sheria mpya ambayo hii ardhi ipewe title deed kulingana na mtu anapokaa au kulingana na vile sheria imesema haiwezi kuipata. Halafu mahali pengine ni kwamba, kwa wenzetu ambao pengine hushikwa na kosa wakawa ni wafungwa. Ukienda kortini kuna wengi mtu hajui sheria, pengine hakusoma hata akiulizwa na jaji hawezi kujieleza. Ningelipendekeza kwamba kuwe serikali inaweza kupeana wakili wa yule raia, anapoenda kortini awakilishwe na lawyer kwa sababu hajui sheria, na hawezi hata kujieleza. Kuna mtu kisa mfano kilifanyika mahali, anaulizwa, akanyamaza hajui lolote. Akaambiwa yeye ni mjeuri akafungwa miaka kumi na mitano kwa sababu ya kuwa mjeuri, na alikuwa hajui afanye nini. Lakini kama angekuwa na wakili amsaidie huyu mtu angalijitetea vizuri. Kisha ningelipendekeza kwamba katika hawa watu wa military police na administration police, hawa wote wa prison, wanapokosa kuwe kuna disciplinary body ambayo inaweza kuwarekebisha tu kama wale. Wasifungwe kama wafungwa

wengine, wawe na body yao warekebishwe kivyao kwa sababu hawa watu ndio tumewapata kwamba wengi wanahusika na hii robbery with violence, kwa sababu ni watu wamehusika na machineries hizi kama bunduki, nini nini. Lakini wakishapata mahali kwao hufungwa wanapokosea na kufanyiwa hali fulani ya urekebishaji. Nafikiri wale watu ikiwa watapata bodies nzuri ambazo zitakuwa zina wa-discipline hawawezi kuja tena huku kwa kutuibia bihdaa kama wanavyofanya.

Tena mfumo huu wetu ambao tunao, mimi binafsi ambao nautaka ni ule wa majimbo, federal government, na wengi wenzangu wamezungumza ndio huo. Mengi ni kwamba mahali kwa biashara nilikuwa napendelea kwamba Katiba itakayokuja ni mengi ambayo yanatusumbua tunapotengeneza Katiba ni kwamba, kuna mengine lazima tuangalie: sheria za kimataifa, mambo ya biashara: Lakini kwa sababu ya mambo ya Kenya ningalisema kwamba control of prices kwa zile bidhaa ambazo ziko muhimu kwa mfano tuseme sukari, unga, nini. Katika ile Katiba ambayo itatengenezwa je mambo kama yale yaregeshwe kwa sababu itafanya yule mwananchi wa kawaida asaidike kidogo. La mwisho.

**Com. Lethome:** Naomba, haya, basi la mwisho.

**Nelson Tsuma:** La mwisho, ni kwamba upande wa elimu, kuna waalimu wa nursery watu wasema ni muhimu sana kwa sababu hawa ndio watu wa elimu ya msingi. Kwa nini serikali inayokuja ama Katiba ambayo itatangenezwa waalimu kama wale wasajiliwe na serikali, waache kuajiriwa na local government. Ni hayo asante Bwana Commissioner.

**Com. Lethome:** Haya asante sana. Peana memorandum huko. Sasa tumuite bwana Benjamin Kabwere. Haya yale ulikuwa unataka kuzungumza sasa yazungumze sasa.

**Benjamin Kabwere:** Hata hivyo ninashukuru sana kwa sababu nimepata hii nafasi ya kuzungumza kitu kama hiki, kama mimi mtu mzima namna hii. Kwanza kitu kimoja.

**Com. Lethome:** Anza kwa jina lako.

**Benjamin Kabwere:** Jina langu naitwa Benjamin Kabwere Ngonyo. Mimi napendelea namna hii. Kwanza mimi mwenyewe nimefanya kazi kutoka mwaka wa sitini na tatu na nikaacha kazi na sijapata pension, pia mimi ni pensionable na sijapata pesa kutoka nitoke. Hiyo si kitu, nayo mengine.

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini?

**Benjamin Kabwere:** Napendekeza kwamba mimi nipewe hata wengine pia nawapate zile pesa zao ambazo ni za kufanya kazi miaka mingi.

**Com. Lethome:** Zisiwe zikicheleweshwa?

**Benjamin Kabwere:** Zisiwe zikicheleweshwa. Mimi sijapata lakini wengine isiwe hivyo.

**Com. Lethome:** Endelea, endelea.

**Benjamin Kabwere:** Na tena kitu ingine ambacho nimekisikia nimekasirika sana au nimeona vibaya kama mtu mzima, ni kwamba hii habari ya family planning, yaani watu wasizae sana, watu wasifanya namna hii namna hii, hiyo kitu nimesikia ubaya tena nimekiona mimi mwenyewe nimefanya nursing miaka hiyo thelathini na sita. Na nilikuta mtu mmoja amekuja kwetu hospitali anataka kufungwa kizazi ana watoto wanne akafunga ana watoto wanne. Mwezi ulipomalizika akaja na mtoto wake anaumwa yule wa nne, akafa wakabaki watatu. Baada ya kubaki watatu akaja tena, mtoto wangu anaumwa, ni wangapi? Bado watakuwa bado wawili. Anaanza kuzungumza je, nimefungwa kizazi mimi. Kumbe mtoto wangu atakufa na huyu pia naye anaumwa, pengine atakufa huyu. Nikaambia hapana Mungu yuko hatakufa. Kwa hivyo napendekeza namna hii, hii habari ya family planning hiyo ingewachwa kabisa, maana watu hawakufika kwa Mungu kusema watabaki wanne na wataendelea kuwa wanne. Mnanicheka?

**Com. Lethome:** Twakubali maoni yako bwana. Twakubali maoni yako mazuri.

**Benjamin Kabwere:** Yaani anasema mimi nataka wanne na halafu mmoja amekufa. Amekufa na mtoto mwingine tena, tumemfunga juzi kumfunga azizae, maana yeye ana wanne.

**Com. Lethome:** Hiyo tumesikia. Haya endelea..

**Benjamin Kabwere:** Basi, kwa hivyo hiyo napendekeza kwamba hivyo kama hii serikali inayokuja mimi nataka majimbo.

**Com. Lethome:** Na ile ya kutoa mimba?

**Benjamin Kabwere:** Na ile ya kutoa mimba hata siipendi kabisa, napendekeza kwamba siitaki, maana mtu si Mungu; anayejua ni Mungu. Ni wangapi ambao hawazai na wanataka kuzaa?

**Com. Lethome:** Endelea.

**Benjamin Kabwere:** Kwa hivyo tafadhali sijui ikiwa nasema mimi pekee yangu, lakini hivyo ninavyozungumza ikiwa hata wale ambao wamezaliwa na Mungu, basi nao wana akili kama zangu, iwe hii kitu iachwe kabisa.

**Com. Lethome:** Ni wagani wamezaliwa na Mungu?

**Benjamin Kabwere:** Wamezaliwa na Mungu kama mimi vile nimezaliwa. Si nimezaliwa sikujua nitazaliwa na nani?

**Com. Lethome:** Haya. Wameumbwa na Mungu.

**Benjamin Kabwere:** Hapana. Wameumbwa Adam na Eva pekee yake, lakini mimi nimezaliwa.

**Com. Lethome:** Na mzazi wako.

**Benjamin Kabwere:** Eeh mimi nimezaliwa na mzazi wangu. Kwa hivyo mama amezaa mimba kumi na sita, na bibi yangu amezaa watoto kumi na nane wa kwanza, wa pili akazaa kumi na sita na ninao mpaka leo.

**Com. Lethome:** Haya pendekeza.

**Benjamin Kabwere:** Moja ndiye yule unamuona pale, eh kale kanakoinama pale.

**Com. Lethome:** Nilikuwa nafikiri ni yule mwingine.

**Benjamin Kabwere:** Yule wacha na kofia yake. Kwa hivyo hii family planning hii ningependa iondolewa kabisa.

**Com. Lethome:** Mtu azae watoto wengi awezavyo?

**Benjamin Kabwere:** Mungu ndiye anajua, hakuna kusema kwamba ni wengi. Wala ukisema ni wengi mbona hujiui ama ukauawa huyu akabaki, wale wanaokuja?

**Com. Lethome:** Haya pendekeza jambo lingine.

**Benjamin Kabwere:** Basi mambo ambayo nilikuwa napendekeza ndiyo hayo, na tena kitu nasisitiza kabisa ni habari ya watu waache kazi na wasipewe zile marupurupu yao, kama mimi.

**Com. Lethome:** Hiyo ulianza nayo.

**Benjamin Kabwere:** Lakini kwa sababu naitaka sana, ndio nizungumze tena.

**Com. Lethome:** Haya.

**Benjamin Kabwere:** Lingine, nafikiri kwa vile sikupanga.

**Com. Lethome:** Na hizi mila za kigiriama kama ile kuhalwa na zingine unasema nini?

**Benjamin Kabwere:** Mila za kigiriama unajua kusema kweli mimi ni mtu mzima na nimeona uzuri na ubaya. Wajua maana ya mtu kusema mtu amekufa, ndugu ya mtu amekufa, na ameacha bibi yake. Sasa yule bibi asipowekwa vizuri itakuwa atazaa, yeye hatapenda kuzaa maana kuzaa ni kwa kawaida, na atazaa awe hana mtu ambaye ndivyo ndugu yake pengine amemweka kama wake. Sasa akizaa, vile akizaa tu, inaonekana kwamba huyu mtu amezaliwa hapa lakini si wa hapa, hata urithi hawezi kupata. Ambapo mimi leo nikijificha kwake nikimchukua itasemekana babake amekufa, lakini huyu mwanamke akachukuliwa na ndugu yake yule aliyekufa. Kwa hivyo hajaitwa mgeni, yeye anaitwa ni mtu wa pale. Kwa hivyo kule kumchukua, sio kumchukua kwa sababu tunapenda …

**Com. Lethome:** Ni mila.

**Benjamin Kabwere:** Ni mila ya kusema *tufiche aibu* (hiyo ni kigiriama). Tufiche aibu kwamba huyu bwanake ameachwa na bwanake ambaye ana ndugu yake. Akiwa hana ndugu hakuna neno, lakini kama ana ndugu yake ile aibu aifiche kama vile zamani tulikuwa.

**Com. Lethome:** Na kuhusu mali? Wanawake wamesema hiyo ufa inatumiwa na wanaume ndugu za mabwana waliokufa, kwa sababu ya mali, ule urithi.

**Benjamin Kabwere:** Kitu kimoja ambacho mimi napendelea mimi kama mtu mzima, mimi nimezaa watoto na ni mtu mzima nimekaa siku nyingi. Ningependa hivi mtu akiolewa, hana urithi kwa ule mji kwa sababu yeye ameenda mji mwingine. Lakini akiwa hajaolewa yule ni wa pale maana yeye hakukataa kuolewa, maana hataita wanaume: njooni hapa unioe, mimi unaweza kunioa, kwa nini usinioe, hataita. Kwa hivyo yeye atakuwa nia yake ataka kuolewa na hapati wanaume. Sasa yule ana haki ya kupata urithi pale wa baba.

**Com. Lethome:** Wa baba. Ndiye huyu aliyeolewa sasa, mume wake akafa, urithi wake ndio …….. (inaudible).

**Benjamin Kabwere:** Sasa yule ambaye ameolewa na bwanake amekufa. Huku si yule bwanake si alikuwa na ndugu yake? Alikuwa na ndugu yake yule, maana mtoto wangu ameolewa, umeoa wewe, vile umemuoa wewe sasa ni mtoto wangu. Sasa wewe umekufa ndugu yako si yuko, unataka kuziba aebu kama ile yangu nimesema.

**Com. Lethome:** Sasa mambo ya kuziba aibu tumeshamaliza mambo ya mali sasa.

**Benjamin Kabwere:** Yule akiwa ameolewa hana urithi kwa pale mji wangu, kwa sababu yeye ni kabila nyingine sasa.

**Com. Asiyo:** Lakini nauliza hivi kama ndugu yako amefariki na ameacha ndugu yake pale na watoto wake, ile mali yake itakuja kwako au itakaa na watoto wake na bibi yake?

**Benjamin Kabwere:** Ile mali itakuwa ni ya bibi yake na watoto wake. Wewe ni bibi tu, kwa vile umeficha kwamba akizaa mwingine asiitwe ni mgeni amekuja. Ni wa pale nyumbani.

**Com. Lethome:** Na sasa na kama yule mwanamke hataki ufa, anasema mimi sitaki?

**Benjamin Kabwere:** Huyo mwanamke akisema hataki ufa, ile aibu hata asizae.

**Com. Lethome:** Sasa, aseme sitaki ni hali yake.

**Benjamin Kabwere:** Basi hiyo uhuru yeye ameolewa pale kwa mji.

**Com. Lethome:** Ameolewa na nani?

**Benjamin Kabwere:** Ameolewa na yule mtu ambaye amekufa.

**Com. Lethome:** Kuolewa na family.

**Benjamin Kabwere:** La. Sisi kwetu hata kama hiyo kawaida sisi mtu akiwa ameolewa hata kama mtu hana mali anaongezwa na mtu mwingine na mtu mwingine, baba yake akiwa hana mali wanapeana, huyu anataka ni haki yule atoe, yule atoe kusudi apate bibi. Awe ni mtu wa pale nyumbani.

**Com. Lethome:** Na ikiwa anaolewa na?

**Com. Asiyo:** Na family. Anaolewa na family?

**Benjamin Kabwere:** Na family. Sasa yeye hawezi kuwachwa ikiwa atakuwa anateseka halafu aambiwe aaa… wewe bwanako amekufa wewe. Nenda huko! Hawezi kuambiwa hivyo.

**Com. Lethome:** Sasa kusaidiwa ni vizuri, lakini kudhulumiwa mali yake?

**Benjamin Kabwere:** Basi hiyo kupokonywa mali, si haki. Lakini mtoto nasema tena, mtoto akiwa ameolewa hana urithi kwa babake, ana urithi kwa bwanake huku. Maana huyo ni kabila ingine sasa. Mimi ni mgiriama, mkiza mimi. Basi kwa ukizani kwangu, bibi yangu yeye atakuwa kwa wakiza mpaka afe, na yule ameolewa na wabaya huko, atakuwako mwabaya mpaka afe.

**Com. Lethome:** Apende asipende.

**Benjamin Kabwere:** Apende asipende, amechukuliwa. Hiyo habari ya pombe sasa. Umeniuliza kitu kizuri na ninakuambia kama mtu mzima ambaye nimekaa siku mbili tatu. Hii habari ya pombe kwanza ukiona hivi nakwambia yule akiolewa hakuwa wa mji huu tena, kwanza yeye mwenyewe ataulizwa: unamtaka huyu? Anapewa kiapo. Sisi ukoo wetu sisi wagiriama, huyo unamtaka, eeh, ni kweli. Wewe nenda uchukue pombe, chupa mbili tatu, hata kama ni moja. Akija pale anaambiwa huyu ndiye amelete pombe huyu, anachukua moja ile pombe inawekwa inapewa huyu msichana. Hii pombe ni ya huyu, unasema ninywe? Ee nasema unywe. Anachukua ile pombe anampa babake, kunywa mimi nitafuata huyu, nitaolewa na huyu. Sasa baba anakunywa pombe mtoto wake amesema yeye ataolewa kule na mimi nimepewa pombe anakunywa. Hili pombe ni kitu moja ambacho kina siri. Ukiwa ni watu wamekosana hiyo itatoa siri. Kwa sababu hiyo pombe akinywa hivi, au akianza kulewa kidogo sasa yeye anatafuta makosa. Hivi leo makosa iko wapi?

**Com. Lethome:** Pendekeza?

**Com. Asiyo:** …. (inaudible).

**Benjamin Kabwere:** Sasa mimi napendekeza hivi pombe ni nzuri kabisa kwa wagiriama kwa sisi.

**Com. Lethome:** Kwa kutoa siri?

**Benjamin Kabwere:** Eeh kwa kutoa siri. Sasa atatoa siri yule baba atasema, mimi ningekupenda wewe mtoto ungeoa mtoto wangu, lakini babako mbona akaja huku kwani ni ndugu yako akafanya matendo mabaya huku kwetu? Huwezi kupata huyu msichana wangu.

**Com. Lethome:** Haya Mzee Kabwere tumeshukuru.

**Benjamin Kabwere:** Sasa una mengine nikuambie au bado? Basi kitu zaidi ninachotaka ni kulipwa pesa, mimi sijalipwa.

**Com. Asiyo:** Na hiyo tutaandika.

**Benjamin Kabwere:** Basi muandike.

**Com. Lethome:** Katambu Hamisi, yuko? Ndiye huyu mwenye camera, haya karibia Bwana Katambu.

**Com. Asiyo:** Na useme vizuri sana kila kitu kimesemwa sasa.

**Hamisi Katambu:** Kwa majina naitwa Hamisi Katambu kama ilivyoandikwa hapa. Kwanza kabisa ningependa kuongea kuhusu mambo ya Katiba, Katiba. Katiba ni lazima iwe majimbo, na ikiwa majimbo ina sababu. Kwanza kabisa sababu yake ni kwamba sisi wa Coast hapa tumezulumika siku nyingi. Kwa sababu gani? Uchumi wetu mkubwa ama mwingi, tuseme kitu kama 95% ya uchumi wetu hapa Coast because katika province zote ambazo ziko Kenya, Coast ndio nambari moja kwa uchumi. Sasa katika pesa zetu za uchumi hapa nyingi sasa zinawafaidi watu wa up-country. Kwa hivyo ki hapa ningependekeza kwamba iwe majimbo ili pesa ile ikipatikana hapa, basi percentage kubwa iwe itabakia hapa hapa na nyingine sasa ipelekwe juu.

**Com. Lethome:** Hebu pendekeza hiyo percentage.

**Hamisi Katambu:** Percentage mimi ningependekeza percentage kama 85% ibakie hapa na 25% ipande kule juu ikasaidie wenzetu.

Point ya pili, ningeongea kuhusu uchumi. Uchumi huu wa Kenya pale mwanzo mwanzo ama kabla hii multi-party uchumi ulikuwa ni mzuri. Kwa sababu utakuta kwamba uchumi huu kitambo sisi tulikuwa tunanunua mkate ilikiwa ni shilingi tatu, lakini baada ya 92 kuja huku juu, uchumi umeharibika kabisa. Na uchumi haungeharibika bila shaka ni Rais wetu, ndiye aliyeuharibu uchumi.

**Com. Lethome:** Sasa pendekeza.

**Hamisi Katambu:** Sasa ningependekeza hivi, ningependekeza ya kwamba serikali irudie ule mfumo wake wa kitambo wa Controlling Board kuwa mfukoni kwa serikali, kwa sababu ile ndiyo ambayo itasaidia mwananchi ya kwamba zulma haitatembea. Kwa sababu ikiwa mkate ni shilingi mbili hapa, imaanishwa kwamba hata Isiolo mkate ule ule utakuwa wa shilingi mbili. Ama kama ni sukari shilingi kumi hapa, hata Isiolo iwe hiyo hiyo shilingi kumi. Kwa hivyo ningependekeza kwamba hii Controlling Price Board irudi mfukoni kwa serikali, na uchumi utabadilika.

Point nyingine, ningeongea kuhusu mambo ya education, elimu: mimi sioni haja ya kwamba elimu saa hizi imekuwa juu, kushinda pale mahali pa mwanzo. Na hali ya kwamba hakuna mabadiliko yoyote kwanzia miaka ya sitini mpaka saa hii. Elimu ni ile ile. Lakini utakuta kwamba saa hizi elimu imekuwa gharama kwanzia nursery school mpaka umalize university. Sasa mimi

kitu ningependelea hapa katika education, education system iwe bure as from nursery school upto class eight, iwe bure. Halafu pengine kule secondary school from form one kuendelea kule mbele mpaka university, ikiwa utatozwa pesa basi fees zile ziwe reasonable. Iwe hali ya kwamba iko chini hali ya kwamba, hata yule maskini wa mwisho ataweza kumfundisha mtoto wake secondary school. Utakuta kwamba hapa Coast, especially hapa Coast watu wamerudi nyuma ki-elimu kwa sababu ya kwamba pesa hakuna, watoto wanapita vizuri, lakini sasa pesa hakuna ya kumpeleka huyu mtoto secondary school. Kwa hivyo ningependekeza ya kwamba, gharama ya secondary school ipunguzwe na gharama ya primary school iondolewe haswa, iwe free.

Kitu ingine, ambayo pengine ni ya nne hiyo, point ya nne, ningeongea kuhusu corruption. Corruption hii mimi naonelea haingetokea hapa Kenya, isipokuwa corruption imeanza kwa watu wale wakubwa, ambao they are the most corrupted people.

**Com. Lethome:** What do we do?

**Hamisi Katambu:** What we should do, ni kufanya namna hii. Kwa sababu ukiangalia kama Rais amepewa mamlaka makubwa sana, ambapo hapa sasa ndiyo corruption ilipoanzia. Kwa sababu gani, ikiwa mimi niko hapa na Rais yuko karibu na mimi, mimi nikifanya ukorofi wowote hapa, Rais pale ni lazima atani-protect, kwa sababu yeye yuko above the law. Nikianza kuwa pinched off yule anasema achaneni na huyo mtu, sasa hata ukipelekwa kortini hakuna lolote linalofanyika. Kwa hivyo ningependelea ya kwanza, kwanza mamlaka Rais asipewe vile alivyonayo saa hizi, apokonywe. Na awachiwe kile kiwango chake kama Rais anachotakikana akae nacho. Hapo naonea corruption tunaweza kuimaliza kabisa Kenya hii.

Kitu ingine, ningeingilia upande wa land: nitapiga chap chap kwa sababu wakati ndio huo, sasa nitaguza guza tu mbio mbio. Ningeingilia upande wa land: upande wa land, okay, hii problem ni nationwide, lakini utakuta kwamba to some parts of the country wamegandamizwa zaidi. Na tukiangalia especially hapa Coast hatuwezi kufananisha hapa Coast kwa upande wa land au mashamba na watu wa bara. Watu wa bara wameendelea kwa sababu moja. Sababu ambayo imefanya wale wenzetu wameendelea sisi tumekaa chini huku ni kwamba, title deed ndio kitu muhimu ambacho kinaweza kumuinua mtu. Ya kwamba mtu akipata title deed yake, kama ni ya shamba ama ni nyumba kama hizi amepata title deed, yeye ana uwezo kwenda katika benki yoyote hapa Kenya na kwenda kuchukua pesa. Sasa utakuta ya kwamba sisi wa Coast tutachukua vipi pesa ikiwa title deeds zenyewe hatuna? Ikiwa title deeds sisi hatuna itakuwa vipi? Haiwezekani na hiyo ndiyo ni kitu ambayo inaweza kutuendeleza sisi watu wa Coast. Ndio maana utakuta kule watu wa bara wao wameendelea kwa sababu ya kuchukua ma-titles yao na kupeleka katika benki na kuchukua mapesa na kujiendeleza wenyewe. Kwa hivyo ningependekeza ya kwamba title deeds zihakikishwe ya kwamba hii *cake* ya title deed iwe itasambazwa Kenya mzima. Si kwamba hapa Coast pekee yake pafanyiwe hivyo, kwingine kuwe kutazidi kugandamizwa, hapana. Inatakikana hii mambo iwe sawa sawa kila mahali.

**Com. Lethome:** Malizia Bwana Hamisi.

**Hamisi Katambu:** Nikimalizia, ningependa kuongea mambo ya pombe: mambo ya pombe ijapo mtu kama mimi pombe siitumii, lakini nikiangalia kwa mbali hivi kuna watu ambao walifaidika na pombe. Na wengine bado wanafaidika mpaka saa hii na pombe. Sasa utakuta ya kwamba ikiwa kuna sheria inayomzuia mtu kuenda kugema na kuuza ile pombe. Ikiwa kuna sheria ambayo inamzuia mtu vile, kwa nini sheria ile ile isimzuie yule mtu anatengeneza pombe kwa kiwanda? Because mimi nikienda nikinunua bia, nitalewa na kama nitaenda kufanya uhalifu mimi nitaenda kufanya uhalifu kwa sababu nimelewa. Mimi nikinywa mnazi pale, nimeamua kwenda kufanya uhalifu, definitely ni lazima naenda kufanya uhalifu. Lakini kwa nini mnywaji wa bia aonekane yeye ni mzuri, mnywaji wa pombe ya mnazi aonekane ni mbaya? Sheria kama hiyo inatakikana kubadilishwa mara moja, ili because serikali iko na njia nyingi za kutengeneza vitu kama hivyo. Ndio maana hata bia yenyewe unakuta kwamba iko katika kiwanda, inatengenezwa vizuri watu wanauziwa kule na watu wanakunywa hiyo bia bila matatizo yoyote. Kwa hivyo mfumo huo huo uliofanywa kutengeneza hiyo bia, pia ya pombe ya mnazi nayo ipatiwe mfano huo huo, na itengenezwe vizuri, na watu wakunywe hii pombe ya mnazi. Kwa sababu wako watu wengi sasa hata wengine ni ma-lawyers, wengine ni ma-ministers na wamesoma na pombe ya mnazi. Sasa vipi huyu minister alisoma pombe ya mnazi, leo mimi babangu anaambiwa hakuna ruhusa ya kugema hapa, ama hakuna ruhusa ya kuuza mnazi. Why? Hiyo ni lazima tuiangalie vizuri. Kwa hayo machache, nilikuwa na mengi, lakini kwa sababu ya wakati.

**Com. Asiyo:** Umeongea mambo ya bia, na ukalinganisha na la mnazi. Je, bia inajengwa na watu wenyewe, wanaitengeneza pale wanauza. Kwa nini watu walio na mnazi hawawezi kujiunga pamoja wakatengeneza mnazi, kiwanda cha mnazi wakauza? Hakuna kitu kitasajiwa juu ya kufanya hivyo.

**Hamisi Katambu:** Well, unajua kitu iliyoko ni kwamba, si kwamba hawawezi kukaa chini na kutengeneza kitu kama hiyo. Wanaweza kukaa chini wakatengeneza kitu kama hiyo, lakini kitu iliyo pale ni guidance. Wanataka kuwa guided because hata kule kitambo, ile miaka ya sitini huko nyuma au miaka ya sabini, kulikuwa kuna vilabu ambavyo vimewekwa special vya minazi, special vya minazi, building kama hii, time kama hizi watu wamejazana huku, wanakunywa mnazi pole pole na halafu wanaenda kwa nyumba. Sasa kuwa formed mpaka iwe kama vile watu wa bia, inatakikana guidance wale watu wenye elimu zaidi wakuje wakae chini na hawa wazee wapange vile ambavyo pengine wanaweza kupata pengine kama machines za kutengeneza, za packing ya ule mnazi. Then definitely wao wata-pack huo mnazi na watauza hata ma-nchi za nje.

**Com. Lethome:** Haya asante Bwana Hamisi kwa maoni yako hayo. Jiandikishe pale. Oscar yuko hapa? Pastor Jane yuko hapa? Washaakwenda. Haya tuna James Ngumbao?

**Com. Asiyo:** Hawa wameongea.

**Com. Lethome:** Walizungumza. Timothy Mwapo. Ni wewe Timothy, karibu. Edward yuko? Edward Shambayo? Hayuko. Haya basi wewe ndio mtu wa mwisho hapa.

**Timothy Mwapo:** Majina yangu mimi ni Timothy Mwapo, nakaa Bofa. Kwanza jambo la kwanza, ningelitaka kuongea juu ya mnazi: nasikia mnazi watu wengi wa Pwani wanatetea mnazi juu ya pombe, lakini ni kwamba hawajui kwamba mnazi una faida nyingi, hata si pombe pekee yake. Kwa hivyo nafikiri ingelikuwa vizuri kama wangelitetea zile faidi zingine ziko kwa mnazi, ndio sasa mnazi uonekane maana yake.

**Com. Lethome:** Sasa uzitetee, tetea wewe.

**Com. Asiyo:** Wewe.

**Timothy Mwapo:** Kuna mnazi unatoa hata mbao, tunaweza pata mbao kutoka kwa mnazi, tunaweza kupata mafuta kutoka kwa mnazi. Na hata mnazi tunaweza pata hata kuni, maana ukitoa zile nini zake zile za nazi, hizo tayari ni kuni.

**Com. Asiyo:** …. (inaudible).

**Timothy Mwapo:** Makuti pia tunapata kwa mnazi. Kwa hivyo watu wamesahau faida zile za maana kwa mnazi lakini wanatetea pombe. Kwa hivyo mimi ningependekeza kwamba hawa wa Pwani wenyewe watoe faida za mnazi kwanza, ndio mnazi uhalalishwe. Na hata ukihalalishwa kupitia kwa pombe, lakini uwe tumepata faidi zingine nyingi kutoka kwa ule mnazi.

Jambo la pili ningelitaka kusema, ni kuhusu hizi mobile phones: hizi mobile phones zinatusaidia sana, lakini kupitia kwa hawa ma-dereva wetu zimekuwa mbaya. Na tunaona hata accident nyingi sasa zinatokea kwa sababu ya hizi mobile phones. Na kwa sababu polisi wetu wako pale barabarani kama picha, kula tu, ndio tunaona kwamba hawachukulii umuhimu wa kuangalia na hasa kuangalia kwa nini tunaendelea kuumia kwa sababu ya ma-dereva wetu ambao hawajali.

**Com. Lethome:** Pendekeza.

**Timothy Mwapo:** Ningelipendekeza kwamba kukiwezekana kuwe na ma-CIDs ambao watakuwa wakiingia kwa zile matatu na ku-check. Akiona dereva yeyote anaongea na mobile phone wakati anapeleka gari, ashikwe.

**Com. Lethome:** Dereva wa matatu pekee yake, ama dereva yeyote?

**Timothy Mwapo:** Dereva yeyote ambaye anaenda kwa barabara. Hata kama yule CID hayuko kwa ile gari, lakini anaweza kuwa kwa gari ingine anaona ile akiongea na mobile phone kwa gari ingine upande ule, amfuate na amuulize kwa nini anafanya vile. Ili tuone kama hizi ajali zitapungua, na hapo hapo kupitia hata kwa hizi miraa, unaona pia hiyo miraa inaleta majeraha, ama inaleta ajali katika barabara. Maana dereva anaenda huku amesahau, huku anatafuta mraa wake sijui umeanguka wapi. Kwa hivyo ningependekeza kuwe na mambo kama hayo.

Na mimi singelikuwa na mengi ningelitaka kuongea juu ya hizi sheria zetu, ama hawa wabunge, watu wanaotengeneza sheria. Hizi sheria zinazotengenezwa bunge, nafikiri huwa ni za kila mtu hata mbunge mwenyewe ambaye anazitengeneza, anafaa kuzifuata. Lakini tunaona mara ingine sisi tunapopigana tukipelekwa kortini tunahukumiwa. Lakini tunaona mbunge anahukumiwa anaenda anafuata fuata ile kesi, mara ingine hata inaisha hujui imeisha vipi, na mwingine anahukumiwa labda miezi mitatu, lakini unasikia amefungwa siku tatu ametoka ile kesi imeisha. Kwa hivyo tungelitaka wale ambao wanatunga hizo sheria, kwanza wao wazifuate.

Langu la mwisho, ni kuhusu msafara wa Rais. Haswa hapa Pwani. Mimi nishakaa Nakuru nishaona President hata akibishana na magari mengine yanapita na yeye anapita. Lakini hata Pwani President akija huwa tuko na shida kubwa sana, maanake mara ingine unaweza kusimamishwa hata nusu saa kwa barabara na President yuko Mtwapa na wewe umesimamishwa hapa Mnarini, unakaa for half an hour ndio President apite. Kwa hivyo ningependekeza ikiwezekana kuwe na muda wa pale mahali President anafika, ndio magari yanasimamishwa ama watu wanawekwa kando. Ningependekeza kuwe na muda fulani ama wale ambao wanasimamisha watu, wahakikishe kwamba ni hatua gani ambao inafaa mtu asimamishwe ndio President apite. Kwa hivyo yangu ni hayo.

**Com. Lethome:** Kuhusu msafara wa Rais, ningependa kuuliza: Rais anapokwenda nje huandamana pengine na mawaziri na watu wengi, kwa vile pengine mawaziri kumi au kadhaa wamefuatana naye. Pia utakuta amekwenda pengine kufungua kiwanda fulani, pengine ni kiwanda cha kilimo kinahusiana na mambo ya kilimo. Wanakuja mawaziri wote wako pale, wabunge wengi watakuwa pale, itakuwa hakuna shughuli nyingine ni ile. Sijui unapendekeza nini?

**Timothy Mwapo:** Kuhusu hawa wabunge?

**Com. Lethome:** Ule msafara wa Rais kuwa na watu wengi ndani yake ma-waziri, wajumbe?

**Timothy Mwapo:** Mimi langu ningependekeza maana nafikiri siku hiyo ofisi nyingi huwa ziko tupu, hazina watu. Kwa hivyo ningependekeza yule mwenye ambaye anahusika na ile wizara, yeye na katibu wake na wale wadogo zake kwa ile ofisi, hawa wanafaa kufuatana na Rais. Lakini wengine hasa Vice President yeye ndiye anatakikana kuwa kule ambapo Rais anashinda kule, yeye aangalie mambo ya kule. Lakini yeye utamuona na yeye yuko hapo na Rais, je, ni nani wamemuacha huko? Kwa hivyo ningependekeza kwamba watu wote wabaki kwa ma-ofisi zao kuhudumia wananchi, na yule ambaye anahusika katika ile wizara awe na Rais katika ule msafara.

**Com. Lethome:** Haya twashukuru sana Bwana Mwapo. Nikiangalia hapa namuona Ouko ushazungumza. Mzee ulipeana jina lako, na unataka kuzungumza dakika moja? Njoo hapa uzungumze, peana jina na uzungumze dakika moja.

**Allan Isiaho Shitakwa:** Asante sana siku kama ya leo mweneyekiti. Mimi naitwa Allan Isiaho Shitakwa, ni mzaliwa wa Kakamega lakini naishi Pwani hapa. Napendekeza hivi hii Tume isiwe ya kufuatiliwa mbio na uchaguzi ujao. Naona ni Tume ya maoni ambayo watu wataweza kujirebekishia, tabia na mambo mengi ambayo yataweza kusaidia Kenya hii. Langu la kupendekeza, siku nyingi tumefanya na wahindi na wazungu kazi kimshahara, utaweza kufanyia shilingi tano na mzungu muhindi ataweza kukufanyia shilingi mia nane, kwa siku.

**Com. Lethome:** Hapo unapendekeza nini?

**Allan Isiaho Shitakwa:** Napendekeza tuangaliwe sana sisi waafrika ambao tunafanya na wahindi na wazungu pamoja.

**Com. Asiyo:** Mambo ya kazi na mishahara?

**Allan Isiaho Shitakwa:** Mambo ya kazi na mishahara. Unaweza fanya na muhindi ama na mzungu pia anafanyia shilingi mia nane kwa siku na wewe unafanyia shilingi tano, na duka ni moja. Kwa hivyo langu, pendekezo langu ni hilo.

**Com. Lethome:** Asante sana. Kuna mwingine ambaye amejiandikisha? Umejiandikisha? Unataka kusema? Sema.

**Mwangiri Mugomba:** Kwa majina naitwa Mwangiri Mugomba. Ningependekeza hasa mambo ya shule kutoka nursery mpaka class eight. Tuseme elimu ya msingi iwe bure kabisa na iwe lazima kwa mzazi kupeleka mtoto wake skuli.

**Com. Lethome:** Kama hatampeleka?

**Mwangiri Mugomo:** Awe anaweza kuchukuliwa hatua ya kisheria. La pili, ningependekeza hospitali zetu ziwe za bure, hizi za serikali. Hospitali zote za serikali ziwe bure na ziwe zikijengwa mpaka vijijini. Na ningependekeza Katiba ya serikali ya majimbo kwa mfumo ujao, lakini 50% ya economy ya hapo mahali ya hilo jimbo ibaki pale pale, nyingine ziende kwa serikali kuu ambapo serikali kuu itasaidia majimbo mengine yasiyojiweza. Tusichukue 65 au 70%, ni juu sana. Tubaki na 50% another 50% iwe inaweza kuenda kwa serikali kuu, kwa sababu mapato ya majimbo si sawa sawa. Kwa hayo machache asanteni sana.

**Com. Lethome:** Haya asante. Nafikiri kwa kufikia hapo tumefika mwisho kwa vile hatuna wenyeji waliobaki hapa naona mluhya mmoja na mluo mmoja ndio waliobaki hapo. Lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu na wale wote waliokuja tunawatakia mrudi kwa heri na sisi tunaomba Mwenyezi Mungu abariki kazi yetu na tuende kwa amani. Tunawashukuru nyote, na wafikishieni ujumbe wengine wale ambao bado wana maoni haina maana kuwa baada ya sisi kuondoka ndio mwisho wa kutoa maoni, mtu anaweza kuwasilisha maoni yake wakati wowote. Anaweza kuandika, na kuleta kwa Tume yetu. Mnaye mwakilishi wenu hapa wa Kilifi District mpeni maoni yenu yatatufikia. Yule pale bwana, unaitwa nani, Daniel Mwaringo.

**Com. Asiyo:** Kuja karibu watu wakujue pia.

**Com. Lethome:** Watu wa Kilifi wanasema hawakujui. Sasa ndiye huyu Bwana. Mnaweza kuwakilisha maoni yenu kupitia kwake yatatufikia. Huyu ndiye mwakilishi wa district ya Kilifi. Kwa hayo tunawashukuru, asanteni, Mungu awabariki.

**Com. Asiyo:** Mungu awabariki.

**Meeting ended at 5.45 pm.**

*********************************************